Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Saba – Tarehe 29 Aprili, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

***D U A***

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi kuwasilisha Hati. Kwa siku moja na nusu nilikuwa na udhuru kidogo na kuna wakati nilikuwa naibia ibia hivi katika vyombo nilivyopewa kusikilizia na kuonea kule nyumbani.

Napenda niwashukuru sana Wenyeviti wote Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Job Ndugai na Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, kwa kazi nzuri sana ambayo wameifanya ambayo inakuwa ni faraja kubwa kwetu. Nawashukuru sana na nimeona shukrani hizi nizitoe waziwazi. Ahsante sana. (*Makofi*)

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE)**

Taarifa ya Mwaka wa Hesabu za Shirika la Bima la Taifa kwa mwaka 2007 *(The Annual Report and Accounts of the National Insurance Corporation of Tanzania Limited for the year 2007)*

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI (K.n.y. KABWE Z. ZITTO) - MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA:**

Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwa mwaka Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2007.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 83

**Ukubwa na Wingi wa Kazi za OWM – TAMISEMI**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inahusika katika shughuli za Wizara za Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, upande wa shule za Msingi na Sekondari, ujenzi wa Miundombinu, ujenzi wa mabwawa na kadhalika:-

(a)Je, Serikali haioni kuwa Ofisi hii ni kubwa mno na husababisha mlundikano wa kazi?

(b)Je, kwa nini masuala ya Wizara ya Afya kama magari na watumishi yasiwe chini ya Wizara ya Afya?

(c)Je, Serikali haioni kwamba Wakurugenzi wa Halmashauri wamepewa mzigo mkubwa wa hurundika malalamiko ya Wizara nyingi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 26/6/2007 katika Mkutano wa Nane wa Bunge lako Tukufu, ofisi yangu ilijibu swali Na. 87 la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, linalofanana na swali hili.

Swali hilo liliulizwa na Mheshimiwa Kaika Telele, Mbunge wa Ngorongoro, kwa niaba ya Mheshimiwa Laizer. Ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ndiyo husimamia shughuli mbalimbali katika Mikoa na katika Halmashauri zote nchini. Shughuli hizo siyo tu zile zinazohusu Sekta ya Afya bali ni pamoja na Sekta ya Maji, Elimu, Barabara, Kilimo, Maliasili, Uvuvi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 1982, Serikali iliamua kwa makusudi kuanzisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kama vyombo vya kutekeleza shughuli mbalimbali zilizo chini ya Serikali zikiwemo zile nilizozitaja hapo juu. Bunge lako Tukufu katika kutekeleza azma hiyo lilitunga sheria mbalimbali za Serikali za Mitaa zikiwemo Sheria Na. 7, Sheria Na.8, na Sheria Na.9 za mwaka 1982. Azma hii ilitokana na Sera za Chama Tawala za kupeleka Madaraka kwa wananchi kwa mujibu wa Ibara ya Katiba yetu Namba 145 na 146, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Mheshimiwa Spika, naamini Waheshimiwa Wabunge, wamekwishakuona matunda ya utekelezaji wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (*Decentralization by Devolution*) kwa jina maarufu kama *D by D.*

Aidha, kwa mujibu wa Sheria ya Tawala za Mikoa na zile za Serikali za Mitaa, majukumu ya Serikali Kuu ni pamoja na kutunga Sera za Kitaifa, Mafunzo ya Kitaalamu na kuweka vigezo vya utendaji katika sekta husika. Hayo ndiyo maeneo yanayohusiana moja kwa moja na Wizara za Kisekta. Jukumu kuu la ofisi yangu ni kuratibu kwa makini mahusiano muhimu baina yake na Wizara za Kisekta, Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau mbalimbali wa maendeleo. Kwa sasa shughuli za utekelezaji ikiwa ni pamoja na watumishi na vitendea kazi katika ngazi ya Halmashauri zitaendelea kuwa chini ya vyombo hivyo kulingana na matakwa ya Katiba na Sheria zilizotungwa na Bunge lako Tukufu.

(c) Mheshimiwa Spika, naomba nisikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba Wakurugenzi wa Halmashauri wamepewa mzigo mkubwa wa kurundika malalamiko ya Wizara nyingi. Halmashauri hundwa na watendaji kwa upande mmoja na Madiwani kwa upande mwingine. Halmashauri nyingi zina Idara zisizopungua nane na vitengo vitatu kulingana na mahitaji ya Halmashauri husika.

Aidha, kuna Kamati mbalimbali zinazoundwa na Waheshimiwa Madiwani. Kwa kushirikiana na Sekta zote majukumu ya msingi ya Mkurugenzi ni kuwa Msimamizi Mkuu wa shughuli zinazotekelezwa katika eneo lake. Shughuli hizo ni pamoja na kutoa huduma kwa wananchi, kuhakikisha kwamba kuna uhuru na amani katika jamii; na kudumisha ustawi wa kiuchumi na kijamii katika eneo lote la Halmashauri.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa, ni kweli madaraka yamepelekwa kwenye Serikali za Mitaa, lakini kazi kubwa imepelekwa na hakuna wataalam. Ukienda kwenye Kata na Vijijini hakuna wataalam wa kutosha. Je, Serikali haioni kwamba kulundika kazi bila wataalam ni tatizo?

La pili, kwa kuwa, magari yote yanayohitajika katika Wizara mbalimbali yananunuliwa na Wizara ya Miundombinu siyo busara sasa kila Wizara wanunue magari yao kuliko kulundika magari yote kwenye Wizara ya Miundombinu kupewa jukumu la kununua magari yote kwa kila Wizara?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikubaliane naye kwamba kweli tuna upungufu wa wataalam katika sekta mbalimbali kwenye Halmashauri zetu.

Lakini kama mnavyofahamu kwamba Serikali sasa hivi imechukua jukumu kubwa la kutoa elimu au kutoa mafunzo ya kitaaluma katika sekta mbalimbali ili kuhakikisha kwamba huo upungufu katika vyombo vyetu vya Serikali za Mitaa unapungua.

Kwa mfano, Wizara ya Kilimo inaajiri wataalam wengi wa kilimo sasa hivi na tunao wataalam wa kutosha na bado tunahitaji wataalam hao. Upande wa Afya pia katika mpango wa MAM nao wanajitahidi kwa kiasi kikubwa kutoa wataalam mbalimbali ili kuweza kukidhi matakwa ya mahitaji katika Serikali za Mitaa.

Kwa hiyo, jukumu la Serikali kuu kama nilivyosema ni kuhakikisha kwamba wanatoa wanataaluma wengi, walimu, Madaktari, Manesi na katika sekta mbalimbali ili kuziba pengo katika Serikali za Mitaa mpaka hapo hali itakavyokuwa nzuri nina uhakika kwamba kuanzia ngazi ya Kata kutakuwa na Mabwana Shamba, Madaktari, Manesi na Walimu wa kutosha kwa sababu Serikali inajitahidi sana katika kutoa mafunzo kwa wanataaluma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la magari naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi Serikali iliamua kwamba magari yote yawe ya Serikali za Mitaa, yawe ya Wizara yananunuliwa na Wizara ya Miundombinu kwa sasa hivi. Zoezi hili limefanyika, kuna mapungufu ambayo yametokea hapa na pale. Lakini tutakaa kama Wizara na wenzetu wa Wizara ya Miundombinu ili tuangalie ni njia gani ambayo itakuwa rahisi ili kuwezesha magari hayo yanunuliwe kwa wakati muafaka ili tuweze kutekeleza majukumu yetu kwa urahisi. *(Makofi)*

Na. 84

**Kuweka Lami Barabara ya Tarime – Nyamwaga**

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA (K.n.y. CHARLES N. MWERA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya Tarime – Nyamwaga, Wilayani Tarime haijafanyiwa matengenezo makubwa kwa muda mrefu na ni mbaya na inapitika kwa shida sana:-

Je, Serikali ina mipango gani ya kuiwekea lami barabara hiyo ili iweze kupitika kwa wakati wote?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Mwera, Mbunge wa Tarime, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kipande cha kutoka Tarime hadi Nyamwaga chenye kilomita 24 kipo katika barabara ya Tarime - Nyamwaga- Mugumu – Nata yenye urefu wa kilometa 124 ambayo ni barabara ya Mkoa inayosimamiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *TANROADS* Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Spika, naomba nisikubaliane na Mheshimiwa Mbunge ya kwamba kipande cha barabara ya Tarime – Nyamwaga haijafanyiwa matengenezo makubwa kwa muda mrefu, kwani Serikali imekuwa na jitihada za mara kwa mara za kuifanyia matengenezo barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekwishaanza kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami hatua kwa hatua. Hadi kufikia mwaka wa fedha 2007/2008 jumla ya kilometa 1.65 za lami zimekamilika kwa gharama ya shilingi milioni 395.4.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Serikali ilitenga jumla ya shilingi milioni 120 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Jumla ya kilometa 2.5 kuanzia Rebu hadi Kibumayi zimepangwa kujengwa. Zabuni kwa ajili ya ujenzi huo zilifunguliwa tarehe 6 Aprili, 2009. Kazi ya uchambuzi wa zabuni hizo inaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sikubaliani kwamba barabara hiyo haijafanyiwa matengenezo makubwa kwa muda mrefu.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri ambalo sikuridhika nalo. Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba mwaka 2007/2008 wameweza kujenga barabara hiyo kwa kilomita 1.65 kwa kiwango cha lami; na shilingi milioni 120 zilizotengwa mwaka 2008/2009 wameweza kujenga kilomita 2.5 wastani wa jumla ya kilomita 4. 15 kwa muda wa miaka mitatu. Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba barabara yenye kilomita 24 ikiwa kila mwaka wastani wa kilomita 1.5 ndiyo inajengwa, ina maana barabara hiyo itamalizika mwaka 2025. Je, huo ndiyo utawala bora, haoni kwamba huko ni kudidimiza maendeleo ya wananchi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, suala la msingi hapa lilijielekeza kwa kusema kwamba barabara hiyo haijafanyiwa matengenezo makubwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, na mimi nimesema hapa kwamba barabara hiyo imekuwa ikifanyiwa matengenezo mara kwa mara. Kwa mfano, katika mwaka 2005/2006 Serikali ilitenga jumla ya shilingi milioni 48 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida, lakini mwaka 2006/2007 Serikali ilitenga jumla ya shilingi milioni 11 katika kutengeneza barabara hiyo katika matengenezo ya muda maalum.

Kwa hiyo, katika miaka mitatu, Serikali imekwishatumia kiasi cha shilingi milioni 421.9 kwa matengenezo ya mara kwa mara kwenye maeneo yale korofi. Lakini hayo

matengenezo ya lami ndiyo mpango ambayo unafanyika katika kipande kile ambacho kipo katika eneo ambalo limepangwa kutengenezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilichokuwa nimesema hapa ni kwamba si kweli barabara hii haifanyiwi matengenezo ya mara kwa mara, na kwa hiyo, nataka tu nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba huo ni Utawala Bora na Serikali inawajali wananchi wa Tarime ndiyo maana inatenga fedha mara kwa mara. (*Makofi*)

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kushukuru sana sana kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tatizo la barabara la Tarime Nyamwaga linafanana sana na tatizo la barabara ya Nzega-Tabora na linafanana sana na barabara ya Manyoni-Itigi-Tabora-Urambo-Kigoma. Tumesikia mengi kuhusu barabara hizi mbili, lakini mpaka sasa hivi Serikali inafanya nini hususan barabara ya Nzega – Tabora kwa sababu ni fupi? Naomba jibu na ufafanuzi wa Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, mimi kwanza nikubaliane naye kabisa kwamba barabara hizi alizozitaja zinahitaji matengenezo na kama ambavyo tumekwishatoa kauli hapa mara kwa mara kwamba mipango ya Serikali ni katika kuzitengeneza barabara hizi ni kutafuta fedha ili ziweze zikatengenezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitakachokisema hapa ni kwamba jitihada za Serikali kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo zinaendelea, na kadri tutakavyokuwa tunapata fedha na bajeti kuruhusu tutaendelea kuzitengeneza barabara hizo kwa sababu ndiyo azma ya Serikali kuhakikisha kwamba barabara hizo zinatengenezwa na zinapitika wakati wote ili kuondoa matatizo ya wananchi.

Na. 85

**Hatua za Kisheria kwa waliosababisha Hasara katika Zoezi la Uuzwaji wa Nyumba za Serikali**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:- Kwa kuwa, wakati wa Mkutano wa 14 wa Bunge Serikali ilikiri kuwa zoezi la Uuzwaji wa Nyumba za Serikali lilikuwa na dosari nyingi na kwa namna moja au nyingine limeiingiza Serikali hasara:-

Je, waliosababisha hasara hiyo wamechukuliwa hatua gani mpaka sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge ya kwamba katika Mkutano wa 14 wa Bunge, Serikali ilikiri kuwepo na dosari katika zoezi la uuzwaji wa nyumba za Serikali. Katika zoezi la kufuatilia na kurekebisha dosari zilizojitokeza katika uuzwaji wa nyumba hizo, Serikali pia iliainisha kuhitajika kwa kiasi cha shilingi bilioni 1,216,118,410 kwa ajili ya kuwarejeshea watu mbalimbali waliouziwa nyumba kimakosa na kufutiwa mikataba ya mauzo ya nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuainisha kiasi cha fedha zinazohitajika kurekebisha dosari hizo, Serikali pia imekwishachukua hatua za kiutendaji kwa baadhi ya watumishi waliosababisha dosari zilizojitokeza kwa kuwaondoa katika madaraka Mameneja wa Mikoa minne na kumbadilisha kazi Meneja mmoja Mwandamizi wa Wakala wa Majengo Makao Makuu.

Aidha, Serikali inaendelea kufuatilia sababu na vyanzo vya dosari zilizojitokeza katika zoezi la kuwauzia watumishi nyumba na kuchukua hatua kadri itakavyoonekana inafaa

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili mazito sana ya nyongeza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kwa kuwa, kwa kweli zoezi hili lilitawaliwa na tabia zote za rushwa, ulanghai na vitu vingi ambavyo havipendezi machoni mwa wananchi wa Tanzania.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni sasa hao wote waliosababisha hasara kubwa kwa Serikali ya nchi yetu pamoja na kuwapa adhabu hiyo wajulikane kwa wananchi wa Tanzania kwa makosa waliyoyafanya na kuhakikisha kwamba hawarudie tena na watumishi wengine hawatarudia kufanya makosa hayo?

Lakini la pili, kwa kuwa, zoezi hilo lilisaidia sana Serikali kupata fedha; na wafanyakazi wetu wengi wa maeneo ya vijijini na Mawilayani, manesi, walimu, wauguzi, wakunga wanaendelea kuishi katika nyumba duni na maisha duni yasiyostahili kabisa.

Je, Serikali inakubaliana na mimi sasa fedha hizo zilizopatikana badala ya kuendelea kuwanufaisha wafanyakazi hao kwa njia hizo zisizopendeza, wakajengewe nyumba sasa watumishi niliowataja wakianzia na Jimbo la Peramiho? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa maswali mazito ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ya kwamba zoezi hili lilitawaliwa na rushwa na vitendo vingine visivyopendeza.

Mheshimiwa Spika, nataka tu niseme kwamba katika zoezi hili zilijitokeza dosari kadhaa ambazo katika jibu langu la msingi nimesema kwamba tumekwishaanza kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, lakini juu ya kuwafahamu wahusika ninayo orodha ya hao watumishi niliowataja hapa, kwa hiyo, nitampatia Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu fedha ambazo zimepatikana kutokana na zoezi la uuzaji wa nyumba. Wakala wetu wa Majengo nchini kwa kweli ndiyo kazi ambayo inafanywa sasa hivi ya kujenga nyumba kwa ajili watumishi mbalimbali. Nataka tu niahidi kwamba kazi inayofanywa na Wakala Majengo nchini sasa hivi ni nzuri kwa sababu inaendelea na ujenzi wa nyumba kwa ajili ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuzitumia fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kuhakikisha kwamba tunaondoa tatizo la ukosefu wa nyumba kwa watumishi wetu nchini.

**SPIKA:** Kabla Mheshimiwa Aloyce Kimaro hujauliza swali. Waheshimiwa Wabunge, nasikitika siwezi kupokea karatasi zinazotambulisha wageni saa hizi zinakuwa nyingi na utaratibu mnaufahamu tayari orodha ya wageni ni rasmi ipo hapa.

Taarifa zikifikishwa saa moja na nusu au saa mbili wanaweza kutambulishwa, lakini mkiniletea hapa mezani karatasi nyingine hazisomeki vizuri inakuwa shida kidogo. Mheshimiwa Aloyce Kimaro swali la nyongeza.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya maswali mazito ya Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, waliouza nyumba za Serikali ni Wizara ya Miundombinu, waliokiri kwamba kulikuwa na dosari kubwa ni Wizara ya Miundombinu, wanaofanya zoezi la kurudisha ama kurejesha hizo nyumba ni Wizara ya Miundombinu. Wahenga wanasema, " kesi ya ngedere ukimpelekea kwa nyani huwezi kushinda kwa kuwa wote ni wezi wa mahindi mabichi."

Sasa swali, kwa nini Serikali isiunde Kamati huru ya kushughulikia zoezi hilo kwa haraka ili limalizike kwa utaratibu ambao utaridhisha kila mtu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nitambue kwamba Mheshimiwa Aloyce Kimaro alikwishaleta hoja binafsi hapa kuhusiana na suala hili la uuzwaji wa nyumba za Serikali. Mimi nataka tu niseme kwamba hata katika zoezi hili la kubaini hizi kasoro kwa kweli limetokana na hoja yake aliyoileta hapa Bungeni.

Kwa hiyo, kutokana na Azimio hilo na Bunge lako Tukufu lilikwishapata taarifa hapa na kutoa maelekezo ya kwamba tuendelee sasa kutekeleza Maazimio ambayo yalitokana na Bunge hili na hayo ndiyo tunayoyatekeleza. Endapo kama kungelikuwa na wazo kama hili ambalo Mheshimiwa Mbunge analitoa hapa likawekwa katika Maazimio yale Serikali isingeweza kusita kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa hivi tunayo maelekezo rasmi ya Bunge hili, Maazimio ya Bunge ambayo yanatutaka tuyatekeleze katika njia hizi tunazozichukua. (*Makofi*)

**SPIKA:** Niwakumbushe tu wenzetu upande wa Serikali kuna Maazimio mengi mnasuasua kuyatekeleza na ni Maazimio ya Bunge. Sasa kwenye Mkutano wa Bajeti, msije mkamlaumu Spika nitakuwa tu natekeleza wajibu wangu. (*Makofi*)

Na. 86

**Uwekezaji katika Kilimo**

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH (K.n.y. MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, misingi ya uchumi wa kilimo hivi sasa inaonyesha wazi umuhimu wa kilimo cha mkataba (*contract farming*) kilimo ambacho kinawashirikisha wakulima wadogo wa maeneo ya karibu (*outgrowers*) kama vile kilimo cha miwa Kilombero:-

(a)Je, kwa nini Serikali inachukua muda mrefu kutoa maamuzi mara mwekezaji anapojitokeza ili kuanzisha mradi husika, hasa katika eneo la upatikanaji wa ardhi?

(b) Kwa vile rasilimali na fedha haisubiri ucheleweshaji wa maamuzi na urasimu. Je, kwa nini Serikali imechukua takribani zaidi ya miaka miwili (2) kukubali mwekezaji awekeze katika kilimo cha mkataba katika eneo la Gendagenda katika Jimbo la Handeni?

(c) Je, kwa kuwa, hivi sasa msisitizo ni katika kilimo cha chakula na biashara, ucheleweshaji huo wa maamuzi siyo kwamba unaashiria haja ya kurekebisha Sheria ya Ardhi katika eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni, napenda kutoa maelezo kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kilimo cha Mkataba ni makubaliano ya hiari kati ya mkulima na mnunuzi wa zao husika, ambapo mkulima huhakikishiwa soko la mazao yake na huduma nyingine kulingana na makubaliano baina yao. Katika kilimo cha mkataba mkulima hupaswa kuzalisha mazao katika ubora, uwingi na wakati unaokubalika. Kilimo cha Mkataba ni budi kitekelezwe kwa mujibu wa sheria ya Mkataba (*the Law of Contract*). Kwa sasa Tanzania haina sheria ya Kilimo cha Mkataba.

Mheshimiwa Spika, ili kilimo cha Maktaba kiendeshwe kwa ufanisi ni budi masuala muhimu kama vile upatikanaji wa ardhi yawekwe bayana.

Baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hakuna ucheleweshaji wowote unaofanywa na Serikali katika kutoa maamuzi mara mwekezaji anapojitokeza. Ili kutoa ardhi ya kijiji kisheria wawekezaji kuhitaji hati ya kumiliki ardhi (*Certificate of Occupancy*) badala ya hati miliki ya kimila (*Certificate of Customary Right of Occupancy*) ambayo kisheria inapaswa kutolewa kwenye ardhi ya kijiji.

Hati miliki ya ardhi inatolewa tu kwenye ardhi ya jumla (*general land*) ambayo iko chini ya Kamishna wa Ardhi na hati miliki ya kimila inatolewa kwenye Ardhi ya kijiji ambayo iko chini ya usimamizi wa Halmashauri ya Kijiji.

Mheshimiwa Spika, sababu za kuchelewa kutoa maamuzi zinatokana na wawekezaji kutaka hati miliki ya ardhi katika ardhi ya kijiji kabla ya ardhi hiyo haijabadilishwa kwenda kwenye ardhi ya jumla , ili kuthibitisha ukweli wa mwekezaji pamoja na maslahi ya umma kwani ardhi ya kijiji inapobadilishwa kuwa ardhi ya jumla na wanakijiji wanakuwa hawana mamlaka nayo tena.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine ni kwamba ingewezekana kutoa hati miliki ya kimila haraka iwezekanavyo kwa mwekezaji ambayo ingeweza kuendana na Sheria ya Ardhi Na. 5 ya mwaka 1999 inavyotaka isipokuwa tatizo ni kwamba hati miliki ya kimila hutolewa kwenye vijiji ambavyo vina masijala ya ardhi.

Katika kijiji cha Gendagenda kazi ya kupanga matumizi ya ardhi bado inaendelea kufanyika ili kubainisha matumizi mbalimbali ya ardhi hivyo kabla ya kutolewa kwa mwekezaji.

(b)Mheshimiwa Spika, sababu kubwa ya kuchelewa kumkubali mwekezaji aliyetaka kuwekeza katika eneo la Gendagenda ni aina ya hati anayohitaji kama nilivyoeleza katika kipengele (a). Taarifa kutoka Wilaya ya Handeni zinaonyesha kwamba mwekezaji huyo anataka kuwekeza katika zao la miwa. Ili zao la miwa liweze kuzalishwa kibiashara (*Economic Justification*) miwa lazima ilimwe katika mashamba makubwa.

Kutokana na sababu hiyo mchakato wa kupata ardhi ya kutosha bila kuathiri matumizi ya ardhi na sehemu nyingine kama mifugo, kilimo cha mazao mengine na makazi sio suala la muda mfupi.

(c)Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji katika kutoa hati miliki za ardhi sio tatizo la sheria bali ni tatizo la watumiaji wa Sheria ya Ardhi. Wananchi na wawekezaji wengi wanashindwa kutofautisha maana ya kuwepo kwa Sheria ya Ardhi Na. 4 na Sheria ya Ardhi Na. 5 ya mwaka 1999.

Mheshimwa Spika, kuhusu kurekebisha Sheria ya Ardhi iliyopo, endapo itadhihirika ina mapungufu yanayosababisha ucheleweshaji wa maamuzi kwa wawekezaji ikiwa ni pamoja na eneo la Gendagenda, Serikali kupitia Bunge lako Tukufu itafanya marekebisho katika sheria hiyo ili kurahisisha masuala mbalimbali na yale yanayohusu uwekezaji katika kilimo kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge bila kuathiri haki za vijiji zinazolindwa na Sheria Na. 5 ya mwaka 1999.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Sheria za Ardhi zinasema wazi kwamba wageni wote ambao watamilikishwa ardhi inabidi kumilikishwa kwao iwe kwa mkataba. Lakini Mheshimiwa Naibu Waziri umezungumzia hapa kwamba mwekezaji inabidi apate hatimiliki *(Certificate of Occupancy)* sasa huoni hiyo kwamba ni kupingana na Sheria ya Ardhi ambayo imewekwa?

Je, utakubaliana na mimi sasa kwamba wawekezaji wengi wanaokuja kuwekeza katika kilimo ni busara Serikali ikaweka utaratibu mzuri kama unawekeza basi uwe ni ubia kati ya mzalendo pamoja na yeye mwekezaji kutoka nje ili iwe ni *joint venture project* au mradi wenyewe. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, sina hakika kwamba *Certificate of Occupancy* haiwekewi kiwango cha miaka. Mimi ninavyojua ni kwamba ni miaka 90 kwamba anavyopewa lazima inapofika miaka hiyo lazima a-*renew* kile cheti alichopewa, lakini hata hivyo tutajaribu kuangalia hili suala la ardhi zaidi tutajaribu kuangalia sheria hiyo inasemaje.

Swali lake la pili, utaratibu wa kilimo kwa maana ya *joint ventures* na wawekezaji wanaotoka nje nadhani ni ushauri mzuri tu. Lakini nadhani tunapokuwa tumeandaa sheria ya kilimo cha mkataba hii ingeweza kuelekeza zaidi kusudi hata mwekezaji wa nje na mwekezaji wa ndani wawe wanajua kuwe na *win win situation* kusiwe na kwamba wawekezaji wa nje wanawalalia zaidi wawekezaji wa ndani au kinyume chake.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa hati zinazotolewa za umilikaji ardhi vijijini yaani *customary land ownership* ambao zinafanyika taratibu zake kule vijijini zinaweza kabisa zikasababisha ardhi kubwa ya nchi hii ikachukuliwa kwa utaratibu usio wazi na hao matajiri wakubwa wanaohitaji ardhi kama mfano tulivyoona Kagera Sugar ambapo wamechukua eneo kubwa sana la wananchi kwa kukubaliana tu kule kijijini.

Mimi nilidhani pengine Serikali ilitaka kusema nini juu ya utaratibu mzima wa namna ya hawa wakulima wakubwa wanaotaka kuchukua ardhi kubwa ku-*deal* tu na watu wa kule kijijini. Je, hii hali inasemaje Serikali ikizingatia na sheria ilivyo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimwa Simbachawene kwamba kuna baadhi ya maeneo kwa mfano siku za hivi karibuni kuna baadhi ya wawekezaji wamekwenda katika mikoa ambayo tunalima chakula, maeneo ambayo tunayategemea kwa ajili ya chakula wamekwenda na kuomba ardhi kubwa vijijini kwa ajili ya kulima zao la *jetropha.*

Ni kweli kabisa vijiji na uongozi wa Wilaya na Mikoa wasipoangalia ardhi yetu itaishia kwenye mikono ya watu wenye fedha na hivyo kuhatarisha hata maeneo ambayo wanakijiji wanaweza wakakosa maeneo ya kulima lakini pia maeneo ya kuishi.

Lakini taratibu za ardhi ambazo kwa ardhi ya vijiji ambayo iko chini ya Halmashauri ya Wilaya lazima ardhi ile ipimwe hata kama mwekezaji anahitaji lazima ardhi ile ipimwe ili iingie kwenye masijala ya kijiji, hapo ndipo hatimiliki ya kimila inaweza ikatolewa. Lakini hatimiliki ile kwa wawekezaji wakubwa ile ya kimila wao hawaipendi wanataka hatimiliki inayotolewa na Kamishna wa Ardhi. Kwa hiyo, lazima Kamishna wa Ardhi aangalie kwamba kuna maslahi ya umma kwenye ardhi hiyo inayoweza kutolewa kabla ardhi hiyo haijatolewa ndipo mwekezaji atapewa hatimiliki ya ardhi kwa muda wa miaka mingi.

Kwa hiyo, hilo suala la ardhi ni muhimu sana tuliangalie hasa katika vijiji katika mikoa ili tuweze kuhakikisha kwamba hatuingii kwenye matatizo kama yale ya Zimbabwe.

Na. 87

**Matibabu Nje ya Nchi**

**MHE. SAID A. ARFI** aliuliza:-

Kwa kuwa, suala la kupata matibabu nje ya nchi ni haki ya kila Mtanzania pale inapothibitika kuwepo kwa ulazima huo:-

Je, kwa nini baadhi ya wahanga wanaopata ajali pamoja na viongozi hawapewi fursa hiyo kama inavyofanyika kwa viongozi hao?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, pamoja na mabadiliko ambayo mimi nimeyapata sasa hivi sikuwa nimeyaona katika meza yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kupata matibabu nje ya nchi ni haki ya kila Mtanzania pale ambapo kuna ulazima huo. Wahanga wowote wale wanaopata ajali na wenyewe wana haki sawa ya kuweza kupata matibabu ya nje pale inapokuwa ni azima kufanya hivyo. Hata hivyo ni lazima mtu yoyote anayetaka kupata huduma hizo za kutibiwa nje aweze kufuata utaratibu ili aweze kwenda kutibiwa nje.

Mheshimiwa Spika, sina hakika sasa kwa mabadiliko hayo kwamba yeye wahanga hayo anaozungumzia ni wapi lakini kwa vyotevyote vile mimi nilipokuwa najibu swali hili nilikuwa najibu kuhusiana na wafungwa kwa hiyo nikasema sijawahi kupata taarifa ya mfungwa ambaye alitakiwa aende kutibiwa akakosekana. Lakini kama alimaanisha wahanga basi tungepata taarifa ni wahanga gani anaowazungumza yeye ili labda tuweze kulijibu vizuri. Kwa sababu sisi tumejibu kama wafungwa kwa hiyo hatukujibu kama wahanga na wahanga ni kitu kikubwa huwezi ukatolea jibu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa sababu swali limebadilika kabisa kutoka athari kwa wafungwa limekuwa kwa wahanga wote. Ni dhahiri Serikali inahitaji sasa muda kuweza kulijibu kwa ufasaha kwa namna hiyo. Kwa hiyo, tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 88

**Kupunguza Kasi ya Kuenea Kwa Ugonjwa wa UKIMWI**

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakati Mheshimiwa Rais akihutubia Bunge tarehe 21 Agosti, 2008 alitaja sehemu tatu zinazoongoza kwa maambukizo ya UKIMWI, ambazo ni Mbeya (13%). Iringa (14%) na Chalinze (15%):-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani madhubuti ili kupunguza kasi hiyo?

(b) Kwa kuwa, kutahiri wanaume ni moja ya njia zinazotumika katika nchi nyingine kupunguza kasi ya maambukizi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha wanaume wengi nchini watahiriwe?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, kwanza napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, utafiti wa viashiria vya UKIMWI na Malaria wa Mwaka 2007 ni utafiti wa pili kufanyika nchini. Utafiti mwingine wa aina hiyo ulifanyika hapa nchini mwaka 2003-2004. Tafiti hizo mbili za Kitaifa zililenga kutoa makisio ya viwango vya maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI na Malaria.

Mheshimiwa Spika, matokeo muhimu ya utafiti wa mwaka 2007 ni kama yafuatayo:-

- Wastani wa asilimia 5.7 wanawake na wanaume wa Tanzania Bara wenye umri wa miaka 15 – 49 wameambukizwa Virusi vya UKIMWI. Viwango vya maambukizi miongoni mwa wanawake ni asilimia 6.8 na wanaume ni asilimia 4.7.

- Asilimia 10.6 ya wanawake wanaoishi mijini wameambukizwa Virusi vya UKIMWI (VVU) na asilimia 5.3 kwa wanawake wanaoishi vijijini.

- Asilimia 6.4 ya wanaume wanaoishi mijini wameambukizwa VVU na asilimia 4 kwa wanauame wanaoishi vijijini.

- Mikoa mitano ilionyesha viwango vya maambukizi ya VVU vilivyo juu zaidi ya wastani wa Kitaifa wa asilimia 5.7. Mikoa hiyo ni Iringa 14.7%, Dar es Salaam 8.9%, Mbeya 7.9%, Shinyanga 7.6% na Tabora 6.1%.

Baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Kutokana na janga la UKIMWI kuendelea kuwepo kwa viwango tofauti nchini, Serikali imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti UKIMWI (2008-2012). Mkakati huo ambao unaratibiwa na Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI unajikita katika maeneo matatu (3) makuu ambayo ni:-

- Udhibiti wa maambukizi mapya ya VVU;

- Matunzo na dawa kwa watu waishio na Virusi vya UKIMWI; na

- Kukabiliana na athari zitokanazo na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, mpango huo umeanza kutekelezwa mwaka 2008 na utatekelezwa katika sekta zote na ngazi zote za utawala.

(b)Kutokana na matokeo ya tafiti zilizofanyika Afrika Kusini, Kenya na Uganda hivi karibuni, imethibitika kuwa tohara kwa wanaume imepunguza kasi ya kuenea kwa virusi vya UKIMWI. Kutokana na ukweli huo, Serikali imeandaa mkakati maalum wa kuhamasisha tohara kwa wanaume.

Mkakati huo utahamasisha tohara kwa kutumia huduma zilizopo ikiwa ni pamoja na kutumia sehemu za huduma za afya na za kiutamaduni. Msisitizo utalenga kutahadharisha watu kuwa tohara peke yake haitoshi kudhibiti UKIMWI bali ni lazima itumike sambamba na njia nyingine kama kuacha ngono, uaminifu katika ndoa na matumizi sahihi ya mpira ya kondomu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa taarifa kwamba tohara kwa wanaume, ikitumika pamoja na njia nyingine nilizozitaja hapo juu ni njia sahihi na yenye uhakika kwa kudhibiti kuenea kwa UKIMWI unaoambukizwa kwa njia ya ngono ambayo sio salama.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa jawabu lake zuri lenye matumaini, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Katika mikakati ya kudhibiti UKIMWI Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ni vyema ikaongezwa mikakati ya kuwachukulia hatua kali wale watu wanaoeneza UKIMWI kwa makusudi ili kuzuia athari hiyo?

Mheshimiwa Spika, lakini pili ni kwamba amekubali kwamba tohara ni moja katika mambo ambayo yanazuia maambukizo hayo ya UKIMWI na kiongozi ni kuonyesha njia. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais Jakaya Mrisho Kikwete alikuwa ni wa mwanzo kwenda kupima UKIMWI. Sasa katika suala hili la tohara Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba hivi sasa umeshafika wakati kwamba na sisi Wabunge ambao bado hatujawa na tohara kuonyesha njia ya mwanzo ya kuchukua hatua hii ili kupunguza maambukizo hayo ya UKIMWI na tuanze katika kikao cha Bajeti kijacho? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, wewe utajuaje kwamba ….......…(*Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza amezungumzia kuhusu suala la kuwachukulia hatua kali wale ambao wanaeneza virusi vya UKIMWI kwa makusudi.

Mheshimiwa Spika, kama tutakumbuka Bunge letu Tukufu lilipitisha hapa sheria inayohusiana na UKIMWI. Kwa hiyo, sheria hii itatumika kama tulivyoipitisha sisi Wabunge ili iweze kuwabana wale ambao wanaeneza virusi kwa makusudi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuonyesha njia katika suala zima la kufanya tohara. Napenda tu kama nilivyosema katika jibu langu la msingi sisi kama Wizara tumetoa maelekezo kwamba tohara kwa wanaume inasaidia sana kupunguza maambukizo ya virusi. Kwa hiyo napenda tena kurudia kwamba natoa wito kwamba tohara kwa wanaume inasaidia sana kupunguza maambukizi ya UKIMWI. Kwa hivi wale wote ambao wanaona kwamba hii inawagusa basi watumie busara zao ili kuweza kuhakikisha kwamba wanajitahidi ili waweze kupunguza maambukizi haya mapya. Ahsante sana.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza suala dogo la nyongeza.

Kwa kuwa njia mojawapo ya kupunguza maambukizi ya VVU na UKIMWI ni pamoja na kutumia mipira ya kike na ya kiume. Pia *data* zinaonyesha kwamba wanawake wanapata maambukizi zaidi kuliko wanaume, lakini mipira ya kike imekuwa haipati kipaumbele ni pamoja na kuwa na bei ya juu kuliko ile ya kiume. Vile vile

hamasa haipo kubwa sana katika kuhamasisha wanawake watumie mipira hiyo. Je, Wizara inasema nini kuhusu hili, ili kuhakikisha kwamba wanawake wanafanya ngono salama?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli maambukizi kwa wanawake ni makubwa zaidi kuliko kwa wanaume na kwamba matumizi ya mipira ya kike imekuwa ni midogo sana kwa kulinganisha na wanaume wanavyotumia mipira kama kinga dhidi ya UKIMWI.

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia vitengo mbalimbali pamoja na taasisi nyingine huwa ikitoa mafunzo lakini vile vile tulikuwa tunaangalia ni jinsi gani mahali ambapo tuna *dispense condom* katika maeneo ya wazi kwa kondomu za wanaume na zenyewe huwa tunaweka na kondomu za wanawake.

Labda nitakachotaka kusema tu ni kwamba nataka niwaombe tu akinamama waamini kwamba mpira wa mwanamke unasaidia sana kuzuia maambukizi na iwapo mtu ataonyeshwa jinsi ya kuitumia vizuri atapata urahisi kabisa ya kuitumia na hivyo atajikinga. Kwa hivi sisi kama Wizara tutahakikisha kwamba kondomu zitapatikana na suala la bei tutalizingatia vile vile.

Na. 89

**Matumizi ya Maji ya Ziwa Victoria**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna makubaliano ya pamoja na nchi wanachama wa *NILE BASIN INITIATIVE (NBI)* juu ya matumizi ya maji ya Ziwa Victoria:-

(a) Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu hatua ya nchi ya Uganda kuamua kuingia kwenye mkataba wa siri na nchi ya Misri juu ya matumizi ya maji ya Ziwa Victoria bila kuzihusisha nchi nyingine wanachama?

(b)Je, mkataba huo una athari gani kwa Tanzania endapo Uganda itafungulia maji mengi kwenye Mto Nile kwenda Misri ili kuinufaisha nchi ya Uganda pekee katika kuzalisha Nishati ya Umeme?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haina taarifa yoyote rasmi kuhusu mkataba wa siri au vinginevyo, kuhusu hatua ya nchi ya

Uganda kuamua kuingia kwenye mkataba wa siri na nchi ya Misri juu ya matumizi ya maji Ziwa Victoria.

Vile vile, Serikali ya Tanzania inatambua kwamba, Uganda kama nchi, ina uhuru na haki ya kuingia katika majadiliano na makubaliano na nchi yoyote kwa masuala ambayo itaona yana manufaa kwa nchi yao *(Bilateral Relations).*

Hata hivyo ni mategemeo yetu kuwa kama matokeo ya makubaliano hayo yataihusu Tanzania kwa namna yoyote ile itabidi yawasilishwe rasmi kwa Serikali ya Tanzania kwa kupitia vyombo vyetu vya ushirikiano vilivyopo kama vile *NILE BASIN INITIATIVE* au Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(b)Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika sehemu (a) ya swali la Mheshimiwa Mbunge, Serikali yetu haina taarifa rasmi kuhusu Mkataba unaozugumziwa. Hata hivyo, napenda nielezee kuwa athari zinazoweza kutokea kwa kuruhusu maji mengi zaidi kutoka katika mitambo hiyo ya kuzalisha umeme pale Jinja, zaidi ya kiwango kilichokubaliwa (*Agreed Curve*) ni pamoja na kushuka kwa kina cha maji katika Ziwa Victoria kama ilivyotokea miaka ya 2000 hadi 2007, miundombinu ya maji safi Mijini, hususan vidakio (*water intakes*) kushindwa kufanya kazi vizuri, meli kushindwa kutia nanga bandarini na kupakia mizigo na watu chini ya uwezo wake na hivyo kukosa mapato. Vile vile, mazalia ya samaki kuharibika na kusababisha kupungua kwa samaki na mapato yake kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Watanzania wote kwamba Serikali itaendelea kuheshimu na kutekeleza mikataba ya makubaliano ambayo Tanzania imeridhia kuhusu usimamizi, udhibiti na matumizi ya maji shirikishi ili mradi tu makubaliano hayo hayaathiri Tanzania wala nchi nyingine yoyote hususan katika nchi kumi za Bonde la Mto Nile ambazo ni Tanzania, Sudan, Misri, Uganda, Kenya, Burundi, Rwanda, Kongo *DRC, Eritrea* na Ethiopia.

**MHE. JOHN P. LWANJI**: Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri anakiri kabisa kwamba kati ya mwaka 2000 na 2007 kulitokea tatizo la kina cha maji katika Ziwa Victoria na sababu kubwa mojawapo inayozungumzwa inaweza kuwa hiyo ya Uganda kuruhusu maji mengi kupita pale Jinja. Je, anaweza ni kunitaarifu ni mamlaka ipi iliyoiruhusu Uganda kufungulia maji mengi yaweze kupita pale Jinja na kuendelea nchi za Misri pamoja na Sudan?

Pili, ningependa kujua Serikali ina mpango gani baada ya kuona kwamba mradi huu wa kusambaza maji kutoka Ziwa Victoria kuja Shinyanga mpaka Kahama uliridhiwa na nchi wanachama wa *NILE BASIN INITIATIVE* na unakwenda vizuri.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza sasa kutoa maji hayo kuja mikoa kame kabisa ya Singida na Dodoma?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu Uganda ni mamlaka ipi iliruhusu Uganda kutoa maji yale wakati ule. Sina kumbukumbu yoyote kwamba kuna mamlaka iliyokuwa imeruhusu Uganda kuchukua maji yale, lakini ninavyojua ni kwamba uko utaratibu ambao tumejiwekea kwa wananchi au nchi wanachama katika nchi zile 10 ambazo zinashirikiana maji ya Mto wa Nile kinachojitokeza hapa ni kwamba lazima tukubaliane kabla maji yale nchi moja haijayatumia.

Tumekaa vikao vingi tumekubaliana lakini bado kuna vipengele vichache ambavyo kwa bahati mbaya hatujaweza kukubaliana kati ya nchi hasa Misri na Sudan kuweza kukubaliana katika kipengele kimoja kikubwa zaidi kinachoruhusu nchi hizo kutumia maji ya ziada.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo naomba niseme kwamba bado majadiliano yanaendelea na tutakapofikia muafaka basi sisi pia tutaridhia. Lakini mpaka sasa hivi bado kuna kipengele kimoja kuhusu kushirikiana kwenye maji hayo. Kwa hiyo naomba niseme kwamba katika hilo suala ni mamlaka ipi mimi sina hakika kama kuna mamlaka iliyotoa. Lakini naomba nitamtafutia jibu sahihi nisije nikasema kuna mamlaka ilitoa au ikakataa.

Kuhusu Ziwa Victoria, maji yake kuja katika mikoa mingine, kwanza nataka niseme kwamba sisi tunatumia maji kiasi cha lita 80,000 za ujazo kutoka katika Ziwa Victoria, hatua ambayo tumeifikia hadi sasa ni kwamba tayari maji yale tunayatumia kuja katika mikoa ile ya Shinyanga na Mwanza, lakini bado tunaendelea kusambaza maji haya, hatujakamilisha hata ile awamu ya kwanza. Kwa hivyo naomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira kidogo kwamba tukamilishe hata kusambaza katika vile vijiji tulivyoanisha katika *phase* ya kwanza ya mradi huu halafu ndipo tuangalie sasa kama maji haya yanaweza yakatumika katika maeneo mengine.*(Makofi)*

Lakini kama yatatumika katika maeneo mengine niseme kwamba hili tena halitahitaji kuridhiwa maana yake tayari tutakuwa tunatumia maji yale ambayo tunayotumia hivi sasa, lakini endapo tutatakiwa kutumia tena zaidi basi tutafuata utaratibu huo huo kwamba turidhie au wenzetu nao waridhie haya makubaliano ambayo tumeingia tangu zamani.

Na. 90

**Mradi wa Maji Katika Mji wa Kibiti**

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mji wa Kibiti ulikuwa miongoni mwa Miji minane (8) iliyokuwa ipatiwe maji chini ya mradi unaofadhiliwa na Serikali ya Ufaransa; na kwa kuwa, Serikali

ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliamua kuchukua mradi huo mara Serikali ya Ufaransa iliposhindwa kuuendeleza:-

(a) Je, tangu Serikali ichukue jukumu hilo imetoa kiasi gani cha fedha kwa ajili ya mradi huo?

(b) Je, ni lini mradi huo utakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mbunge wa Kibiti, napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Ni kweli Mji wa Kibiti ulikuwa miongoni mwa Miji 9 iliyokuwa ipatiwe ufadhili na Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika lake la Maendeleo *AFD.*

Miji mingine ni Utete, Mpwapwa, Ikwiriri, Kilosa, Gairo, Mvomero, Turiani na Kibaigwa. Fedha iliyotengwa na Serikali ya Ufaransa haikutosha kutekeleza miradi katika Miji yote 9. Hivyo, iliamriwa kuwa, kazi ya kufanya usanifu wa kina na kuandaa makabrasha ya zabuni ifanyike kwa Miji yote 9 na ujenzi wa mifumo ya maji ufanyike kwa Miji 2 ya Utete na Mpwapwa.

Kazi ya usanifu wa kina na kuandaa makabrasha ya zabuni ilikamilika Januari, 2008 na ujenzi wa mifumo ya maji umeshaanza katika Miji ya Utete na Mpwapwa kwa ufadhili wa Serikali ya Ufaransa.

Baada ya Serikali ya Ufaransa kupunguza ukubwa wa miradi kutoka Miji 9 hadi 2 katika hatua ya ujenzi, na kwa kuwa tayari hatua ya usanifu imekwishakamilika kwa Miji yote 9, Serikali yetu imeamua kutekeleza ujenzi wa miradi ya maji katika Miji 7 iliyobaki kwa kutumia fedha za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

Fedha za ujenzi wa mifumo ya maji kwa Miji hiyo 7 iliyokosa ufadhili kutoka Serikali ya Ufaransa zimeishatengwa na zabuni za kumpata mkandarasi kwa Miji yote zimetangazwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kuuchukua mradi huu wa Kibiti, zabuni ya kutafuta Mkandarasi wa ujenzi wa mradi imetangazwa na kufanyiwa uchambuzi. Mkandarasi anatarajiwa kupatikana mwezi Mei, 2009.

Fedha zilizotumika hadi sasa ni *Euro* 190,667 sawa na shilingi Milioni 336 kwa ajili ya kuwalipa Mhandisi Mshauri aliyefanya usanifu wa mradi na kuandaa makabrasha ya zabuni, Mkandarasi wa uchimbaji wa visima vya utafiti na Mtaalam Mshauri aliyefanya mapitio na kutoa mapendekezo ya kisheria kuhusu chombo kitakachosimamia shughuli za uendeshaji na matengenezo baada ya mradi huo kukamilika.

(b) Mheshimiwa Spika, Mradi huu unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 18 baada ya kuanza ujenzi wake mwezi Mei, 2009.

Aidha, kwa kutumia mapendekezo ya Mtaalam Mshauri wa masuala ya kisheria, uongozi wa Wilaya kwa kushirikiana na Wizara yangu, utaunda chombo cha kusimamia shughuli za uendeshaji wa mradi huo kisheria.

**MHE. ABDUL JABIR MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na Majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninataka kujua, kwa sababu Mji wa Kibiti unatarajia kupata umeme hivi karibuni. Je, Serikali itakuwa tayari yule mkandarasi ambaye atakayeshinda zabuni hii. Kuweza kutumia pampu zitakazotumia umeme badala ya zile za mafuta ya *diesel* au *petrol* kwa kuwa ni ghali sana?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza niseme nafurahia ushauri na mawazo ya Mheshimiwa Mbunge lakini niongeze pia kwamba hayo ni masuala ya kuitendaji na kiutaalam kwa sababu kama yalikwisha ainishwa hapo awali na kama inatakiwa yabadilishwe kwa faida ya mradi huo na kwa faida ya wananchi na kama itakuwa inaonyesha kwamba tutafaidi kiasi fulani kwa kutumia umeme; hayo basi mimi nina hakika kabisa yanaweza kujadiliwa yakaenda kwenye meza tena yakaangaliwa upya. Kwa hiyo, hilo naomba tuachie tutaliangalia na ninamshukuru kwa ushauri huo.

**MHE. PROF. IDRIS ALI MTULIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Ujenzi wa mradi wa Maji kwa Mji wa Utete umeleta faraja kubwa sana na naipongeza Wizara.

Lakini kwa vile Ikwiriri nayo ina matatizo makubwa na imetajwa katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nauliza. Je, ujenzi wake utaanza sambamba na ujenzi wa Kibiti mwezi Mei mwaka huu, 2009?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza tukubaliane kwamba kama nilivyosema katika jibu la msingi. Miji ile saba pamoja na Ikwiriri tayari Serikali imeshaanza kazi na uamuzi na fedha zake zipo tayari zimekwishatengwa. Basi naomba tuendelee kuwasiliana nae ili angalau tuwe na hakika kwamba ni mwezi gani tunaweza tukaanza kazi hiyo ili nisije nikasema mwezi Mei halafu baadae ikawa mwezi Juni. Maana katika utaratibu wa ujenzi mambo mengine yanajitokeza. La msingi hapa ni kwamba tayari fedha zimetengwa na mradi huo sasa tumekamia kuutekeleza katika mwaka huu, 2009.

Kwa hiyo asiwe na wasiwasi. Naomba kama anataka maelezo zaidi basi tuwasiliane kwenye ofisi yangu.

Na. 91

**Kuendesha Sekta ya Uvuvi Nchini**

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI** aliuliza:-

Kwa kuwa Ilani ya Uchaguzi wa CCM mwaka 2005 imebainisha kuwa Sekta ya Uvuvi itapewa kipaumbele kwa kuwasaidia wavuvi kutumia maarifa ya kisasa; zana za kisasa pamoja na kuvutia wawekezaji katika viwanda vya kusindika samaki:-

(a)Je, mpaka sasa ni mazingira gani mazuri yametengenezwa ili kuwasaidia wavuvi kupata zana za kisasa bila vikwazo?

(b)Je, Serikali imevutia wawekezaji wangapi katika kuanzisha viwanda vya kusindika samaki katika ukanda wa mwambao wa bahari?

(c)Je, ni viwanda vingapi vya zana za uvuvi vimejengwa kutokana na ushawishiwa Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahman Msomi, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a), (b) na c, kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kuwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) inabainisha kuwa Sekta ya uvuvi itapewa kipaumbele.

Hadi sasa mazingira mazuri yaliyotengenezwa katika kuwasaidia wavuvi ni pamoja na kuwepo na Sera ya Uvuvi ya mwaka 1997, Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2005. Sheria Namba 29 ya mwaka 1994 inayohusu Hifadhi za bahari na Maeneo Tengefu, Sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi wa Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu Namba 17 ya mwaka 2007 na Sheria mbalimbali zinazohusu uvuvi.

Aidha Serikali kwa kushirikiana na nchi za Kenya, Uganda, imeweka utaratibu wa kupunguza ama kuondoa kodi kwenye malighafi, mbepejeo na zana za uvuvi ili kuwawezesha wavuvi kumudu kununua zana za uvuvi kwa bei nafuu. Kulingana na *East African Publication (2007) on Common External Tariff*, injini za uvuvi, malighafi zinazotumika kutengeneza zana za uvuvi na zana mbalimbali na viambata vyake vinavyonunuliwa kutoka nje ya nchi hupewa punguzo la kodi ama kufutiwa kodi kabisa.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada zingine za kuboresha pato la mvuvi, Desemba,2005 Serikali kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia ilianza kutekeleza Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani *(Marine and Coastal Environment Management Project – MACEMP*) Mradi unaowezesha wananchi kuibua miradi ya ujasiliamali. Hadi sasa jumla ya miradi 124 yenye thamani ya shilingi bilioni 1.3 imeibuliwa.

Vilevile kupitia maeneo tengefu ya bahari, Serikali katika kuwajengea jamii ya wavuvi uwezo Wizara yangu imetekeleza mpango wa kubadilishana zana haribifu, kwa zana bora za uvuvi endelevu katika maeneo tengefu. Hadi sasa wanajamii 275 kutoka Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia na 217 kutoka Hifadhi ya Bahari ya Ghuba ya Mnazi na mwingilio wa Mto Ruvuma wamenufaika na utaratibu huo.

(b)Mheshimiwa Spika, katika Ukanda wa mwambao wa Bahari ya Hindi wawekezaji wamehamasishwa kujenga viwanda vya uchakataji wa mazao ya uvuvi na kuuza katika soko la ndani na nje. Viwanda vitatu vinavyouza mazao ya uvuvi soko la ndani na nje kwenye Jumuiya ya Ulaya ni *Bahari Food Ltd* cha Dar es Salaam, Tanpesca kilichopo *Mafia na Sea Product* kilichopo Tanga.

Vilevile kuna Viwanda vingine vitatu ambavyo vinauza mazao ya uvuvi soko la ndani na nje ya *EU.* Viwanda hivyo ni *Asmara Trading Company, Shamez Enterprises na Fruit de ler Mer* ambavyo vyote vipo Dar es Salaam. Vilevile kuna viwanda viwili vipo katika hatua za mwisho za ujenzi navyo ni *Alpha Krust Ltd*, *Royal Africa Lobster Tropical* vyote vya Dar es Salaam.

Aidha, kuna maghala manne (4) ya kuhifadhia mazao makavu ya uvuvi (makombe, simbi na mwani) katika ukanda huo. Maghala hayo ni *Novea Associates, Aqeel Traders na Fagon International Ltd.* ya Dar es Salaam na Mwani Mariculture kiko katika Mkoa wa Lindi.

(c)Mheshimiwa Spika, Serikali imebainisha fursa ya wawekezaji kwenye utengenezaji wa nyavu na uvuvi na kuwashawishi wananchi kutengeneza katika eneo hili. Hadi sasa kuna viwanda viwili vya kutengeneza vifaa vya uvuvi viwanda hivyo ni *Fanaka Fishnet Tanzania Ltd* kilichopo Nyamagana na *Imara Fishnet (T) Ltd.* ambacho kipo eneo la Keko Mwanga, Dar es Salaam. Viwanda hivi vinamilikiwa na Kampuni Binafsi na vina uwezo wa kusambaza nyavu nchi nzima.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI**: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa kuna mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Ukanda wa Pwani –MACEMP, lakini kwa bahati mbaya mradi huu wavuvi wengi hawajaufahamu.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu ili wananchi au wavuvi wanokusudiwa waweze kutumia vyema mradi huu wa MACEMP ukiacha wenzetu wa Mafia ambao kwa kweli wameufahamu vizuri?

Pili, kwa kuwa Serikali ilitoa msukumo katika Sekta hii ya Uvuvi, kwa maana hata kuanzisha Wizara maalum kwa ajili ya shughuli za uvuvi. Je, kwa madhumuni hayo hayo sambamba na hilo Mheshimiwa Waziri haioni kama ni muhimu sasa pia kufuta kodi kwa zana za uvuvi ziingiziazo nchini ili lengo linalokusudiwa na Serikali kuwezesha wavuvi lifanikiwe kwa uzuri zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mradi huu ulianza Desemba 2005 ambapo ulianzia katika Wilaya ya Kilwa, Rufiji na Mafia. Wahamasishaji wa Uvuvi ulianzia hapo.

Lakini katika mwaka huu umeenea katika Wilaya na Manispaa 13 na uhamasishaji unaendelea. Ili wavuvi waweze kuutekeleza kwa vizuri ni lazima elimu itolewe na hii elimu ndiyo inaendelea na itaendelea kutolewa. Kuhusu kufuta kodi kama nilivyosema tulipokubaliana na nchi za Kenya na Uganda, sehemu kubwa ya zana za uvuvi zinazoingia tumezitolea kodi.

Mfano kuna nyavu ziliwahi kukwama pale bandarini lakini tulifanya mpango zikaondolewa.

Nakubaliana kwamba ili wavuvi waweze kujikomboa zana za uvuvi zinatakiwa zitolewe kodi na hilo Serikali litaendelea kulihimiza na kulitekeleza.

Na. 92

**Kutunga Sheria Juu ya Matumizi ya Bajaji Nchini**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali inahamasisha utumiaji wa vyombo vya moto vinavyotumia mafuta kidogo kama vile pikipiki aina ya Bajaji na kwa kuwa hivi karibuni kumekuwa na ajali nyingi za Bajaji;

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutunga Sheria maalum ya kuwalinda watumiaji wa vyombo hivyo kama ilivyo katika tahadhari juu ya Bata na Kondoo?

(b) Kwa kuwa, moja ya sababu ya kuongezeka kwa ajali hizo ni madereva wa bajaji kupokezana na kuendeshwa na watu wasio na leseni.

Je, Serikali haioni ni vema madereva wa bajaji wasio walemavu wabandike picha zao ndani ya vyombo hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDAN IYA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tayari wadau wa usalama wa barabarani yaani Polisi, *SUMATRA, TBS, NIT, VETA* na Wizara ya Miundombinu wamekwishatunga Kanuni ambazo zitaanza kutumika baada ya taratibu za kisheria kukamilika.

Kanuni hizo ni pamoja na mambo mengine zitaainisha matumizi sahihi ya vyombo hivyo, mipaka ya kutoa huduma hiyo, sifa na masharti ya leseni za udereva mipaka ya huduma zake na adhabu zitakazotolewa kwa ukiukwaji wa matumizi ya vyombo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kuthamini usalama wa maisha yao wananchi na mali zao. Hivyo, Kanuni hizo zimelenga kuwalinda watumiaji wa vyombo hivyo wakiwemo madereva, abiria na watumiaji wengine wa barabara. Kuanza kutumika kwa Kanuni hizo kutakidhi yale yote yaliyobainishwa na Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa nitoe pongezi kwa Wizara pamoja na Taasisi ya Polisi kwa ujumla *IGP* Mwema na Mzee Kova kwa jinsi ambavyo wanashughulikia masuala ya usalama barabarani.

Pamoja na hayo naomba niongeze maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekuwa ikijitahidi mara kwa mara kutunga Sheria na Kanuni nzuri lakini katika ufuatiliaji wa utekelezaji imekuwa na mapungufu kidogo; na kwa kuwa imekuwa ni suala la kawaida madereva wa vyombo mbali na Bajaj kukiuka taratibu za barabarani ikiwemo ku-*park* magari njia panda pamoja na kuendesha vibaya barabarani.

Je, Wizara haioni ni vema ikashirikisha Jeshi la Wananchi katika Idara ya JKT kupata vijana ambao watakuwa kama Askari Kanzu ambao watakaa katika maeneo hayo na kuweza kuripoti matukio kama hayo na faini zao kuwa ni sehemu ya kuwalipa mishahara?

Swali la pili, kwa kuwa kesi za madereva zinapokwenda Mahakamani kama nilivyoshuhudia hivi karibuni, nimeona kwamba zinacheleweshwa wakati mwingine kutokana na kudaiwa kutoa barua za dhama ambazo hazitoki kwa Wenyeviti wa Serikali ya Mtaa. Ni kweli Serikali ndivyo ilivyo katika Sheria zetu kwamba barua kutoka kwa Serikali za Mitaa hazistahili kuwa kama ni sehemu ya barua za dhamana?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwa wakati mwingine uzoefu katika ufuatiliaji wa mambo fulani lakini hiyo kama nilivyosema ni kwamba tunajaribu kadri tuwezavyo kutizama sera nzima na tunajaribu kubadilisha sera nzima ya mambo ya usafirishaji. Sheria imefanyiwa marekebisho mwaka huu mwezi Januari, 2009.

Lakini nimwambie kwamba ingawa Sheria imefanyiwa marekebisho lakini bado mwaka jana hizi Bajaj zilikuwa zinafanya kazi kabla hata Sheria haijakuwepo. Ingawaje hili suala kweli linatupiwa kwetu upande wa Serikali lakini pia lilichukua mtizamo wa

kisiasa. Kwa sababu wapo wabunge kabisa ambao walilisimamia kidete kwamba ingaweje Sheria haikuwepo lakini watu ilikuwa ni lazima wapate ajira kwa vijana na kadhalika. Kwa hiyo tuna matatizo na naomba tushirikiane katika hili. Lakini kusema kwamba tuweke vijana kutoka Jeshi la Wananchi au JKT nafikiri kwamba huko hatujafika, tunajiweza na tunajitosheleza na ni kiasi cha kujipanga na nadhani matatizo tunayakabili na yako ndani ya uwezo wetu.

Kuhusu kesi, kusema kweli zipo sehemu mbili hapa. Kuna upande wetu sisi Polisi ambao tunapeleka mashtaka. Lakini pia iko sehemu ya Mahakama. Sisi tunapeleka kesi zetu Mahakamani, lakini nini Mahakama inaamua hilo ni jambo jingine. Sasa kama Mahakama itasema kwamba haitambui barua au uwakilishi unaotoka katika Serikali za Mitaa nadhani hilo ni suala linaloweza likatizamwa na upande wa pili wa Mahakama. Lakini kama kweli hilo lipo mimi nadhani upo wajibu mkuwa wa kulitizama. Ahsante.

Na. 93

**Kukarabati Shule ya Sekondari ya Mwenge**

**MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MHE. MOHAMED GULAM DEWJI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, mpango wa MMES umepata mafanikio makubwa katika kipindi chake na bado unaendelea, na kwa kuwa shule ya sekondari ya Mwenge ambayo ni kongwe haijafaidika kupata mpango huo;

Je, Serikali ipo tayari kuifanyia ukarabati shule hiyo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa uzio ili kulinda na kuzuia uharibifu wa mali za shule?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Gulam Dewji, Mbunge wa Singida Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua hali mbaya ya miundombinu ya shule ya Sekondari ya Mwenge, ikiwa ni pamoja na mahitaji ya vyoo, mabweni, mfumo wa maji safi na taka pamoja na samani. Kwa kuwa, Shule ya Sekondari Mwenge ni miongoni mwa shule zitakazofanyiwa ukarabati pindi fedha zikipatikana Serikali inaahidi kutoa kupaumbele kwa shule hiyo katika Bajeti ya 2009/2010.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Pamoja na majibu haya mazuri nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Shule ya Mwenge Sekondari inakabiliwa pia na upungufu mkubwa wa walimu pamoja na vifaa vya maabara, pamoja na kemikali zake.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kupeleka walimu pamoja vifaa vya maabara na kemikali zake ili ukarabati mkubwa utakaofanywa uende sambamba na utoaji wa taaluma katika shule hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza yeye pamoja na Mheshimiwa Dewji kwa namna ya kipekee wanavyoshiriki katika kuhamasisha masuala ya elimu katika Mkoa wao.

Pili tunakubali ni kweli pamoja na changamoto ya ukarabati lakini pia kunahitajika hivyo. Kwa kadri tutakavyopata walimu na fedha kwa ajili ya kuboresha maabara tutapeleka kwa ufanisi wa kizazi chetu.

Na. 94

**Malipo ya Wazabuni wa Shule za Sekondari**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa ulipaji wa fedha kwa wazabuni wa shule za Sekondari hasa za Bweni huchelewa sana hali ambayo husababisha upungufu wa chakula, migomo ya wanafunzi na shule kufungwa:-

(a)Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapa wazabuni hao kipaumbele cha malipo yao ili kuzuia migomo mashuleni?

(b)Kwa kuwa, idadi na ikama ya wanafunzi hujulikana kabla, kwa nini utoaji wa fedha hizo usiwe wa kikamilifu na Wizara husika kupelekewa kasma hiyo mapema ili maandalizi ya malipo yafanywe kwa wakati?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inaona umuhimu wa kuwapa wazabuni kipaumbele ili kuzuia migomo shuleni ambapo kuanzia Januari 2009 Serikali inawalipa wazabuni moja kwa moja kupitia shule. Aidha kuhusu madeni machache yaliyosalia ya kipindi kilichoishia mwezi Machi 2008 fedha kiasi cha shilingi milioni 360 zimeshapatikana na hivi sasa hundi zinakamilishwa. Uhakiki wa madeni ya wazabuni kunzia Aprili hadi Desemba, 2008 umekamilika na tarehe 30 mwezi wa nne kwa maana ya kesho taarifa itawasilishwa Wizarani tayari kwa kuombea fedha Hazina.

(b) Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2008/2009 Wizara yangu iliomba Serikali Kuu ipatiwe shilingi Bilioni 29 kwa ajili ya chakula cha wanafunzi 73,500 kwa siku za masomo 270. Hata hivyo fedha iliyotengwa ni kiasi cha shilingi bilioni 7.3.

Mheshimiwa Spika, fedha za chakula cha wanafunzi hutolewa kila mwezi na Hazina kupitia Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Wazira hiyo. Hivyo haziwezi kutolewa kwa mkupuo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatafuta njia bora zaidi ya kulisha wanafunzi.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu yenye kuridhisha ya Naibu Waziri kwa kuwa tatizo la madai ya wazabuni ni ya muda mrefu; na kwa kuwa wazabuni hawa asilimia kubwa hutegemea kukopa kuchukua mikopo kwenye Mabenki na kuchukua mikopo yenye riba. Kwa kuwa Serikali iko kwenye mchakato wa kuandaa utaratibu mzuri ambao utawezesha malipo hayo. Je, Serikali haioni ingekuwa busara sasa kukabidhi madaraka Ofisi ya RAS ili waweze kuhakiki madai hayo na kufika kwa wakati Wizarani kuliko ilivyokuwa sasa wanahakiki madai Wizarani na kisha yanarudi Mikoani?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba niseme kwamba ni kweli tunatambua wazabuni walio wengi hukopa kwenye mabenki na kadri Serikali inavyochelewa kuwalipa ndivyo wanavyopata taabu.

Hatuna njia ya mkato, madeni ya Serikali lazima yahakikiwe, anayehakiki ni Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali na yeye ameshatupatia hiyo taarifa kama nilivyosema, kesho atamkabidhi Waziri mwenye dhamana.

Baada ya hapo tutawalipa kadri tutakavyopata fedha. Kugatua madaraka kwa *RAS* ndilo zoezi linafuatia kuanzia Julai Mosi shule zote za Sekondari zitakuwa chini ya TAMISEMI. Kwa hiyo, uhakiki na kila jambo linalohusu Sekondari litafanywa huko na kwamba huenda likarahisisha. Hata hivyo nimpongeze tu na kuona kama na yeye ni mmoja kati ya wazabuni basi tutasaidiana.

Na. 95

**Matumizi ya Nishati Mbadala**

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI** aliuza:-

Kwa kuwa hivi sasa zimegundulika aina mbalimbali za nishati. Kwa mfano nishati ya mifugo, nishati itokanayo na mabaki ya mkonge, nishati itokanayo na kinyesi cha binadamu na kadhalika.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani kuhusu matumizi ya nishati hizo mbadala?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani za kuwaelimisha wananchi juu ya matumizi ya kinyesi cha binadamu ili kuondoa mawazo finyu kuhusu kinyesi hicho?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, taasisi mbalimbali hapa chini zimekuwa zikijihusisha na uendelezaji wa teknolojia ya bayogesi.

Taasisi hizo ni pamoja na Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini *(CAMARTEC)* ya Arusha, Miradi ya Gesi ya Samadi Dodoma *(MIGESADO)*, Kanisa la Kiinjili la Kilitheri Tanzania (KKKT), Shirika la Viwanda vidogo *(SIDO)* na Asasi nyingine zisizokuwa za Kiserikali ambayo ni pamoja na *SURUDE* ya Turiani, Mkoani Morogoro na Bodi ya Katani inayozalisha umeme kutokana na bayogesi ya mabaki ya mkonge.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mpango wa kazi, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini imekuwa ikiendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali kama *CAMARTEC* ambayo hivi sasa wanasimamia mradi wa *Biogas for Better Life* ambao unakusudia kuendeleza teknolojia ya bayogesi chini ya ufadhili wa Serikali ya Uholanzi.

Mradi utaendeleza mitambo midogo ya biogas kwa ajili matumizi ambayo yanatarajiwa kuwa ya gharama nafuu kwa ajili ya matumizi ambayo yanatarajiwa kuwa ya gharama nafuu zaidi kuliko mitambo iliyokuwa inajengwa hapo awali katika maeneo mbalimbali nchini ikiwepo Dar es Salaam, Arusha na Kilimanjaro.

Mitambo hiyo ilikuwa ni mikubwa kuliko mahitaji ya gesi kwa watumiaji. Moja ya mikakati ya *CAMARTEC* ni kubadili ukubwa wa mitambo hiyo kulingana na mahitaji ya gesi na pia kutoa ruzuku kusaidia wakulima wadogo kumudu mitambo hiyo. Ukubwa wa mitambo uliokubalika kitaalam utakuwa meta za ujazo 4, 6, 9 na 13. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Asasi zisizo za Kiserikali inaendelea kuhamasisha matumizi ya bayogesi inayotokana na vyanzo mbalimbali kama vile kinyesi cha binadamu, wanyama na pia mabaki ya mkonge.

Tayari mitambo ya bayogesi inayotumia kinyesi cha binadamu imeshajengwa Dodoma chini ya Miradi ya Gesi ya Samadi. Uzoefu huu pia upo Arusha.

(b)Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa wananchi wengi wamekuwa na uelewa mdogo kuhusu kuzalisha bayogesi kwa kutumia kinyesi cha binadamu.

Ni vizuri ikaeleweka kwamba teknolojia hii imeandaliwa kwa namna ambayo kinyesi huingia moha kwa moja katika mtambo wa kuzalisha bayogesi bila ya kuonekana au kushikwa na binadamu.

Baada ya bayogesi kuzalishwa, mabaki ya kinyesi yanakuwa hayana harufu na hivyo hayawezi kuleta magonjwa *(Pathogen Free)* na hatimaye hutumika kama mbolea. Hata hivyo Serikali inaendelea kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi kwa kuwapa maelekezo mazuri kwa lengo la kuondokana na dhana ya kuwa kinyesi cha binadamu hakifai kwa kuzalisha bayogesi.

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini naomba Wizara izidi kutoa elimu zaidi hasa kuhusu hiki kinyesi cha binadamu. Kwa vile naona hakina hasara sana wala gharama kubwa sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi tunakusudia kutoa elimu hasa kwenye matumizi ya kinyesi cha binadamu kwa mitambo midogo midogo ambayo inaweza ikatumika kwenye umeme kuwashia taa, majiko ya kupikia na pia kwenye mashule na maeneo ya mkusanyiko wa watu wengi ambapo rasilimali hiyo inaweza ikapatikana kwa wingi.

Kwa hiyo, tuna mpango wa kuliweka kwenye Sera ya Nishati kwa Mpango wa Nishati mbadala.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali ni kama umefikia kikomo, lakini tunafidia kidogo namna tulivyopokea zile taarifa za awali. Kwa hiyo, tutayamaliza maswali haya.

Na. 96

**Fidia kwa wananchi wa Ludewa Watakaopisha Ujenzi wa Miradi ya Nishati**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali inaendesha mchakato wa kutoa fidia kwa wananchi wa Mkomang’ombe na Liganga (Ludewa) watakaolazimika kupisha shughuli za uendelezaji wa miradi ya Chuma na Makaa ya Mawe:-

(a) Je, mchakato huo utakamilika lini?

(b) Je, ni fedha kiasi gani imetengwa kwa ajili ya kukidhi fidia hiyo?

(c) Je, ni changamoto gani zimejitokeza katika mchakato huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Raphael Benedict Mwalyosi, Mbunge la Ludewa, lenye sehemu (a), (b) na (c), napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mawaziri lilielekeza kuwa utekelezaji wa Miradi ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Chuma wa Liganga iliyoko Wilaya ya Ludewa, Mkoani Iringa, ufanyike kwa njia ya ubia kati ya Serikali kupitia *NDC* na wawekezaji wakubwa wenye uwezo wa kifedha na kiufundi.

Aidha, waraka uliagiza kuwa wawekezaji wateuliwe kwa njia ya ushindani na uwazi. Kamati ya watalaam iliundwa ili kusimamia utekelezaji wa miradi hii. Mtalaam Mwelekezi aliteuliwa ili kuishauri Serikali namna bora ya kutekeleza miradi hii. *NDC* ikishirikina na Mtalaam Mwelekezi iko katika hatua ya mwisho ya kuwapata wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, katika kujiandaa na utekelezaji wa miradi hii, *NDC* na Uongozi wa Wilaya ya Ludewa waliandaa ratiba ya mchakato wa kulipa fidia kwa wananchi watakaoathirika na miradi hii. Mchakato huo uligawanywa katika awamu nne:- Awamu ya kwanza ilikuwa ni kutoa elimu kwa wananchi, awamu ya pili ni kutambua mipaka ya maeneo ya miradi, awamu ya tatu ni kuandaa matumizi ya ardhi na awamu ya nne ni kulipa fidia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, maandalizi ya kutosha yanahitajika kabla ya kulipa fidia kwa wananchi watakaolazimika kupisha ujenzi wa miradi ya Liganga na Mchuchuma. Kama nilivyotangulia kusema mchakato wa fidia huo umeandaliwa katika awamu nne.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali iko katika hatua ya mwisho ya kuwapata wawekezaji wa miradi ya Liganga na Mchuchuma. Aidha, wawekezaji wataainisha matumizi ya ardhi kwa shughuli za miradi kama maeneo ya uchimbaji, mitambo ya kuzalisha umeme, mitambo ya kuzalisha chuma, makazi ya wafanyakazi na maeneo ya miundombinu mingine husika itakayofanyika. Tathmini ya kina ya mali zote zilizopo ndani ya maeneo yatakayoainishwa kwa ajili ya shughuli za miradi itafanyika ili kujua gharama halisi ya fidia. Aidha, baada ya kujua gharama halisi ya fidia, kiasi cha fedha kitatengwa ili kukidhi fidia hiyo.

(c) Mheshimiwa Spika, changamoto zilizojitokeza ni uhamisho wa wananchi waliopo ndani ya eneo la mradi ili kupisha utekelezaji wa miradi hii mikubwa. Wananchi walikwishaelezwa juu ya mpango wa Serikali wa kutekeleza miradi hii mikubwa, nao walikwishatoa ridhaa yao ya kuhamishwa. Wananchi wa maeneo husika walikwishaelezwa kuwa watafidiwa mali zao kufuatana na taratibu na sheria za nchi.

Utambuzi wa maeneo ya mipaka ya mradi wa Mchuchuma umekwishafanyika. Changamoto iliyopo ni kufanya tathmini ya mali zilizopo katika maeneo yaliyo ndani ya mradi wa Mchuchuma ambayo wananchi wake watahitajika kuhamishwa. Kazi ya utambuzi ya mipaka kwenye mradi wa Chuma cha Liganga, bado haijafanyika. Kazi ya kufanya tathmini ya mali ya wananchi itafanyika baada ya wawekezaji kupatikana. Suala hili litashughulikiwa kikamilifu kulingana na makubaliano yatakayojili baina ya mwekezaji na Serikali.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, majibu ni mazuri, lakini nitauliza maswali mawili: La kwanza, najua kwamba Serikali imeamua kutekeleza miradi hii miwili mikubwa katika awamu kubwa mbili; moja, mradi mdogo ambao unaitwa Mradi wa Kasi Mpya wa Kuzalisha Chuma ghafi, na mradi wa pili ni Mradi Funganishi wa kuzalisha Chuma cha Pua. Sasa, kwa vile mradi wa kuzalisha chuma ghafi wa kasi mpya ambao ulitakiwa ifikapo 2010 uwe umekamilika, unategemewa kuanza hivi karibuni.

Je, kazi hii ya kuainisha matumizi ya ardhi na kuainisha rasilimali za wananchi utafanyika katika kipindi gani ili mradi huu uwe kweli wa kasi mpya? La pili; kwa kuwa wananchi wa maeneo haya wamezuiwa kufanya maendeleo yao katika maeneo yao kwa muda wa zaidi ya miaka kumi, kitendo hiki ni cha unyanyasaji na kuwanyima wananchi haki zao za msingi.

Waziri anaweza akaniambia sasa kwa uhakika, ukamilishaji wa kufidia wananchi hawa na kuhamishwa kwenye maeneo mapya ili waweze kujifanyia maendeleo yao kama wanavyotaka. Anaweza akazungumzia utafanyika katika kipindi gani, miaka kiasi gani wasubiri? Miaka 10, 20, 5 au miwili?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mradi huu umechelewa kwa muda mrefu kidogo. Kusema kweli Mheshimiwa Spika, namna ya mradi wa Mchuchuma na Liganga, suala lote la mradi ulikuwa umekwama kwa muda mrefu kwa sababu ya namna ya utekelezaji wa mradi ule ulivyokuwa unataka kufanyika. Miradi ile ni mikubwa sana na kwa namna ile ilibidi kwa muda mrefu tusimame ili kupata ushauri kwa wale ambao wanaitambua miradi hii kwa upana wake.

Nadhani Profesa anafahamu pia kwamba mwanzoni fikra ilikuwa kutekeleza mradi huu kwa njia ya wawekezaji wadogo wadogo, lakini imeonekana kwamba mradi ule kwa sababu utaathiri mpaka Bandari ya Dar es salaam, Bandari ya Mtwara, Reli mpya n.k., ilibidi tupate Mshauri Mwelekezi ambaye alifanya kazi inayojulikana kama *Transaction Options Analysis* ambayo imebaini ni namna gani ambavyo twende na uwekezaji huo. Sasa ile kazi ya Mshauri Mwelekezi wa Uingereza, *Piper Elelay*, imeishamalizika. Kwa hiyo, sasa hivi *NDC*, Serikali inafanya kazi ya kutambua uwekezaji ule unaofanyika. Na kulingana na uwekezaji ule unaofanyika, ndiyo sasa tutabaini kwamba kinachohitajika ni moja mbili, tatu na katika maeneo haya wananchi wapishe, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba niseme kwamba, kwa kuwa tumefikia hatua hii ya tatu ya *procurement* na kazi inaendelea na *NDC* wako kwenye mchakato wa kukamilisha masuala ya uwekezaji. Mimi namwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba naye kwa sababu yuko karibu sana na utekelezaji wa mradi huu, tuendelee kuhimiza kwamba suala la mwekezaji limalizike haraka ili tuingie kwenye suala hili la mchakato wa kuhamisha watu kwa kujua kabisa kwamba maeneo yanayohitajika ni haya, kwa hiyo wanaweza wakahamia maeneo yaliyo jirani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nitambue kwamba kwa majibu hayo, nimejibu swali la (a) na (b) kama alivyo…naomba tuvute subira, lakini tunalifuatilia kwa karibu.

Na. 97

**Kukataliwa kwa Sarafu Zilizochakaa**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwepo na malalamiko kuwa wafanyabiashara na wenye maduka huko vijijini hukataa kupokea sarafu zinazoonekana kuchakaa toka kwa wananchi ambao wengi wao hawana uwezo wa kuzipeleka mahali popote:-

Je, ni hatua gani zinachukuliwa kuweza kutoa sarafu bora?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Jimbo la Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inazo taarifa za kuwepo malalamiko kuwa wafanyabiashara na wenye maduka vijijini hukataa kupokea sarafu zinazoonekana zimechakaa na pia baadhi ya matawi ya Benki kukataa kuzipokea sarafu hizo.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi wa Nane, mwaka 2008, Benki Kuu iliagiza Benki ya Biashara kupokea sarafu zinapoletwa kwao kama amana kwenye akaunti za wateja wao au kwa ajili ya kuzibadilisha. Benki Kuu ilitoa agizo hilo kutokana na kujitokeza mtindo wa baadhi ya wafanyabiashara kutokuzipokea sarafu hio.

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu kupitia Benki za Biashara, kila baada ya muda hutoa sarafu mpya kuziba pengo la zile zilizochakaa na ambazo huondolewa kwenye mzunguko. Sarafu ya Tanzania zina ubora stahiki ila mara nyingi utunzaji wake katika mzunguko ni chanzo kikuu cha kuchakaa haraka. Napenda kushauri wafanyabiashara kuwa siyo busara kutokupokea sarafu yetu ya Tanzania kwa kisingizio kuwa imechakaa,

kwa sababu ambayo haijatolewa kwenye mzunguko wa fedha kwenye uchumi, ni fedha halali kwa malipo yanayolingana nayo.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:- Kwa kuwa Naibu Waziri katika majibu yake amesema, naomba kumnukuuu: "Benki Kuu kupitia Benki za Biashara kila baada ya muda hutoa sarafu mpya kuziba pengo la zilizochakaa". Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sarafu za zamani, kama senti tano, senti hamsini, shilingi, shilingi tano, ukiiokota leo mchangani na ukiisafisha, ubora wake unakuwa ule ule kama mpya. Je, ni *material* gani yanayotumika chini ya kiwango kutengenezea sarafu hizi za shilingi 100 na shilingi 50? Na Serikali inachukua hatua gani kudhibiti ubora wa utengenezaji wa sarafu hizo ili kujiepusha na hasara hii ya mara kwa mara?

Mheshimiwa Spika, kuwa wananchi wa Namtumbo na wananchi walio wengi nchini wenye hali ya chini na wenye biashara ndogo ndogo, mzunguko wa mitaji yao hutegemea kukua kwake kwa kutegemea makusanyo ya sarafu kutoka katika biashara zao. Je, Benki Kuu haioni kuwa kukataliwa kulikoenea kwa sarafu hizi kumeathiri ukuaji wa kipato chao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu *material* zinazotumika kwenye sarafu zetu: zile sarafu ambazo zinaonekana kama ni za shaba, sarafu ya shilingi tano, kumi, kuni na tano mpaka mia, zinatumia chuma cha pua pamoja na brass. Na ile sarafuya shilingi mia mbili inatumia *brass* na *nickel.* Ilivyo ni kwamba chuma cha pua kinapopakwa *brass* hakipendi sana maji au jasho.

Kwa hiyo zile sarafu zikikutana na maji au jasho zinabadilika rangi na zinaonekeana kwamba zimechakaa wakati sivyo ilivyo. Kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, ndiyo sababu ni kweli kama ukiokota leo sarafu ya shilingi 5 au senti 5 na ukaisafisha, itaonekana kuwa ni mpya.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili linahusu kuathirika kwa wananchi wake au wananchi wengine kutokana na kukataliwa kupokewa na Benki au wafanyabiashara kwa sarafu hizi. Ninakubaliana naye kwamba hilo litatokea.

Lakini pia, ninaamini kwamba hata wafanyabiashara wenyewe wanajipunguzia kasi ya biashara yao kwa sababu mara nyingi biashara inategemea kasi ya kuzungusha fedha zenyewe. Kwa hiyo, nakubaliana naye na ni jambo ambalo kama alivyosema, tutaendelea kulipigia debe kwanza kuwaomba wafanyabiashara wasikatae kupokea hizi fedha, kama wakishazipokea, kama wanaona kwamba hawazitaki, wazipeleke benki za biashara na Benki za Biashara wenyewe kuna utaratibu wa kuzirejesha Benki Kuu ili Benki Kuu ifanye tathmini ya kuziondoa kwenye uchumi au kuzifanyia mabadiliko yanayostahili.

Na. 98

## Kuimarishwa Ofisi ya Msajili wa Hazina

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Ofisi ya Msajili wa Hazina imeanzishwa kwa mujibu wa sheria ya Msajili wa Hazina *(Treasury Registrar Ordinance Cap.418)* ikiwa ni mhisa pekee *(sole shareholder)* wa amana, hisa na vitega uchumi vingine katika makampuni na mashirika ya Umma kwa niaba ya Serikali; na kwa kuwa Msajili wa Hazina ni shirika pekee lenye uwezo wa kuchukua, kuendeleza au kuuza mitaji, kudai na kudaiwa kama ilivyo Makampuni au Mashirika ya kawaida:-

Je, Serikali imechukua hatua gani madhubuti za kuhakikisha kwamba Ofisi ya Msajili wa Hazina inaimarishwa ili kuweza kutekeleza majukumu yake katika viwango vya hali ya juu ili kukuza ufanisi wa kiutendaji na Mashirika ya Umma?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Jimbo la Wete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuimarisha Ofisi ya Msajili wa Hazina ili iweze kutekeleza majuku yake kwa kiwango cha juu kwa kukuza ufanisi wa kiutendaji hasa katika kusimamia kwa karibu utendaji wa mashirika ya Umma, taasisi na wakala za Serikali. Katika kutekeleza hili Ofisi ya Msajili wa Hazina katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 yaani mwaka huu, imeajiri watendaji saba na itaendelea kuajiri watendaji zaidi hadi kufikia kiwango kinachohitajika cha watumishi 51. Aidha, Serikali itaendelea kuipatia Ofisi hii vitendea kazi muhimu kulingana na ongezeko la watumishi na shughuli za Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, juhudi nyingine muhimu zinazokusudiwa za kuimarisha Ofisi hii ni pamoja na Serikali kuwajiri Mtalaam Mwelekezi atakayeshiriki katika kubaini kasoro zilizopo ndani ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ambazo zinaathiri utendaji kazi wa Ofisi hii na pia atatoa mapendekezo ya kurekebisha kasoro hizo.

Aidha, Serikali kwa kupitia Mtalaam Mwelekezi huyu, itaandaa mfumo na utaratibu unaofaa wa kukusanya na kuchambua takwimu muhimu za Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali. Mfumo huu unatarajiwa kukamilika mwaka huu wa fedha wa 2008/2009 na kuanza kutumika mwaka ujao 2009/2010. Utakapokamilika, mfumo huo utarahisisha sana upatikanaji wa taarifa na takwimu sahihi za Mashirika ya Umma na taasisi za Serikali kwa muda unaotakiwa.

**MHE MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali madogo mawili

ya nyongeza. Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali za kukuza vitendea kazi na watenda kazi, lakni utakubaliana na mimi kwamba maboresho ya maslahi ya wafanyakazi ni moja kati ya mambo muhimu ambalo ni la kukuza ufanisi katika kazi. Je, Serikali iko tayari sasa kupitia maslahi ikiwemo mishahara na marupurupu mengine ya wafanyakazi hawa ili kuongeza ufanisi wa kazi?

Mheshimiwa Spika, na kwa kuwa Ofisi ya Msajili wa Hazina ina uhaba wa fedha za mtaji kwa ajili ya kuwekeza katika mashirika mbali mbali. Je, sasa Serikali iko tayari kuipatia Hazina fedha za kutosha kukuza mtaji wake katika kuwekeza katika miradi tofauti?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwanza, swali linalohusu maslahi: Ni kweli maslahi zaidi kwa watumishi wa Serikali ni muhimu katika uhamasishaji wao wa utendaji kazi; na kwa kuwa wafanyakazi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina ni sehemu ya wafanyakazi wengine wa Serikali, basi pale mishahara au maslahi mengine yanapobadilishwa ama kutathminiwa, na wao wenyewe wanakuwa sehemu ya wafanyakazi wa Serikali ambao wanapata hiyo tathmini.

Kwa hiyo, hilo litafanyika pamoja na wafanyakazi wengine wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mtaji; mara kwa mara kwa kuwa Msajili huyu wa Hazina anasimamia mashirika mengi ya umma, utoai na upatikanaji wa mitaji unategemea sana na mahitaji ya shirika husika na mfano mzuri wa hivi karibuni ni *TIB* pale ambapo Serikali iliidhinisha *TIB* kupewa bilioni 21 kuongeza kwenye mtaji wake, na hivi karibuni bilioni 3 kwa ajili ya kuanzisha Dirisha la Mikopo kwa ajili ya Sekta ya Kilimo.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu!

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu, Kanuni ipi?

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 63(3).

**SPIKA:** Endelea!

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, “Mbunge mwingine yeyote anaweza kusimama mahali pake na kutamka Kuhusu Utaratibu”.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu akijibu swali langu la nyongeza, alisema kwamba mimi ni Mzabuni. Mheshimiwa Spika, nataka niseme hapa na ku-*declare* kwamba mimi siyo Mzabuni.

Kilichokuwa kinafanyika, nilikuwa nawapeleka wazabuni wenye madai mbali mbali kama Mwakilishi wa eneo hilo. Lakini kwa sababu yeye ni mtani mwenzangu, basi

mara nyingi huwa ananitania, nadhani amechukua hilo. Lakini kwa kuweka sawa *Hansard*, mimi siyo Mzabuni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Nadhani kwa kauli hiyo, jambo hilo limesikika, limeeleweka na linabaki daima katika Kumbukumbu ya Vitabu vya *Hansard* vya Bunge. Kwa hiyo, tuendelee kuvumiliana katika hayo. Ahsante sana! *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda umepita. Matangazo, nikianza na wageni:-

Nafurahi kuwaarifu kwamba katika *Speaker's Gallery* pale tuna wageni ambao wamealikwa mahsusi, kwa sababu leo ni siku yetu ya Kupokea Mpango Mkakati wa Miaka Mitano wa Bunge ambao tunaupokea saa 7.00. Sasa baadhi ya waliotoka Dar es salaam ni:-

Mheshimiwa Allain Nodehoo ambaye ni *Country Director* wa *UNDP*. *Could I ask you Sir to stand up please so that the House can acknowledge you?*

*Thank you very much. It's a pleasure to welcome you to Dodoma, we know over the years what UNDP has been doing in terms of progess and development for the people of Tanzania. Thanks for the good work of UNDP here in Tanzania*. Pamoja naye yupo Bwana Stephen Lee,…naona hayupo….*oh that is Stephen Lee, thank you, you most welcome*.

Pia yupo Bwana Audax Ruta – *Team Leader* masuala ya *governance.* Huyu ni Mtanzania anafanya kazi hapo na ni rafiki yetu Bwana Theo Caspers – Mshauri wa mambo ya utawala kutoka *European Union. Thanks very much once again for being here. (Makofi)*

Wageni wengine ni kama ifuatavyo: Wapo wageni wa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Christopher Chizza na Mheshimiwa Felix Kijiko, ambao ni wakulima 40, viongozi na watalaam wa kilimo cha umwagiliji maji mashambani kutoka Wilaya ya Kibondo. Wanaongozwa na Katibu wa Mbunge wa Jimbo la Buyungu, Bi. Regitha Mathias Mrefu.

Naomba apunge mkono Bi. Regitha. Na Afisa Umwagiliaji Bwana Alfred Swai, naomba apunge mkono! Karibuni sana, tunafurahi kuwaona hapa kutoka mbali hapo Kibondo. Ahsante, mnaweza kuketi. *(Makofi)*

Kuna Mgeni wa Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, ambaye ni Diwani wa Kata ya Masasi, Wilayani Ludewa katika Mkoa wa Iringa, Mheshimiwa Lawrance Mahundi. Naomba asimame tafadhali! Ahsate sana, karibu sana, karibu sana!

Wapo wageni wa Mheshimiwa Mturura A. Mtutura, ambao ni Hussein Hemed Kaisi, ambaye amekuja na familia yake. Naomba asimame. Yeye ni msaidizi wa

Mheshimiwa Mbunge wa Tunduru. Pia wapo wageni wa Mheshimiwa Joel Bendera, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo ambao ni wanafunzi 30 kutoka Chuo cha Ualimu (Awali) Korogwe. Karibuni sana kutoka Korogwe, ahsante sana.

Wapo wageni 21 wa Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Wabunge wanaotoka maeneo ya mifugo. Hawa wageni 21 wanatoka Wilaya za Nkasi, Mpanda, Sumbawanga, Kilosa na Rufiji. Nadhani bado wanajadiliana na wakubwa huko.

Wageni wa Mheshimiwa Michale Laizer ni James Ole Milya - DC Longido, Bwana Joseph Sadira – Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido na Dr. Ndossy, daktari wa Wilaya ya Longido. Bahati mbaya nadhani pengine wako nje hapo.

Tunao wanafunzi 40 kutoka Chuo cha Biashara *(CBE) Compus* ya Dodoma, nadhani wapo katika Ukumbi mwingine. Ala, wapo, karibuni sana. Ahsante sana. Wapo wageni 6 kutoka Shirika lisilo la kiserikali la utoaji misaada ya kisheria *NORA* kutoka Dar es salaam wakiongozwa na Ndugu Clement Mashamba. Ahsante Bwana Clement, karibuni sana.

Tunao pia leo wanafunzi 40 kutoka shule ya Sekondari Msalato Dodoma, nadhani pamoja na walimu wao. Ningeomba wasimame hapo walipo. Ahsante sana na tunawatakia mema katika mafunzo yenu. Sekondari yenu ni maarufu sana, natumaini na ninyi mtafanya kazi nzuri itaendeleza sifa nzuri za Msalato.

Wapo Wahariri Watendaji wa Magazeti ya Mwananchi na *Citizen* ambao ni Ndugu Theophil Makunga na Bakari Machumu. Tunao pia wanafunzi 20 kutoka shule ya Sekondari ya Ihumwa. Sijui wapo au wamewekwa kwenye Ukumbi ule mwingine. Mwisho, wanafunzi 14 wa Chuo Kikuu Dodoma wanaochukua Shahada ya Uzamili katika Fani ya Uhusiano wa Kimataifa. Nadhani nao wanaweza kuwa katika ukumbi wa *basement*.

Matangazo mengine ya kazi:-

Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, anahitaji wajumbe wa Kamati hiyo mkutane saa 6.00 Ukumbi namba 231.

Katibu wa Kamati ya Miundombinu, Ndugu James Warburg, ameniomba nitangaze kwamba leo, kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo ya Miundombinu saa 5.00 asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa, Ukumbi mdogo B.

Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, anahitaji wajumbe wote wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira mkutane leo saa 5.00 asubuhi ukumbi namba 227 jengo la utawala.

Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara anahitaji wajumbe wote wa Kamati ya Viwanda na Biashara mkutane leo saa 5.00 asubuhi ukumbi namba 133. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini anaitisha kikao cha Kamati hiyo saa nane mchana katika Ukumbi Namba 227. Kwa hiyo, Kamati ya Nishati na Madini saa nane au mara baada ya hafla ya *Cooperate Plan* Ukumbi Namba 227 jengo la utawala.

Waheshimiwa Wabunge imeonekana idadi kubwa kidogo ya Waheshimiwa Mawaziri hawaonekani humu Bungeni hii ni kwa sababu mimi nimedadisi asubuhi na nimepewa sababu halali kabisa ambayo ni kwamba sasa hivi kule Arusha kuna Mkutano muhimu sana wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo nchi zote tano Rwanda, Burundi, Kenya, Uganda na Tanzania tuna mazungumzo ya kuelekea soko la pamoja, sasa Wizara nyingi zinaguswa na hilo, ndiyo maana imebidi wawepo huko. Kwa hiyo, hayo ndiyo maelezo.

Waheshimiwa Wabunge jambo la pili ninalitaka kueleza ni kwamba, juzi Waheshimiwa Wabunge wengi walikuwa wanasema maswali yao yamekaa labda mwaka mmoja au zaidi, maelezo ni mepesi tu. Maswali yanayokuja mezani kwa Katibu mara nyingine yanatimia 500 au hata zaidi. Tunapokaa Bunge la wiki mbili yanajibiwa mia moja. Kwa hiyo, siyo kwamba Wizara hazijajibu, Wizara wanakuwa wameandika majibu lakini sasa maswali 400 yanarudi ili yajibiwe kwenye Mkutano mwingine.

Kwa hiyo, hilo ndilo tatizo, yanaandikwa tena na kadri hali inavyobadilika lina haririwa lakini kwa kweli yanakuwa yamefika Wizarani, yamepata majibu lakini hayakupangwa kusikilizwa. Kwa hiyo, hayo maswali yanaonekana kama vile yamechelewa sana kujibiwa ili hali Wizara zimekwishajibu.

Waheshimiwa Wabunge, mwisho kabisa na siyo kwa umuhimu leo saa saba mchana Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kufika Ukumbi wa Pius Msekwa, tutakuwa na hafla ya kupokea taarifa mbili, moja ni taarifa ya utekelezaji wa Bunge hili kwa miaka mitatu kuanzia Januari, 2006 hadi Desemba, 2008.

Lakini la pili ambalo nadhani ni kubwa zaidi ni kuupokea sasa rasmi mpango mkakati wa Bunge letu kwa miaka mitano, mpango huu ni muhimu mtakumbuka imepita takribani miezi kumi na nane ambapo mmetupa mawazo mbalimbali tumekaa katika Tume ya Huduma tumewasiliana na Serikali na sasa tumejipangia mpango ambao ni jambo zuri. Bunge haliwezi kwenda bila mpango wenye mkakati. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo tutakuwa pale na Mheshimiwa Waziri Mkuu atazindua na mtagawiwa nakala za mpango wa miaka mitano na pia taarifa ya utekelezaji ya miaka mitatu na kipeperushi cha Kiswahili maana yake ule mpango upo kwa lugha ya kiingereza. Tunazitafuta dola, hata Bunge linatafuta dola haliwezi kukaa tu, tunajua Bajeti ni finyu sasa wale wahisani ili tuweze kuelewana nao basi ipo katika lugha ya Kiingereza. Lakini muhtasari upo katika aina ya kipeperushi kwa lugha ya Kiswahili. Ni hafla muhimu na ninatarajia Waheshimiwa Wabunge wote tutaweza kuwa pale,

haitachukua muda mrefu lakini baada ya hapo kuna chai na vitafunwa na kadhalika na ni kitu kizuri tuwepo ili tuweze kushiriki.

Waheshimiwa Wabunge baada ya maelezo hayo na kwa kuwa nina wageni wengi sana leo ofisini, namwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Jenista Mhagama, aje aendeleze shughuli za leo.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA**: Kuhusu utaratibu Kanuni

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68 kwamba ulipokuwa unatoa maelezo ya maswali ya Bunge kwamba yanakuja mengi na muda ni wiki mbili. Kwa hiyo, muda haututoshi, hali kadhalika hata shughuli za Bunge ukiziona jinsi zilivyopangiliwa safari hii tunazipeleka kwa *speed* ya haraka sana kiasi kwamba mengine tunalipua tu(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako, huoni kwamba katika mazingira haya kuna sababu tosha ya ofisi yako kuielezea Serikali kwamba tunahitaji muda mrefu kama Mabunge mengine mathalani nchi ya Kenya, wenzetu wa Kenya wapo kila siku Bungeni, wanatoka wanakwenda kwenye *reassess* wanarudi tena kufanya kazi, kwa utaratibu huu wa wiki mbili mbili hatuwezi kuwatendea haki Watanzania, naomba Mwongozo wako. (*Makofi*)

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, tumelieleza hili mapema labda nikariri tu sasa, sababu zenyewe ni dhahiri kutokana na mtikisiko wa hali ya uchumi duniani. Kanuni yetu inaruhusu na taratibu tulizojiwekea mikutano mifupi ya Bunge inatakiwa iwe wiki tatu. Lakini kutokana na gharama zinazohusika imeshindikana kufanya hivyo. Hilo ndiyo tatizo la muda ambalo tunalipitia hivi sasa. Kila sehemu ya *Vote* ya Serikali imebidi wapunguze matumizi, sisi ni sehemu hiyo hiyo tunatoa huko huko Hazina. Kwa hiyo nawaomba muwe na subira kidogo tuendelee kufanya kazi zetu katika hali ngumu hii pengine hali itabadilika na tutarudi kutekeleza katika siku zijazo inavyotakiwa kwamba ni wiki tatu tulizokwisha ziomba hazijafutwa, zimepata athari kutokana na kutokupewa fedha za kutosha kuendesha shughuli zenyewe.

Waheshimiwa Wabunge ahsante sana. Naomba Mheshimiwa Mwenyekiti Jenista Mhagama, achukue nafasi.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na hatua inayofuata na ninaomba nimwite Katibu atupe mwongozo.

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

*(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya Marekebisho ya Sheria ya Wakala wa Serikali wa Mwaka 2009**
***(The Executive Agencies (Amendment) Bill, 2009)***

*(Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa kwa Mara ya Kwanza*)

**HOJA ZA KAMATI**

**Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge majadiliano yanaendelea na mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Mohammed Rished Abdallah na Mheshimiwa Halima Mdee, ajiandae.

**MHE. MOHAMMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kwanza asubuhi hii kuchangia taarifa ya kazi za Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali ya mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa iliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali bado tuna matatizo ya *financial discipline*, na nidhamu ya fedha katika Serikali yetu inaathiri sana maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni pesa nyingi ambazo zinatumika bila kufuata taratibu za kimahesabu, hii kunakuwa na mwanya wa upotevu wa fedha, kwa njia nyingine ni ujanja ujanja wa kuzitafuna hizo pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati zetu hizi tatu kwa kusimamiasuala zima la kudhibiti matumizi ya fedha za Serikali, bado sheria zetu pamoja na kwamba tumetengeneza sheria mbalimbali za kudhibiti hiyo hali, lakini bado kuna mianya na hii mianya inabidi tuirekebishe kwa sheria hizo hizo lakini kutokana na uzoefu ambao unaonekana katika kaguzi, mimi naamini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ataendelea kuona ni jinsi gani tuendelee kudhibiti matumizi mabaya ili tuende vizuri na tuhakikishe kwamba fdha za wananchi zinatumika vizuri kwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti Kamati hizi bado kama Bunge ambapo Bunge lenyewe linaendeshwa kwa kanuni zetu kuna haja ya kutazama Kanuni zetu hususani katika Kamati hizi tatu zinazosimamia mahesabu ya Serikali, tuone tunafanya nini kuisaidia Serikali, pamoja na kwamba tunaisimamia lakini kuna haja ya kuisaidia na kubaini mambo mengine na tuone Bunge linakuwa na nafasi ya kutoa ushauri na maelekezo na kufuata taratibu ambazo Serikali itaambiwa na iweze kuchukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)* mambo mengine Kamati inagundua ambayo hayaingii akilini kwamba watendaji wetu katika ofisi za Serikali Wizara zote na hiyo inajirudia Wizara zote na mifano ya sawasawa, hata suala la *book keeping* imekuwa ni tatizo kubwa sana, mpaka afike *CAG* agundue yale awaambie suala la kuweka vitabu vyako sawasawa, kitu gani kimeingia na kitu gani kimetoka, fedha zimeingia kwa utaratibu wake na zimetoka kwa utaratibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hiyo hoja kuambiwa na Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti Mkuu wa Serikali wanapewa muda na hatimaye ule muda waliopewa wanarekebisha yale mambo, kwanini hawafanyi ile kazi mpaka aingie *CAG?*(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti kama ni risiti hivi waliponunua au vocha zinapotolewa wakati ule wanatoa kwanini hawakamilishi mpaka aje Mkaguzi Mkuu ndiyo aje agundue hilo na akishagundua halafu ndiyo warekebishe, hapa inatutia wasiwasi sisi Kmati kuona kwamba huu utaratibu siyo mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu mimi nasema tutashauriana kwenye Kamati tutamwambia Mwenyekiti tutafute dawa ya hili, haiweekani Mkaguzi akishatoa taarifa yake au akienda kukagua halafu waambie warekebishe na wanarekebisha na kwa nini isirekebishwe toka mwanzo hili linatupa taabu kwa hiyo tutaona tutafanyaje kwa kushirikiana ndani ya Kamati ili tuweze kurekebishe suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatumia gharama kubwa sana katika miradi kama taarifa inavyosema, kama bajeti imetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara, barabara ni bilioni 50 mkataba kati ya Serikali na Mkandarasi uko wazi, inafika pahala Mkandarasi anashindwa kulipwa au anacheleweshwa kulipwa na hatimaye kunakuwa na penalties kwa mujibu wa Mkataba wenyewe kwamba ukinicheleweshea malipo inabidi uongeze gharama za ulipaji, hii kwa kweli pia haiingii akilini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba mradi ni huu na muda gani ikifika phase hii inabidi alipwe kwa nini halipwi, sababu zinazotolewa bado haziridhishi. Mimi nafikiri tutazame utaratibu mzuri zaidi wa kuingia hii mikataba hatimaye inafika pahala barabara ya bilioni 50 tunalipa mpaka bilioni 120, hizi ziada tungetengeneza barabara zingine mbili kama zile na hayo tumeyagundua *physically* katika kukagua barabara zetu na kuuliza maswali majibu yake siyo ya kuridhisha kama watalaamu wa mahesabu wanavyokuwa wamesomea na kukaa katika maeneo yao na kuhakikisha kwamba kila kitu kinakwenda vizuri, hii nayo bado pia Serikali ifanye kazi ya ziada na sisi Wabunge tutaendelea kuishauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Wizara kutumia fedha za  ziada kuliko ile bajeti iliyowekwa, hili ni tatizo kubwa.

Kwanza hawapati kibali cha Hazina, halafu utaratibu kwamba fedha hizi za ziada ni lazima ipitishwe na Bunge hili, hivi wao wanapata wapi nguvu ya kutumia fedha za wananchi bila ya kupata idhini ya Bunge nakibali kutoka Hazina, hili pia sisi tunalifanyia kazi kama Kamati tuone kwamba sasa utaratibu huu ukome. Ama sivyo tutakuwa sasa nini majukumu ya Bunge, nini majukumu ya Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunafuata taratibu zetu kama Bunge kuwapitishia Bajeti lakini wao bado wanasema kwamba tutatumia halafu itakuwa nini. Ndiyo maana yake. Itakuwa ni maana yake nini? Ndiyo jeuri yenyewe hiyo ya kutumia fedha wewe bila ya kupata kibari kwa mujibu wa Sheria zetu. Hayo mimi naona itatupa taabu na kila siku *CAG* atatuletea taarifa za kasoro zinazorudia mwaka hadi mwaka.

Mimi nimwombe *CAG* pamoja na kwamba tupitisha Sheria lakini bado tunaona kwamba *CAG* bado hajapewa meno makali zaidi. Sasa hebu tizameni tena hizi Sheria, nyinyi mnaelewa na sisi tunaelewa isifike pahali sasa na sisi tubadilishe Kanuni zetu za Bunge ili kufanya kazi za *CAG* na hilo tunaweza. Hakuna atakayetuzuia.

Lakini mtatuambia kwamba tunaingilia mambo ya jikoni. Lakini basi msitutumie sisi ili kupitisa mambo ambay hayakubaliki hilo ndilo tatizo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kama Sheria zinakasoro zinahitaji ziongezwe mengo basi Serikali ifanye juhudi impe *CAG* meno mengine zaidi ili na sisi turidhike kwamba sasa kwele mbano unakuwa mkali zaidi. Kama sivyo basi mimi nalishauri Bunge hili tukae sisi kama Bunge na tuone tunafanyaje katika Kanuni zetu ili tukomeshe hili tatizo la *financial discipline* katika Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti nilikuwa na angalizo hilo na nikushukuru kwa kunipa nafasi Ahsante sana.

**MWENYEKITI**: Nakushukuru sana Mheshimiwa Rished, kwa mwongozo nilio nao nitoe utaratibu wa kuhitimisha hoja hizi ili wote tuweze kujua hatua zitakazofuata zitakuwaje.

Waheshimiwa Wabunge watakapomaliza Waheshimiwa Wabunge kuchangia tunaendelea kuwapa Serikali nao wachangie ku-*respond* yale mambo ya haraka lakini watachangia kama wachangiaji, lakini Waheshimiwa Wenyeviti wawili wa Kamati husika watapata nusu saa kila mmoja kuhitimisha hoja yake, na tutakapofikia wakati huo hoja mmoja baada ya nyingine itahitimishwa kwa utaratibu si wa pamoja ni kwa utaratibu wa hoja moja baada ya nyingine. Kwa hiyo huo ndiyo utaratibu tutakaoufuata.

Waheshimiwa Wabunge kwa hali hiyo kwa muda nilionao ninadhani Mheshimiwa Halima Mdee atakuwa mchangiaji wa mwisho ili tuendelee kupata nafasi sasa ya kusikiliza *respond* na ili tupate muda wa saa nzima kutoka kwa wenyeviti wawili, vinginevyo muda hautaruhusu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kuniwezesha nami kuchangia kwa uchache kutokana na hali halisi ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati kabisa wenyeviti wawili wa Kamati ya *PAC* na *LAAC* pamoja na wajumbe wao kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwa lengo zima la kuwezesha Watanzania kuweza kufahamu ni kwa kiasi gani fedha zao zinatumika. Mimi nitazungumzia vitu vitatu, kitu cha kwanza ambacho nitakizungumza ni kuhusiana na *value for money auditing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti mzungumzaji aliyepita amezungumza hoja ambayo ni ya msingi sana, kwamba unakuta *CAG* anahoji kwa Wakurugenzi kwamba viambatanisho kadha wa kadha havipo na kwa mantiki hiyo hati yao inakuwa inamgogoro ama inakuwa inatoa maelekezo fulani halafu mwaka unaofuata ama baada ya muda fulani unakuta zile *document* zote zinakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti mimi nadhani kwamba tatizo la Halmashauri zetu nyingi wamekuwa ni maarufu sana wa kutengeneza risiti ambazo nyingi ni feki, kwa hiyo sasa ukiangalia risiti na mahesabu unakuta kwamba vitu vinajithaminisha lakini ukienda kuangalia kwenye *field* ama sehemu ambako iko *project* yenyewe kunakuwa kuna matatizo makubwa sana, kwa mantiki hiyo nadhani kuna umuhimu mkubwa sana kwa Serikali kuangalia watatumia utaratibu gani ili kuhakikisha kwamba hii ofisi ya Mkaguzi Mkuu inapanuliwa *to the effect* kwamba tunakuwa tuna watalaam ambao wanaenda wanafanya *value for money* ili kujua kama thamani iliyoandikwa kwenye vitabu na risiti ndiyo thamani halisi ya kazi iliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti nazungumza hili kwa sababu nimepitia kwa uchache sana ripoti ya *LAAC* na baada ya kupitia ripoti ya *LAAC* inaonekana kwamba walipotembelea Mkinga na Monduli walikuta vitu vya ajabu.

Kwa mfano Mkinga wakati wanapitia makaratasi waliambiwa kwamba kuna choo kimejengwa ambacho wametumia mifuko 100 ya simenti na wametumia mabati sabini, lakini walivyoenda kukagua kwanza wakaambiwa kwamba choo husika kimejengwa kwa nguvu za wananchi na mabati waliyoyakuta pale ni mabati matatu ambayo yameezeka hicho choo kwa mantiki hiyo kama wasingeenda kufanya *value for money apart from* taarifa ya *CAG* na taarifa za Halmashauri wasingeweza kupata huu ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti mfano wa pili ni Monduli, Halmashauri inaonyesha kwamba inmepewa pesa na Serikali, kama milioni 34 wanaonesha wamejenga nyumba ya Mwalimu kumbe ile nyumba imejengwa na *TANAPA* kwa asilimia mia moja na Tanapa ikakabidhi funguo, sasa hizi milioni 34 hazijulikani zimeenda wapi, kwa mantiki hiyo hawa watendaji wamehisika kwa namna mmoja au nyingine kuzitumia.

Kwa hiyo *aspect* ya *value for money auditing* ni muhimu sana tutakuwa kila siku tunaimba hapa kwamba tunapeleka pesa nyingi Halmashauri lakini tunakuwa hatuoni maendeleo kumbe hizo pesa zinaishia kwa wajanja wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika kuna umuhimu mkubwa sana wa kuimarisha usimamizi wa miradi ya Halmashauri, ukiangalia ripoti ya *CAG* ambayo ameitoa sasa hivi ameonesha *concern* kubwa sana ya jinsi ambavyo kunakuwa hakuna usimamizi madhubuti na kwamba kunakuwa na timu ambazo ni dhaifu labda kwa vile timu nyingi zinaundwa na wanasiasa, sasa kuna kuwa kunaleta matatizo makubwa sana.

Miradi inakuwa haigawanywi kwa jinsi ambavyo inapaswa kuwa, au miradi inakuwa inagawanywa kutokana na *interest* labda ya mtu ambaye yupo powerful pale kwenye Halmashauri na wengi wa hawa watu ni wanasiasa ambao inawezekana ni Meya au ni wenyeviti wa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti nalizungumza hili kwa sababu matukio kama haya ya kutozingatia ugawaji sawa wa rasilimali umetokea katika Manispaa ya Kinondoni, Madiwani wa Kinondoni wamekuwa wanalalamika kwamba kwanza shule unakuta kata mmoja inajengewa shule nane walitolea mfano Kata ya Kibamba inajengewa shule nane na unakuta Kata zingine haipati shule hata mmoja au hata kama shule ikijengwa kwa nguvu za wananchi unakuta kwamba wananyimwa mgao wa fedha, kumbe wanasiasa wetu hasa ambao wapo katika ngazi Halmashauri, wanachokifanya kama watendaji kupitia michakato mizima ya Zabuni waki-*propose* wajenzi wa aina fulani wanawakatalia kwa dhana ya kwamba wanawaleta mainjinia wao ili katika hao waweze kupata *ten percent.*

Mheshimiwa Mwenyekiti tunatatizo kubwa sana katika Halmashauri zetu ambazo inabidi tuziangalie kwa makini mkubwa sana ili tuweze kuhakikisha kwamba fedha zetu zinaenda kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti suala la pili ambalo nataka kulizungumzia ni majukumu mazima ya usimamizi wa hizi fedha zetu ambazo zinaenda kwenye Halmashauri.

Ukiangalia majukumu ya Mhasibu Mkuu, katika Serikali za Mitaa hana majukumu, ukiangalia sheria za fedha za umma ya mwaka 2001 ambayo imerekebishwa mwaka 2004 inampa mamlaka mhasibu Mkuu kuweza kuzifuatilia fedha kwenye Wizara na idara za Serikali au mamlaka zake mbalimbali.

Lakini sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 iko kimya haijulikani ni nani ambaye ana mamlaka ya kufuatilia fedha zilizokuwa katika Serikali za mitaa, kutokana na kwamba Sheria kutokuwa wazi kunafanya zile pesa zetu ambayo kwa hii *programme* yetu ya *D by D* zinazopelekwa kule chini kwenye Serikali za Mitaa zinashindwa kusimamiwa ipasavyo matokeo yake ni kwamba wajanja wachache wanazitumia na matokeo yake ni miradi ambayo kila siku tunakuwa tunaipitisha kila siku hapa Bungeni na fedha za maendeleo zinaishia mifukoni mwa watu wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti mimi nashauri kwamba kuna umuhimu wa kuifanyia marekebisho hii sheria ya Serikali za Mitaa ili kuweza kuweka mazingira ambayo kutakuwa kuna mtu ambaye ana mamlaka ya kusimamia hizi fedha, na kama haiwezekani

basi Mhasibu Mkuu ambaye kwa mujibu wa sheria za Fedha za Umma ana mamlaka ya kusimamia tu Idara za Serikali na Wizara apelekwe hadi huku chini awe na uwezo wa kuangalia fedha ambazo zinaenda kule zinaenda kufanya kazi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti hali kama hiyo itatusaidia kwa kiasi kikubwa sana kuepuka matumizi mabovu ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti vile vile nikubaliane na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya *LAAC* hasa yenye madhumuni ya kurudisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma, pndekezo (e) pendekezo hili ni muhimu sana na ninashauri Bunge letu Tukufu lipitishe kama sehemu ya maamuzi yake ili kuweza kudhibiti fedha zetu ambazo zinatumika vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wetu wa Halmashauri wamekuwa kwa miaka nenda rudi wanatumia fedha za Halmashauri kwa manufaa yao na hakuna hatua zozote zinazochukuliwa dhidi yao.

Yameandikwa sana kwenye magazeti watu wanaweza wakadhani labda mimi nina bifu watoto wa mitaani wanasema hivyo na Mheshimiwa Londa labda, lakini mimi nilitolea mfano wa Kinondoni kwa sababu ninafahamu uchafu unaoendelea pale, yanaandikwa mengi lakini hakuna hatua yeyote inayochukuliwa.

Ukiangalia historia ya Manispaa ya Kinondoni imeingiwa mikataba ya *billions of shillings*. Halafu *worse enough* Baraza la Madiwani linakataa kupitisha lakini unakuta mtu mmoja kwa mamlaka yake ama sijui kwa nguvu ambazo amepewa na nani anapitisha anapelekea Manispaa kupata hasara kubwa sana. Sasa kwa kuwa watu ni wajanja wanachokifanya ni kutengeneza risiti kuweka mahesabu, wanajua *auditors* wakija wanaangalia makaratasi wana-*compare then* biashara imekwenda.

Lakini ukija ukiangalia thamani halisi hakuna thamani halisi ya fedha iliyotumika. Kwa hiyo, mimi ninakubaliana nao kabisa kwamba kuna umuhimu mkubwa wa watu wa aina hii kuchukuliwa hatua, kuna ushahidi wa dhahiri unaoonyesha kwamba Meya wa Kinondoni alisababisha hasara zaidi ya milioni 800 kwa kuingia mkataba ambao amejiridhia yenye mwenyewe. Baraza la Madiwani limekataa. Kuna ushahidi unaoonyesha kwamba Meya wa Kinondoni ameongeza bei ya matrekta ya matrela zipo *evidence* lakini watu wanasema vinaandikwa, hatua hazichukuliwa. Kwa hiyo, mimi naamini kabisa hili pendekezo ni muhimu lifanyiwe kazi. (*Makofi*)

Watu wanauza viwanja vya Serikali unaleta taarifa *worse enough* Wizara inayohusika inamsafisha kwa *documents* ambazo ni fake. Kwa hiyo, unakuta kuna tatizo siyo kuanzia *local government* peke yake hadi Wizara za juu ambazo zinatakiwa zisaidie. Lakini zenyewe badala ya kusaidia zina-*act politically* kuangalia hii hoja labda imeletwa na nani. Kwa hiyo, mimi nadhani hili pendekezo la akina Dr. Slaa ni muhimu sana na ni muhimu tuanze kulifanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema ninashukuru na ninaunga mkono hoja nikiamini kwamba sasa tutaanza kufanyakazi hatutabakia kupiga blabla. Nashukuru. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mbalimbali na niishukuru sana Kamati ya *LAAC* kwa ushirikiano wa karibu ambao wameipa Wizara yangu. Kwa kweli kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati hiyo tunashirikiana kwa karibu sana ili kuangalia mapungufu mbalimbali ambayo yanatokea katika Halmashauri mbalimbali ili tuweze kuyarekebisha kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge, kwamba wanaposema fedha nyingi za Serikali zinakwenda kwenye Halmashauri za Wilaya wawe na *facts* kwamba je, ni asilimia ngapi inayokwenda kwenye Serikali za Mitaa? Serikali za Mitaa ziko Halmashauri 133 bajeti ya Serikali inayokwenda kwenye Serikali ya Mitaa ni asilimia 17 ya Bajeti ya Serikali. Naomba hilo walielewe. Siyo asilimia kubwa kama wanavyosema kwamba fedha nyingi zinakwenda huko.

Kwa hiyo, hilo tuliweke sawa kwamba ni asilimia 17 ya Bajeti ya Serikali. *Simple arithmetic* ni kwamba bajeti ya Serikali ni trilioni 7 *point something* na fedha zinakwenda kwenye Serikali za Mitaa ni trilioni 1.2. Kwa hiyo, utakuta kwamba ni asilimia 17 tu ya fedha zote aidha *OC* na *PE* au fedha za maendeleo. Fedha nyingi zinazokwenda kwenye Serikali za Mitaa naomba niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge kwamba asilimia kubwa ni *personal emolument* mishahara ya wafanyakazi kwa sababu Serikali za Mitaa ndizo zenye wafanyakazi wengi zaidi. Kwa hiyo, *PE* inachukua fedha nyingi sana.

Fedha za wahisani zinazokwenda kwenye Serikali za Mitaa kati ya trilioni 2 ni milioni 327 tu ndizo zinazokwenda kwenye Serikali za Mitaa. Naomba hili niliweke sawa ili tusione kwamba fedha nyingi zinakwenda huko bali mimi napenda kutambua mchango wa wananchi kwamba kwenye maendeleo mchango wa wananchi ni mkubwa zaidi kama tungekuwa tunaweka kwenye mzani wa hali halisi wa kifedha, mchango wa wananchi ni mkubwa kuliko fedha nyingine zozote zile. Tungesema kweli ule mchango wa wananchi ambao wanatoa *in kind* wanaochangia nguvu, wanauchangia kifedha kwa kweli ni mchango mkubwa sana.

Kuhusu udhibiti wa wa fedha za Serikali kwa upande wa Serikali za Mitaa naomba niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge kwamba kwenye Serikali za Mitaa uwazi na uwajibikaji ni mkubwa zaidi. Mimi naweza nikasema ni mkubwa zaidi tukilinganisha na upande wa Serikali Kuu nikiwemo pamoja na mimi kama Wizara. Kule *transparency* ni kubwa sana kwa sababu kuanzia ngazi ya kijiji kama mradi haukufanyika barabara haikujengwa, zahanati haikujengwa kuonekana kwake ni rahisi zaidi kuliko miradi ambayo iko Serikali Kuu. Tukianza katika ngazi ya kijiji kuna Kamati ya ujenzi katika kijiji. Kamati ya Ujenzi ndiyo inayosimamia miradi yote pale kijijini aidha, mradi wa shule, aidha, mradi wa zahanati na kadhalika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, katika ngazi ya kijiji kitu kisipofanyika *watch dog* namba moja anayeangalia mradi huu unakwenda au hauendi ni mwananchi mwenyewe. Kwa hiyo, pale tunasema kwamba wananchi wenyewe ni ma-auditor ambao wanadhibiti hiyo miradi iende. Isipokwenda wananchi wenyewe utakuta wanaongea au wanapeleka Serikalini.

Niwape tu mfano mdogo tu kule Kagera kuna mradi wa *TASAF* ambao ulikuwa haukufanyika. Yule aliyepewa zile fedha pale pale kijijini wakaona wenzako mabadiliko tu amenunua TV, amenunua dish, amepiga bati nyumba zake. Wananchi wakajiuliza mwenzetu hela katoa wapi pale pale kijijini ikaonekana kwamba amechukua hela za *TASAF*. Walichofanya wananchi pale wameita mkutano wa kijiji wakahakikisha kwamba wanang'oa bati kwenye nyumba wamechukua *TV,* wamechukua dish wamekwenda kuviuzwa. Kwa hiyo, ma-*auditor* ni wenyewe, maskari ni wenyewe, mahakama ni wenyewe katika level ya kijiji. Nataka kuwaonyesha tu uwajikaji katika ngazi ya Kijiji. Kwenye Halmashauri kama tunavyofahamu kuna Kamati mbalimbali, pia *audit committee* nayo inafanyakazi hiyo, baraza la Madiwani linafanyakazi hiyo, wapo wakaguzi wa ndani, wakaguzi wa nje, Kamati ya *LAAC, CAG* kwa hiyo, utakuta kwenye Serikali za Mitaa kuna *watch dogs* wengi zaidi.

Kuhusu suala la Kinondoni niunganishe hapo hapo ambalo amesema Mheshimiwa Halima Mdee jamani mimi nasema hivi tuwe tunaheshimu taarifa ambayo inatolewa na Mdhibiti na Mkaguzi wa Serikali. Kwa Kinondoni hoja zao ziko humu, hoja anazotoa Mheshimiwa Mbunge ni vyema akazileta na *evidence*. Lakini alichosema yeye na kilichoandikwa humu ni vitu tofauti.

Sasa je, tumsikilize Mbunge au tumsikilize huyo *CAG*? Kwa hiyo, mara nyingi tuwe tunafuata ambayo yanaandikwa kwenye vitabu.

Kwa hiyo, kwa upande wa Serikali za Mitaa mimi nasema kwamba tutazidi kuendelea kuwasimamia ili kuhakikisha kwamba *value for money* inapatikana. Niseme tu huko nyuma tulikuwa na matatizo mawili, tulikuwa na tatizo la vitabu vyetu kutowekwa sahihi. Mahesabu yalikuwa hayafungwi vizuri.

Sasa hivi kwa kweli kwa hilo tumefanikiwa ndiyo maana unaona kwamba vitabu vyetu vinafungwa kwa wakati na ni vizuri kwa sasa hivi hata wenzangu Kamati ya *LAAC* wanasema kwamba kuhusu vitabu sasa hivi hawana matatizo.

Tatizo lililopo ni *value for money* ndiyo maana tunashikiriana na Kamati ya *LAAC* na *inspection committee* katika Wizara yangu kuhakikisha kwamba kile kilichoandikwa na wenzetu kwenye taarifa za fedha kinalingana na kile kitu ambacho kinafanyika kule kwenye *grand* kama miradi mbalimbali na kadhalika hilo kwa kweli tunashirikiana kwa karibu sana Kamati ya *LAAC* kuhakikisha kwamba kule chini miradi inakwenda kama kawaida. Kwa hiyo, suala la ufungaji wa mahesabu kwa sasa hivi hatuna matatizo linakwenda vizuri, karibu Halmashauri zote zinafungwa kwa wakati na hoja nyingi za mkaguzi Mkuu wa Serikali sasa hivi zimepungua hata kama utaangalia

kitabu cha mwaka jana na mwaka juzi vilikuwa vikubwa sana kwa sababu hoja zilikuwa nyingi zaidi lakini sasa hivi hoja zimepungua.

Kwa hiyo, kwa upande wa udhibiti wa fedha niliona niliongelee sana ili Waheshimiwa Wabunge waelewe kwamba kwa kweli tunalisimamia kwa karibu na kwa kweli tunatambua michango yao na tunatambua utendaji mzuri ambao unafanywa na Kamati ya *LAAC*. Kuhusu suala la fedha ile asilimia 20 ambayo inakwenda kwenye vijiji Waheshimiwa Wabunge ile asilimia 20 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida siyo kwa ajili ya fedha za maendeleo. Kwa hiyo, asilimia 20 inapotolewa kwenda kwenye kijiji ni kwa ajili ya fedha za matumizi (*OC*).

Baadhi ya sehemu ni kweli wametekeleza hilo la asilimia 20, lakini baadhi ya sehemu wameona kuna ugumu wa aina fulani kwa sababu zifuatazo, kwamba kwa mfano *OC* ya mwezi katika Halmashauri ya fidia ni shilingi 12 katika milioni 12 asilimia 20 ambayo inatakiwa kwenda kijiji ni shilingi karibu milioni 2. Sasa milioni mbili ukichukua uigawe kwa vijiji 100 au vijiji 70 unaona kwamba ni hela ndogo sana. Ukisema uwapelekee monthly ni kwamba unawapelekea unawaambia kwamba sasa hizi mzitumie kwa kitu chochote ambacho mnataka.

Kwa hiyo, baadhi ya Halmashauri wanafanya kama ku-accumulate kwamba ziwe nyingi ili wakiwapelekea pale wafanye kitu mmoja au wachangie kwenye mradi au wafanyie vitu ambavyo vitawasaidia katika kuendeleza ofisi zao. Wengi wanatumia hiyo asilimia 20 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za vijiji, mambo ya *stationary* na kadhalika. Kwa hiyo, tutaendelea kuwasisitiza kwamba hiyo asilimia 20 ni muhimu lakini tutapanga namna bora zaidi ya kupeleka hiyo asilimia 20 katika level ya vijiji ili tusiende kuzipeleka kule badala ya kuzitumia kwa makusudi yaliyotakiwa, watatumia kwa makusudi mengine. *(Makofi)*

Kuhusu asilimia 10 ya wanawake na vijana kwa kweli naishukuru Kamati ya *LAAC* wamewabana sana Wakurugenzi katika Halmashauri mbalimbali. Sasa hivi karibu asilimia 82 ya Halmashauri wameshatoa hizo fedha kwa ajili ya kuchangia miradi ya wanawake na vijana katika Halmashauri mbalimbali. Kikubwa zaidi ni kwamba fedha hizi badala ya kukopeshwa wanawake na vijana inaonekana kabisa kwamba wanawake wamerudisha hiyo mikopo lakini kwa upande wa vijana hawakurudisha hiyo mikopo kwa hiyo, nitoe rai tu kwa vijana ambao wamekopa mikopo hii waweze kurudisha ili iweze kuwasaidia watu wengi zaidi. Lakini kwa sasa hivi kwa kweli urudishaji siyo mzuri.

Nawapongeza akina mama wa Tanzania waliokopeshwa hiyo mikopo kwa kurudisha vizuri sana mikopo hiyo. Baadhi ya Halmashauri mikopo hii imerudishwa mpaka asilimia 85 lakini kwa baadhi ya Halmashauri wamerudisha asilimia 40, 50 kwa hiyo huo mfuko unalegalega kwa sababu ya kutokurudisha kwa fedha hizo. Hiyo asilimia 10 Waheshimiwa ikishatolewa mara moja kwa sababu ile ni *revolving fund* ikishatolewa mara moja ndio hiyo hiyo inaendelea kuzungusha kwenye ule mfuko.

Siyo kwamba kila mwaka zinatolewa hizo asilimia kumi. Mwongozo wetu ni kwamba asilimia 10 inatolewa *once and for all* siyo kila mwaka wanatoa asilimia 10.

Hiyo asilimia 10 ni kutokana na mapato ya Halmashauri yenyewe *(own sources)* siyo *total budget* kwa hiyo, wengine wanachanganya kwamba lazima ni asilimia 10 ya fedha zote za Halmashauri hapana ni asilimia 10 ya makusanyo ya Halmashauri husika. Kwa hiyo, niziagize tu zile Halmashauri ambazo hazijafanya hivyo waweze kuchangia ili tuondokane kabisa na tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala mengine ambayo tumeshayachukua, tumeshaelewana na Kamati ya *LAAC* kwamba tunayafanyia kazi ili tuweze kuleta ufanisi katika Halmashauri zetu. Kwa yale masuala binafsi mimi nasema hivi Waheshimiwa Wabunge, ofisi yangu iko wazi namsikiliza kila Mbunge, naithamini kila hoja ya Mbunge inayotolewa katika Bunge lako tukufu sitadharau hata hoja moja ambayo inatolewa na Mheshimiwa Mbunge.

Kwa hiyo, kama unaona kuna matatizo mimi nawaomba tuonane ofisini tuweze kulitatua, tuweze kulifuatilia kwa karibu zaidi ili tuone kwamba tunapata suluhu ya matatizo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri hujaunga mkono hiyo hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hii ni hoja ya Kamati kwa hiyo inapowekwa ndani ya Bunge ni hoja yetu sisi wetu wote.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ulionipa na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba niseme machache yanayotokana na taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali inayohusu Hesabu za Serikali za mwaka 2006/2007. Namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati hii Mheshimiwa John Cheyo pamoja na wanakamati wenzake kwa kazi kubwa ambayo kutokana na taarifa iliyo mbele yetu lazima wameifanya na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao wamepata fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali imetoa maoni na mapendekezo mengi ambayo ingawaje yameelekezwa kwenye hesabu za Serikali za mwaka 2006/2007 ni dhahiri kwamba bado mpaka mwaka huu 2008/2009 yanahitaji ama kushughulikiwa ama kuyapa tafakari ili kuboresha uandaaji na utoaji wa hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge katika mapendekezo yake imeanza kwa kutoa raia kwa Serikali kurudisha Kampuni ya *TANSORT* nchini kutoka London ni ile Kampuni inayoshughulikia Almasi ili mapato yanayotokana na kazi ya Kampuni ile yaweze kudhibitiwa na kubaki nchini na kuongezwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali,

na mimi ninaishukuru Kamati kwa ushauri huu na ninaihakikisha kwamba juhudi hizo zinaendelea na zitakapokamilika bila shaka Bunge lako Tukufu litataarifiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini maoni mengine na mapendekezo mengine ya Kamati yanahusu umuhimu wa kuongeza nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria za fedha na sheria za ununuzi na hili sote tunalikubali. Ni dhahiri ukitazama ripoti ile ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuna maeneo mengi ambayo hayaridhishi na tuna changamoto hapo kama Serikali na wasimamizi wa mapato ya Serikali kwa upande wa matumizi kuhakikisha kwamba matumizi yanafanya kazi kama yalivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine ambao unaendana na huo ushauri wa kupunguza matumizi ya Serikali ni ili kupunguza basi matumizi ya kawaida ya Serikali na tupate salio la kupeleka kwenye matumizi ya maendeleo, na tunakumbuka dhahiri kwamba katika bajeti ya mwaka 2008/2009 kwa makusudi Serikali ilifanya uamuzi wa kusema basi imetosha sasa matumizi ya kawaida yatalipwa na makusanyo ya ndani yanayotokana kwa sehemu kubwa na juhudi za *TRA* na tukaweza kufanya hivyo, na kwa kufanya hivyo, kilichotokea ni kwamba misaada yote basi ikawa sasa inaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo. Tunaamini kwamba ni muhimu tukaendelea na msimamo huo na matarajio yetu katika kuandaa bajeti ya mwaka 2009/2010 ambayo tunafanya sasa dhana hiyo ambayo ni ya msingi itazingatiwa. Ninaishukuru sana Kamati kwa kutukumbusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu Maafisa Masuuli ambao wanakumbushwa kutekeleza ushauri wa Kamati na pia ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu mambo mbalimbali ambayo yanakuwa yameibuliwa wakati wa ukaguzi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ama na Kamati yenyewe. Mimi ninakubali kwamba kutofanya hivyo ni uvunjaji wa Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 ambayo tumeipitisha hapa Bungeni na ukweli kwamba tusingetegemea kwamba jambo hili litaendelea ikiwa kuna mambo ambayo yameibuliwa na yanataka majibu basi ni vyema Serikali kupitia Maafisa ambao wanatakiwa kujibu wakajibu.

Kwa hiyo, ninakubaliana na Kamati ya Bunge kwamba kuna umuhimu wa kuongeza juhudi katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna pendekezo lingine na maoni ya umuhimu wa kusimamia mikataba ambayo Serikali inaingia hili pia bila ya kuwa na haja ya kulisisitiza ni jambo ambalo ni la msingi. Tumeona jinsi ambavyo mikataba ambayo imeonekana kwamba ina upungufu imetuenyesha, ninakubali kwamba jitihada ni muhimu kuchukuliwa kuhakikisha kwamba mikataba yoyote ile ambayo Serikali ama Taasisi za Serikali zinaingia mikataba ile isiwe na mapungufu ambayo dhahiri inapelekea kwa maslahi ya Taifa kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipitie upya mfumo wa kubakiza fedha katika maeneo ya makusanyo yaani zile *retention scheme*s ambazo zimepewa baadhi ya Mashirika yetu.

Jambo hili tumelianza katika Sheria ya Fedha kwenye Bajeti ya mwaka jana mwezi Agosti, ule na pale ambapo tulirekebisha Sheria mbalimbali za Mashirika na Taasisi mbalimbali kuwe na majadiliano kati ya yale Mashirika na Mawaziri wa Wizara mbalimbali na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ili wakubaliane ni kiasi gani ambacho kitalipwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na ili basi Taasisi na Mashirika haya yachangie zaidi kwenye Mfuko na kwenye mapato ya Serikali.

Tutaendelea na utaratibu huo. Ninashukuru kwamba katika taarifa ya Kamati wamekwenda zaidi ya kutukumbusha kwamba hili siyo suala la hiari ni suala linatokana na matakwa ya Katiba, ni suala la Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001, na kwa hiyo ni lazima kufanya hivyo.

Ninaihakikishia Kamati kwamba hili litafanyika na tutaendelea kuangalia sheria hizi ambazo zinasimamia Taasisi mbalimbali na Mashirika mbalimbali na kuona jinsi ambavyo tunaweza kuzileta Bungeni kuzirekebisha hili liwezekane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali irekebishe vifungu vya sheria vinavyokinzana kifungu kwa kifungu, lakini vilevile ambavyo vinakinzana na misingi ya utayarishaji wa taarifa za fedha.

Hili litawezekana kupigiwa hatua zaidi pale ambako tutakuwa tumeingia kikamilifu kwenye utaratibu wa kutengeneza na kutayarisha hesabu na taarifa za mahesabu ya Serikali kwa kutumia *International Financial Report standards*, na kwa hiyo, hapa siyo tu kutazama sheria zinazokinzana katika kutayarisha hizi taarifa, lakini vilevile ni kuharakisha na kuweka mfumo zaidi kwenye matumizi ya hizo *standards* nilizozisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuhakikisha kwamba takwimu sahihi zinapatikana kuhusu deni la Taifa. (Makofi)

Ninakubali na hili ni jambo la muhimu sana kwa sababu deni la Taifa lina mambo mawili. Kwanza, lina ile *principle* yenyewe na ule mtaji wenyewe ambao unakuwa umekopwa, lakini vilevile kuna riba mara nyingi ambayo inaambatana na ule mtaji wa msingi uliokopwa.

Lakini pamoja na hilo ni njia nzuri unapokuwa na takwimu ambazo zina uhakika kwamba unapunguza malumbano kwenye kitu ambacho unadaiwa ama ni nini ambacho unadai. Kwa hiyo, ninashukuru Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu kwa kutukumbusha jambo hili, na niseme kuwa ni jambo ambalo linafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Masuuli wasishinikizwe na wanasiasa katika kupanga matumizi ya fedha, na mimi ninakubaliana wasishinikizwe, na ninavyofahamu mimi…!

*(Hapa kengele ililia kuashirika kumalizika muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri hiyo ni kengele ya pili.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Ni kengele ya pili hiyo.

**MWENYEKITI:** Ndiyo**.**

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nilikuwa napata hamasa ya kuendelea kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ninaunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* na Wajumbe wote, kwa kazi nzuri waliyoifanya kukagua mahesabu ya Wizara mbalimbali, Mikoa na kadhalika. Ninachopendekeza sasa hivi ni Wizara nyingi na Mikoa wameanza kuandika na kupanga mahesabu yao, yaani vitabu vizuri; kinachotakiwa kutiliwa mkazo ni *performance audit* na *value for money*, pamoja na manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ni lazima Bajeti ya Kamati ya *PAC, LAAC* na *POC* ziongezwe, badala ya kukagua hesabu Dar es Salaam na Dodoma sasa waende kwenye maeneo ya miradi maana huko ndiko unakokwenda kuthibitisha kama fedha zilizotolewa na Serikali na kupangwa vizuri kwenye vitabu zimefanya kazi iliyotakiwa na kwa kiwango kinachotakiwa. Pia huko ndiyo mtaona kama manunuzi yaliyofanywa yanaendana na misingi iliyowekwa. Pia kuna tatizo la watumishi ambao wamekaa kituo kimoja cha kazi kwa muda mrefu sana, wanajenga mazoea mpaka wanasahau miiko ya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naunga mkono taarifa ya Kamati kwa asilimia mia moja.

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naipongeza Kamati ya *PAC*, kwa mashirikiano mazuri na *CAG*, pamoja na *TRA* katika usimamizi mzuri wa ukusanyaji mapato na kuzuia matumizi mabaya ya fdha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo liangaliwe zaidi na Shirika la Umma la TBS na hasa suala la magari. Ukweli *CAG* wafuatilie kwa karibu Shirika hili kwenye tozo ya magari mabovu yanayoingizwa nchini. Fedha hizo zikusanywe hapa nchini, kwa sababu gari moja dogo linatozwa *USD. 170* na gari kubwa *USD. 200* na kama hukulipia kwenye wakala wao wa nchi yanakotoka magari kwa wingi, unatozwa Sh. 800,000 kwa gari dogo na Sh. 2,000,000 kwa gari kubwa. Tozo kubwa hizo unatozwa ili ulipie nje ya nchi, ambako fedha zile hesabu yake huzioni.

Mawakala wanaowatumia hawafanyi ukaguzi ila ni kutoa *certificate* ya *TBS* tu sio ukaguzi na haieleweki mawakala hao ni asilimia ngapi wanawalipa. Mawakala hao wanaweza kuzifanyia biashara fedha hizo kwa sababu haijulikani muda wa makabidhiano au akaunti gani aingize wakala.

Ukiangalia historia ya Manispaa ya Kinondoni imeingiwa mikataba ya *billions of shillings*. Halafu *worse enough* Baraza la Madiwani linakataa kupitisha lakini unakuta mtu mmoja kwa mamlaka yake ama sijui kwa nguvu ambazo amepewa na nani anapitisha anapelekea Manispaa kupata hasara kubwa sana. Sasa kwa kuwa watu ni wajanja wanachokifanya ni kutengeneza risiti kuweka mahesabu, wanajua *auditors* wakija wanaangalia makaratasi wana-*compare then* biashara imekwenda.

Lakini ukija ukiangalia thamani halisi hakuna thamani halisi ya fedha iliyotumika. Kwa hiyo, mimi ninakubaliana nao kabisa kwamba kuna umuhimu mkubwa wa watu wa aina hii kuchukuliwa hatua, kuna ushahidi wa dhahiri unaoonyesha kwamba Meya wa Kinondoni alisababisha hasara zaidi ya milioni 800 kwa kuingia mkataba ambao amejiridhia yenye mwenyewe. Baraza la Madiwani limekataa. Kuna ushahidi unaoonyesha kwamba Meya wa Kinondoni ameongeza bei ya matrekta ya matrela zipo *evidence* lakini watu wanasema vinaandikwa, hatua hazichukuliwa. Kwa hiyo, mimi naamini kabisa hili pendekezo ni muhimu lifanyiwe kazi. (*Makofi*)

Watu wanauza viwanja vya Serikali unaleta taarifa *worse enough* Wizara inayohusika inamsafisha kwa *documents* ambazo ni fake. Kwa hiyo, unakuta kuna tatizo siyo kuanzia *local government* peke yake hadi Wizara za juu ambazo zinatakiwa zisaidie. Lakini zenyewe badala ya kusaidia zina-*act politically* kuangalia hii hoja labda imeletwa na nani. Kwa hiyo, mimi nadhani hili pendekezo la akina Dr. Slaa ni muhimu sana na ni muhimu tuanze kulifanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema ninashukuru na ninaunga mkono hoja nikiamini kwamba sasa tutaanza kufanyakazi hatutabakia kupiga blabla. Nashukuru. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mbalimbali na niishukuru sana Kamati ya *LAAC* kwa ushirikiano wa karibu ambao wameipa Wizara yangu. Kwa kweli kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati hiyo tunashirikiana kwa karibu sana ili kuangalia mapungufu mbalimbali ambayo yanatokea katika Halmashauri mbalimbali ili tuweze kuyarekebisha kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge, kwamba wanaposema fedha nyingi za Serikali zinakwenda kwenye Halmashauri za Wilaya wawe na *facts* kwamba je, ni asilimia ngapi inayokwenda kwenye Serikali za Mitaa? Serikali za Mitaa ziko Halmashauri 133 bajeti ya Serikali inayokwenda kwenye Serikali ya Mitaa ni asilimia 17 ya Bajeti ya Serikali. Naomba hilo walielewe. Siyo asilimia kubwa kama wanavyosema kwamba fedha nyingi zinakwenda huko.

Kwa hiyo, hilo tuliweke sawa kwamba ni asilimia 17 ya Bajeti ya Serikali. *Simple arithmetic* ni kwamba bajeti ya Serikali ni trilioni 7 *point something* na fedha zinakwenda kwenye Serikali za Mitaa ni trilioni 1.2. Kwa hiyo, utakuta kwamba ni asilimia 17 tu ya fedha zote aidha *OC* na *PE* au fedha za maendeleo. Fedha nyingi zinazokwenda kwenye Serikali za Mitaa naomba niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge kwamba asilimia kubwa ni *personal emolument* mishahara ya wafanyakazi kwa sababu Serikali za Mitaa ndizo zenye wafanyakazi wengi zaidi. Kwa hiyo, *PE* inachukua fedha nyingi sana.

Fedha za wahisani zinazokwenda kwenye Serikali za Mitaa kati ya trilioni 2 ni milioni 327 tu ndizo zinazokwenda kwenye Serikali za Mitaa. Naomba hili niliweke sawa ili tusione kwamba fedha nyingi zinakwenda huko bali mimi napenda kutambua mchango wa wananchi kwamba kwenye maendeleo mchango wa wananchi ni mkubwa zaidi kama tungekuwa tunaweka kwenye mzani wa hali halisi wa kifedha, mchango wa wananchi ni mkubwa kuliko fedha nyingine zozote zile. Tungesema kweli ule mchango wa wananchi ambao wanatoa *in kind* wanaochangia nguvu, wanauchangia kifedha kwa kweli ni mchango mkubwa sana.

Kuhusu udhibiti wa wa fedha za Serikali kwa upande wa Serikali za Mitaa naomba niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge kwamba kwenye Serikali za Mitaa uwazi na uwajibikaji ni mkubwa zaidi. Mimi naweza nikasema ni mkubwa zaidi tukilinganisha na upande wa Serikali Kuu nikiwemo pamoja na mimi kama Wizara. Kule *transparency* ni kubwa sana kwa sababu kuanzia ngazi ya kijiji kama mradi haukufanyika barabara haikujengwa, zahanati haikujengwa kuonekana kwake ni rahisi zaidi kuliko miradi ambayo iko Serikali Kuu. Tukianza katika ngazi ya kijiji kuna Kamati ya ujenzi katika kijiji. Kamati ya Ujenzi ndiyo inayosimamia miradi yote pale kijijini aidha, mradi wa shule, aidha, mradi wa zahanati na kadhalika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, katika ngazi ya kijiji kitu kisipofanyika *watch dog* namba moja anayeangalia mradi huu unakwenda au hauendi ni mwananchi mwenyewe. Kwa hiyo, pale tunasema kwamba wananchi wenyewe ni ma-auditor ambao wanadhibiti hiyo miradi iende. Isipokwenda wananchi wenyewe utakuta wanaongea au wanapeleka Serikalini.

Niwape tu mfano mdogo tu kule Kagera kuna mradi wa *TASAF* ambao ulikuwa haukufanyika. Yule aliyepewa zile fedha pale pale kijijini wakaona wenzako mabadiliko tu amenunua TV, amenunua dish, amepiga bati nyumba zake. Wananchi wakajiuliza mwenzetu hela katoa wapi pale pale kijijini ikaonekana kwamba amechukua hela za

*TASAF*. Walichofanya wananchi pale wameita mkutano wa kijiji wakahakikisha kwamba wanang'oa bati kwenye nyumba wamechukua *TV*, wamechukua dish wamekwenda kuviuzwa. Kwa hiyo, ma-*auditor* ni wenyewe, maskari ni wenyewe, mahakama ni wenyewe katika level ya kijiji. Nataka kuwaonyesha tu uwajikaji katika ngazi ya Kijiji. Kwenye Halmashauri kama tunavyofahamu kuna Kamati mbalimbali, pia *audit committee* nayo inafanyakazi hiyo, baraza la Madiwani linafanyakazi hiyo, wapo wakaguzi wa ndani, wakaguzi wa nje, Kamati ya *LAAC*, *CAG* kwa hiyo, utakuta kwenye Serikali za Mitaa kuna *watch dogs* wengi zaidi.

Kuhusu suala la Kinondoni niunganishe hapo hapo ambalo amesema Mheshimiwa Halima Mdee jamani mimi nasema hivi tuwe tunaheshimu taarifa ambayo inatolewa na Mdhibiti na Mkaguzi wa Serikali. Kwa Kinondoni hoja zao ziko humu, hoja anazotoa Mheshimiwa Mbunge ni vyema akazileta na *evidence*. Lakini alichosema yeye na kilichoandikwa humu ni vitu tofauti.

Sasa je, tumsikilize Mbunge au tumsikilize huyo *CAG*? Kwa hiyo, mara nyingi tuwe tunafuata ambayo yanaandikwa kwenye vitabu.

Kwa hiyo, kwa upande wa Serikali za Mitaa mimi nasema kwamba tutazidi kuendelea kuwasimamia ili kuhakikisha kwamba *value for money* inapatikana. Niseme tu huko nyuma tulikuwa na matatizo mawili, tulikuwa na tatizo la vitabu vyetu kutowekwa sahihi. Mahesabu yalikuwa hayafungwi vizuri.

Sasa hivi kwa kweli kwa hilo tumefanikiwa ndiyo maana unaona kwamba vitabu vyetu vinafungwa kwa wakati na ni vizuri kwa sasa hivi hata wenzangu Kamati ya *LAAC* wanasema kwamba kuhusu vitabu sasa hivi hawana matatizo.

Tatizo lililopo ni *value for money* ndiyo maana tunashikiriana na Kamati ya *LAAC* na *inspection committee* katika Wizara yangu kuhakikisha kwamba kile kilichoandikwa na wenzetu kwenye taarifa za fedha kinalingana na kile kitu ambacho kinafanyika kule kwenye *grand* kama miradi mbalimbali na kadhalika hilo kwa kweli tunashirikiana kwa karibu sana Kamati ya *LAAC* kuhakikisha kwamba kule chini miradi inakwenda kama kawaida. Kwa hiyo, suala la ufungaji wa mahesabu kwa sasa hivi hatuna matatizo linakwenda vizuri, karibu Halmashauri zote zinafungwa kwa wakati na hoja nyingi za mkaguzi Mkuu wa Serikali sasa hivi zimepungua hata kama utaangalia kitabu cha mwaka jana na mwaka juzi vilikuwa vikubwa sana kwa sababu hoja zilikuwa nyingi zaidi lakini sasa hivi hoja zimepungua.

Kwa hiyo, kwa upande wa udhibiti wa fedha niliona niliongelee sana ili Waheshimiwa Wabunge waelewe kwamba kwa kweli tunalisimamia kwa karibu na kwa kweli tunatambua michango yao na tunatambua utendaji mzuri ambao unafanywa na Kamati ya *LAAC*. Kuhusu suala la fedha ile asilimia 20 ambayo inakwenda kwenye vijiji Waheshimiwa Wabunge ile asilimia 20 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida siyo kwa ajili ya fedha za maendeleo. Kwa hiyo, asilimia 20 inapotolewa kwenda kwenye kijiji ni kwa ajili ya fedha za matumizi (*OC*).

Baadhi ya sehemu ni kweli wametekeleza hilo la asilimia 20, lakini baadhi ya sehemu wameona kuna ugumu wa aina fulani kwa sababu zifuatazo, kwamba kwa mfano *OC* ya mwezi katika Halmashauri ya fidia ni shilingi 12 katika milioni 12 asilimia 20 ambayo inatakiwa kwenda kijiji ni shilingi karibu milioni 2. Sasa milioni mbili ukichukua uigawe kwa vijiji 100 au vijiji 70 unaona kwamba ni hela ndogo sana. Ukisema uwapelekee monthly ni kwamba unawapelekea unawaambia kwamba sasa hizi mzitumie kwa kitu chochote ambacho mnataka.

Kwa hiyo, baadhi ya Halmashauri wanafanya kama ku-accumulate kwamba ziwe nyingi ili wakiwapelekea pale wafanye kitu mmoja au wachangie kwenye mradi au wafanyie vitu ambavyo vitawasaidia katika kuendeleza ofisi zao. Wengi wanatumia hiyo asilimia 20 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za vijiji, mambo ya *stationary* na kadhalika. Kwa hiyo, tutaendelea kuwasisitiza kwamba hiyo asilimia 20 ni muhimu lakini tutapanga namna bora zaidi ya kupeleka hiyo asilimia 20 katika level ya vijiji ili tusiende kuzipeleka kule badala ya kuzitumia kwa makusudi yaliyotakiwa, watatumia kwa makusudi mengine. *(Makofi)*

Kuhusu asilimia 10 ya wanawake na vijana kwa kweli naishukuru Kamati ya *LAAC* wamewabana sana Wakurugenzi katika Halmashauri mbalimbali. Sasa hivi karibu asilimia 82 ya Halmashauri wameshatoa hizo fedha kwa ajili ya kuchangia miradi ya wanawake na vijana katika Halmashauri mbalimbali. Kikubwa zaidi ni kwamba fedha hizi badala ya kukopeshwa wanawake na vijana inaonekana kabisa kwamba wanawake wamerudisha hiyo mikopo lakini kwa upande wa vijana hawakurudisha hiyo mikopo kwa hiyo, nitoe rai tu kwa vijana ambao wamekopa mikopo hii waweze kurudisha ili iweze kuwasaidia watu wengi zaidi. Lakini kwa sasa hivi kwa kweli urudishaji siyo mzuri.

Nawapongeza akina mama wa Tanzania waliokopeshwa hiyo mikopo kwa kurudisha vizuri sana mikopo hiyo. Baadhi ya Halmashauri mikopo hii imerudishwa mpaka asilimia 85 lakini kwa baadhi ya Halmashauri wamerudisha asilimia 40, 50 kwa hiyo huo mfuko unalegalega kwa sababu ya kutokurudisha kwa fedha hizo. Hiyo asilimia 10 Waheshimiwa ikishatolewa mara moja kwa sababu ile ni *revolving fund* ikishatolewa mara moja ndio hiyo hiyo inaendelea kuzungusha kwenye ule mfuko.

Siyo kwamba kila mwaka zinatolewa hizo asilimia kumi. Mwongozo wetu ni kwamba asilimia 10 inatolewa *once and for all* siyo kila mwaka wanatoa asilimia 10. Hiyo asilimia 10 ni kutokana na mapato ya Halmashauri yenyewe *(own sources)* siyo *total budget* kwa hiyo, wengine wanachanganya kwamba lazima ni asilimia 10 ya fedha zote za Halmashauri hapana ni asilimia 10 ya makusanyo ya Halmashauri husika. Kwa hiyo, niziagize tu zile Halmashauri ambazo hazijafanya hivyo waweze kuchangia ili tuondokane kabisa na tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala mengine ambayo tumeshayachukua, tumeshaelewana na Kamati ya *LAAC* kwamba tunayafanyia kazi ili tuweze kuleta ufanisi katika Halmashauri zetu. Kwa yale masuala binafsi mimi nasema hivi Waheshimiwa Wabunge, ofisi yangu iko wazi namsikiliza kila Mbunge, naithamini kila hoja ya Mbunge

inayotolewa katika Bunge lako tukufu sitadharau hata hoja moja ambayo inatolewa na Mheshimiwa Mbunge.

Kwa hiyo, kama unaona kuna matatizo mimi nawaomba tuonane ofisini tuweze kulitatua, tuweze kulifuatilia kwa karibu zaidi ili tuone kwamba tunapata suluhu ya matatizo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri hujaunga mkono hiyo hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hii ni hoja ya Kamati kwa hiyo inapowekwa ndani ya Bunge ni hoja yetu sisi wetu wote.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ulionipa na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba niseme machache yanayotokana na taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali inayohusu Hesabu za Serikali za mwaka 2006/2007. Namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati hii Mheshimiwa John Cheyo pamoja na wanakamati wenzake kwa kazi kubwa ambayo kutokana na taarifa iliyo mbele yetu lazima wameifanya na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao wamepata fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali imetoa maoni na mapendekezo mengi ambayo ingawaje yameelekezwa kwenye hesabu za Serikali za mwaka 2006/2007 ni dhahiri kwamba bado mpaka mwaka huu 2008/2009 yanahitaji ama kushughulikiwa ama kuyapa tafakari ili kuboresha uandaaji na utoaji wa hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge katika mapendekezo yake imeanza kwa kutoa raia kwa Serikali kurudisha Kampuni ya *TANSORT* nchini kutoka London ni ile Kampuni inayoshughulikia Almasi ili mapato yanayotokana na kazi ya Kampuni ile yaweze kudhibitiwa na kubaki nchini na kuongezwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, na mimi ninaishukuru Kamati kwa ushauri huu na ninaihakikishia kwamba juhudi hizo zinaendelea na zitakapokamilika bila shaka Bunge lako Tukufu litataarifiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini maoni mengine na mapendekezo mengine ya Kamati yanahusu umuhimu wa kuongeza nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria za fedha na sheria za ununuzi na hili sote tunalikubali. Ni dhahiri ukitazama ripoti ile ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuna maeneo mengi ambayo hayaridhishi na tuna changamoto hapo kama Serikali na wasimamizi wa mapato ya Serikali kwa upande wa matumizi kuhakikisha kwamba matumizi yanafanya kazi kama yalivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine ambao unaendana na huo ushauri wa kupunguza matumizi ya Serikali ni ili kupunguza basi matumizi ya kawaida ya Serikali na tupate salio la kupeleka kwenye matumizi ya maendeleo, na tunakumbuka dhahiri kwamba katika bajeti ya mwaka 2008/2009 kwa makusudi Serikali ilifanya uamuzi wa kusema basi imetosha sasa matumizi ya kawaida yatalipwa na makusanyo ya ndani yanayotokana kwa sehemu kubwa na juhudi za *TRA* na tukaweza kufanya hivyo, na kwa kufanya hivyo, kilichotokea ni kwamba misaada yote basi ikawa sasa inaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo. Tunaamini kwamba ni muhimu tukaendelea na msimamo huo na matarajio yetu katika kuandaa bajeti ya mwaka 2009/2010 ambayo tunafanya sasa dhana hiyo ambayo ni ya msingi itazingatiwa. Ninaishukuru sana Kamati kwa kutukumbusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu Maafisa Masuuli ambao wanakumbushwa kutekeleza ushauri wa Kamati na pia ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu mambo mbalimbali ambayo yanakuwa yameibuliwa wakati wa ukaguzi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ama na Kamati yenyewe. Mimi ninakubali kwamba kutofanya hivyo ni uvunjaji wa Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 ambayo tumeipitisha hapa Bungeni na ukweli kwamba tusingetegemea kwamba jambo hili litaendelea ikiwa kuna mambo ambayo yameibuliwa na yanataka majibu basi ni vyema Serikali kupitia Maafisa ambao wanatakiwa kujibu wakajibu.

Kwa hiyo, ninakubaliana na Kamati ya Bunge kwamba kuna umuhimu wa kuongeza juhudi katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna pendekezo lingine na maoni ya umuhimu wa kusimamia mikataba ambayo Serikali inaingia hili pia bila ya kuwa na haja ya kulisisitiza ni jambo ambalo ni la msingi. Tumeona jinsi ambavyo mikataba ambayo imeonekana kwamba ina upungufu imetuenyesha, ninakubali kwamba jitihada ni muhimu kuchukuliwa kuhakikisha kwamba mikataba yoyote ile ambayo Serikali ama Taasisi za Serikali zinaingia mikataba ile isiwe na mapungufu ambayo dhahiri inapelekea kwa maslahi ya Taifa kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipitie upya mfumo wa kubakiza fedha katika maeneo ya makusanyo yaani zile *retention scheme*s ambazo zimepewa baadhi ya Mashirika yetu.

Jambo hili tumelianza katika Sheria ya Fedha kwenye Bajeti ya mwaka jana mwezi Agosti, ule na pale ambapo tulirekebisha Sheria mbalimbali za Mashirika na Taasisi mbalimbali kuwe na majadiliano kati ya yale Mashirika na Mawaziri wa Wizara mbalimbali na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ili wakubaliane ni kiasi gani ambacho kitalipwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na ili basi Taasisi na Mashirika haya yachangie zaidi kwenye Mfuko na kwenye mapato ya Serikali.

Tutaendelea na utaratibu huo. Ninashukuru kwamba katika taarifa ya Kamati wamekwenda zaidi ya kutukumbusha kwamba hili siyo suala la hiari ni suala linatokana na matakwa ya Katiba, ni suala la Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001, na kwa hiyo ni lazima kufanya hivyo.

Ninaihakikishia Kamati kwamba hili litafanyika na tutaendelea kuangalia sheria hizi ambazo zinasimamia Taasisi mbalimbali na Mashirika mbalimbali na kuona jinsi ambavyo tunaweza kuzileta Bungeni kuzirekebisha hili liwezekane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali irekebishe vifungu vya sheria vinavyokinzana kifungu kwa kifungu, lakini vilevile ambavyo vinakinzana na misingi ya utayarishaji wa taarifa za fedha.

Hili litawezekana kupigiwa hatua zaidi pale ambako tutakuwa tumeingia kikamilifu kwenye utaratibu wa kutengeneza na kutayarisha hesabu na taarifa za mahesabu ya Serikali kwa kutumia *International Financial Report standards*, na kwa hiyo, hapa siyo tu kutazama sheria zinazokinzana katika kutayarisha hizi taarifa, lakini vilevile ni kuharakisha na kuweka mfumo zaidi kwenye matumizi ya hizo *standards* nilizozisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuhakikisha kwamba takwimu sahihi zinapatikana kuhusu deni la Taifa. (Makofi)

Ninakubali na hili ni jambo la muhimu sana kwa sababu deni la Taifa lina mambo mawili. Kwanza, lina ile *principle* yenyewe na ule mtaji wenyewe ambao unakuwa umekopwa, lakini vilevile kuna riba mara nyingi ambayo inaambatana na ule mtaji wa msingi uliokopwa.

Lakini pamoja na hilo ni njia nzuri unapokuwa na takwimu ambazo zina uhakika kwamba unapunguza malumbano kwenye kitu ambacho unadaiwa ama ni nini ambacho unadai. Kwa hiyo, ninashukuru Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu kwa kutukumbusha jambo hili, na niseme kuwa ni jambo ambalo linafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Masuuli wasishinikizwe na wanasiasa katika kupanga matumizi ya fedha, na mimi ninakubaliana wasishinikizwe, na ninavyofahamu mimi…!

*(Hapa kengele ililia kuashirika kumalizika muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri hiyo ni kengele ya pili.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Ni kengele ya pili hiyo.

**MWENYEKITI:** Ndiyo**.**

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nilikuwa napata hamasa ya kuendelea kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ninaunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu ili aweze kuhitimisha hoja yake wakati huo Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa naye akijiandaa. Mheshimiwa John Cheyo tafadhali.

**MHE. JOHN M. CHEYO - MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kutoa shukrani nyingi sana kwa Waheshimiwa Wabunge jana kutusikiliza kwa makini kabisa.

Pia niliona kila mmoja alikuwa mkimya kabisa hii ndiyo inaonyesha kwamba mambo haya ambayo tulikuwa tunazungumza yalichukuliwa kwa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa utangulizi kwamba jambo hili la kudhibiti au ku-*oversight* ni jambo letu wote. Ni kweli Kamati zetu tatu ndiyo zinaenda kwa undani zaidi.

Lakini *Sector Committees* ndizo ambazo tunazitegemea sana kuhakikisha kwamba wanaifuatilia Serikali katika utendaji wa mambo yake yote na hii ni kazi ya Kamati ya Katiba, na mimi ninafikiri katika miaka hii mitatu ambayo nimekuwa Mwenyekiti naona Bunge letu linazidi kupata sifa sana katika kuifuatilia Serikali, tuendelee na utaratibu huu kwa sababu ndiyo wananchi wanategemea Bunge lao lifanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, mimi ninaona mambo yote ambayo tunazungumza bado hayajafikia tamati, sisi tungependa kufikia mahali ambapo haya tunayozungumza yaweze yakatumika wakati wa kutoa fedha kwa Maafisa Wahasibu, yaani isiwe mtu kila wakati hapati hati safi.

Kwa hiyo, *Sector Committees* wachukue basi ripoti zetu hizi, wachukue na ripoti ya *CAG* mnapompa huyo fedha kwa mwaka unaofuata muulizeni kwanza kwamba ni vipi hajatimiza hayo yote ambayo ameagizwa na *CAG* na ni vipi hajatimiza mambo yote ambayo ameelezwa na Kamati ya *PAC*.

Sasa kwa hiyo, tukifanya hivyo kama wazungu wanavyosema basi ripoti zetu hizi zitakuwa *instrument of budget* yaani inakuwa ni kigezo cha kumpa Afisa Mhasibu au Wizara fedha kwa mwaka unaofuata. Nimeona niseme hili kwa utangulizi.

Lakini jambo lingine la utangulizi ni kuwa Bajeti na fedha hizi ambazo tunazipitisha hapa na baadaye zinatumiwa na serikali, ni fedha za wananchi. Kwahiyo

ripoti kama ambayo tumefanya leo kusema kweli tulikuwa tunaripoti kwa wananchi kwamba 2006/2007 serikali muliwapa hiki na haya ndio matokeo yake. Kwahiyo mimi nataka kusema kwamba naushukuru sana uongozi wa Bunge kwamba kama kuna kitu ambacho mimi ninasema *is a tool for accountability,* yaani chombo ambacho kinaonesha uwajibikaji ni Bunge liko katika *TV*. Kwamba wananchi wanatuona tunavyojibu maswali na wananchi wanaona tunavyosema Serikali yao imefanya nini juu ya fedha zao. Hili ni jambo ambalo ni la maana sana na sisi tufanye nini juu ya fedha zao.

Hili ni jambo ambalo ni la maana sana. Na sisi katika Kamati ya *Public Accounts Committee ((PAC)* katika miaka inayokuja sasa tunajiandaa tunapokuwa tunawahoji Maafisa Wahasibu, tutafanya mbele ya kamera na nitaomba Bunge tutafute fedha ili haya yaonekane kama vile Bunge linavyoonekana.

Hili ndilo linalofanyika Uganda, Ghana, na sehemu nyingine ambazo tumepata fursa ya kuweza kujifunza. Niliona nitoe hayo maneno ya utangulizi; ripoti hii ni ya Bunge, ripoti hii ni ya wananchi wa Tanzania. Tuifanyie kazi, tuisome na nishukuru sana kwamba Wabunge, waliisikiliza kwa makini.

Mheshimwia Mwenyekiti, baada ya kusema haya naomba nifanye mambo ambayo ni ya kawaida. Kwanza natoa shukrani sana kwa watu wote ambao walichangia na kwa listi ambayo ninayo hapa waliochangia kwa njia ya kuzungumza, ni Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir ambaye ni Mwanakamati, Mheshimiwa Selelii, namshukuru sana, Mheshimiwa Rished Abdallah ambaye ni Mwanakamati, Mheshimiwa Jeremiah Sumari, ambaye ni waziri *incharge* wa karibu mambo yote ambayo tumezungumza katika ripoti yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Aloyce Kimaro na Mheshimiwa Issa Kassim Issa. Nawashukuru sana kwa kuchangia lakini kama unavyofahamu kusema kweli kulikuwa na wachangiaji wengi zaidi kwenye listi ambayo inaonesha kwamba waheshimiwa Wabunge wengi wangependa kutoa maoni juu ya mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama nikijaribu kujibu hoja, kwanza nianze na hoja ya Mheshimiwa Waziri ambayo ni mchango wake. Na hii niseme sitatumia muda mrefu kwasababu mengi Mheshimiwa Waziri umekubaliana na sisi na hili ninakushukuru.

Kwa hiyo, kilichobakia na hapa natoa kazia kubwa kwamba kama nchi zote za *common wealth* ambazo tumerithi, kuna utaratibu wa kujibu hoja zote za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa serikali. Kuna utaratibu wa kujibu mapendekezo ya Kamati ya Fedha za seriikali; mimi naona utaratibu huu tuufanye, ni jambo moja tu ambalo kila mwaka tunalizungumza. *It is called a treasury note* kwahiyo yule *Pay Master General* na sasa tumeweka ndani ya sheria ya ukaguzi anawajibika kujibu na ninajua Maafisa wahasibu wengi wanafanya vizuri katika vikao vyetu. Lakini kiujumla Serikali bado haijapata utamaduni huo ambao unahitajiwa na sheria. Kwahiyo mimi ningesisitiza hilo. Lakini nakushukuru sana umezungumza juu ya nidhamu ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli sisi inatusikitisha sana kwamba tunarudia mambo yaleyale kila mwaka. Hakuna risiti, hakuna vocha, tunataka kuondokana na hili, dunia yote imeshaondokana na hilo.

Wakati huu wa makompyuta na nini na kila kitu kusema kweli kukutwa kama mtu huna vocha inasikitisha sana na ndio maana inaleta mashaka kwamba labda huu ni wizi mtupu. Na kama unaweza kutengeneza hata risiti na baadaye zinaonekana ndio inaleta mashaka kila mahali. Mimi naona uwezo tunao na tumeona wengine wameanza kuondokana na hii kitu. Hatutaki kuona watu wamepewa masurufu hawarudishi, tuondokane na mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utegemezi. Hapa hatuna la kufanya ni lazima tutafute fedha ya ndani kila mahali. Kule tulikokuwa tunategemea na kwenyewe mwaka umewaka. Wale wenzetu wanaotusaidia hapa sasa na wenyewe wanakopa katika mabenki yao. Huwezi ukategemea Muingereza akope halafu aje akupe wewe msaada.

Kwahiyo hili ningeona ni changamoto kubwa sana ya serikali na muiwekee kila mikakati. Kila mahali ambapo tunaweza kupata fedha tukokotoe tupate, mikataba kama haitupatii pesa tuiangalie tupate. Mwenyezi Mungu ametupa uwezo na kila kitu cha kuweza kujitegemea na kuweza kupeleka misaada kwa baadhi ya nchi ambazo zamani zilikuwa zinatupa sisi misaada.

Halafu misaada jamani mimi nataka kuwaambia, zamani ilikuwa ni ufadhili; sasa misaada ni *control*. Mtu anakwambia usipofanya hili mimi sikupi fedha, hiyo ndivyo ilivyo na mimi sitaki kurudia iliyoonekana, jana tumepitisha Muswada lakini ukiuangalia Muswada ule ni *control* kwamba usipopitisha huu Muswada wa maji katika kipindi hiki kwenye bajeti hatukupi fedha. Sasa hii hatuwezi sisi kila mwaka tunatawaliwa kwa njia ya ujanja ujanja; tuweke umuhimu kwa jambo hili na tuna uwezo kabisa wa kuweza kupata fedha ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi Mheshimiwa amezungumzia juu ya *IPSUS*, sasa nimeambiwa na ninataka kutoa pongezi sana kwa *Accountant General* wetu pamoja na matatizo mbalimbali lakini ameweza kuelekea huko. Na niaambiwa kuwa ripoti ambayo tumepewa jana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali juzi, kwamba imeelekea upande huo.

Kwahiyo basi tukazane, kama kuna haja ya kumpa fedha zaidi, wataalamu zaidi, tufanye hivyo ili Serikali kila mwaka tujue, hivi *committment* zetu ni zipi? Sisi tumeangalia, unakuta Wizara inaomba bilioni 220, *committment* zake kwa mfano kama miundombinu ambazo zimeiva ni bilioni 220 sasa tutapata maendeleo ya namna gani? Kwahiyo hii hali tunapaswa kujua Serikali ina *committment* zipi? Hata tunapopitisha bajeti ijulikane kabisa kwamba hii kodi itakuwa ni bajeti ya maendeleo na sio bajeti ya kulipa tu yale ambayo tayari yameshafanikiwa. Mimi naona mengine yote nakubaliana na Mheshimiwa Waziri, deni la taifa na mambo mengine kwahiyo tunaomba tu asome ripoti yetu vizuri ili aweze kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mgana Msindai ambaye pia amechangia yeye zaidi amesisitiza umuhimu wa kwenda kuona miradi. Hili ni jambo la maana sana na sisi tumeenda kuona mradi kwa mfano wa barabara tumeshangaa. Watu munaanza na bilioni 51 munaishia na bilioni 126; mara mbili na ushehe kidogo!

Kwahiyo barabara moja imechukua fedha ya mabarabara mawili, sasa hali hii hatuwezi kujenga barabara za kutosha. Ni vizuri tukaenda tukaangalia na nina matumaini uongozi wa Bunge utatoa fedha nyingi sana kwa upande huu ili tuweze kuangalia miradi kweli inafanana na ripoti tunazopata? Kwahiyo namshukuru sana Mheshimiwa msindai.

Mheshimiwa mwenyekiti, Mheshimiwa Kimaro, nakushukuru sana pia na wewe ni mtu ambaye tumekuwa pamoja na ninakushukuru sana kwa mchango wako lakini zaidi umejikita katika manunuzi. Tuangalie manunuzi na pia umezungumzia juu ya mashangingi ambayo kwa maoni yako ni matumizi mabaya ya fedha wakati watanzania wanakula mlo mmoja kwa siku.

Kwahiyo Mheshimiwa Waziri Mkuu amesisitiza Benki Kuu na *EPA*, ujenzi wa majengo pacha na mambo kama hayo yote ambayo tumeshayazungumza katika kamati yetu.

Lakini hili la ununuzi ninataka kulisistiza kuwa 80% ya fedha yote ambayo inakwenda kwa ajili ya maendeleo ni ununuzi. Na mwaka jana tumetenga fedha karibu trilioni nne kwa ajili ya maendeleo na baadhi ya maendeleo na baadhi ya fedha za matumizi ya kawaida.

Kwa hiyo unapozungumza ununuzi miradi mingi ya barabara kwa mfano, na hili ninatumaini ndugu yangu wa upande wa mitaa ataliona zaidi, kwamba inachelewa na mara nyingine kwa sheria yenyewe. Kwamba una tenda miezi mitatu hupati, halafu hupati Makandarasi wazuri wanapoanza na wenyewe wanakimbia, unaanza tena miezi mitatu, mvua zinaingia, mwisho wa mwaka unajiona unajirudia mahali palepale. Lakini zaidi ya haya yote ni kwanini hatutumii utaalamu katika kuchagua wakandarasi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe kabla hujaanza kwa mfano barabara unafanya *bill of quantities*, unafanya *feasibility study,* sasa unakuta unashangaa kuwa unakuwa na mtu ambaye anakuja mkandarasi pale anakuletea bei ambayo iko chini kwa 50%, mwingine anakuletea bei ambayo iko 100% na mwingine anakuletea bei ambayo iko labda 10% au labda 20% chini au juu. Ukisoma sheria ya ununuzi na mtu yeyote ambaye amesoma haya mambo anajua kwamba kwa kawaida mtu yeyote ambaye kweli ni halisi hawezi akapita 10% juu au 105 chini.

Kwa  hiyo, ukitoa kwa mkandarasi ambaye amekupa nusu ndio matatizo hayo; kwanza atakimbia mradi na pili unaachiwa magofu kama yalivyo magofu mengi kwenye shule na tatu unaweza ukapata barabara ambayo haifai. Kwa mfano barabara ya Mwanza kwenda *junction* ya Shinyanga sasahivi tunajenga barabara upya.

Kwa hiyo, tunachotaka kusema ni tufuateni sheria kwa akili kwa vile tulivyofundishwa kwa misingi na tusione kwasababu ni rafiki au ni nchi rafiki kwahiyo unampa *contract.* Utampa *contract* mwishoni utajenga barabara mara mbili mara tatu. Kwahiyo kwa upande huu mimi ningeshauri kama Mheshimiwa Kimaro anavyosema kwamba hii ni *area* ambayo tunahitaji kabisa kuangalia; matatizo yote ambayo wameyapata Benki Kuu ni kwasababu ya sheria ya ununuzi kutofuatwa. Kwahiyo kwa hili naona ni kazia ambayo imetosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru Mheshimiwa Issa Kassim Issa. Yeye ameisadia sana Kamati juu ya jambo hili la *TBS.* Waheshimiwa Wabunge, nchi hii ni omba ombani kwanini tunafanya utaratibu ambao unatuondoshea fedha? Wewe unafanya utaratibu kila gari linapoingia katika nchi hii linalipa dola 150; kuna takribani magari 80,000 ambayo yanaingia kila mwaka. Ndio kusema nchi hii tunawapelekea Dubai tena kwa mfuko dola za Kimarekani takribani bilioni 62 katika utaratibu wote ambao *TBS* walikuwa wamejiwekea.

Tumeangalia *TTBS* mapato yake wanasema ni milioni 653 katika miaka mitatu ambayo wamefanya utaratibu huu, unatumia bilioni 62 kupata milioni 653! Mimi naona hii ni biashara ambayo sitaki kusema neno ambalo sio la kibunge, lakini ninyi wenyewe munaelewa. Na wala watu wetu hawakagui, unachotaka kujua tu ni *address* anakuletea ile *sticker* tayari biashara imeisha. Jambo hili tunaiomba Serikali isitishe mara moja; kwasababu ni mrija mkubwa wa kutuondoshea fedha. Tumetoa utaratibu, acha mtu alete gari lake kama ni bovu ni nini liingie. Likishaingia hakuna kuliandikisha mpaka limekaguliwa na *TBS* na analipa hapa hapa. Kama ni dola 150 basi alipe hapa hapa yawe ni mapato ya Serikali na sio kuchukua mkoba unapeleka mapato Hongkong, unawapelekea watu Dubai halafu unaanza kuomba omba kwa Muingereza tafadhali nisaidie barabara. Jamani hebu komesheni jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kwamba sasa wameona ni utamu pale wanataka bidhaa zote za nchi nzima zinazoletwa hapa na zenyewe zikaguliwe huko huko. Na ukaguzi tutakagua namna gani? Ninyi Waheshimiwa Wote mumetembea hebu niambie kama unaenda Japan kweli Japan utaenda vipi na gari gani kwenda kukagua kitu gani? Kwasababu ukienda tu na gari kutoka *Movenpick* mpaka Kilimanjaro, inakuchukua masaa mawili; mtu yeyote ambaye anajua ni msongamano ulivyo. Leo niambie nyundo inanunuliwa pale, mshumaa unanunuliwa pale, sijui taulo linanunuliwa pale, na hiki kingine kimenunuliwa pale, fanicha inanunuliwa pale, ni nani atakayeweza kufanya ukaguzi wa mambo haya? Tutarudi hukohuko.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ninyi wenyewe mulishaona jinsi mulivyokuwa munapoteza fedha kwa kutumia *SGS* na *COTECNA* tukafuta ile. Tukaona nkwamba mambo yote yanayokuja Tanzania yatakuwa *inspected at the destination* hapo hapo kwenye *port* na kama kuna nini tutafanya hapohapo na imefanyika. Na hiyo tumechukuliwa hela nyingi kwa miaka mingi, sasa ndugu zangu wameonja kwenye magari wameona ah aah, kumbe nchi hii imelala twende tena hata kwa bidhaa zote. Mwaka jana tumeagiza karibu trilioni nne za bidhaa mbalimbali. Na mnajua zamani

tulikuwa tunachajiwa 1%, kama tukienda kwa utaratibu wa namna hii *four trillion point eight* hizo ni dola. Kwahiyo itakuwa ni fedha nyingi sana, sisi tume-*calculate* zaidi ya bilioni 65 tutakuwa tunapeleka mwaka hadi mwaka kwa watu sijui Dubai wengine sijui Hongkong; wewe omba omba ni kwanini usiziangalie pesa zako nchini ukazitumia kwa barabara, ukazitumia kwa shule? Mama leo ametuambia kwamba hana fedha ya kulisha watoto wa shule, anahitaji bilioni 29 amepewa saba. Lakini wewe kwa nguvu kabisa unabeba furushi la fedha unampelekea mtu Hongkong bilioni 65, bure tu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunasema bidhaa ziingie zikishapita tu pale kwenye *port* zinaandamana na mtu wa *TBS* zinaandamana na Kamishna wa *Fare Trade*, zinaandamana na polisi, kama ni feki zinateketezwa na wewe unashitakiwa palepale. Na baadaye sasa tukiziona mule tujue kwamba hawa watu wa *TBS* na watu wengine hawakufanya; hakuna uopotevu wa fedha. Jamani yaangalieni haya mambo, kuna watu wengine kazi yao ni kutumia sheria tunazotunga hapa kujilimbikizia fedha na hakuna hata uwazi. Haya ndio mambo ambayo yanalitwa ufisadi, haya ndio mambo ambayo yanaitwa rushwa na vitu vingine. Mimi nina hakika tunaweza tukaisaidia nchi hii vizuri kabisa kwa kufanya haya mambo. Mtu mwingine aliyechangia kwa kusema alikuwa ni Mheshimiwa Selelii, lakini Mheshimiwa Seleli zaidi amejikita kwa upande wa mwenzangu ambaye nitamuachia nafasiila tu nataka kusisitiza jambo moja ambalo Mheshimiwa Seleli amelizungumza, *Internal Auditor*. Yeye alikuwa nashauri kwamba basi *Internal Auditor* awe chini ya *CAG*. Mimi naona hii kitaalamu labda Waheshimiwa Walio *Accountant* watalieleza hili vizuri zaidi lakini kitaalamu hili halikubaliki. Manaake *internal Auditor* ni *instrument* ya ndani ya kuwashauri watu wa ndani ili wajiandae hata wakati ambapo *external auditor* akija atakuwa ameweka mambo yote bayana. Lakini mimi naona kuna mantiki ya kuliangalia hili jambo ni jinsi gani labda huyu mtu anaweza akaambatanishwa na *Accountant General*. Kwahiyo yule Mhasibu Mkuu awe ndio kiongozi wa *Internal Auditors* wote katika nchi nzima, labda hili linaweza likasaidia.

Baada ya kusema hayo kwasababu muda hautoshi, mimi nilikuwa nataka kutumia nafasi hii kuwashukuru wote ambao mumechangia. Na sasa sijui nitoe hoja sasa iungwe mkono? Kwahiyo kwa Mujibu wa Kanuni namba 89(1) ya Kanuni za Bunge toleo la 2007 naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lipokee na liikubali taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo kwenye taarifa hiyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za seriikali, John Momose Cheyo, kwa kuweza kuhitimisha hoja yake. Na baada ya kuihitimisha naona Waheshimiwa Wabunge, mumeiunga mkono hoja hii, wengi wajumbe wa Kamati na hata wasio wajumbe wa

Kamati. Kwahiyo hoja hii naona imepata uzito wa pekee. Sasa baada ya hoja hii kutolewa na kuungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge, sasa nitapata ridhaa ya Bunge zima. Nitatumia nafsi hii sasahivi baada ya kupata ridhaa yenu kuwahoji. Waheshimiwa wabunge, ninaomba kuwahoji kwamba Bunge sasa lipokee na kuikubali taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo kwenye taarifa hiyo.

*(Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali ilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kusema hoja hii imeungwa mkono na imepitishwa rasmi. Basi nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wajumbe wa Kamati, Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla na tuiombe Serikali sasa kuyapokea hayo mapendekezo na maoni yaliyotolewa ili muweze kutusaidia, kuyasimamia na kuyafanyia kazi kwa mujibu wa sheria za nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana na sasa tutaingia kwenye hoja ya pili. Ninaomba sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, ili naye aje aweze kuhitimisha hoja yake na baadaye tutaendelea na hatua nyinginezo. Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa. *(Makofi)*

**MHE. WILLIBROD P. SLAA – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nihitimishe hoja yetu ambayo niliitoa jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nihitimishe kwa kuwashukuru sana sana Waheshimiwa Wabunge, ambao katika ujumla wao wote wameiunga hoja hii kwa michango ambayo imetolewa kwa kusema na kwa michango ambayo tumepokea kwa maandishi, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, nitamrudia baadaye kwa jinsi alivyotusaidia katika kujibu baadhi ya hoja.

Kwa kufuatana na utamaduni wetu wa Bunge naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge, waliochangia hapa ndani ya Bunge kwa kusema, nao ni Mheshimiwa Msindai, Mheshimiwa Lucas Seleli, Mheshimiwa Rished Abdallah, Mheshimiwa Hilda Ngoye, Mheshimiwa Halima Mdee na hatimaye alikuwa Mheshimiwa Selina Kombani, Waziri wa Nchi – *TAMISEMI. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi nao pia ni Mheshimiwa Msindai, Mheshimiwa Bernadetha Mshashu, Mheshimiwa Halima Omar Kimbau, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Martha Umbula na Mheshimiwa Anna Chaurembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Mwera Charles Nyanguru, Mheshimiwa Juma Kilimbah, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Suzan Lyimo na Mheshimiwa Beatus Lyamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyoona pamoja na muda kuwa mfupi kwa kweli Waheshimiwa Wabunge, wametusaidia sana katika kuboresha hoja yetu kwa kuchangia kwa maandishi pamoja na kwa kusema hapa Bungeni, naomba nirudie kuwashukuru wote. nitaomba nigusie hoja za jumla ambazo zimetoka kwa pande zote na kwa waliozungumza pia hapa Bungeni. Hoja hizo zimejikita katika maeneo kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja moja ambayo imetoka pande zote ni hoja ya ubora wa vitabu ambayo inaendana na uaminifu na uadilifu wa watendaji. Naomba nimshukuru Mheshimiwa Kombani, ameshalieleza hili pia, kwa kifupi sana niseme ni kweli vitabu vyetu vimeonekana kuboreka. Vitabu vyetu vimeanza kuandikwa na kama tulivyosema jana vitabu vinapoandikwa vizuri hati safi inapopatikana ndio nafasi kwetu sisi Bunge pamoja na madiwani sio sana kushangilia, kwasababu hati safi ni hatua tu moja katika kuonesha kilichoko ndani. Ni sawa na nyumba inayokuwa nzuri, unaiona nzuri kwa nje lakini milango imefungwa na hujui kuwa ndani kuna nini. Ukifungua milango unaanza kuona kilichoko ndani, labda kama kuna buibui, labda haifagiliwi, labda haifanywi nini. Na hiki ndicho tulichogundua katika ukaguzi wa vitabu hivyo. Kwamba sasa vitabu vinaandikwa, nyaraka nyingi zinawasilishwa mbele ya Kamati, tunapitia kila waraka unaowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani unaona bati ziko ngapi zimetumika katika kujenga chumba cha darasa. Lakini kama haikuandikwa vizuri huwezi kujua bati hizo zimetumika vizuri au hapana. Kwahiyo sasahivi ninaomba sanasana Waheshimiwa Wabunge ambao wanaingia kwenye Halmashauri, tusiishie kuridhika na hati inayotolewa na *CAG* kwamba ni hati safi. Na kwa hapa ninaomba nitoe tahadhari, sisi kwenye Kamati tumemuhoji sana *CAG*, kwamba hati yako safi maana yake ni nini? Akatupa mambo mawili mazito sana. la kwanza anasema yeye anafanya *sample auditing,* hakagui kila karatasi, nakagua yale aliyokabidhiwa. Kwahiyo suala la yale ambayo hakukabidhiwa yeye hawezi kuliona. Ni kazi ya mwenye mali ambaye ni Halmashauri pamoja na Kamati yetu kwa niaba ya Bunge kuingilia yale ambayo yeye hakuyaona. Kwahiyo ni jukumu letu Waheshimiwa Wabunge, kuliona hilo.

La pili akatuambia kwamba yeye katika ukaguzi wake anakagua mfumo, hatafuti wizi, hatafuti ubadhirifu, hatafuti matumizi mabaya. Kazi hiyo ni ya mwenye mali na mwenye mali ni Halmashauri kwa maana ya madiwani na Kamati za Bunge kwa niaba ya Bunge zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo tumefarijika kupata hilo na kwa kweli tulichogundua katika kupita katika maeneo mbalimbali ni kuona yale aliyosema *CAG* ni ya kweli kwamba yeye ameandika vizuri, Halmashauri ina hati safi, lakini ndio ile aliyokuwa amesema mmoja wetu hapa kwamba unaenda kwenye eneo bati zinazotajwa kwenye kitabu ni 70, lakini kwenye jengo lenyewe ziko bati tatu tu. kwahiyo haya ndio

yanatusaidia kuona ni kitu gani sasa tunahitaji kufanya baada ya kuwa vitabu vimeanza kuwa vizuri.

Sasa jana nilitoa tahadhari kwamba kwa bahati mbaya Halmashauri zilizoanza kufikia mahali pazuri, na tukapata Halmashauri 100 mwaka huu kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008 zimepungua.

Tunaomba sana Halmashauri na hasa watendaji wawe makini, waandike vitabu vizuri, tulitegemea kwamba mwaka huu hakuna Halmashauri tena itapata hati isiyoridhisha lakini bahati mbaya zimepatikana Halmashauri kadhaa. Tunaomba sana tujirekebishe katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la uaminifu na uadilifu katika matumizi ya fedha za umma. Nalo limesemwa sana na wote walioandika na hata waliozungumza kwa mdomo. Na hili niliunganishe na suala la usimamizi wa fedha.

Ni kweli kwamba kwa kiwango kikubwa sasa fedha zinaanza kusimamiwa; hili ni lazima tuliseme. Kwa kiwango kikubwa fedha zetu zimeanza kusimamiwa, matumizi yameanza kuonekana kwamba ni mazuri katika maeneo mengi.

Lakini kama tulivyosema jana maeneo machache bado kuna wazembe wachache, na nilitumia neno wazembe wachache. Na hawa wazembe wachahce tusiwaache kuharibu kazi nzuri inayofanywa na asilimia kubwa. Na sisi katika ngazi ya Halmashauri hasa maana ya Wenyeviti na Madiwani, na sisi kwenye kamati na sisi kama wabunge lakini na Mheshimiwa Waziri wetu, tusaidiane katika kuwashughulikia ipasavyo kwa mujibu wa sheria hao wazembe wachache.

Hatuwezi kuwaacha hao wachache wakaharibu kazi nzuri inayofanyika, wakaharibu matumizi ya fedha nyingi zinazopelekwa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu na haya yakaonekana kuachwa.

Nitoe pia tahadhari hapo kwamba, jana CAG ameeleza kwenye taarifa yake kwamba, hili tutalisema sana mwaka kesho, tumeligundua pia mwaka huu na tumelikemea sana kila mahali kwamba, kuna utamaduni sasa fedha zinafika kwenye ngazi ya Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa shule, zahanati, barabara ambazo ziko vijijini; fedha zile zinahamishwa. Kwa hiyo, Halmashauri imebaki kuwa *clearing house*, hili ni jambo la hatari sana. Halmashauri haiwezi kuachwa ikawa ni *clearing house*, kwa maana ya kwamba, inapokea kutoka Hazina inahamisha ilivyopokea inaripoti kwa CAG kile kilichohamishwa, huu siyo ukaguzi hata kidogo. Ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge, mkirudi kwenye Halmashauri zenu, mtaona kitu cha ajabu kwenye taarifa zinazoletwa; watakuwa wameandika kwenye taarifa zao ukaguzi, sifuri, sifuri, iliidhinishwa labda laki saba na senti, ilitolewa laki saba na senti hamsini, zimetumika laki saba na senti hamsini. Haiwezekani kwa akili yoyote ya kawaida kwamba, iliyoidhinishwa miezi tisa kabla ikaenda kutolewa hivyo hivyo na ikatumika hivyo hivyo. Kwa wataalamuu wa fedha, hiyo peke yake ni dalili ya wizi. Kwa wale wanaojua mahesabu, katika enzi za kikoloni senti inamfunga mtu na senti tano ya fedha isipo-

*balance* maana yake kuna mamilioni nyuma yake yamefichwa katika senti tano ile. Kwa hiyo, tuwe wakali; sisi kama Kamati kwa niaba yenu, tumekuwa wakali na kwa kweli Halmashauri wanajua sisi ni wakali katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo ambalo jana katika ripoti labda kwa sababu ya muda sikulipata, kwa kuwa limehojiwa naomba nitumie nafasi hii kulifafanua vizuri. Suala la usimamizi liko maeneo mengi sana, lakini nitaje mawili ambayo ni makubwa; matumizi ya fedha katika magari ya Serikali hatujaona kama ni mlango mkubwa sana wa ufisadi na uwizi. Katika idara moja unakuta mafuta yaliyotumika ni mengi na niwape mfano; kwenye Halmashauri siikumbuki kichwani, sasa tumepiga hesabu ya lita zilizotumika kwa Halmashauri moja tu kwa mpango mmoja tu sio kwa idara zote za Halmashauri kwa mpango mmoja tu; lita zilizotumika zilikwenda kilomita yaani ukitumia ile *average* ya kilomita nadhani wataalamuu wanajua lita moja kwenye gari la kawaida zinakwenda kilomita sita. Kwa *average* ile ukitumia kilomita zilizotumika kwa mafuta yaliyotolewa ni sawa na kilomita 85,000 kwa programu moja; huwezi kupata kilomita 85,000, kilomita 85,000 ni kwenda London na kurudi zaidi ya mara ishirini. (*Makofi*)

Kwa vyovyote vile hapa kuna maswali, kwa hiyo, tumekuwa wakali na kwa *audit* zinazokuja wajiandae kwenye eneo la mafuta tutaendelea kuwa wakali zaidi; kwa sababu haiwezekani kila mpango ukawa na kilomita nyingi sana. Haiwezekani mpango mmoja tu ukawa na fedha kwa kilomita hizo hata kama ukubwa wa Halmashauri ile unajulikana. Tumeanza kuomba taarifa pia ya *distances* katika Halmashauri, lakini kuna taarifa ambayo nashukuru pia na *CAG* ameiona jana; kuna hesabu ambazo hazifungwi na hizi tutaomba ushirikano mkubwa sana kati ya Hazina na idara zote zile zinazotoa fedha kama zinapita TAMISEMI, sina hakika lakini sisi tumegundua hasa inatokea Hazina kwenda MSD.

Kinachofanyika hapa ni kwamba, fedha zinapelekwa MSD, Halmashauri hazijulishwi kwamba imepelekewa fedha kiasi gani. Wakurugenzi tunasukumana mpaka tunawaambia msiondoke hapa, nendeni MSD kwa miguu mkahakikishe shilingi zenu ni ngapi; wanakuta wana milioni 200, milioni 300 lakini wenyewe walikuwa hawajui na wananchi hawapati dawa. MSD hazipeleki *statement*; hii ni hali ya hatari. Jana tulikuwa tunazungumza na CAG akatupa pia kitu ambacho ni *serious* zaidi; dawa hizi zinapochukuliwa haziingizwi kwenye *register* ya Halmashauri, mwisho wa mwaka hakuna *stocktaking*, kuna kelele za wananchi ambazo tunazisikia lakini tusizidharau kwamba, dawa nyingi zinaondoka kwenye *store* zetu zinaenda kwenye maduka binafsi.

Sasa hizi tumezikuta; kwa mfano nadhani ni Halmashauri ya Hanang', tumekuta vitanda vya hospitali havina *bed sheets*. Tumekwenda tukauliza ziko wapi wakasema ziko *laundry*, tumeenda *laundry* tukakuta zipo tatu, *laundry* wanasema ziko *store*, tukakuta maboksi mawili tu; Shuka mpya kabisa haizafunguliwa, tukasema na hili box la pili ambalo liko wazi liko wapi; hatukuziona. Sasa hali iko hivyo hivyo kwa dawa ambazo hazina *stocktaking, register* hazitunzwi. CAG amesema tuna tatizo kubwa katika eneo hilo na nadhani TAMISEMI mtusaidie kuweka maelekezo yaliyo wazi kwa

Halmashauri ili tunapokagua sisi na ninyi twende katika lugha inayoeleweka na tukubaliane kwa pamoja. *(Makofi)*

Hapa pia ni dhana ambayo ameieleza mwenzangu Mheshimiwa John Cheyo, dhana ya *internal auditor;* tunaposema haya yafanyiwe ukaguzi; tunayetegemea afanye ukaguzi ni *internal auditor,* ndiyo anapaswa kuwa jicho la Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya sisi pamoja na CAG kuomba *internal auditor* aondolewe chini ya Mkurugenzi, kwa sababu *internal auditor* amekuwa sehemu ya Halmashauri; anashiriki kwenye maandalizi, anashiriki kutengeneza zile nyaraka hata ikiwa lazima kuzikarabati usionekane wizi anashiriki; na tumewagombeza sana katika sura hiyo. Tunao ushahidi na tumewaambia hapana hii hatuwezi kuvumilia; sasa jibu haiwezekani tu kuwa wakali na kuwakemea, jibu ni kuwatengenezea mfumo ambao unawaruhusu wawe huru. Namna moja ya kuwa huru sio chini ya CAG, tukiweka chini ya CAG tutakuwa tumefanya makosa kwa sababu watakuwa wanaingiliana wale wale ambao tena ni wakaguzi; lakini nikiwaweka chini ya *Accountant General*, ambaye ni Mhasibu Mkuu wa Serikali; huyu anapaswa kukagua kutoka juu mpaka chini.

Kwa hiyo, akiwekwa kule atakuwa huru, hafungwi tena na Mkurugenzi na kutokea hapo hawi tena kwenye Kamati zile anazopaswa kuwa kama Katibu wa Kamati ya Tenda. Kamati sijui ya nini kule kwenye Halmashauri, kama Ofisa wa Mkurugenzi hapa tutasaidia fedha nyingi zinazokwenda kule chini. Tunaiomba sana Serikali, ikiwa lazima Mheshimiwa Waziri wangu akubali, afanye utafiti wa kina aone tunacholalamikia. CAG analalamika lazima kuna sababu hapa, haiwezekani upokee malalamiko kutoka sehemu mbili tofauti na hasa sisi ambao tunaenda *field* halafu kusiwe na tatizo zito hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona tatizo kubwa la kuchelewa kwa fedha za miradi na hili limelalamikiwa na Waheshimiwa Wabunge; miradi yao haikamiliki. Hapa kuna mambo mawili:-

La kwanza, sisi huwa tunauliza kwa nini fedha zimebaki na kama mnakumbuka; jana katika taarifa mpya ya CAG, kuna bilioni 99 zimebaki hazikutumika kwa mwaka huu unaomalizika; sasa hili huwezi kulaumu upande mmoja tu. Kuna sura kadhaa hapa, sura ya kwanza, Serikali inapokea fedha kutoka kwa wahisani zikiwa zimechelewa; sasa zikishachelewa ni wazi kwamba, haziwezi kutekelezwa kwenye mwaka ule wa fedha.

Pili, hata yule anayepokea Serikalini labda Hazina mpaka afuate *bureaucracy* ya kawaida ya Serikali kupeleka TAMISEMI, kama anapeleka TAMISEMI au Wizara ya Elimu ile inachukua muda na fedha nyingi tumezikuta zinafika tarehe 25 ya Juni. Sasa fedha zikifika 25 na tunawataka waandike tarehe ya kupokea na wanaleta kwetu nyaraka wamepokea tarehe fulani, kwa hiyo, hatubahatishi pale kwamba, zimebaki kwa sababu zimefika zimechelewa. Sasa katika hili, mtusaidie sana Serikali; miradi mingi; bilioni 99 itafanya *difference* kubwa sana katika miradi yetu. Athari yake kubwa ni nini na hili amesema tena CAG; athari kubwa kabisa ni kwamba, hatuna *system* ya kutambua hizo fedha kwa mwaka ujao wa fedha, kama zinatumika kweli hizo 99 bilioni na kama zinatumika tunaziona wapi. Tumewasukuma sana Wakurugenzi wetu, watuletee taarifa

ya mwaka unaofuata, lakini kwa kuwa hakuna bajeti ya mwaka unaofuata wa fedha hizo, hatuna namna ya kudhibiti kama kweli zilitumika kama zilivyopangwa.

Kwa hiyo, tunaomba TAMISEMI kwa hili mtusaidie kuweka maelekezo; je, zile zinazobaki bilioni 99 kwa mfano zinaingiaje mwaka unaofuata ziwe *budgeted* kwa mwaka unaofuata au zitengenezewe utaratibu gani ambao hata sisi tunapokagua na CAG anapokagua, aweze kuona kwamba zinakagulika. Hili ni suala ambalo tusipoliangalia fedha nyingi zitapotea, hakuna atakayejua zinakwenda wapi na miradi yetu mingi itakuwa imekosekana. Halmashauri nyingi kushindwa; hili limesemwa pia na Waheshimiwa Wabunge, naomba nikazie tutakuwa wakali kwa niaba yenu Wabunge mtuelewe hili; tumeeleza kwa kifupi jana kwa sababu Halmashauri hushindwa kesi nyingi kwa jinsi tulivyozigundua katika nyaraka. Kesi inafunguliwa mtu anasemekena ametuhumiwa kuiba fedha kwa njia fulani, kwa udanganyifu wa kalamu au sijui kwenye mkataba au sijui kwa njia gani anapelekwa mahakamani.

Watumishi wa Halmashauri wanaokwenda kusimama kwa niaba ya Halmashauri, hawaendi kwenye kesi, tutahitaji kujua kwenye kesi walienda mara ngapi na hata wakienda tunataka kujua vilevile wamepeleka nyaraka zipi, kwa sababu kwenye kesi nyingi nyaraka hazipelekwi. Kwa hiyo, tunashindwa kesi tunapoteza mamilioni ya pesa, kumbe kuna ushirikiano; anayesimama mahakamani ni mwenzake yule aliyekula fedha. Sasa ulitegemea kitu gani, kuna mtu alieleza hapa ni kesi ya ngedere kwenda kwa nyani. Kwa hiyo, tunaomba tusaidiane, kila mmoja katika idara kwanza awe na maadili yanayostahili, lakini pili, tusimamie. Hili tunawaomba sana wanasheria, wasimamie vizuri masuala ya kesi katika Halmashauri zetu.

Suala la taarifa ya mapato na matumizi ni tatizo la msingi; tumeona kwamba fedha nyingi sana zinachangwa na wananchi wapo tayari kushiriki wanaposhirikishwa katika miradi yao; iwe ni elimu, iwe ni zahanati au barabara, lakini wanataka kuona matunda, inapofika mahali hawaambiwi fedha zilizokusanywa ni kiasi gani na mahali pengine zinakusanywa hata risiti hazitolewi.

Hawasomewi kiasi gani kimekusanywa, zimetumika kiasi gani; ni wazi wataona kwamba, hatuna sababu ya kuchangia na hiyo imetokea kwenye jimbo langu; wanasema kwa nini tuchange wakati tulizotoa nyuma hatuoni ziko wapi. Kwa hiyo, naomba TAMISEMI mtusaidie na sisi kwa upande wetu kama Kamati, tunaweka sharti tunaongeza mzigo kwa Wakurugenzi bila mwongozo kutoka kwako Mheshimiwa Waziri, haitasaidia. Tumewaomba kila wakati watuambie ni vijiji vingapi vimesoma taarifa ya mapato na matumizi, hii itasaidia katika kuwasukuma. Kwa hiyo, Mkurugenzi anapokuja kwetu ni lazima ajue ni vijiji vingapi katika mwaka ule vimesoma taarifa ya mapato na matumizi. Ukiweka maelekezo kwa Mkurugenzi itatusaidia na kututia nguvu ili kuwe na maelekezo yanayofanana kwa nchi nzima.

Bila hiyo, wananchi wetu watafika mahali watachoka watakataa kuchangia, jambo ambalo kwa kweli kwa jinsi walivyochangia sasa wanahitaji pongezi kubwa sana. Unakuta Serikali imechangia darasa moja, katika madarasa manne, mengine yote

wamejenga wao. Sasa sisi hata lile moja tulilowasaidia ili tuweze kutambua ile nguvu yao waweze kurejeshewa pia na taarifa ya mapato na matumizi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lililolalamikiwa na Wabunge wangu ambao wamechangia kwa maandishi na hasa Mheshimiwa Lyamba, ni suala la kuhamisha watendaji wabovu kwamba; ameharibu hapa halafu anahamishwa anapelekwa kwingine. Kwenye Kamati yetu, Mheshimiwa Lulida sijui kama yupo; amefika mahali anasema nchi hii watendaji wanaoharibu sasa wamefanya mahesabu kwamba kila akiharibu mahali anapelekwa Lindi, anapelekwa Kilwa, anapelekwa sijui wapi, sasa kwa nini wanapelekwa siwezi kujibu. Mheshimiwa Lulida amefika mahali anasema, sasa ukanda wetu unageuka kuwa magereza ya watu wanaoharibu. Tunaomba sana kwa hili tusishirikiane watu wawili, tunaomba tushirikiane kwanza Madiwani, Wenyeviti wa Halmashauri na Madiwani wao, kwa sababu mtu anayeharibu anajulikana pale kwenye Halmashauri.

Ni jukumu lao kumchukulia hatua kwa mujibu wa kanuni zinazoongoza Halmashauri, usianze kusema sasa TAMISEMI wamchukulie hatua. TAMISEMI ni hatua ya mwisho sana lakini ninyi kwanza chukueni hatua, fuateni taratibu zote za kinidhamu. Kamati za Fedha zote katika Halmashauri na katika Manispaa ni mamlaka ya nidhamu; sasa mkianza kusema TAMISEMI mhamisheni; mnampeleka wapi; mwisho mnapeleka kansa na kama kawaida yake kansa haiachi. Tuna ushahidi wa mtu ambaye mahali palikuwa pabaya, ameenda mahali ambapo ni pazuri; alipofika tu kule kukawa kubaya; sasa unahitaji kutafuta ushahidi gani wa zaidi hapo? Kwa hiyo, ninaomba sana katika hilo, kwa sababu ya muda nigusie maeneo machache tena moja moja.

Kuna hili suala la asilimia 20 na asilimia 10 ya wanawake, Mheshimiwa Waziri amelijibu vizuri. Kamati yetu kwa niaba ya Bunge, imekwisha kutoa maelekezo. Mheshimiwa Waziri, nakushukuru sana kwa kauli yako ambayo kimsingi imeungana na kauli yetu na kwa asilimia 20 tumetoa *deadline* walipwe mpaka tarehe 30 Desemba, kwa sababu kule ndiyo tunakotaka kuondoa umaskini. Umaskini uko kule vijijini, sasa umekaa na asilimia 20 ya watu wanahitaji kujenga shule zao, wanahitaji kujenga ofisi, wanahitaji kujenga madarasa; wapelekewe waweze kujenga madarasa yao. Kwa hiyo, hilo tumesisitiza na Kamati yetu haina huruma katika hilo, wale waliopita mbele ya Kamati wanajua na watakapokuja tena safari hii watajua, tutaendelea kuwa wakali zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Selelii, ametusaidia sana, tunamshukuru sana amesema, kazi ya Kamati hasa kwenda kutembelea ni nzuri. Mheshimiwa Selelii, tunakuthibitishia ni kweli kazi hii tumeifanya tumeona mambo ambayo hatuamini, tumekwenda Manispaa ya Morogoro, kwa macho yetu kabisa tuliona tunadanganywa kwamba, wametengeneza mtaro wa umwagiliaji kilomita 1.5, lakini kwa macho tunaona tunaambiwa kumbe umeishia kwenye kona pale mita 7. Kwa hiyo ni mambo ambayo katika *performance audit, site visitation* ni muhimu sana kama tunataka kupata *value for money.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taarifa yetu umeona kule nyuma, zahanati ina gharama ndogo kuliko choo; hivi zahanati gani hii inakuwa na bei ndogo kuliko choo

acha ile ya bati 70 ambayo nimeeleza? Tumekuta hizo nyingi tu, anacheka rafiki yangu nafikiri kule kwake tulikuta mambo ya namna hiyo. Kwa hiyo ni sura hii ambayo tunasema tusaidiane Waheshimiwa Wabunge, wakati mnatembelea kwenye maeneo, ombeni taarifa kwa Halmashauri ya miradi iliyokwenda kwenye eneo unaloenda kutembelea. Chukua ile taarifa nenda kakague, utakuta kitu hakipo kabisa; kama utafanya hivyo mara mbili, tatu, wataogopa kwa sababu watajua tunagundulika. Mheshimiwa Waziri, tusaidie ile timu yako inayokwenda tunaomba uongeze wataalamu. Tunaongeza pia safari zao waweze kukagua, tukishafanya kazi hii labda kwa miaka mitano ijayo, watu wote tutarudi kwenye mstari hatutahitaji tena *site visitation*. Tukifanya kwa miaka mitano, inawezekana huko mbele hatutahitaji tena. Kwa hiyo, tunaomba katika hatua hii ya awali, tuweze kushirikiana tuondoe udhaifu huu mkubwa.

Mheshimiwa Selelii, ametoa pendekezo zuri sana Waziri tunakuachia; la namna gani sasa hizi taarifa ziingie kwenye *District Consultant Councils*, pamoja na RCC kwenye mikoa yetu. Nadhani ni muhimu sana hizi taarifa zikiingia kwao, lakini ziingie zikiwa na *details* kwenye RCC. Mimi nilikuwa nagombana, sikuwa naelewa kabla sijaingia kwenye LAAC. Hivi wewe unatuletea hii taarifa ya miradi yetu imeandikwa zero, zero, hii zero maana yake nini; mnaondoka pale hamjakubaliana ni kitu gani. Sasa sisi kwenye LAAC tumewaambia kuwa Madiwani wapelekewe taarifa ile wanayoleta LAAC, kwa sababu ina *details,* inachambua kama ni misumari, wanakwambia kilo ngapi za misumari au wa inchi ngapi na kama ni mbao watakwambia. Kwa hiyo, ziende kwa Madiwani kwa utaratibu huo na kwenye DCC na kwenye RCC; zikienda hivyo tutapunguza na hatutahitaji usimamizi huko mbele. Kwa sababu tukiwa-*empower* DCC na RCC, sisi tutarudi nyuma, wale ndiyo wenye mali tuwape nguvu na tuwajengee uwezo ili waweze kusimamia kwa niaba yetu sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala ambalo Mheshimiwa Rished amelisema sana; kwa nini wakati tuna mhasibu mwenye cheti lakini tunapata *unvouched, not in ledger,* imepelekwa benki haipo kwenye *register*, iko kwenye *register* lakini haipo benki. Sisi tumefika mahali tumekuwa wakali, najua kanuni za fedha zinaruhusu wakaguzi kurudi mara ya pili, lakini sote tunajua kwamba, unapojua mara ya pili wanakwenda dukani kununua hizi risiti na mimi nimewakamata mara kadhaa wanakwenda kununua risiti, wakirudi wanakwambia risiti hii hapa. Sisi tumetoa kwa wakaguzi wetu wa CAG na tumekubaliana, hawarudi tena kwenda kufanya ukaguzi kwa sababu hakuna maelezo kwa nini mtu mwenye sifa asiwe na *batch* yake *complete* kabla hajafanya manunuzi. Si hivyo tu, kanuni za fedha zinasema mhasibu hatakiwi kufanya malipo kama nyaraka hazijakamilika; kwa nini alilipa na alilipaje? Tukifika hatua hiyo, tutaanza kuchukua hatua nyingine na Waziri tutakuomba na wewe uwe mkali sana katika hilo.

Alilipa nini wakati hizi nyaraka hazipo na unasema imekuwa *misplaced;* kwa nini ziwe *misplaced* na wewe ndiyo *custodian* wa hizi nyaraka muhimu; kama zimekuwa *misplaced* basi kuna uzembe na tutakuadhibu kwa uzembe wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa hoja hiyo, naomba Bunge sasa lipokee taarifa, pamoja na maoni na mapendekezo ya Kamati yetu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nichukue nafasi hii pia, nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, kwa kuweza kuhitimisha hoja yake vizuri na kutoa maelezo ya ufafanuzi kwa hoja mbalimbali zilizotolewa na Wabunge na hoja ya Kamati yake.

Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati na Wabunge wengine, kwa ridhaa yao wameunga mkono hoja hii. Sasa nitaomba kulihoji Bunge ili nipate ridhaa ya Bunge zima kwamba, Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, pamoja na Mapendekezo na Maoni yaliyomo kwenye Taarifa hiyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa ilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge wote, wameiunga mkono hoja hiyo na Taarifa hii imepitishwa rasmi na Bunge letu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kama kawaida, basi niiombe Serikali kupitia Wizara husika, ihakikishe wanatusaidia kusimamia mapendekezo haya yaliyopitishwa na Bunge ili yaweze kufanyiwa utekelezaji wa kina na wa kutosha kwa mujibu wa sheria za nchi yetu ya Tanzania. Basi nichukue nafasi hii, kuwapongeza na kuwashukuru sana Mwenyekiti wa Kamati na Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Wajumbe wote wa Kamati husika na Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kuweza kuchangia hoja hii na kuweza kuipitisha kwa siku hii ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, hoja inayofuata sasa ni kupitia Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, lakini kwa muda niliobakiwa nao, nina dakika chache sana ambazo zipo hapa mbele yetu; ninaamini hazitaweza kabisa kumtosha Mwenyekiti wa Kamati hiyo kusoma taarifa yake na hivyo kuanza mchango wa jumla. Kwa hiyo, hoja hii tutaanza nayo kipindi cha saa kumi na moja jioni.

Baada ya kusema hayo, sina matangazo Mezani, ninaomba sasa nisitishe shughuli hizi za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.50 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**MHE. KABWE Z. ZITTO – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na ninapenda kuchukua nafasi hii, kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge, kuweza kutoa Taarifa ya

Mwaka ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, kama yalivyokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kupitia taarifa yake iliyowasilishwa Bungeni mwezi Machi, 2008. Taarifa hii ina viambatanisho takriban 10, ambavyo kwa Waheshimiwa Wabunge ambao watahitaji kuwa na nakala hizi za viatambatanisho, watawasiliana na Ofisi ya Katibu wa Bunge kwa ajili ya kupata viambatanisho hivyo, maana hatuwezi kuvisoma vyote; Mashirika ni mengi na masuala ni mengi sana katika mashirika ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Mheshimiwa Spika, kama Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni za Bunge, kwa wazo mahususi la Kamati hiyo kuunda, pamoja na Kamati nyingine, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma. Kuundwa kwa Kamati hii ni fursa ya kipekee kwa Bunge letu kuweza kuyasimamia mashirika na taasisi nyingine za umma, kuwajibika zaidi kutoa taarifa za fedha zilizoidhinishwa kwao, kwa nia ya kutoa huduma bora kwa Watanzania.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba, kwa takriban kipindi cha miaka kumi, hapakuwa na Kamati kama hii kwenye Bunge. Kwa hiyo, taarifa hii ni taarifa ya kwanza ya Kamati hii na inaweka misingi kwa ajili ya taarifa zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hii ni ya kwanza ya Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, tangu Kamati hii iundwe mwanzoni mwa mwaka 2008, kufuatia maboresho ya Kanuni za Bunge. Ikumbukwe pia kwamba, hata Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali, alitoa taarifa kuhusu hesabu za Mashirika ya Umma, kwa mara ya kwanza mwaka jana. Hivyo, Kamati haina rejeo la Taarifa zilizopita tunapotoa taarifa hii. Hata hivyo, kwa taarifa hii, tunajenga misingi ya taarifa zijazo, lengo likiwa ni kuongeza uwajibikaji kwa fedha za Umma.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, katika Mwaka wa Fedha ulioishia Juni 30, 2007 palikuwa na Mashirika ya Umma yapatayo 158 hapa nchini. Kamati hii imekwisha kujadili na kuchambua taarifa za hesabu zilizokaguliwa za mashirika 78 kati ya Hesabu zilizokaguliwa za Mashirika 91, kiasi ambacho ni sawa na asilimia 85.7 ya mashirika yote katika muda wa siku 45 ambazo Kamati ilifanya kazi. Hata hivyo, bado kuna tofauti juu ya idadi kamili ya Mashirika ya Umma, kutokana na taarifa za Msajili wa Hazina kuonesha idadi tofauti kama tutakavyoona na kushauri hapo baadae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati yameainishwa katika sehemu ya tatu ya nyongeza ya nane ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, chini ya Kanuni ya 115, kifungu cha 13 katika fasili ndogo (a) hadi (e). Majukumu hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Kushughulikia taarifa za kila mwaka za hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma.

(b) Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za Mashirika ya Umma yaliyoainishwa katika taarifa za kila mwaka za Mashirika hayo na kutoa mapendekezo na ushauri wa namna ya kuyaondoa matatizo hayo.

(c) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati hiyo ili kuondoa matatizo hayo.

(d) Kutathmini ufanisi wa Mashirika ya Umma.

(e) Kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** katika kutekeleza majukumu hayo, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma ilitumia nyenzo zifuatazo:-

(a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara na hasa kuhusu mamlaka ya Bunge na Kamati zake.

(b) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007.

(c) Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (kwa Mwaka ulioishia 30 Juni, 2007).

(d) Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2004, Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 200 na Sheria iliyoanzisha kila Shirika husika.

(e) Taarifa za Msajili wa Hazina kama Mwenye hisa Mkuu katika mashirika yote ambapo Serikali imewekeza.

(f) Taarifa za mahesabu za kila Shirika kwa Mwaka wa Fedha unaojadiliwa, ikiambatanishwa na majibu ya hoja za Ukaguzi kutoka katika Manejimenti ya kila Shirika lililojadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitumia mbinu mbalimbali ili kutekeleza wajibu wake, zikiwemo:-

(a) Semina za mafunzo kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Msajili wa Hazina na Bodi ya Uhasibu (NBAA). Lengo la semina hizi za mafunzo lilikuwa ni kupata taaluma ya jinsi ya kusoma na kutafsiri mahesabu.

(b) Kujadili na kuchambua taarifa za hesabu zilizokaguliwa za Mashirika mbalimbali kwa kuwaita Maafisa Masurufu (*Accounting Officers*) na Wenyeviti wa Bodi mbele ya Kamati.

(c) Kufanya ziara za kujiridhisha na thamani na uhakika wa kuwepo kwa miradi/mashirika husika (*value for money audit*).

(d) Kuunda Kamati Ndogo ili kufuatilia masuala ambayo Kamati ilihitaji maelezo ya kina kuhusiana na hesabu za Shirika husika.

(e) Kukutana na Watendaji Wakuu wa Mashirika yote ya Umma kwa pamoja ili kukubaliana misingi ya kufanya kazi kwa pamoja kati ya Shirika na Kamati.

(f) Kuandaa Mkutano wa Uwajibikaji wa Mashirika ya Umma (*Parastatals Accountability Conference*) na kujadili kwa kina utendaji na changamoto za Mashirika kadhaa ya Umma yaliyoteuliwa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbinu hizi ziliisaidia sana Kamati kuyajua vizuri mashirika tuliyokuwa tunayashughulikia, kuchambua changamoto zao na kutoa mapendekezo na maagizo mwafaka ili kuongeza ufanisi katika utendaji wa mashirika ya Umma na hivyo kutoa huduma bora za kuzalisha faida na kwa yale yanayofanya biashara kutoa gawio serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna Mashirika mengi ya Umma na Kamati haiwezi kutoa Taarifa ya Shirika moja moja hapa Bungeni, sehemu ya mwisho ya Taarifa hii imeainisha changamoto tulizoziona katika mashirika 10 tuliyoyachagua. Mashirika haya yameteuliwa kutokana na umuhimu wake katika uchumi wa nchi na kama mifano tu ya mashirika mengine. Mungu akijalia katika Ripoti yetu ijayo, ambayo itakuwa ni Taarifa ya mwisho ya Kamati katika Bunge hili la Tisa, tutaweza kuainisha Mashirika mengine na kuainisha changamoto zake na mapendekezo ya kurekebisha changamoto hizo. Vilevile katika taarifa hii, tutatoa mapendekezo maalumu kuhusu zoezi la ubinafsishaji na hasa ubinafsishaji wa mashamba katika Mikoa ya Mbeya na Manyara, ambapo Kamati ilipata nafasi ya kufanya ukaguzi maalumu. Tutatoa pia mapendekezo ya jumla, kuhusu Sera ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmiliki wa mali zote za Serikali kwenye Mashirika ya Umma ni Msajili wa Hazina. Kwa mujibu wa Sheria ya Msajili wa Hazina (*Treasury Registrar Ordinance Cap 418*), Msajili wa Hazina ndio mhusika pekee (*Sole Shareholder*) wa hisa, amana na vitega uchumi vingine katika Makampuni na Mashirika kwa niaba ya Serikali. Kwa mujibu wa Sheria hii, Msajili wa Hazina ni Shirika la kipekee (*Corporation Sole*), akiwa na uwezo wa kuchukua (*acquire*), kuendeleza au kuuza mitaji, kudai au kudaiwa kama vile mashirika au makampuni ya kawaida.

Kamati ilikutana na Msajili wa Hazina ili kupata taarifa ya uwekezaji wa mitaji ya Umma katika Mashirika na Taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kama ilivyoelezwa hapo juu, mpaka tarehe 30 Juni mwaka 2007, kulikuwa na Mashirika ya Umma 158 hapa nchini ambayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, aliweza kupata kumbukumbu zao. Miongoni mwa mashirika hayo, Mamlaka za Maji zipo 32, Bodi za Usimamizi (*Regulatory Bodies*) 27, Vyuo vya Elimu ya Juu 27, Mashirika ya Umma (*Public Parastatals*) 53 na Taasisi za Serikali 19. Muhtasari wa Utendaji wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu

za Serikali kwa mwaka unaoishia Juni 30, 2007, umeambatishwa katika Taarifa hii kama Kiambatisho Na. 2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha ulioishia 30 Juni 2007, Serikali iliwekeza kiasi cha Shilingi 4.1 trilioni katika jumla ya mashirika 193. Serikali ilikuwa na hisa asilimia 100 katika Mashirika na Taasisi 152 (hizi ndizo zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kama inavyooneshwa katika Taarifa na ilivyoelezwa hapo juu). Katika jumla ya mashirika 9, Serikali ilikuwa na hisa asilimia 50 au zaidi na katika mashirika 32 Serikali ilikuwa na hisa chini ya asimilia 50. Taarifa ya Msajili wa Hazina imeambatishwa katika Taarifa hii kama Kiambatisho Na. 1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mashirika 193 ya umma, mashirika 48 ni ya kibiashara, taasisi 119 ni za huduma, mashirika 13 yako kwenye hatua mbalimbali za ubinafsishaji na mengine 13 yako kwenye ufilisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashirika yote ambayo Serikali inashikilia hisa asilimia 50 na chini ya hapo hayana usimamizi (*oversight*) wa kibunge na hivyo Kamati hii haikupata fursa ya kukagua hesabu zao na hatimae kutokujua mtaji wa umma unaendeshwa namna gani. Miongoni mwa Mashirika hayo ni pamoja na BP, Zain, TRL, Aboud Soap Industries, NBC, Kilombero Sugar na kadhalika. Kamati imekwishawasilisha mapendekezo ya mabadiliko ya Kanuni za Bunge ili kutimiza agizo lako la kuhakikisha kuwa, Mashirika yote ambayo Serikali ina hisa yakaguliwe na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uwezekano mkubwa kuwa thamani ya uwekezaji mitaji ya umma itakuwa ni kubwa zaidi kutokana na Taasisi nyingine 51 ambazo zipo kwenye orodha ya Msajili lakini hazijawasilisha hesabu zao za sasa zilizokaguliwa. Vilevile kuna taasisi mpya ambazo hazikuwa zimekaguliwa hesabu zao. Miongoni mwa Taasisi hizo ni pamoja na Kampuni ya Buhemba Gold Mine (MEREMETA) na TanGold, ambayo imekuwa ikizua mijadala mikali ndani ya Bunge na kwenye jamii. Kamati inaamini kuwa, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atahakikisha kuwa, Mashirika haya yanawasilisha hesabu zao kwa ukaguzi ili kuhakikisha mitaji ya umma haipotei au kutumika vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika ya Umma yaliweza kuchangia mapato serikalini kutokana na gawio, mikopo na riba, pamoja na michango mingine. Gawio kutoka Mashirika ya Umma liliongezeka kutoka shilingi 12.2 bilioni mwaka 2005/2006 hadi kufikia shilingi 13.4 bilioni mwaka 2006/2007. Kwa ujumla, Mashirika ya Umma yalichangia serikalini makusanyo ya gawio na kiasi kingine cha michango ya jumla ya shilingi 26.05 bilioni, ukilinganisha na shilingi 60.7 bilioni mwaka uliotangulia. Makusanyo haya ni pungufu ya zaidi ya asilimia hamsini na ni faida ya chini ya 10% ya mtaji uliowekezwa kwa mwaka mzima wa 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gawio na michango mingine (*remittances*), inategemea sana utendaji wa Mashirika ya Umma kwa mwaka husika. Kupungua kwa gawio na michango mingine kutoka Mashirika ya Umma kwenda serikalini ni ishara kuwa

Mashirika ya Umma yamepunguza ufanisi na/au udhibiti na hivyo kupata hasara. Kamati imemtaka Msajili wa Hazina, aimarishe usimamizi wa Mashirika ya Umma ili yafanye kazi kwa ufanisi na kutoa faida kwa nchi. Taarifa hii pia imeainisha sababu mbalimbali za utendaji mbovu wa Mashirika ya Umma na kutoa mapendekezo ya jinsi ya kuboresha utendaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni matatizo sugu yaliyoainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa Hesabu za Mashirika ya Umma zinazoishia Juni 30, 2007. Hapa ningependa kulijulisha Bunge lako Tukufu juu ya hali halisi ya utekelezaji wa Sheria na Kanuni zinazotawala mwenendo wa mashirika na taasisi nyingine za umma nchini. Kamati inajua ya kuwa, Sheria na Kanuni hizo zipo kwa ajili ya kuleta ufanisi katika mashirika na taasisi hizo; hivyo, zinapokiukwa ufanisi na tija vinarudishwa nyuma, kiasi cha kusababisha huduma mbovu kwa wananchi na hasara kwa taifa. Matatizo yatakayoorodheshwa hapa chini yanaonekana kuwa sugu, kwa sababu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amezielekeza mara kadhaa Menejimenti za Mashirika hayo kurekebisha kasoro hizo, japo zinaonekana kuendelea kujirudia. Mfano ni katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 30 ya Sheria ya Fedha za Umma, 2001, inalitaka kila Shirika kuwa na Kamati ya Ukaguzi wa Ndani kwa lengo la kuongeza nidhamu zaidi katika kusimamia fedha za umma na kuweza kugundua mapema na kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma. Hata hivyo, bado yapo mashirika kadhaa ambayo mpaka mwaka wa fedha wa 2006/2007 unamalizika, yalikuwa bado hayana vitengo hivyo na Kamati za Ukaguzi wa Ndani. Mashirika hayo ni pamoja na Tume ya Vyuo Vikuu Nchini (TCU), Bodi ya Chai Nchini, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka za Singida na Songea, Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Shirika la Masoko la Kariakoo, Shirika la Bima la Taifa, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na Chuo cha Ushirika Moshi.

Madhara ya kutokuwa na Kamati za Ukaguzi wa ndani ni pamoja na kuzorota kwa mfumo wa udhibiti wa mali za umma katika shirika husika; kukosekana kwa viwango sahihi katika maandalizi ya taarifa za hesabu za shirika husika; na kukosekana kwa ubora wa kazi za ukaguzi wa ndani.

Kamati ilikutana na Watendaji wa baadhi ya Mashirika na Taasisi za Umma, kutaka wajieleze kuhusiana na hoja hii ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Jambo moja kubwa la kustusha ni kwamba, kwenye Mashirika mengi ya Umma, kitengo cha ukaguzi wa ndani kipo chini ya Menejimenti ya Shirika badala ya kuwa chini ya Kamati ya Ukaguzi wa Ndani ya Bodi ya Wakurugenzi.

Hali hii inahatarisha sana uhuru wa vitengo vya ukaguzi na madhara yake ni wakaguzi wa ndani kushirikiana na watendaji kufuja mali ya Umma. Sababu kubwa tuliyokutana nayo inayopelekea Mashirika ya Umma kutokuwa na Kamati za Ukaguzi wa Ndani na Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani ni pamoja na udhaifu mkubwa wa Bodi za Wakurugenzi na woga wa Watendaji. Vilevile Mashirika mengine na hasa Taasisi za Serikali, zinazotegemea ruzuku kutoka serikalini kama Shirika la Utangazaji la Taifa

(TBC), Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na kadhalika, hayana watumishi wa kutosha katika idara za uhasibu na hivyo kushindwa kuwa na kitengo cha ukaguzi wa ndani.

Kuhusiana na Kamati za Ukaguzi za Bodi za Wakurugenzi, mashirika mengi yamekuwa yakiogopa kuongezeka kwa gharama za uendeshaji. Kamati imeagiza mashirika yote ya umma kuteua Kamati za Ukaguzi wa Ndani na Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani ili kuongeza udhibiti wa matumizi ya fedha za mashirika hayo. Kamati haitasikiliza kisingizio chochote cha kushindwa kutekeleza agizo hili na watakaoshindwa, tutatumia vifungu mahususi vya Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge dhidi ya maafisa masurufu *(Accounting Officers)* wa Mashirika husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu Na. 3 (1) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya 2004, kinaelezea Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi kama ni kitengo au idara katika kila chombo cha Umma, kikishughulikia utekelezaji wa shughuli za ununuzi. Lazima kisheria kwa Shirika la Umma kuwa na kitengo cha manunuzi na pia kuwa na maafisa ugavi, kwani kulingana na Sheria iliyonakiliwa hapo juu, kifungu Na. 34 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma kinataka kila chombo kinachofanya ununuzi, kiunde kitengo cha usimamizi wa ununuzi kikiwa na watumishi kulingana na kinavyotakiwa. Wakati wa mijadala, Kamati ilibaini kuwa Mashirika ya Umma mengi hayajaanzisha vitengo vya manunuzi na hivyo kupelekea manunuzi mengi kufanyika bila kufuata sheria na kanuni husika. Vilevile kutokuwepo kwa vitengo vya manunuzi katika mashirika ya umma kunapelekea rushwa, kwani sehemu kubwa ya fedha za mashirika zinaenda kwenye manunuzi.

Mashirika ambayo hayakuwa na vitengo hivi ni kama vile TBC (zamani TUT), Bodi ya Tumbaku Tanzania, Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira Tanzania (NEMC), Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Babati na kadhalika. Kamati imeagiza Mashirika yote ya Umma kuanzisha mara moja vitengo hivi ili kuhakikisha kuwa, manunuzi yanafuata sheria na kanuni husika na vilevile kupata thamani ya pesa katika manunuzi ya umma. Hata hivyo, changamoto kubwa ni mashirika ya umma yanayopata ruzuku kutoka serikalini, kwani kuanzishwa kwa vitengo hivi ni kuongeza wafanyakazi na hivyo gharama za uendeshaji. Serikali na Wizara husika zinapaswa kuongeza fedha za bajeti zinazokwenda katika mashirika haya na pia Idara ya Utumishi itoe vibali vya ajira haraka.

Kamati inamwagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, atoe Taarifa yenye kuonesha thamani ya fedha ya manunuzi holela kwenye mashirika ya umma ili umma uweze kuona madhara kifedha ya kutofuata sheria na kanuni za manunuzi kwenye mashirika ya umma. Kwa mfano, Bodi ya Tumbaku Tanzania, katika mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, mwaka 2007, ilifanya ununuzi wa huduma na bidhaa mbalimbali zenye thamani ya shilingi 224 milioni bila kufuata taratibu za ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia imeliona tatizo la mashirika ya umma kufanya manunuzi kiholela bila kuzingatia mpango wa manunuzi (*procurement plan*), uliowekwa kwa mwaka husika na kwenda kinyume na Kifungu Na. 45 cha Sheria ya

Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004, kwani uwepo wa mipango ya manunuzi husaidia Mashirika na Taasisi za Umma kuepuka ununuzi wa dharura kila inapowezekana na vile vile husaidia kuunganisha makadirio na mpango wa matumizi (*action plan*) waliojiwekea. Mfano ni kwa Shirika la Magazeti ya Serikali (TSN), kutofuata utaratibu wa ununuzi ambapo lilinunua akiba ya vifaa vya kuchorea vya thamani ya shilingi 26.3 milioni, lakini hakuna ushahidi unaoonesha kwamba, utaratibu wa ushindani wa zabuni ulikuwepo. Kamati ililitaka Shirika hili kutoa maelezo ya kina kuhusiana na hoja hii ya ukaguzi ambayo ilipelekea Kamati kutembelea Shirika hili ili kuona vifaa hivyo vilivyonunuliwa bila kufuata taratibu. Shirika limerekebisha kasoro hiyo na kuiahidi Kamati kuwa manunuzi yote yatafuata Sheria ya Manunuzi ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watumishi katika mashirika na taasisi mbalimbali za umma, wanakatwa kiasi fulani cha fedha ambacho mwajiri anapaswa kukiwasilisha katika vyombo vinavyohusika na kupokea makato hayo kama vile Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (PPF, NSSF na PSPF), kwa ajili ya kufanikisha malipo ya uzeeni au bima za afya kwa watumishi waliokatwa. Kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma tano zilishindwa kuwasilisha makato ya kisheria kwa mamlaka husika, ikiwemo Mamlaka ya Kodi Tanzania (TRA). Mashirika na Taasisi hizo ni Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Halmashauri ya Biashara ya Nje (BET), Shirika la Posta (TPC) na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), ambayo yalishindwa kurejesha makato ya kisheria yenye jumla ya shilingi 29.3 bilioni. Madhara ya kutorejesha makato hayo ni tozo kubwa ambazo mashirika husika yanatozwa, kama adhabu ya kutotimiza sharti hilo la kisheria, lakini pia uzembe kama huo usipodhibitiwa mapema, husababisha matatizo katika ulipaji wa mafao ya watumishi wanapofikia nyakati za kustaafu. BET ilishindwa kuwasilisha kodi ya ardhi kwenye mamlaka husika ya jumla ya shilingi 143 milioni wakati Shirika la Posta lilishindwa kuwasilisha mapato ya Bima ya wafanyakazi ya shilingi 6 milioni na michango ya SACCOS ya wafanyakazi ya shilingi 197 milioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana na Mashirika na Taasisi zote za Umma zenye tatizo hili sugu sana na kupata maelezo yao kuhusiana na hoja hii ya Mdhibti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mashirika yote yalikiri kuwepo kwa tatizo hili na kuwa wamechukua hatua za kulirekebisha. Tutaona hatua hizo zilizochukuliwa kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka unaoishia Juni 30, 2008. Kwa upande wa BET, tatizo la kodi ya ardhi linatokana na kupandishwa kwa thamani ya ardhi, kufuatia kujengwa kiholela kwa magereji katika eneo la Maonesho ya Sabasaba na hivi lipo katika hatua ya kutatuliwa. Kamati inaomba mamlaka husika, kushirikiana na BET ili kumaliza tatizo hili kwani linatoa sura mbaya katika vitabu vya hesabu za BET ilhali lilitokana na uthamini mbovu wa ardhi na shughuli zinazofanyika katika eneo hilo. Kamati imeyaagiza mashirika yote ya umma na Taasisi za Serikali kuhakikisha kuwa, makato halali yanawasilishwa kwa mamlaka husika wakati mwafaka na watendaji wa mashirika watakaokiuka wachukuliwe hatua mara moja kwa kuhatarisha maisha ya ustaafu ya watumishi wao na kukwepa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika ya Umma yana matatizo makubwa sana ya mitaji ya kuwekeza (*recapitalization*). Mpaka tunaposoma taarifa hii, kuna maombi ya

fedha zinazofikia zaidi ya shilingi 60 bilioni kwa ajili ya mahitaji ya mtaji kwa mashirika ya umma katika Ofisi ya Msajili wa Hazina. Mahitaji ya mtaji ni kwa ajili ya kuokoa baadhi ya mashirika yasifungwe na pia kama mchango kwa baadhi ya mashirika ambayo serikali ina ubia. Kukosekana kwa mtaji kunaathiri mashirika ya umma kuendeshwa kwa ufanisi na kuhatarisha maslahi ya Serikali kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa yapo Mashirika kama vile Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), Shirika la Umeme Nchini (TANESCO), Mamlaka zote za Maji Nchini, Shirika la Bima la Taifa (NIC), Halmashari ya Biashara ya Nje (BET), Shirika la Ndege la Taifa (ATCL) na Shirika la Mafuta (TPDC), ambayo yanafanya kazi kwa kusuasua kwa sababu ya kuwa na kiasi kidogo cha mtaji. Kamati inashauri Serikali iangalie uwezekano wa kuyaongezea mashirika hayo mitaji ili yaweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ambayo Mashirika ya Umma yanazidai asasi na watu mbalimbali ni mengi sana na mashirika hayo yanashindwa kabisa kukusanya madeni hayo. Kwa upande wa mashirika ya huduma kama vile TANESCO na DAWASCO, tatizo hili ni kubwa zaidi kwani kuna mwingiliano mkubwa sana na wanasiasa pale ambapo watendaji wa mashirika hayo wanapochukua hatua za kukusanya madeni. Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imetoa mikopo kwa watu binafsi na kushindwa kukusanya madeni hayo na hivyo kuhatarisha ukwasi wa mashirika hayo. Kwa mfano, Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF), linadai watu mbalimbali zaidi ya shilingi 35 bilioni na juhudi za kukusanya madeni haya zimegonga mwamba. Katika madeni haya, Kampuni mbili binafsi za Kagera Sugar Ltd. (Sh. 16 bilioni) na *General Tyre East Africa Ltd (*Sh.13 bilioni) zinadaiwa zaidi ya shilingi 20 bilioni na Shirika la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na mikopo hii ilidhaminiwa na Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifahamishwa kuwa, deni la Kampuni ya Kagera Sugar Ltd. sio kwa NSSF peke yake, bali na mifuko mingine ya hifadhi ya jamii na mabenki ikiwemo Benki ya Rasilimali (TIB). Hali hii iliifanya Kamati ifanye ziara rasmi kukitembelea Kiwanda cha Sukari cha Kagera ili kujionea wenyewe uwekezaji huo mkubwa na kuzungumza na mwekezaji kwa nini hajaanza kulipa deni hilo. Kamati iliona uwekezaji huu mkubwa sana katika sekta ya kilimo, unatakiwa sana kwa maendeleo ya nchi na hasa katika juhudi za nchi kujitosheleza na chakula. Hata hivyo, iwapo mkopo huu hautalipwa kwa mujibu wa uwekezaji huu, imani ya mabenki katika kukopesha Sekta ya Kilimo itapungua sana na hivyo kuhatarisha maendeleo ya nchi. Kamati ilishauriana na mwekezaji na Uongozi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuufanyia mabadiliko muundo wa mkopo na kumtaka mkopaji aanze kulipa mara moja mkopo huu ili kuhakikisha kuwa fedha za umma zinakuwa salama. Kamati inatarajia kupata majibu ya Serikali katika suala hili katika Mkutano huu wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Mashirika ya Umma nayo hayalipi madeni yao na hasa mikopo kutoka serikalini au dhamana za Serikali. Katika mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2007, dhamana ya jumla ya shilingi 175. 4 bilioni zilizotolewa na serikali kwa mashirika ya umma zilikuwa bado hazijalipwa. Kamati haikupata maelezo

yoyote ya kuridhisha kuhusiana na tatizo hili kubwa sana kutoka kwa wakopaji wala mdhamini.

Kamati inaitaka Serikali itoe ufafanuzi hapa Bungeni, juu ya hatua wanazochukua za kuhakikisha kuwa, Mashirika ya Umma yanalipa mikopo yao kwa muda muafaka ili kuepuka kuitwa kwa dhamana. Vilevile ni vizuri Serikali ikatoa dhamana kwa mashirika ambayo yanaonekana kufanya kazi kwa ufanisi na hivyo kuwa na uwezekano wa kulipa mikopo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na dhamana hizo ambazo Serikali ilidhamini mashirika ya umma ili yakope, Serikali pia ilitoa mikopo kwa mashirika ya umma. Jumla ya shilingi 63 bilioni zimeshindikana kulipwa kutoka katika mashirika ya umma mpaka mwezi Juni, 2007. Kiasi cha shilingi 15 bilioni ni deni la Kampuni ya TTCL kwa Serikali, ambapo Serikali inataka kuanza mchakato wa kuhamisha deni (*debt swap*) ili kumaliza deni hilo. Kamati haijaridhika na maelezo ya Serikali kuhusu deni hili la Serikali kwa TTCL na hata mchakato mzima wa ubinafsishaji wa TTCL, kuanzishwa kwa Kampuni ya Celtel (sasa *Zain*) na ukweli kuhusu hisa za Serikali katika kampuni hiyo na jinsi mali za TTCL zilivyouzwa kupitia Kampuni ya SIMU2000. Kamati inataka maelezo ya kina kutoka serikalini kuhusu suala hili ili Taifa liweze kujua hatma ya TTCL na uwekezaji wa Serikali katika Kampuni ya *Zain*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mikopo ya Serikali kwa mashirika ya umma ni kubwa mno na madeni mengi hayalipiki. Kwa mfano, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ameonesha katika ripoti yake kuwa mpaka 30 Juni, 2007 madeni ya jumla ya shilingi 46 bilioni zilizokopeshwa kwa mashirika ya umma hazilipiki. Miongoni mwa mashirika yanayodaiwa ni pamoja na Steel Rolling Limited, ambayo tayari imebinafsishwa, TACOSHILI, TRC na TTCL. Kamati inaitaka Serikali kuongeza kasi ya kushughulikia mikopo hii ili iache kujirudia mwaka hadi mwaka katika taarifa ya mkaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo Mashirika na Taasisi mbalimbali za Umma, ambazo kwa muda wa miaka mingi hazijakidhi matakwa ya kisheria ya kuwa na Hatimiliki za mali zao hususan ardhi. Wasiwasi wa Kamati ni kwamba:-

(a) Mazingira kama hayo yanaweza kuwa tata kwa mashirika hayo inapotokea ugomvi juu ya umiliki halali wa mali hizo.

(b) Hali kama hiyo yaweza kufikiriwa kuwa kiashiria muhimu kuhusu uzembe wa watendaji katika kujali mali zao.

(c) Hali kama hiyo yaweza kuwa kikwazo kwa mashirika hayo yanapohitaji mikopo kutoka kwa taasisi kopeshaji.

Mashirika hayo kwa uchache ni pamoja na Bodi ya Sukari Nchini (kitalu Na. 45 kilichopo Barabara ya Agha Khan Mjini Dar es Salaam, Nyumba 6 katika Kitalu Na. 303 na nyumba za makazi zilizopo Makambako Mjini Iringa); Kampuni ya Ranchi za Taifa

kutokuwa na hatimiliki kwa ranchi za Ruvu, Kongwa, Mabale na kadhalika na kuwa na hatimiliki za Ranchi ya Misenyi na Kitengule zisizokuwa na jina la Kampuni ya NARCO; Shirika la Reli Tanzania (Kitalu Na. 228 kilichopo Kurasini Mjini Dar es Salaam); Vitalu viwili vilivyopo Ofisi ya DCE Mjini Dodoma; na Klabu ya Shirika la Reli iliyopo Barabara ya Uluguru Mjini Tabora); Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Singida (Magari ya Mamlaka yenye thamani ya shilingi 43.1 milioni na majengo yenye thamani ya shilingi 150.9 milioni hayakusajiliwa kwa jina la Mamlaka); na Taasisi ya Utafiti na Maendeleo ya Viwanda - TIRDO (Kitalu Na.1408).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata maelezo ya kutosha kutoka kwenye mashirika ya umma kuhusu tatizo hili sugu la kutokuwa na hatimiliki za majengo na viwanja wanavyomiliki. Iwapo suala hili halitapatiwa ufumbuzi wa haraka, kuna hatari ya mashirika ya umma kupoteza mali zao. Mashirika yanalalamikia urasimu uliopo katika Wizara ya Ardhi, kuhusiana na mchakato wa kupata hati za kumiliki ardhi. Kamati inaitaka Serikali kufanya programu maalumu ya kuhakikisha mali za Mashirika ya Umma zinapata hatimiliki kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha ulioishia 30 Juni, 2007, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ilibainisha kuwepo kwa Mashirika na Taasisi mbalimbali za Umma zipatazo 158. Hata hivyo, Ofisi hiyo iliweza kukagua kikamilifu taarifa za Mashirika 91 tu kwa sababu mashirika 50 yalichelewesha kuwasilisha taarifa zao kwa wakati na mashirika 17 hayakuwasilisha kabisa taarifa za hesabu zao kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kamati inapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, kufuatia zoezi la ubinafsishaji wa mashirika ya umma, kumbukumbu za mashirika ya umma hazina usahihi. Kwa mfano, Mkaguzi ana orodha ya mashirika ya umma 158 na Msajili wa Hazina ana orodha ya mashirika 193. Vilevile chombo kingine kinachoweka kumbukumbu ni Shirika Hodhi Linaloshughulikia Madeni na Mali (CHC) lililorithi PSRC. Katika Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika ya Umma, imeonekana kuwa wakati Serikali ilibakiza hisa katika baadhi ya mashirika iliyobinafsisha, uwekezaji katika baadhi ya mashirika uliondolewa katika orodha ya Msajili wa Hazina katika mazingira ya kutatanisha na bila maelezo ya kuridhisha. Mashirika husika na hisa za Serikali zilizoondolewa, yaani ambazo Serikali haina hati nazo na hatujajua kama bado ni za Serikali ama vipi ni pamoja na Tanzania Tea Authority Lupembe Branch (30%); Morogoro Shoe Company (30%); Moro Tanneries (45%); Industrial Promotion Services (30%); Tanzania Electrical Goods Manufacturer (30%); na Kilombero Sugar Company (25%). Hizo ni hisa ambazo zilikuwa ni za Serikali na zina thamani ya zaidi ya bilioni 240 lakini hazipo kwenye *record* yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeshtushwa na taarifa ya kwamba, mali za Serikali zinaweza kuondolewa kwenye orodha ya mali kirahisi namna hii na hivyo kupelekea kupoteza mali hizi. Kamati inaungana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kutaka hati za hisa za Serikali katika mashirika haya zirudi kwenye kumbukumbu za Serikali na pale ambapo kuna mabadiliko yoyote kuhusiana na umiliki huo, basi mabadiliko hayo yatolewe maelezo. Pale ambapo ubia unazalisha faida ni

vizuri Serikali iangalie uwezekano wa kuuza hisa zake katika Soko la Mitaji la Dar es Salaam (DSE) ili kumilikisha uchumi kwa wananchi wengi zaidi na kuimarisha uwazi katika uendeshaji wa makampuni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa hapo awali, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, imepewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 13(e) ya nyongeza ya nane ya Kanuni, Toleo la Mwaka 2007. Katika eneo hili Kamati inatoa taarifa kuhusu jinsi ilivyotekeleza wajibu huu, kwa kuzingatia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ripoti ya Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zinaonesha kwamba, mpaka 30 Juni, 2007 mashirika 277 na vitengo 366 vilikuwa vimebinafsishwa na mikataba ya mauzo kusainiwa au makampuni hayo kupelekwa kwa mfilisi. Katika kipindi hicho, Serikali ilipata mapato ya jumla ya shilingi 120 bilioni kutokana na ubinafsishaji huo. Vilevile Serikali bado inadai baadhi ya wawekezaji jumla ya shilingi 8 bilioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kuna mashirika 183 yenye thamani ya uwekezaji wa jumla ya shilingi 276 bilioni, yakiwa katika hatua mbalimbali ya ubinafsishaji. Mashirika 15, yenye thamani ya shilingi 21 bilioni, kati ya haya yapo katika hatua ya kufilisiwa au kufungwa kabisa. Mashirika yenye thamani ya shilingi 113 bilioni yapo katika hatua ya kubinafsishwa, yakiwemo mashirika kama Shirika la Bima la Taifa, National Microfinance Bank (NMB) na Tanzania Cotton Lint and Seed Board (TCLSB). Kamati inapongeza uamuzi wa Serikali kukubaliana na pendekezo la Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, kutokuuza Shirika la Bima la Taifa na hivyo kuzuia ubinafsishaji wake. Vilevile Kamati inaipongeza Serikali kukamilisha uuzaji wa hisa za Benki ya NMB kwa wananchi. Hata hivyo, Kamati inaitaka Serikali ihakikishe mali za mashirika yaliyo katika hatua za ubinafsishaji zinalindwa wakati tunaangalia upya zoezi hili na manufaa yake kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeingia ubia na wawekezaji binafsi katika mashirika kadhaa yaliyobinafsishwa. Kamati ilipewa taarifa kuwa mashirika 25 yenye thamani ya shilingi 275 bilioni yana ubia (*Joint Venture*) na Serikali kwa viwango mbalimbali vya hisa. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ana mashaka makubwa kama masharti ya ubia yanafuatwa kama makubaliano ya manunuzi yalivyoingiwa. Kamati inapendekeza uchunguzi maalumu wa Kibunge ufanyike katika mashirika yote yaliyobinafsishwa kwa kuwa na ubia wa Serikali ili kuweza kutambua uendeshaji wa Mashirika haya na usalama wa hisa za Serikali na vilevile kushauri uwezekano wa hisa hizo za Serikali kuuzwa kwa wananchi wengi zaidi kupitia soko la Hisa la Dar es Salaam. Uchunguzi huo pia upendekeze hatua za kisheria dhidi ya wawekezaji ambao wataonekana kukiuka makubaliano ya ubia *(terms of joint venture)* ikiwemo kurejesha Shirika kwenye mikono ya Serikali.

Mashirika 25 ya kufanyiwa uchunguzi wa kibunge kupitia kamati ni yafuatayo (hisa za Serikali kwenye mabano): Aboud Soap Oil Industry (20%), ubia na Aboud Soap Ent. Ltd; BP(T) Ltd (50%), ubia na BP Africa Ltd; Celtel (sasa Zain) (40%), Ubia na Celtel

International; Datel Tanzania Limited (35%); Friendship Textile (49%), ubia na Dieqiu Textile and Printing Group; General Tyre EA Ltd (74%), ubia na Continetal NA; Keko Pharmaceuticals Ltd (40%), Ubia na Diocare; Kilimanjaro Airport Development Company Ltd (24%), Ubia na Mott-Macdonald Ltd, SA infrastructure fund na Inter Consult Ltd; Kilombero Sugar Co. (25%), Ubia na Ilovo & ED & F. Man; Kiwira Coal Mines (30%), Ubia na TAN Power Resources; Light Source Manufacturers (49%), Ubia na TATA Exports; Mbeya Cement Co. Ltd (25%), hatukuelezwa ubia na kampuni gani binafsi; Mbinga Coffee Curing (43%), Ubia na Vyama vya Ushirika; Mbozi Coffee Curing (32%), Ubia na Vyama vya Ushirika; Mwananchi Engineering – MECCO (25%), Ubia na Sisi Construction Ltd; New Africa Hotel (23%), Ubia na TADEMA Oversees Ltd; TANICA (10%), Ubia na Vyama vya Ushirika; TBL (4%), Ubia na Indol International BV; TCC (2%), Ubia na RJ Reynolds, JT International Hold BV na Watanzania kupitia Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE); Tanzania Daesung Cables (29%), Ubia na East African Cables Kenya; Tanzania Pharmaceutical Ltd (40%), Ubia na Pharmaceutical Investments Ltd; Tanzania Planting Co (25%), Ubia na Sukari Investment Co.; TAZARA (50%), Ubia na Serikali ya Jamhuri ya Zambia; TIPER (50%), Ubia na Oryx Oils; na Williamson Diamond Mines (25%), Ubia na Wilcroft Co. Ltd.

Tunapenda tuweze kufahamu kwa undani kama makubaliano ya manunuzi haya yanafuatiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma ni zoezi ambalo kwa ujumla wake, linahitaji kufanyiwa uchunguzi ili kujua mafanikio na upungufu wa zoezi zima. Tayari Kamati imeiagiza CHC kufanya uchunguzi na tathmini ya zoezi zima la ubinafsishaji na kuwasilisha taarifa yao ya uchunguzi kwa Kamati kabla ya kuwasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imejadili kwa kina mchakato wa ubinafsishaji na hasa hatua ya kuliorodhesha shirika kabla ya kuanza mchakato. Hatua hii kwa Kiingereza inaitwa *Specification.* Wakati huu wa ku-*specify* shirika, shirika linazuiwa kufanya uwekezaji wowote; haliruhusiwi kukopa na hata kupata misaada ya kiundeshaji. Matokeo yake ni kuwa, shirika linakondeshwa na mpaka kufikia wakati wa kubinafsishwa linakuwa limekwisha kabisa na hivyo kuuzwa kwa bei ndogo sana. Mfano ni athari zilizotokea kwa Kampuni ya Madini ya Taifa (STAMICO) na Shirika la Posta (TPC), ambayo kwa muda mrefu yalikuwepo tu bila kufanya shughuli zozote za uzalishaji yakisubiri kubinafsishwa.

Shirika la STAMICO ambalo lilikuwa *specified* mwaka 1996, lilijikuta likipoteza makampuni yake tanzu yote na hata hisa zake ilizokuwa nazo katika makampuni kama Bulyanhulu Goldmine, Williamson Diamond na Kiwira Coal Mine. Iwapo STAMICO isingekuwa imekuwa *specified*, sehemu kubwa ya lawama ambazo wananchi wanazitoa leo katika sekta ya madini, zingekuwa zimepungua kwani Taifa lingekuwa linamiliki sehemu ya migodi ya madini iliyopo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitoa pendekezo mahususi serikalini kuwa, STAMICO iondolewe katika orodha ya mashirika ya kubinafishwa (*despecified*) kama ilivyopendekezwa awali na Kamati ya Rais kuhusu Sekta ya Madini (Kamati ya Bomani).

Vilevile Kamati inapendekeza kuwa, mali zote ikiwemo hisa zilizokuwa za STAMICO, ambazo bado hazijauzwa na zinashikiliwa na Msajili wa Hazina, zirejeshwe STAMICO na pia ipewe mtaji wa kutosha ili iweze kushiriki kikamilifu katika uwekezaji wa Sekta ya Madini kama *Resource Development Company* na hivyo Taifa kufaidika. Kamati inatarajia kupata maelezo ya Serikali kuhusu suala hili katika mjadala wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapendekeza kuwa, kwa kuwa uchunguzi unafanyika kuhusu zoezi la ubinafsishaji na kwamba ubinafsishaji kwa sasa utasimama mpaka hapo taarifa ya uchunguzi itakapotolewa Bungeni, suala la masharti ya *specified companies* liangaliwe upya, kwani utaratibu huu umeingiza hasara kubwa sana kwa nchi kufuatia mali nyingi za mashirika kupotea katika kipindi hiki cha *specification*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Ubinafsishaji ilikuwa ni nguzo muhimu ya mabadiliko ya uchumi katika miongo miwili iliyopita. Kuna maeneo ambayo kuna mafanikio kama tulivyoeleza hapo awali na kuna maeneo ambayo tulikosea sana. Baadhi ya sababu ambazo Kamati imeziona zilipelekea makosa katika zoezi hili ni kama vile kutokuwepo kwa sheria zenye nguvu na taratibu za udhibiti na hivyo kukosekana kwa uchunguzi wa kina (*inadequate due diligence*), udhaifu katika mikataba na uteuzi mbovu wa wawekezaji (*strategic investors*). Wakati ubinafsishaji ni njia tu ya kuelekea katika ukuaji wa kasi wa uchumi, hapa nchini zoezi hili liliendeshwa kama vile ndio mwisho (*an end in itself*) na hivyo mashirika mengi hayakufanya yale ambayo yalitakiwa kufanya kwa mujibu wa mikataba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ziara maalumu kuangalia ubinafsishaji katika Sekta ya Kilimo, ubinafsishaji wa mashamba. Hii inatokana na ukweli kuwa, kilimo bado ni sekta muhimu sana kwa uhai wa Taifa letu na ubinafsishaji wa mashamba umekuwa na lawama nyingi sana kutoka kwa wananchi sehemu mbalimbali nchini. Hivyo, Kamati ilifanya ziara ya kiuchunguzi katika Wilaya za Mbozi na Mbarali Mkoani Mbeya na Wilaya ya Hanang Mkoani Manyara ili kujionea utekelezaji wa zoezi la ubinafsishaji wa mashamba na pia kusikiliza maoni ya wananchi. Taarifa za ziara zimeambatishwa katika taarifa hii kama Viambatisho Na. 3 na Na. 4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara ya Mkoani Mbeya ilianzia katika Wilaya ya Mbozi, kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma, kwa maana ya mashamba saba ya kahawa na shamba moja la mahindi. Mashamba hayo ni Shamba la Kahawa la Ruanda (ekari 51) ; Shamba la Kahawa la N'gamba (ekari 156); Shamba la Kahawa la Shiwanda (ekari 157); Shamba la Kahawa la Ihanda (ekari 120); Shamba la Kahawa la Ndugu (ekari 140); Shamba la Kahawa la Tukumbi (ekari 132); Shamba la Kahawa la Ishera (ekari 88); na Shamba la Mahindi la Mbozi (ekari 12,000).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijionea katika ziara hii jinsi ambavyo mamlaka zinazohusika na zoezi la ubinafsishaji hazina takwimu sahihi za mali ilizokuwa inazibinafsisha. Kamati itatoa mifano miwili; mmoja Wilayani Mbozi na mwingine Wilayani Mbarali, kuthibitisha jinsi ambavyo watu walikuwa wanakaa maofisini Dar es

Salaam na kuuza mali bila hata kujua mali wanazouza na madhara yake ni kuleta ugomvi katika nchi na hata kutishia amani.

Kamati iliarifiwa na msimamizi wa ubinafsishaji, Shirika la CHC kwamba, mashamba saba yaliyokuwa yanalimwa kahawa, yaliuzwa na Serikali kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi mwaka 2005 kwa jumla ya shilingi 176.1 milioni. Hata hivyo, kiasi kilicholipwa na Halmashauri hiyo ni shilingi 46.0 milioni tu. Kiasi kilichobaki kinasubiri makusanyo ya Halmashauri kutoka kwa wakulima wanaoendelea kuuziwa mashamba madogo madogo. Hata hivyo, msimamizi huyo alibainisha kwamba, Halmashauri haina mpango mkakati wowote iliouandaa kwa ajili ya kukusanya fedha kutoka kwa wakulima hao ili kulipa deni lililobaki (shilingi 130.1 milioni). Serikali nayo kwa upande wake, haijafanya juhudi zozote za makusudi za kuwasiliana na Halmashauri hiyo ili kupanga namna ya kulipana deni hilo.

Mashamba yote saba yana jumla ya ukubwa wa ekari 844, lakini tangu yauzwe kwa Halmashauri ni ekari 150 tu zilizogawiwa kwa wakulima wadogo wadogo. Kamati haikupewa majibu ya kuridhisha kwa nini kiasi hicho tu kiligawiwa wakati mahitaji ya wakulima kupata mashamba ya kulima ni makubwa? Kamati imeiagiza CHC na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kuhakikisha kuwa, mashamba yote yaliyobakia ambayo bado hayajauzwa, yagawiwe kwa wananchi ili waweze kupata ardhi ya kulima na kuzalisha mali. Kamati inasisitiza kuwa, mashamba haya yasikodishwe kwa wananchi bali wananchi wagawiwe kwa utaratibu ambao Halmashauri itauweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa, upo mkanganyiko mkubwa juu ya takwimu za ukubwa sahihi wa Shamba la Shiwanda ambalo Halmashauri ilimuuzia Mwekezaji Ndg. Cornel Lundu Apson. Wakati CHC wanaonesha kuwa Shamba hilo lina ukubwa wa hekta 157, Halmashauri ilionesha ukubwa wa hekta 257.33 wakati Mwekezaji alionesha ukubwa wa hekta 280. Zaidi ya hapo, wakati CHC inasema haijalipwa na Halmashauri kubabaika kuhusu suala hili, mnunuzi wa shamba hilo alionesha vielelezo vyote kwa Kamati kuwa amelipa pesa zote alizopaswa kulipa katika kununua shamba hilo tangu mwaka 1997.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati haikufurahishwa na uzembe *(incompetence)* wa aina hii kutoka katika Shirika la CHC na hasa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi. Kutokuwa na habari au kupotosha habari kama hizi, kunaweza kujenga hisia kuwa mnunuzi alifanya ujanja ujanja katika manunuzi ya shamba hili na hivyo kujenga chuki kwenye jamii. Kamati ilimpongeza Ndugu Apson Lundu sio tu kwa kuweka kumbukumbu zote sahihi, lakini pia kwa kufanya uamuzi wa busara wa kutumia maisha yake ya ustaafu kwenda kulima na hivyo kuongeza uwezo wa nchi kuzalisha mali katika Sekta ya Kilimo. Kamati imeiagiza CHC kupata takwimu sahihi za mashamba yote nchini, yaliyobinafsishwa na yaliyo katika mchakato huo, kwa kufanya ziara za kuona badala ya kutolea takwimu maofisini na hivyo kutojua uhalisia wa mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji katika Shamba la Mahindi la Mbozi (*Mbozi Maize Farm Company)*, ambalo lipo chini ya CHC, ambalo uzalishaji wake umekuwa ni wa kusuasua tangia mwaka wa 1996/1997, ambapo katika Shamba lenye ukubwa wa

hekta 4,840 zililimwa na kupandwa hekta 32 tu badala ya hekta 499 zilizolimwa na kupandwa katika msimu wa 1995/1996. Kwa kuwa Serikali imeonesha hatua za kutaka kulibinafsisha Shamba hili tangia mwaka 1992; na kwa kuwa lengo la ubinafsishaji ni kuinua uchumi wa nchi na wananchi; na kwa kuwa wananchi wapatao laki moja na nusu wa vijiji vinavyolizunguka Shamba hilo wanahitaji ardhi ya kulima na wanao uwezo wa kununua Shamba hilo kwa matumizi hayo; Kamati inaishauri Serikali kugawa shamba hili kwa wananchi ili wapate ardhi ya kulima na kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula nchini. Kamati ilipata taarifa kuwa, Kampuni ya Tanzania Breweries ilikuwa imeomba hekta 500 katika shamba hili ili kulima shayiri. Kamati inaomba maelezo ya Serikali kuhusu suala hili na Serikali izingatie ushauri wa Kamati katika uamuzi wowote utakaoamuliwa kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilayani Mbarali Kamati ilitembelea Shamba la Mpunga la Kapunga, lililobinafsishwa kwa Kampuni ya Export Trading Co. Ltd na Shamba la Mpunga la Mbarali lililo chini ya Highlands Estate Limited. Shamba la Kapunga liliuzwa kwa shilingi 3.5 bilioni wakati lile la Mbarali liliuzwa kwa shilingi 2.311 bilioni. Mashamba yote haya yalikuwa chini ya Shirika la Umma la NAFCO na miradi hii ilikuwa ni misaada kutoka kwa nchi rafiki ili kuiwezesha nchi kuzalisha chakula cha kutosha. Wakati Shamba la Kapunga lilikuwa ni msaada kutoka Serikali ya Japani, lile la Mbarali ilikuwa ni msaada kutoka Serikali ya China. Mashamba haya yalikuwa na miundombinu ya umwagiliaji, kinu cha kukoboa mpunga na hata mradi wa umeme wa maji (*mini hydro*). Ilikuwa ni miradi kabambe iliyojengwa na Serikali ya Awamu ya Kwanza na ya Pili katika juhudi za kujenga taifa imara na lenye uwezo wa kujilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pana utata juu ya ukubwa halisi wa eneo lililobinafsishwa katika Shamba la Kapunga. Mwaka 1984 Shirika la NAFCO liliwaomba wanakijiji ardhi kwa ajili ya mradi huu mkubwa wa kulima mpunga na Kijiji kikakubali kutoa hekta 5, 500 kwa NAFCO (rejea muhtasari wa Serikali ya Kijiji wa tarehe 14/11/1984 katika Mkutano wa kujadili maombi ya NAFCO kupatiwa Shamba la Kapunga). Tangazo la Serikali (GN) na pia Tangazo la kuuza shamba hilo katika magazeti (The Guardian la tarehe 12/07/2004), lililotolewa na PSRC, yalionesha kuwa eneo la shamba linalobinafsishwa ni hekta 5, 500. Ukubwa huu wa shamba ni sawa na ndio ambao uliidhinishwa na Serikali ya Kijiji, ilipokuwa inaridhia kuipatia NAFCO Shamba hilo la Kapunga**.** Hivyo, ukubwa wa shamba uliopaswa kuuzwa ni hekta 5,500 ambazo ndio Kijiji kilitoa kwa Shirika la NAFCO kwa ajili ya Mradi wa Shamba la Mpunga la Kapunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kubinafsishwa kwa Shamba la Mpunga la Kapunga, mkataba wa mauzo unaonesha kuwa Kampuni ya Export Trading Co. Ltd iliuziwa jumla ya hekta 7,370, yaani ziada ya hekta 1870 kutoka hekta ambazo Kijiji kilitoa kwa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara ya uamuzi huu unaotokana na maofisa wa iliyokuwa PSRC na sasa CHC wa kukaa Dar es Salaam kwenye viyoyozi na kuandika mikataba ni kwamba, Serikali imejikuta ikiuza kijiji kizima kwa mwekezaji na

mwekezaji kihalali kabisa anawaambia wanakijiji wahame katika eneo hilo. Suala hili halikubaliki hata kidogo. Hata kama tunataka uwekezaji wa kutoka kwa Mungu, hatuwezi kukubali aibu hii ya kuuza kijiji!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini pia kwamba, hapana maelewano kati ya Mwekezaji na Wanakijiji. Kamati inashauri Serikali ifuatilie ukweli wa maelezo ya Wanakijiji kwamba, mwekezaji amekuwa akiwanyanyasa kwa kuwachapa viboko na kuwapeleka jela pindi anapowakuta wakipita kwenye njia zilizopo kwenye mashamba yake.

Hata hivyo, mwekezaji amejibu tuhuma hizo kwa Kamati na kusema kuwa, sio kweli kwamba anawanyanyasa wananchi walio jirani naye. Mwekezaji anakiri kuwa tatizo la mpaka ndio chanzo cha matatizo yote na kuwa yupo tayari mazungumzo kufanyika ili kutatua tatizo hilo. Wananchi walitueleza pia kuwa, mwekezaji halimi mpunga bali analima jatropha (mibono kaburi), kitu ambacho mwekezaji amepinga na kusema hana mpango huo wa kulima jatropha. Kamati imemtaka mwekezaji azingatie makubaliano ya mauzo na kwamba, Serikali ifanye tathmini ya mradi huu baada ya miaka mitano kama inavyooneshwa kwenye Mkataba wa mauzo (*Sales Agreement*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nyaraka za Serikali zinathibitisha kuwa eneo halisi la Shamba la Kapunga lililobinafsishwa kwa mwekezaji ni kubwa kuliko kiasi stahiki cha hekta 5,500 ambacho NAFCO ilipewa kihalali na kijiji. Kamati inapendekeza yafuatayo:-

Eneo Hilo la ziada la hekta 1870 lirudishwe kwa kijiji husika ili kiwagawie wanakijiji wenye shida ya ardhi. Kwa kuwa mwekezaji alinunua eneo hilo la ziada kwa kufuata sheria na taratibu zote za manunuzi na ubinafsishaji, Serikali iwajibike kumfidia mwekezaji ama ikubaliane na kijiji kuhusu namna ya kuwafidia wanakijiji hilo eneo la ziada lililochukuliwa kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliridhishwa na kazi zinazofanywa na Mwekezaji katika Shamba la Mpunga la Mbarali, Kampuni ya Highlands Estates Limited. Wanakijiji walikiri kuwa na mahusiano mema na Mwekezaji huyo, kwa maana kwamba, amekuwa akiwasaidia kusafisha mifereji ya maji, akisaidia ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo, akisambaza kiasi cha umeme wanaozalisha kutumika katika nyumba za wananchi wenye uwezo wa kulipia gharama, akiwakodisha mashamba kwa bei nafuu na akiwapatia ajira katika mashamba hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo awali, Kamati ilifanya ziara ya ufuatiliaji wa zoezi la ubinafsishaji wa mashamba katika Mkoa wa Manyara. Ziara hii ilifanyika katika Wilaya ya Hanang, kwa kutembelea baadhi ya Mashamba yaliyokuwa chini ya NAFCO na yaliyokuwa yanaunda kitu kinachoitwa H.W.C. (Hanang Wheat Complex) huku Bassotu Plantation Ltd likiwa ni shamba mama.

Jumla ya Mashamba hayo na mwaka wa uanzishwaji katika mabano ni kama ifuatavyo: Bassotu Plantation Ltd (1968); Setchet Wheat Co. (1975); Mulbadaw Wheat

Farm (1979); Murjanda Wheat Co. (1980); Gawal Wheat Co. (1982); Gidagamowd Wheat Co. (1983); Warret Wheat Co. (1984); na CMSC – Central Maintenance Services Centre Ltd. (1984).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilizuru Shamba la Gidagamowd, Setchet na Murjanda, ambayo yameuzwa kwa M/S Ngano Ltd mwaka 2006 kwa jumla ya shilingi 3.45 bilioni. Shamba la Setchet lina ukubwa wa eneo la hekta 6, 300, Gidagamowd lina ukubwa wa hekta 6, 330 na Murjanda ni hekta 5,160.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba haya kwa pamoja yana jumla ya hekta 17,790 na yalianza kulimwa katika msimu wa 2007/2008 na yameshaendelezwa kwa 56% na mwekezaji ana mikakati ya kuyaendeleza hadi kufikia 65% katika msimu huu wa 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokutana na Mwekezaji, pamoja na Wananchi, ilibaini yafuatayo: Mwekezaji kusuasua katika uendelezaji wa Mashamba hayo; kutokuwepo kwa uhusiano mzuri baina ya Mwekezaji na Wananchi mfano ni kwa mwekezaji huyo kuzuia utumikaji wa lambo lililotengenezwa na Serikali kwa ajili ya mifugo lililopo pembeni ya shamba; na uzuiaji wa watu kupita katika njia zilizokatiza ndani ya shamba wakati mwingine huwakamata na kuwapeleka jela na kuzuia mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilibaini kuwa, mwekezaji huwa si muwazi na mkweli pale anapohitajiwa kutoa taarifa ya suala lolote linalohusiana na mashamba hayo; mfano alisema kwa ekari moja anapata magunia matatu ya ngano, jambo lililopingwa vikali na wananchi kwa kuwa wao wanazalisha ekari moja magunia manane hadi kumi; Mwekezaji kutofahamu mipaka ya mashamba yake, kwani wananchi wanalalamika kuwa amezidisha eneo la mashamba; kutokuwepo na uhakika wa ulipaji kodi na uharibifu wa maji ya bwawa kwa dawa za mimea katika bwawa linalotumika na binadamu na mifugo. Mwisho wa kikao hicho, mwekezaji alikubali shamba lipimwe ili kujua mipaka yake na kuwa gharama za upimaji huo atazitoa yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali isimamishe ubinafsishaji wa mashamba yaliyobakia mpaka hapo tathmini ya zoezi la ubinafsishaji itakapokamilika, kama ilivyoagizwa na Kamati hii kwa Shirika la CHC. Tathmini itaweza kuepuka mtindo wa sasa wa kumrundikia mwekezaji mmoja mashamba mengi. Wakati wa zoezi la upimaji wa mipaka, Serikali kupitia CHC ifanye yenyewe kwa kushirikiana na mamlaka za Serikali za Mitaa na mamlaka nyingine zote zinazohusiana na ardhi ili kuhakikisha kuwa, mwekezaji anabakia na shamba lile tu ambalo ameuziwa na kuepuka hali ya Kapunga ambayo tumeieleza hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inaishauri Serikali kufanya uchunguzi wa maji yaliyo katika Bwawa yanayolalamikiwa kuwa huwa yanaingia sumu ya dawa anayotumia mwekezaji ili kujua usalama wa maji hayo kwa matumizi ya binadamu na mifugo. Vile vile Wataalamu wa Kilimo wa Halmashauri waweze kutoa ushauri unaofaa wa namna ya kulima kwa mwekezaji huyo bila ya kuathiri chanzo hicho cha maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Kamati imemtaka mwekezaji kujitahidi kuendeleza na kuzalisha katika eneo lililobaki ili afikie 100%, kwani akifanikiwa kufanya

hivyo Pato la Taifa litaongezeka na ajira kwa wananchi wanaozunguka eneo hilo zitaongezeka. Pia Mwekezaji ahakikishe anakuwa na mahusiano mazuri na wananchi; awe muwazi pale anapohitajika mfano katika utoaji wa takwimu za anachozalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watafiti mbalimbali wamefanya utafiti kuhusiana na suala la ubinafsishaji wa mashamba wakiwemo watafiti wa Taasisi ya HakiArdhi. Watafiti hawa wametoa taarifa mbalimbali za utafiti ambazo watunga na watekelezaji wa sera, wanapaswa kuzisoma na kuona hatua za kuchukua kuhusiana na suala zima la ubinafsishaji wa mashamba. Kamati inashauri uchunguzi maalumu ufanywe na maelezo yake kutolewa Bungeni kuhusiana na wawekezaji ambao wamepewa mashamba na hasa mwekezaji wa RAI Group, ambaye analalamikiwa sana na Wananchi wa Hanang. Itakumbukwa kuwa ni mwekezaji huyu huyu wa RAI Group, ambaye alilileta zogo kubwa hapa Bungeni kufuatia yeye kubinafsishiwa Kiwanda cha Karatasi cha Mgololo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shamba la Mulbadaw lenye ukubwa wa hekta 5,390 na Karakana ya CMSC limeuzwa kwa M/S Haydom Lutheran Hospital mwaka 2005 kupitia mufilisi wake Tadayo Advocate & Co.  Shamba hili liliuzwa kwa shilingi 1.09 bilioni. Hali ya uzalishaji katika Shamba ni ya kuridhisha, kwani hekta 4,047 tayari zimeshalimwa, hata uhusiano uliopo baina ya Mwekezaji na Wananchi ni mzuri na wameweza kuanzisha Mradi wa Chakula Salama (*Food Security*), ambapo kiasi cha shilingi 42 milioni zinazotokana na shamba hilo zimetumika na familia zaidi ya 198 zimefaidika na mradi huo.  Vile vile wameshatumia kiasi cha shilingi 3 milioni kwa ajili ya kusaidia Shule za Qairo, Gaghata na kituo cha watoto yatima cha Hanang kilichopo katika maeneo ya Karakana ya CMSC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shamba la Bassotu lina ukubwa wa hekta 5,318, ambazo ni sawa na ekari 13,141, liko katika Tarafa ya Bassotu na ni miongoni mwa mashamba yaliyokuwa yamekusudiwa kubinafsishwa. Shamba hili limekaa kwa zaidi ya miaka kumi chini ya mufilisi Tadayo Advocate & Co. likingojea kibali cha Serikali ili liweze kubinafsishwa. Kwa mujibu wa mwakilishi wa CHC, kibali cha kuendelea na zoezi la ubinafsishaji wa Shamba la Bassotu, kimetolewa tarehe 30 Disemba, 2008 hivyo wapo katika mchakato wa kutangaza ili wapate mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Shamba hili Kamati ilikuta mali za umma zikiwa zimekaa kwa muda mrefu huku zikiharibika kutokana na kutokufanya kazi, mali hizo ni mabohari na matrekta ya kulimia yenye uwezo wa kulima ekari 300 kwa saa. Kamati pia ilibaini uwepo wa uvamizi wa wakulima wadogo ndani ya shamba hili, ambao wengi wao wamelima na wanaishi ndani yake, jambo linaloweza kupelekea kutokea kwa mvutano unaoweza kutokea baina ya wakulima hao wadogo na Serikali, pindi atakapotokea Mwekezaji katika shamba hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali ya uzalishaji kuwa ya kusuasua katika mashamba yaliyokwishabinafsishwa, Kamati inaishauri Serikali isimamishe mchakato wa kulibinafsisha Shamba la Bassotu ili wapewe Wananchi wa eneo hilo ambao wameonesha nia na jitihada za kuliendeleza au Shamba hilo wapatiwe JKT au Jeshi la Magereza ili walitumie kwa uzalishaji.  Pia ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali iwe

karibu na mufilisi ili iweze kujua nini kinaendelea katika usimamiaji na ufilisi wa Shamba la Bassotu na mali zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashamba ya Warret na Gawal yalitolewa kwa Wananchi wa Wilaya ya Hanang kwa uamuzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Lengo kuu likiwa ni kuwapatia wananchi walioko kwenye Hifadhi ya Mlima Hanang, ardhi mbadala ili kuuokoa mlima kutokana na uharibifu wa mazingira, kwani mlima huu ni chanzo kikubwa cha maji ambapo wakazi wapatao 79% wanakitegemea.

Shamba la Gawal lenye ukubwa wa ekari 16,605.5 na Warret lenye ekari 14,134.4, yalitolewa kwa matumizi ya kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa mchakato wa mwanzo wa kugawa mashamba haya ulikumbwa na mvutano baina ya jamii ya wafugaji na wakulima, hali iliyotishia upotevu wa amani na hivyo kupelekea zoezi la ugawaji wa ardhi kuchukua muda mrefu. Halmashauri ya Wilaya imejikuta ikitumia gharama kubwa kuendesha zoezi hili. Baada ya kikao kilichoitishwa na Mkuu wa Mkoa cha tarehe 21/7/2008 kilichoshirikisha wadau wote wanaohusika na mashamba haya, muafaka ulifikiwa kuwa mashamba ya Gawal na Warret yakabidhiwe kwa Halmashauri za Vijiji vinavyozunguka mashamba hayo ili Vijiji hivyo vigawe maeneo hayo badala ya Halmashauri ya Wilaya kufanya kazi ya ugawaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugawaji wa mashamba haya pia umehusisha na utengaji wa ekari 500 kwa kila shamba, kwa ajili ya akiba ya ardhi ya Halmashauri. Majengo yaliyokuwa yakitumika kama Kambi ya Gawal, yanatumika kwa huduma za Sekondari na kuanzishwa kituo cha kuhudumia na kufundishia Wafugaji. Kwa zile ekari 500 zilizotengwa ndani ya Shamba la Warret, ekari 200 zimepewa Jeshi la Magereza kwa ajili ya shughuli za kilimo na ilipokuwa Kambi ya Warret inatumiwa na Magereza kama Kambi ya Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na suala la ugawaji wa mashamba haya kuchukua muda mrefu, Kamati inaishauri Serikali kuihimiza Halmashauri ya Wilaya kufuatilia suala hili kwa ukaribu na kuwasisitiza Watendaji wa Serikali za Vijiji kuharakisha zoezi hili na vile vile wajiepushe kutumia suala la ukabila kama kigezo cha kugawa mashamba kwa kuwa nchi yetu haina ukabila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikanganyiko katika takwimu za ukubwa wa maeneo yanayobinafsishwa ikiwa ni pamoja na kutoeleweka vyema kwa malipo yanayofanywa na wawekezaji katika vyombo vya Serikali ni kasoro zisizotakiwa kuwepo katika Tanzania ya sasa. Kamati imebaini pia kwamba, zoezi la ubinafsishaji haliungwi sana mkono na wananchi wa kawaida, wanaozunguka maeneo yaliyobinafsishwa kwa sababu hawakuelimishwa juu ya uendeshaji mzima wa zoezi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inaishauri Serikali isimamie suala la ajira za Wafanyakazi wa mashamba yaliyo chini ya Wawekezaji ili waweze kupata mikataba

au barua za ajira ili wawe na uhakika na ajira zao, kwani itasaidia kujua haki zao kama makato ya NSSF na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya Kamati kuhusu mashirika ya umma imeambatanishwa pamoja na taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya uchunguzi maalumu kuhusu Shirika la Maendeleo la Taifa kuhusu Mradi wa Matinje Gold na hoja nyingine za wananchi kuhusu *NDC* ikiwemo hoja ya Kampuni ya Mwananchi Gold na Mkopo wa Barclays Bank kwa NDC, ambao inatuhumiwa kuwa ulitumika kinyume cha sheria kudhamini kampuni binafsi. Kamati iliunda Kamati Teule kushughulikia suala la NDC na tunapenda kukushukuru kwa kukubali ombi letu la kuunda Kamati Teule, ambayo iliongozwa na Makamu Mwenyekiti, Mama Estherina J. Kilasi, Mbunge wa Mbarali na ilitoa taarifa yake nzuri sana na tumeiambatanisha kama sehemu ya kiambatanisho na kukabidhiwa kwa Ofisi ya Katibu wa Bunge kutoa msaada wote kuhakikisha kuwa Kamati inafanya kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokutana na Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), mnamo tarehe 23 Agosti, 2008 kwa lengo la kuchambua na kujadili Taarifa ya Hesabu zake zinazoishia tarehe 30 Juni, 2007, ilijitokeza hoja ya matumizi ya shilingi 1.5 bilioni bila ya kibali cha Bodi. Fedha hizo zilikwenda kudhamini mkopo uliotolewa na Benki ya Investec ya Mauritius kwa Kampuni moja ya Singapore iitwayo Uhuru Capital Management, kwa ajili ya kugharimia usanifu na ujenzi wa mtambo wa kusagisha miamba na kupembua mchanga ili kuweza kupata dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati kwa kuzingatia Kanuni ya 114, kifungu kidogo cha (18), iliunda Kamati ndogo ili kuweza kufuatilia uwepo wa mtambo huo huko Matinje uliosemekana kununuliwa kwa kutumia kiasi hicho cha fedha. Kamati hiyo ndogo ilifanya ziara ya kwenda Matinje tarehe 6 Januari, 2009 kushuhudia hali halisi iliyopo pale. Kamati iliitaka Kamati Ndogo kufuatilia kuhusu hoja zifuatazo kutokana na hesabu za Shirika la NDC: Hoja za malalamiko ya wananchi kuhusu uuzwaji wa nyumba za NDC; hoja kuhusu utenguzi wa hatimiliki za viwanja kadhaa vilivyokuwa mali ya NDC eneo la Msasani Peninsular; hoja kuhusu hesabu za Kampuni ya Mwananchi Gold Company Ltd kwa miaka mitatu; hoja kuhusu uwekezaji wa NDC katika makampuni ya Matinje Gold Company Ltd na Uhuru Infrastructure Company Ltd.; na hoja kuhusu mkopo wa Benki ya Barclays kwa Shirika la NDC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeziona taarifa za hesabu zilizokaguliwa za Kampuni ya Mwananchi Gold kwa miaka inayoishia Machi 31, 2004, 2005 na 2006. Ukaguzi wa hesabu kwa miaka yote mitatu, umefanywa na Kampuni ya PWC. Kampuni hii ni kampuni binafsi yenye wanahisa wafuatao na asilimia ya hisa wanazomiliki zimeoneshwa: Benki Kuu ya Tanzania – 35%; Mwananchi Trust Group - 30%; Chimera Limited – 20%; na NDC – 15%.

Hata hivyo, Kamati imegundua kuwa kati ya mwaka 2002 wakati kampuni inaanzishwa hadi mwaka 2004, wanahisa walikuwa wawili tu; BOT ikiwa na 57% ya hisa na NDC ikiwa na 43% ya hisa. Makampuni haya mengine yaliingia vipi katika mradi huu; ni suala ambalo Kamati haikulishughulikia na hivyo haiwezi kulieleza Bunge lako Tukufu. Hata hivyo, Kamati ina nyaraka za wamiliki wa makampuni mawili ya Mwananchi Trust Group, ambayo ni kampuni ya hapa nchini na Kampuni ya Chimera Limited ambayo wamiliki wake wanatoka nchini Italy.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Mwananchi Gold ilianzishwa kwa lengo la kuongeza thamani ya madini ya dhahabu hapa nchini ili kuepuka kuuza dhahabu ghafi. Kampuni ilianza shughuli zake kibiashara mwezi Januari, 2006. Kampuni hii ilianzishwa kwa agizo la Serikali la kuifanya sekta isiyo rasmi kwa wachimbaji wadogo kuwa rasmi na kuweza kuwasaidia kupata vifaa vya kisasa na soko kwa madini yao na hivyo kukuza uchumi wa nchi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Matinje Gold ilianzishwa mwaka 2001 kama *special purpose vehicle (SPV)*, kwa ajili ya mradi wa wachimbaji wadogo wadogo wa Matinje *(Matinje Small Scale Mining)*. Kampuni hii ilianzishwa na NDC kwa makubaliano na Serikali ya kuwekeza na kuwaendeleza wachimbaji wadogo wa madini waliopo katika Kijiji cha Matinje, Wilaya ya Igunga, Tabora. Wanahisa wa Matinje ni Kampuni ya Uhuru Infrastructure Fund Ltd., yenye asilimia 60 ya hisa na NDC yenye asilimia 20 ya hisa. Hata hivyo, katika kampuni ya UIF Ltd., NDC inamiliki hisa 50%. Wachimbaji wadogo wenye PML wanamiliki 20% ya kampuni hii. Kampuni ilianzishwa kwa madhumuni yafuatayo: Kusafisha dhahabu ya wachimbaji wadogo kwa kutumia teknolojia rahisi; kuchenjua mchanga wa mabaki ya wachimbaji wadogo kwa teknolojia ya kisasa zaidi na kuzalisha dhahabu; kuirasimisha sekta ya wachimbaji wadogo wa dhahabu; na kuhakikisha kuwa mitambo, zana na mashine zinazotumika katika uchimbaji na usafishaji wa dhahabu vinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi yote miwili, licha ya kuwa ni miradi mizuri kwa kuokoa wananchi na kukuza uchumi wa Taifa, imekwama na imeshindwa kufanya kazi zake kwa sababu mbalimbali. Benki Kuu ya Tanzania ilitangaza kujitoa kama mwanahisa katika Kampuni ya Mwananchi Gold mwaka 2008 na hivi sasa kampuni inapunguza wafanyakazi kwa lengo la kuifunga *(wound up)*. Kampuni ya Matinje ilipata tatizo kubwa sana la mtambo ulionunuliwa kushindwa kufanya kazi na *strategic investor* kuwa ni mtu asiye na mtaji, ambaye ilibidi adhaminiwe mkopo wake na fedha za NDC. Fedha za dhamana hii zimepotea maana zimechukuliwa na Benki huko Mauritius ,baada ya mwekezaji huyo kushindwa kulipa mkopo wake aliouchukua kutoka Benki ya Investec ya Mauritius.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi hiii miwili inahusiana na ni miradi muhimu sana kama ingefanikiwa. Miradi hii ingesaidia kukuza uchumi wa nchi kwa kuongeza Pato la Taifa, ingetengeneza ajira kwa vijana, ingewezesha wachimbaji wadogo kupata teknolojia mpya na ingewezesha Sekta ya Madini kushiriki kikamilifu katika kupunguza umasikini. Kamati ina maoni kuwa miradi hii ifufuliwe upya na kufanikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imepata maelezo ya kina sana kuhusiana na uchunguzi wao juu ya Mradi wa Matinje na upotevu wa fedha za NDC katika mradi huu. Kamati imeiomba Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuipitia Taarifa ya Kamati na kupata maoni ya ukaguzi juu ya tuhuma hizi. Vile vile kama ilivyopendekezwa hapo juu, uchunguzi huu pia utoe majibu ya jinsi ya kufufua miradi hii ili iweze kufaidisha nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo katika matokeo hayo ya uchunguzi kutabainika uvunjaji wowote wa sheria, basi Kamati inaishauri Serikali ichukue hatua za haraka kuwawajibisha wale wote watakaobainika kuhusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetumia muda mwingi katika taarifa hii kulieleza Bunge lako Tukufu yaliyojiri Kamati ilipokuwa inatekeleza majukumu yake, ambayo msingi wake mkuu ni kuhakikisha panakuwepo na ufanisi wa mashirika na taasisi za umma. Hata hivyo, yapo mambo kadha wa kadha ambayo kwa maoni ya Kamati ni vyema kuipongeza na kuitia moyo Serikali yetu. Kamati inapongeza hatua zifuatazo:-

(a) Kuwafikisha mbele ya vyombo vya sheria, watumishi wa umma ikiwa ni pamoja na viongozi mbalimbali wa serikali, waliotuhumiwa kuhusika na ubadhirifu wa fedha na mali za umma katika Benki Kuu. Kamati inashauri hatua kama hizi ziendelee kuchukuliwa kwa umakini mkubwa, kwa lengo la kujenga utamaduni wa nidhamu na uadilifu kwa mali za taifa, tabia ya uwazi na uwajibikaji na uzalendo wa watumishi hao na Watanzania kwa ujumla katika kulitumikia taifa lao.

(b) Kuvunja mikataba yote isiyo na tija kwa taifa. Mfano, Mkataba kati ya Serikali na Kampuni iliyoitwa ya kufua umeme ya Richmond Development Company LLC.

(c) Hatua ya Gavana wa Benki Kuu, Prof. Benno Ndulu, kujitoa katika kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi wa Ndani ya Benki Kuu ili kuongeza uhuru zaidi wa Kamati hiyo katika kutekeleza majukumu yake.

(d) Serikali kuungana na mawazo ya Kamati kwa kumshauri haraka iwezekanavyo, Mhe. Rais kumteua mara moja Mwenyekiti wa Halmashauri ya Biashara za Nje (BET), ambayo utendaji wake ulianza kulegalega.

(e) Wajumbe wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kuacha kusaini hundi za malipo.

(f) Uamuzi wa Serikali kukubaliana na pendekezo la Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kutokuuza Shirika la Bima la Taifa na hivyo kuzuia ubinafsishaji wake.

(g) Serikali kukamilisha uuzaji wa hisa za Benki ya NMB kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ana orodha tofauti ya Mashirika ya Umma (158) na Msajili wa Hazina ana

orodha tofauti (193), Kamati inaitaka Serikali ihakiki usahihi wa taarifa hizi na inaungana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutaka hati za hisa za Serikali katika baadhi ya mashirika, ambapo uwekezaji wa Serikali uliondolewa katika orodha ya Msajili wa Hazina katika mazingira ya kutatanisha na bila maelezo ya kuridhisha, zirudi kwenye kumbukumbu za Serikali na pale ambapo kuna mabadiliko yoyote kuhusiana na umiliki huo, basi mabadiliko hayo yatolewe maelezo ya kutosha.

Kwa kuwa kupungua kwa gawio na michango mingine kutoka mashirika ya umma kwenda serikalini ni ishara kuwa Mashirika ya Umma yamepunguza ufanisi na/au udhibiti na hivyo kupata hasara na kwa kuwa mmiliki wa mali zote za Serikali kwenye mashirika ya umma ni Msajili wa Hazina; hivyo basi, Kamati inamtaka Msajili wa Hazina aimarishe usimamizi wa Mashirika ya Umma ili yafanye kazi kwa ufanisi na kutoa faida kwa nchi. Kutokana na uzito wa majukumu haya ya Ofisi ya Msajli wa Hazina kama Mhisa pekee katika Mashirika na Taasisi za Umma, Kamati inashauri Ofisi hiyo ijitegemee, isiwe chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa uhuru na mamlaka zaidi.

Kamati inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ahakikishe kuwa Mashirika ya Umma ambayo yapo kwenye orodha ya Msajili wa Hazina, lakini hayajawasilisha hesabu zao za sasa zilizokaguliwa na taasisi mpya ambazo hazikuwa zimekaguliwa hesabu zao, pia yawasilishe hesabu zao kwa ukaguzi ili kuhakikisha mitaji ya umma haipotei au kutumika vibaya.

Kwa kuwa Kanuni ya 30 ya Sheria ya Fedha za Umma, 2001, inalitaka kila Shirika la Umma kuwa na Kamati ya Ukaguzi wa Ndani kwa lengo la kuongeza nidhamu zaidi katika kusimamia fedha za umma na kuweza kugundua mapema na kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma; na kwa kuwa bado yapo mashirika kadhaa ambayo mpaka mwaka wa fedha wa 2006/2007 unamalizika yalikuwa bado hayana Kamati za Ukaguzi wa Ndani; hivyo Kamati inayataka mashirika yote ya umma kuteua Kamati au Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani mara moja.

Kwa kuwa Kifungu Na. 3(1) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya 2004, kinaelezea Kitengo cha usimamizi wa manunuzi kama ni kitengo au idara katika kila chombo cha umma, kikishughulikia utekelezaji wa shughuli za ununuzi, hivyo basi, Kamati inayataka Mashirika yote ya Umma kuanzisha mara moja vitengo vya usimamizi wa manunuzi ili kuhakikisha kuwa manunuzi yanafuata sheria na kanuni husika na vilevile kupata thamani ya pesa katika manunuzi ya umma.

Kamati inayataka Mashirika ya Umma kuandaa na kutumia mipango ya manunuzi kwa mwaka ili kuepuka ununuzi wa dharura kila inapowezekana na pia kuepuka kufanya manunuzi ya kiholela ambayo yanayofanyika kinyume na kifungu Na. 45 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2004 na ambayo yanaleta mianya ya rushwa.

Kamati inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa Taarifa yenye kuonesha thamani ya fedha ya manunuzi holela kwenye Mashirika ya

Umma ili Umma uweze kuona madhara ya kifedha na ya kiuchumi ya kutofuata sheria na kanuni za manunuzi kwenye Mashirika ya Umma.

Kamati inayataka mashirika yote ya umma na Taasisi za Serikali kuhakikisha kuwa makato ya kisheria, kama vile makato halali kwa ajili ya malipo ya uzeeni na ya bima ya afya, yanawasilishwa kwa mamlaka husika wakati muafaka ili kuepuka tozo kubwa ambazo mashirika husika yanatozwa kama adhabu ya kutotimiza sharti hilo la kisheria na kuepuka matatizo katika ulipaji wa mafao ya watumishi wanapofikia wakati wa kustaafu. Watendaji wa mashirika watakaokiuka wajibu huu wa kisheria, wachukuliwe hatua mara moja kwa kuhatarisha maisha ya ustaafu ya watumishi wao na kukwepa kodi pia; vilevile mifumo ya mashirika ya kudhibiti hizo fedha iimarishwe.

Kamati inashauri Serikali iangalie uwezekano wa kuyaongezea mtaji mashirika ambayo yanafanya kazi kwa kusuasua kwa sababu ya kuwa na kiasi kidogo cha mitaji ya kuwekeza ili yaweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na ili kuokoa baadhi ya mashirika yasifungwe. Hali kadhalika, Kamati inaishauri Serikali iongeze ruzuku ya uendeshaji kwa taasisi ambazo kwa kawaida hazina wigo mpana wa mapato ili yaweze kumudu gharama za kujiendesha kwa mfano, Chuo cha Wanyamapori Moshi (MWEKA), mapato yake yanategemea zaidi ada za wanafunzi ambazo hazitoshelezi kiasi kwamba, kinashindwa hata kuhudumia magari yake yanayowapeleka wanafunzi katika mazoezi porini. Kamati pia inashauri Kodi ya Usimamizi (*Regulatory Fees)* ya Mazao ya Biashara irudishwe kwa Bodi za Mazao, kwani ilikuwa inazisaidia Bodi hizi kupata mapato ambayo kwa kiasi kikubwa yalitumika kuendesha mashirika hayo.

Kamati inaitaka Serikali kuongeza kasi ya kushughulikia tatizo la mikopo ya Serikali kwa Mashirika ya Umma na madeni mengi ambayo hayalipwi na mashirika haya kwa Serikali au na wadeni sugu kwa mashirika haya ili tatizo hili liache kujirudia kila mwaka katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hali kadhalika, Kamati inaitaka Serikali kujiepusha na utoaji wa Dhamana za Kimikopo (*Loan Guarantee*), kwa mashirika kiholela kwani matokeo yake ni kushindwa kulipa madeni hayo na hivyo kupelekea mashirika hayo kushindwa kujiendesha; mfano, PSPF ilitoa mkopo wa shilingi 53 bilioni kwa Bodi ya Mikopo ambao mpaka sasa bado haujarejeshwa.

Kamati inaitaka Serikali kuwa na programu maalumu ya kuhakikisha mali za Mashirika ya Umma zinapata hatimiliki kwa haraka na zinakuwa na Bima za Mali ili kuzuia uwezekano wa upotevu wa mali hizo pale kunapokuwa na migogoro au majanga yanapotokea.

Kamati inapendekeza uchunguzi maalumu wa Kibunge ufanyike katika mashirika yote yaliyobinafsishwa kwa kuwa na ubia wa Serikali ili kuweza kutambua uendeshaji wa mashirika haya na usalama wa hisa za Serikali na vilevile kushauri uwezekano wa hisa hizo za Serikali kuuzwa kwa Wananchi wengi zaidi kupitia Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE). Hali kadhalika, Kamati inaitaka Serikali ihakikishe mali za mashirika yaliyo katika hatua za ubinafsishwaji zinalindwa wakati tunaangalia upya zoezi hili na manufaa yake kwa Taifa na uchunguzi huo pia upendekeze hatua za kisheria dhidi ya

Wawekezaji ambao wataonekana kukiuka Makubaliano ya Ubia (*Terms of Joint Venture*), ikiwemo hatua ya kurejesha shirika husika kwenye mikono ya Serikali.

Kwa kuwa Kamati imebaini kwamba, zoezi la ubinafsishaji haliungwi sana mkono na Wananchi wa kawaida wanaozunguka maeneo yaliyobinafsishwa, kwa sababu hawakuelimishwa juu ya uendeshaji mzima wa zoezi hilo au kwa kuwa wana migogoro na wawekezaji; na kwa kuwa Kamati imegundua hakuna ufanisi na tija katika mashirika kadhaa ya umma, yakiwemo mashamba mengi ya umma yaliyobinafsishwa au yanayosubiri kufilisiwa na kubinafsishwa; hivyo basi, Kamati inalitaka Shirika Hodhi linaloshughulikia Madeni na Mali (*Consolidated Holding Corporation - CHC*), kufanya tathmini ya zoezi zima la ubinafsishaji na kuwasilisha taarifa yake ya uchunguzi kwa Kamati kabla ya kuwasilishwa Bungeni. Kamati pia inashauri kuwa, wakati uchunguzi huo unaendeshwa, zoezi la kubinafsisha mashirika yote yaliyobakia, lisimame mpaka hapo taarifa itakapotolewa na mapendekezo yake kujadiliwa na kupitishwa au kupingwa.

Kwa kuwa Kamati ilitoa pendekezo mahususi serikalini kuwa STAMICO iondolewe katika orodha ya mashirika ya kubinafishwa (*despecified*) kama ilivyopendekezwa awali na Kamati ya Rais kuhusu Sekta ya Madini (Kamati ya Bomani), vilevile Kamati inapendekeza kuwa mali zote ikiwemo hisa zilizokuwa za STAMICO ambazo bado hazijauzwa na zinashikiliwa na Msajili wa Hazina, zirejeshwe STAMICO na pia ipewe mtaji wa kutosha ili iweze kushiriki kikamilifu katika uwekezaji wa Sekta ya Madini kama Kampuni ya Kuwezesha Maendeleo ya Sekta (*Resource Development Company)* na hivyo Taifa kufaidika. Kwa ujumla, Kamati inapendekeza suala la masharti ya makampuni yaliyoorodheshwa kwa ajili ya kubinafsishwa (*specified companies),* liangaliwe upya kwani utaratibu huu umeingiza hasara kubwa sana kwa nchi kufuatia mali nyingi za mashirika kupotea katika kipindi hiki cha kuorodheshwa kwa ajili ya kubinafsishwa (*specification),* ambapo mashirika haya husimamisha uwekezaji.

Kamati imebaini kuna uzembe na utata mkubwa katika kupima, kukusanya na kuhifadhi takwimu sahihi za ukubwa na umiliki wa mashamba yaliyobinafsishwa na za malipo stahiki ya mashamba yaliyouzwa hivyo inaitaka CHC kukusanya na kuhakiki taarifa zote za malipo, pamoja na kupata takwimu sahihi za mashamba yote nchini yaliyobinafsishwa na yaliyo katika mchakato huo, kwa kufanya ziara rasmi za kuona badala ya kutolea takwimu maofisini na hivyo kutojua uhalisia wa mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna malalamiko kutoka kwa Wananchi kuwa baadhi ya Wawekezaji hawatumii mashamba ipasavyo kama ilivyoagizwa kwenye Mkataba wa Mauzo (*Sales Agreement*), kati ya Mwekezaji na Serikali, mathalani katika Shamba la Mpunga la Kapunga ambapo Wananchi waliieleza Kamati kuwa Mwekezaji halimi mpunga bali analima mibono kaburi (*jatropha*), kitu ambacho Mwekezaji amepinga na kusema hana mpango wa kulima jatropha. Tumeweka kati ya viambatanisho nakala ya barua ambayo wakili aliiletea Kamati kueleza hoja zote ambazo wananchi walizizungumza ili kutenda haki. Kamati inawataka Wawekezaji wote wazingatie makubaliano ya mauzo na kwamba, Serikali ifanye tathmini ya miradi yote ya uwekezaji katika muda muafaka uliooneshwa kwenye mkataba husika na

isimamie/ifuatilie mara kwa mara kuhakikisha kuwa, Wawekezaji hawakiuki hadidu za rejea za mikataba hiyo.

Kamati inaishauri Serikali isimamie suala la ajira za wafanyakazi wa mashamba yaliyo chini ya Wawekezaji ili waweze kupata mikataba au barua rasmi za ajira ili wawe na uhakika na ajira zao, kwani itasaidia kujua haki zao kama makato ya NSSF na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kamati imebaini kutokuwepo kwa uhusiano mzuri baina ya baadhi ya Wawekezaji na Wananchi; kwa mfano, uhusiano tete unaotokana na Mwekezaji katika mashamba ya Gidagamowd, Setchet na Murjanda kuzuia utumikaji wa lambo lililotengenezwa na Serikali kwa ajili ya mifugo lililopo pembeni ya mashamba na uzuiaji wa watu kupita katika njia zilizokatiza ndani ya mashamba na wakati mwingine huwakamata, kuwatoza faini na kuwapeleka jela na kuzuia mifugo yao na ule unaotokana na Mwekezaji katika shamba la Kapunga ambaye Wananchi wanadai amekuwa akiwanyanyasa kwa kuwachapa viboko na kuwapeleka jela pindi anapowakuta wakipita kwenye njia zilizopo kwenye mashamba yake; hivyo basi, Kamati inawataka Wawekezaji wahakikishe kuwa, wanakuwa na mahusiano mazuri na Wananchi vilevile Serikali na Serikali za Mitaa zihakikishe zinachunguza malalamiko ya wananchi na kuhakikisha kuna programu za ujirani mwema za kujenga mahusiano mazuri na kuzuia migogoro kati ya makundi haya mawili, pamoja na kuingia mikataba inayojali haki za Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni ekari 150 tu zilizogawiwa au kuuzwa kwa wakulima wadogowadogo kati ya jumla ya ekari 844 zilizouzwa na Serikali kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, japo eneo lililobakia halitumiwi na Halmashauri kuzalisha kwa tija na kwa kuwa kiasi kilichogawiwa au kilichouzwa hakikidhi mahitaji makubwa ya wakulima kupata mashamba, Kamati inaitaka CHC na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, kuhakikisha kuwa mashamba yote yaliyobakia ambayo bado hayajauzwa, yanagawiwa kwa wananchi ili waweze kupata ardhi ya kulima na kuzalisha mali. Hali kadhalika, Kamati inasisitiza kuwa mashamba haya yasikodishwe kwa Wananchi bali Wananchi wagawiwe kwa utaratibu ambao Halmashauri na Serikali za Vijiji kupitia Mikutano Mikuu ya Vijiji vitauweka kwa mujibu wa Sheria Na. 4 na Na. 5 za Ardhi za 1999. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa uzalishaji katika Shamba la Mahindi Mbozi ambalo lipo chini ya usimamizi wa CHC ni wa kusuasua tangia msimu wa mwaka wa 1996/1997, ambapo katika shamba lenye ukubwa wa hekta 4,840 zililimwa na kupandwa hekta 32 tu badala ya hekta 499 zilizolimwa na kupandwa katika msimu wa 1995/1996 na ilitaarifiwa kuwa, Serikali imeonesha hatua za kutaka kulibinafsisha Shamba hili tangia mwaka 1992; hivyo, kwa kuwa lengo la ubinafsishaji ni kuinua uchumi wa nchi na Wananchi na kwa kuwa Wananchi wapatao laki moja na nusu wa Vijiji vinavyolizunguka Shamba hilo wanahitaji ardhi ya kulima na wanao uwezo wa kununua shamba hilo kwa matumizi hayo, Kamati inaishauri Serikali kuligawa shamba hili kwa Wananchi ili wapate ardhi ya kulima na kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula nchini. Vilevile Kamati inaomba maelezo ya Serikali kuhusu taarifa kuwa,

Kampuni ya Tanzania Breweries imeomba au imepewa hekta 500 katika shamba hili la Mbozi ili kulima shayiri na pia Kamati inaitaka Serikali izingatie ushauri wa awali wa Kamati katika uamuzi wowote utakaochukuliwa kuhusu ombi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utatuzi wa kwa kuwa nyaraka za Serikali zinathibitisha kuwa eneo halisi la Shamba la Kapunga lililobinafsishwa kwa Mwekezaji ni kubwa kuliko kiasi stahiki cha hekta 5,500 ambacho NAFCO ilipewa kihalali na Kijiji husika, Kamati inapendekeza eneo hilo la ziada la hekta 1,956 lirudishwe mara moja kwa kijiji husika ili liwagawie wanakijiji wenye shida ya ardhi. Kwa kuwa Mwekezaji alinunua eneo hilo la ziada kwa kufuata sheria na taratibu zote za manunuzi na ubinafsishaji, Kamati inaitaka Serikali iwajibike kumfidia Mwekezaji huyo; ama ikubaliane na Kijiji kuhusu namna ya kuwafidia wanakijiji hilo eneo la ziada lililochukuliwa kwao ili wapate eneo mbadala la kuzalisha na kuongeza Pato la Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa Mwekezaji wa Mashamba ya Gidagamowd, Setchet na Murjanda alianza kuyalima mashamba haya, ambayo kwa pamoja yana jumla ya hekta 17,790, katika msimu wa mwaka 2007/2008 na yameshaendelezwa kwa 56% tu na kuwa Mwekezaji ana mikakati ya kuyaendeleza hadi kufikia 65% katika msimu huu wa mwaka 2008/2009 kama tulivyoelezwa. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali iangalie upya utaratibu wa kumrundikia mwekezaji mmoja mashamba mengi. Hata hivyo, inamtaka Mwekezaji kuendeleza na kuzalisha katika eneo lililobaki ili afikie 100%, kwani akifanikiwa kufanya hivyo Pato la Taifa litaongezeka na ajira kwa wananchi wanaozunguka eneo hilo zitaongezeka.

Kamati pia ilibaini kutokuwepo na uhakika wa ulipaji kodi na kuwa mwekezaji huwa si muwazi na mkweli, pale anapohitajiwa kutoa taarifa ya suala lolote linalohusiana na mashamba hayo. Mfano, alisema kwa ekari moja anapata magunia ya ngano matatu, jambo lililopingwa vikali na wananchi kwa kuwa wao wanazalisha ekari moja magunia ya ngano manane hadi kumi. Kamati inamtaka Mwekezaji awe muwazi pale anapohitajika kutoa taarifa na inaitaka Serikali ihakikishe inasimamia suala hili ili wananchi wapate haki yao ya Kikatiba (Ibara ya 18) ya kupata taarifa zinazohusu maendeleo yao na ya nchi yao. Vilevile Kamati inaishauri Serikali kufanya uchunguzi wa maji yaliyo katika bwawa, yanayolalamikiwa kuwa huwa yanaingia sumu ya dawa anayotumia mwekezaji ili kujua usalama wa maji hayo kwa matumizi ya binadamu na mifugo. Hali kadhalika, Wataalamu wa Kilimo wa Halmashauri waweze kutoa ushauri unaofaa wa namna ya kulima kwa Mwekezaji huyo bila ya kuathiri chanzo hicho cha maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Shamba la Bassotu lenye ukubwa wa hekta 5,318 ambazo ni sawa na ekari 13,141 ni miongoni mwa mashamba yaliyokuwa yamekusudiwa kubinafsishwa; na kwa kuwa shamba hili limekaa kwa zaidi ya miaka kumi chini ya Mufilisi Tadayo Advocate & Company, likingojea kibali cha Serikali ili liweze kubinafsishwa, kibali ambacho kimetolewa tarehe 30 Disemba, 2008 kwa mujibu wa CHC na sasa lipo katika mchakato wa kutangazwa ili lipate mwekezaji japo kuna uwepo wa wakulima wadogowadogo ndani ya shamba hili, ambao wengi wao wamelima na wanaishi ndani yake, jambo linaloweza kupelekea kutokea kwa mvutano unaoweza

kutokea baina ya wakulima hao wadogowadogo na Serikali, pindi atakapotokea mwekezaji katika shamba hilo; na kwa kuwa Kamati ilikuta mali za umma zikiwa zimekaa kwa muda mrefu huku zikiharibika kutokana na kutokufanya kazi, mali hizo zikiwa ni pamoja na mabohari na matrekta ya kulimia yenye uwezo wa kulima ekari 300 kwa saa; na kwa kuwa kwa ujumla hali ya uzalishaji ni ya kusuasua katika mashamba yaliyokwishabinafsishwa, Kamati inaishauri Serikali isimamishe mchakato wa kulibinafsisha Shamba la Bassotu ili wapewe Wananchi wa eneo hilo, ambao wameonesha nia na jitihada za kuliendeleza au Shamba hilo wapatiwe Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) au Jeshi la Magereza ili walitumie kwa uzalishaji. Pia ni ushauri wa Kamati kuwa, Serikali iwe karibu na Mufilisi ili iweze kujua nini kinaendelea katika usimamiaji na ufilisi wa Shamba hilo na mali zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa mchakato wa mwanzoni wa kugawa Mashamba ya Warret na Gawal ulikumbwa na mvutano baina ya Halmashauri ya Wilaya ya Hanang na Uongozi wa baadhi ya vijiji, pamoja na baina ya jamii ya wafugaji na wakulima. Hali hii ilitishia upotevu wa amani na hivyo kupelekea zoezi la ugawaji wa ardhi kuchukua muda mrefu, ambapo Halmashauri ya Wilaya imejikuta ikitumia gharama kubwa kuendesha zoezi hili. Japokuwa baada ya kikao kilichoitishwa na Mkuu wa Mkoa cha tarehe 21/7/2008, kilichoshirikisha wadau wote wanaohusika na mashamba haya, muafaka ulifikiwa kuwa mashamba hayo yakabidhiwe kwa Halmashauri za Vijiji vinavyozunguka mashamba hayo ili Vijiji hivyo vigawe maeneo hayo badala ya Halmashauri ya Wilaya kufanya kazi ya ugawaji. Kamati imebaini kuwa, bado zoezi hili halijakamilika kikamilifu; hivyo, inaishauri Serikali kuihimiza na kuisimamia Halmashauri ya Wilaya kufuatilia suala hili kwa ukaribu na kwa haki na kuwasisitiza Watendaji wa Serikali za Vijiji kuharakisha zoezi hili na vilevile wajiepushe kutumia suala la ukabila kama kigezo cha kugawa mashamba kwa kuwa nchi yetu haina ukabila na pia maslahi binafsi yadhibitiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia Kanuni 114(17) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, Kamati imeitaka Serikali kuhakikisha Watanzania hawakosi wala hawaingii katika shida ya mgawo wa umeme kwa Mamlaka husika kununua mitambo ya umeme itakayoona inafaa kwa maana ya ubora na uwezo wa mitambo hiyo pasipo kukiuka sheria za nchi. Katika kutekeleza hili, Serikali ijitahidi kwa uwezo wake wote kuhakikisha kuwa, hata huu mgawo unaojirudia hivi sasa mara kwa mara kutokana na kuharibika kwa mashine za SONGAS unakoma mara moja na kuwe na mpango madhubuti wa kuhakikisha kuwa nchi haiingii kwenye giza tena. Hali kadhalika, Kamati inapendekeza yafuatayo kuhusu Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO):-

(i) Shirika linapaswa kuongeza juhudi za kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kupunguza umeme unaopotea kwa kuwekeza katika kukarabati njia za kusafirisha umeme na juhudi zifanyike ili kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutumia gesi, kwani imeonekana kuwa umeme wake ni rahisi sana. Katika kutekeleza hili, Kamati inapenda kurejea ushauri wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Ripoti yake ya mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2007 kwamba, Serikali ipunguze kuingilia utendaji wa TANESCO ili ikitokea suala lolote, TANESCO yenyewe iwajibike, badala ya sasa ambapo hakuna wa kuiwajibisha kwa sababu ya menejimenti hodhi

(*micromanagement*) ya Serikali. Mikataba yote ambayo TANESCO iliingia na wawekezaji haikuingiwa na Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO, iliingiwa na Serikali. Sasa Kamati inashauri kwamba, utaratibu huo ukome. TANESCO yenyewe iingie mikataba na yakizuka ya kuzuka, wao wenyewe wawajibike na siyo hali ambayo inaendelea hivi sasa.

(ii) Kamati ilifuatilia na kuguswa sana na suala la IPTL na kama mnavyofahamu, tuna mkataba wa mpaka mwaka 2024 na IPTL. Kamati inaomba suala hili limalizwe kwa haraka nje ya mahakama ili kuharakisha ubadilishaji wa mtambo huo ili utumie gesi na hivyo kuongeza uzalishaji wa umeme wa 100MW ambao unatakiwa hivi sasa. Waheshimiwa Wabunge, hivi sasa IPTL haiuzi umeme TANESCO na kama mnavyofahamu. wakati IPTL wanakuja waliweka viwango vya kukokotoa ile wanaita *capacity charge* kutokana na mtaji na faida, kama kanuni za kawaida zinavyotakiwa, wakasema mtaji waliowekeza ni bilioni 36, lakini uchunguzi umeonesha kwamba, IPTL waliwekeza shilingi 50,000 tu. Mpaka mwezi Mei, 2007 tayari Taifa limewalipa IPTL jumla ya bilioni 221 na tume-*over pay* sana. Kwa hiyo, Kamati inashauri kwamba, kiwango cha fedha kilichopo kwenye *escrow account* ndicho hicho hicho kitumike kumaliza madeni yaliyopo na vilevile kufanyia marekebisho mtambo huo ili utumie gesi; kuna fedha ambazo zipo kwenye *escrow account* ambazo TANESCO walikuwa wanazilipa IPTL hawajazichukua. Kwa hiyo, Kamati inashauri kwamba, katika mpango mzima wa kuichukua IPTL na kuibadilisha, Serikali isitolee fedha nyingine fedha zile ndiyo zitumike.

(iii) Kufuatia maelezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamati inashauri kuwa mkataba wa SONGAS upitiwe upya ili kupunguza gharama za umeme (*capacity charges)*, kwani ni kubwa mno kuliko kampuni nyingine yoyote inayoiuzia umeme TANESCO; na kwa kuwa Serikali kwa kupitia Mashirika yake matatu (TANESCO, TPDC na TDFL) inamiliki asilimia 46 ya hisa za SONGAS, hivyo majadiliano haya yanapata nguvu zaidi. Katika kutekeleza hili iwapo SONGAS haitakubaliana na Serikali katika azma hii ya kupunguza mzigo mzito kwa TANESCO katika gharama za umeme na hasa suala la *capacity charges;* na kwa kuwa mkataba kati ya SONGAS na TANESCO unamalizika mwaka 2024, basi Serikali au TANESCO inunue hisa zilizobakia (54%) za SONGAS (*hostile take over*), kwa maana hatua hii ya kununua hisa za SONGAS na hivyo kumiliki mradi mzima itakuwa na manuufaa zaidi kwa Taifa kwani nishati ya gesi inakwenda kuwa biashara nzuri sana.

(iv) Kutokana na utajiri mkubwa wa nchi katika eneo la nishati na hasa gesi na maporomoko ya maji, Kamati inaitaka Serikali ihakikishe kuwa, uwekezaji mkubwa unafanyika katika TANESCO ili iwe kampuni kubwa zaidi ya umeme katika eneo la maziwa makuu. Katika kutekeleza hili, TANESCO inapaswa kuendelea kuwa kampuni ya umma, yenye kuongozwa kwa misingi ya biashara na kwa siku za baadae iwe ni mhimili mkuu wa nchi katika siasa za maziwa makuu (*geopolitics*) na hivyo kuorodhesha hisa zake katika Soko la Mitaji la Dar es Salaam. Kuhusiana na hili ikumbukwe kuwa, makampuni ya umma nchini Afrika Kusini yanaunda 40% ya mtaji (*capitalisation*) katika soko la mitaji la Johannesburg; hivyo na TANESCO wanapaswa kupewa nguvu ili kutimiza azima hii. Hali kadhalika, ushauri wa kuunda makampuni mawili ya umma

kutoka TANESCO, moja inayohusika na uzalishaji na usambazaji kwa wateja na nyingine usafirishaji (*Transmission*), unapaswa kufanyiwa kazi kwa maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) inafanya kazi kama mmiliki wa Bandari (*landlord*) na hivyo inakodisha uendeshaji wa kibiashara wa shughuli za Bandari za baharini na nchi kavu; na kwa kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ametoa hoja kadhaa za msingi kuhusu utendaji wa Mamlaka hii; Kamati inatoa mapendekezo yafuatayo kuhusu kuongeza ufanisi katika utendaji:-

(i) Kuhusiana na suala la kuongezwa muda wa mkataba wa Serikali na Kampuni Binafsi ya Huduma za Makontena ya *TICTS*, Kamati inaona kuwa kutochukuliwa maamuzi kunaathiri sana utendaji wa Bandari; hivyo Serikali inashauriwa kuondoa ukiritimba wa *TICTS* kwa kutangaza zabuni ya kuendeleza na kuendesha gati za kutia nanga bandarini (*berths*) namba 13 na 14 ili kupata mwendeshaji mwingine na kuleta ushindani katika kitengo cha makontena. Vilevile maadam Kamati inaona kuwa biashara ya kitengo cha makontena ina faida kubwa, makubaliano yoyote yatakayofikiwa na *TICTS* na kampuni nyingine ya uendeshaji, kwa sababu tumesema tufungue *gate* 13 na 14 yawe na masharti ya kuorodhesha asilimia 25 ya hisa za kampuni katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) ili Watanzania wengi zaidi wafaidi rasilimali ya Bandari kwa kumiliki sehemu ya kampuni hizo. Katika kutekeleza hili, Serikali inashauriwa ianze na Kampuni ya *TICTS* kwa kuwataka kuanza mara moja mchakato wa kuorodhesha hisa 25% katika soko la Hisa la Dar es Salaam kwa bei ya ruzuku (*subsidized price*) ili Watanzania wengi zaidi wamudu kununua hisa hizo. Kamati inapendekeza kuwa mamlaka ibakie kuwa *run-road port* kwa mujibu wa sheria na iweze kusaidia maeneo ambako wawekezaji hawaendi.

(ii) Kamati inapendekeza kuwa wakati umefika kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari iwe hasa mwenye mali badala ya kushindana na waendeshaji ili iweze kuwasimamia vizuri na kuongeza ufanisi; hii itaendana na sheria iliyoanzisha Shirika hilo na pia Mpango Mkakati wake unaotoa mwelekeo wa Shirika. Katika kutekeleza suala hili, nafasi ya Bandari za pembezoni iangaliwe kwa makini ili si kwamba TPA wawe na hatimiliki za bandari hizo, bali pia pale ambapo ni vigumu kupata waendeshaji kutokana na umbali au mazingira ya bishara kuwa magumu, TPA iweze kuendelea kuendesha bandari hizo ili kutoa huduma kwa Wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kwa kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Tanzania inategemea sana mikataba ya kugawana uzalishaji (*Production Sharing Agreements – PSAs*) katika kutafuta mafuta na gesi na yakipatikana TPDC inapata hisa za mpaka 20% na kuweza kuongeza zaidi kwa kulipia; na kwa kuwa Shirika hili limekutwa na changamoto mbalimbali kutokana na uchunguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; Kamati inapendekeza yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa TPDC ina tatizo la kutokuwa na usalama wa hati za kumiliki ardhi katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Ujiji, Kibirizi na Katonga-Bangwe

Mkoani Kigoma na Mpanda Mkoani Rukwa, hali ambayo inahatarisha usalama wa mali za Shirika, Kamati inaitaka TPDC ihakikshe kuwa ina hati za kumiliki ardhi yote inayomiliki nchi nzima;

(ii) Kwa kuwa TPDC ina tatizo kubwa sana la rasilimali watu na jana Mheshimiwa Mudhihir alizungumzia tatizo hili sana, asilimia 25 ya Wafanyakazi wa TPDC wa kada ya juu, ndani ya miaka mitatu, mine, wanakuwa wamestaafu; kwa hiyo, hazina yote nchini *training* yote tuliyofanya kwa wataalamu wa mambo ya mafuta, utakuwa imepotea ndani ya muda huo. *TPDC* wakitaka kuajiri wanaambiwa mpaka Tume ya Utumishi, kwa hiyo, tumependekeza kwamba, Serikali iweze kuangalia suala hili, tusomeshe zaidi wataalamu wa mafuta na gesi lakini pia tuweze kuruhusu TPDC kuwa huru zaidi.

(iii) Kwa kuwa tatizo la fedha za kuwekeza ni sugu sana kwa Shirika hili, hasa kwa sababu linaendeshwa kwa ruzuku ya Serikali ambayo huchelewa sana na fedha zinazotolewa kwa miradi ni kidogo sana, jambo ambalo ni la kushangaza sana kwani mpaka mwezi Januari, 2005 TPDC ilikuwa inabakia na mapato ya gesi kutoka Songosongo na hivyo kuweza kujiendesha yenyewe; ni vigumu kwa Shirika hili kushiriki katika fursa zinazojitokeza; hivyo, Kamati inapendekeza Serikali iangalie upya suala hili ili TPDC iweze kuwekeza katika miradi siku za usoni; hivyo kuzuia lawama ambazo zimeigubika Sekta ya Madini hivi sasa. Kwa hiyo, tunataka sehemu ya *royalty* za mauzo ya gesi zibaki ndani ya TPDC zisiende Hazina ili kuweza kuwekeza, kuigubika Sekta ya Mafuta na Gesi na kuleta vurugu nchini.

(iv) Kwa kuwa katika kutimiza majukumu yake ya kutoa vibali vya kutafuta mafuta na wakati huo huo kuwekeza, Shirika linapelekea kuwa na mgongano wa maslahi, yaani *conflict of interest* kwani Shirika pia lina jukumu la kufuatilia na kudhibiti mikataba ya uzalishaji (PSAs). Kamati inapendekeza Tanzania itumie utaratibu unaotumika katika nchi nyingine kama Norway na Msumbiji, pamoja na Uganda ambayo imegundua mafuta hivi karibuni, ambapo majukumu haya mawili yamegawanywa kwa mashirika mawili tofauti, moja la kushughulikia vibali na lingine la uwekezaji na kufanya biashara.

(v) Kwa kuwa Mkataba wa Malipo ya Kodi ya Makampuni (*Corporation Tax)* kati ya TPDC na Pan African Energy Tanzania Limited una utata mkubwa sana kama ilivyobainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; na kwa kuwa katika mkataba huo endapo kodi ya mapato italipwa na Kampuni ya Pan African Energy Tanzania Limited, kodi hiyo itafidiwa kutoka kwenye faida ya TPDC hivyo kampuni hiyo itapunguzwa kutoka kwenye fedha kutoka mrabaha (*royalty/remittances*) inayolipa serikalini; na kwa kuwa tayari ukaguzi unaonesha kwamba kiasi cha shilingi bilioni mbili kilipunguzwa kutoka kweye mapato yaliyotakiwa kuwasilishwa Serikalini; Kamati inauchukulia huu kuwa ni mmoja wa mikataba ya ajabu kabisa, ambayo nchi hii imeingia kwani Kampuni hii haitakaa ilipe kodi ya mapato daima. Kwa kuwa kodi ya mapato ni ya lazima kwa kila mtu na kampuni na kwamba sheria ya kodi ipo juu ya sheria nyingine zote, kipengele hiki cha mkataba sio halali; hivyo Kamati inaitaka Serikali ikusanye

fedha yote iliyorejeshwa kutoka Kampuni ya Pan African Energy Tanzania Limited tangu ianze kazi hapa nchini.

(vi) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna tatizo la msingi kabisa kuwa Taifa limepoteza uwekezaji mkubwa katika utafutaji wa mafuta katika upande wa Zanzibar, kufuatia mgogoro unaoendelea kuhusiana na suala la mafuta na gesi na Mheshimiwa Rais jana alilitolea ufafanuzi suala hili katika hotuba yake maalum kuwa ni suala la Muungano; na kwa kuwa Kamati inaamini kuwa mafuta na gesi ni suala la Muungano lililo katika orodha ya masuala ya 22 ya Muungano kama yalivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, japokuwa uhalali wa kuwekwa kwake katika Masuala ya Muungano bado ni mjadala mkubwa sana na Rais jana ametoa mwongozo; Kamati inasisitiza kuwa, tatizo kubwa lililopo ni kwamba, TPDC sio Shirika la Muungano ila linashughulikia suala nyeti la Muungano, yaani suala la mafuta na gesi. Hivyo basi, Kamati inadhani kuwa imefikia wakati muafaka kwa Shirika la TPDC kuvunjwa na kuundwa Mamlaka ya Mafuta na Gesi Tanzania, ambayo itakuwa ya Muungano na itakayokuwa na jukumu la kutoa vibali na kusimamia mikataba ya kugawana mapato ya mafuta (PSAs) wakati ambapo kila upande wa Muungano utakuwa umeanzisha Kampuni yake ya mafuta na gesi kwa lengo la kushiriki katika uwekezaji na biashara. Ni imani ya Kamati kuwa, ushauri huu kama ukitekelezwa, utaondoa pia utata wa mgongano wa maslahi uliopo TDPC leo katika suala la kusimamia PSAs.

Kamati inapendekeza pia kwamba, hisa zote za makampuni mbalimbali ambazo zilikuwa zinashikiliwa na TPDC kabla ya kunyanganywa na kupelekwa kwa Msajili wa Hazina, zirejeshwe katika kampuni itakayomegwa kutoka TPDC kwa ajili ya kuwekeza katika miradi ya mafuta na gesi ili Taifa liweze kufaidika na uwekezaji huo. Kamati inaamini kabisa kuwa, haikuwa sahihi kutoa hisa hizo kutoka TPDC.

(vii) Kwa kuwa kumekuwa na tatizo la uhuru wa TPDC katika kufanya kazi zake ambao umesababisha hasara kwa Taifa, mathalani pale TPDC ilipolazimishwa kutoa kitalu kimoja katika Bonde la Rukwa (*Rukwa Basin*), cha kutafuta mafuta kwa kampuni ya Kichina bila kufuata taratibu za ushindani, ambazo TPDC kimsingi imekuwa ikizizingatia sana na kupelekea kampuni hiyo kutosaini PSAs hadi leo na kulipotezea Taifa mapato, ukizingatia kuwa eneo hilo lingeweza kutolewa zabuni kwa makampuni mengine, Kamati inaitaka Serikali ipunguze kuingilia Shirika hili la Umma ili lifanye kazi yake, yaani Serikali itimize majukumu yake ya kisera na Mashirika yatimize majukumu yake ya kiutendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hivi sasa Benki Kuu ya Tanzania (BOT) imekuwa katika matatizo makubwa sana yanayohusiana na wizi/ufisadi na maamuzi mabovu yaliyopelekea Taifa kupoteza mabilioni ya fedha za walipa kodi, Kamati inapendekeza yafuatayo ili kuongeza ufanisi wa udhibiti wa fedha za umma:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna upotevu wa fedha katika Akaunti ya Madeni ya Nje *(External Payment Arrears – EPA),* kati ya jumla ya shilingi bilioni 134 zilizoibwa katika akaunti ya EPA katika BOT, shilingi bilioni 90 zilithibitishwa kuibwa na shilingi bilioni 44 zilikuwa zinahitaji uchunguzi zaidi; Kamati inapenda kukumbusha

kuwa kesi zilizopo mahakamani, ambazo Bunge haliwezi kuzizungumzia kwa kuheshimu mipaka ya mihimili ya dola, zinahusu hizo shilingi bilioni 90 tu; hivyo Kamati imeitaka BOT kuiajiri kampuni ya uchunguzi ya kimataifa ya Lazard ili kubaini uhalali wa malipo ya shilingi bilioni 44 na makampuni yatakayothibitika kuwa yalipata fedha hizi isivyo halali, yafikishwe mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake. Kamati inatarajia taarifa ya BOT katika suala hili ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kamati imepata maelezo ya kina kutoka kwa Kamati Teule ya Kuchunguza NDC, kuhusiana na uchunguzi wao juu ya Mradi wa Matinje Gold na upotevu wa fedha za NDC katika mradi huu, Kamati imeiomba Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuipitia taarifa ya Kamati Teule na kupata maoni ya ukaguzi juu ya tuhuma hizi. Vilevile kama ilivyopendekezwa hapo juu, uchunguzi huu pia utoe majibu ya jinsi ya kufufua miradi hii ili iweze kufaidisha nchi. Iwapo katika matokeo hayo ya uchunguzi kutabainika uvunjaji wowote wa sheria, basi Kamati inaishauri Serikali ichukue hatua za haraka kuwawajibisha wale wote watakaobainika kuhusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ina maoni ya kwamba, Mradi wa Mwananchi Gold ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa; hivyo makosa yaliyotokea yanapaswa kurekebishwa na mradi uweze kuendelea ili Watanzania wafaidike na utajiri wa madini ya dhahabu na kutoa soko la uhakika kwa wachimbaji wadogowadogo. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kuwa, jambo la kuzingatia kwa BOT ni kutojihusisha na biashara na badala yake kubakia katika kazi zake za msingi na hivyo inashauri kuwa hisa zote za BOT kwa Kampuni ya Mwananchi Gold zipewe Shirika la NDC na shirika hili lipate mtaji wa kutosha kuendesha mradi likishirikiana na sekta binafsi. Pia kwa kuwa kuna uwezekano mkubwa sana makampuni makubwa ya madini yamehusika kuhujumu mradi huu, pamoja na mradi mwingine mwenza wa kuwakomboa wachimbaji wadogowadogo ambao umesimama wa Matinje Gold, Kamati inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kufanya uchunguzi maalumu wa miradi hii na kutambua chanzo cha miradi hiyo kushindwa kuanza na kupendekeza jinsi ya kuiendeleza ili iweze kuwa na manufaa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inapenda kutumia fursa hii kutoa mapendekezo haya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kutokana na uzito wa majukumu ya Ofisi ya Msajli wa Hazina kama Mhisa pekee katika Mashirika na Taasisi za umma, Kamati inashauri Ofisi hiyo ijitegemee, isiwe chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa uhuru na mamlaka zaidi. Kamati inashauri kuwa ianzishwe Ofisi ya Mashirika ya Umma (*State Entreprises Office*), kwa ajili ya kuratibu uendeshaji wa Mashirika ya Umma kama ilivyo nchini Afrika Kusini.

(b) *Regulatory Fees* ya Mazao ya biashara irudishwe kwa Bodi za Mazao, kwani ilikuwa inazisaidia Bodi hizi kupata mapato ambayo kwa kiasi kikubwa yalitumika kuendesha mashirika hayo.

(c) Kamati inaishauri Serikali kuongezea ruzuku ya uendeshaji (OC) kwa Mashirika na Taasisi ambazo Hazina wigo mpana wa mapato ili yaweze kumudu gharama za kujiendesha. Kwa mfano, Chuo cha Wanyamapori Moshi (MWEKA), mapato yake yanategemea zaidi ada za Wanafunzi ambazo hazijitoshelezi kiasi kwamba wanashindwa hata kuhudumia magari yao yanayowapeleka wanafunzi katika mazoezi porini.

(d) Serikali kujiepusha na utoaji wa dhamana za kimikopo (*Loan Guarantee*) kwa mashirika kiholela, kwani matokeo yake ni kushindwa kulipa madeni hayo na hivyo kupelekea mashirika hayo kushindwa kujiendesha; mfano, PSPF ilitoa mkopo wa shilingi 53 bilioni kwa Bodi ya Mikopo ambao mpaka sasa bado haujarejeshwa.

(e) Serikali ijitahidi kutolimbikiza madeni yake inayodaiwa na mashirika yanayotoa huduma kwa Wizara zake mfano, DAWASCO inaidai serikali kiasi cha shilingi milioni 998.2. Mashirika mengine ambayo mtaji wake ni wa kulegalega, pamoja na sababu nyingine, kwa sababu ya kutolipwa madeni yake na serikali kwa muda mrefu ni pamoja na TSN na TANESCO.

(f) Serikali kuhakikisha kuwa Mashirika na Taasisi za Umma zinakuwa na sera madhubuti za kiuhasibu ili kuongeza ufanisi katika kutekeleza malengo ya Mashirika na Taasisi hizo.

(g) Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa Menejimenti za Mashirika na Taasisi zake za Umma zinazingatia matakwa ya Sheria kwa kuwasilisha makato ya kisheria kwenye mamlaka husika na kuhakikisha mifumo ya kudhibiti fedha inafanya kazi barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na sababu kwamba, mapato ya Shirika la Taifa la Hifadhi za Wanyama Pori (TANAPA), yanatumika kulipa mishahara na stahili nyingine za wafanyakazi wao, kujenga miundombinu katika hifadhi, kulipa kodi ya mapato serikalini, kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kupitia mpango wa ujirani mwema kwa vijiji vilivyo jirani na hifadhi, kununulia magari na vitendea kazi vingine vya Shirika. Kamati inashauri, mwaka jana tulipitisha sheria hapa za Mashirika haya kuweza kutoa fedha kwa Hazina, kufuatana na mtikisiko wa hali ya kiuchumi ulivyotokea hivi sasa na Sekta ya Utalii kuumizwa sana, tunapendekeza kwamba, Serikali kwa kipindi hiki cha mtikisiko wa kiuchumi na ili kuiwezesha TANAPA kuweza kufanya kazi yake kwa ufanisi kutokana na mapato yake kupungua, isichukue fedha kutoka TANAPA. Fedha za TANAPA zibaki kwa ajili ya kuendeleza kutokana na hiyo *special case* ya TANAPA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukushukuru wewe binafsi kwanza kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii na pia kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo na kwa maelekezo yako pale Kamati ilipoomba maelekezo juu ya utendaji kazi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, naomba nimshukuru sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa Estherina Kilasi, ambaye amenisaidia sana katika kazi hii, pamoja na Wajumbe wenzangu. Kamati kwa kweli ina Wajumbe mahiri sana na ninawaombea tu Mwenyezi Mungu awasaidie wawe na mafanikio makubwa sana katika shughuli zao za kisiasa na ninaomba kuwatambua kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Estherina J Kilasi, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Dkt. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Mohamed G. Dewji, Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi, Mheshimiwa Joelson L. Mpina, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa James P. Musalika, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Elisa D. Mollel, Mheshimiwa Zaynab M. Vulu, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Shally J. Raymond na Mheshimiwa Anthony M. Diallo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, kwa ushauri wake kwa Kamati pale alipotakiwa kufanya hivyo. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Makatibu wetu; Ndugu Dickson M. Bisile na Ndugu Zainab Issa. Napenda kuwashukuru sana watu wa Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*), kwa sababu tunafahamu kwamba, Kamati zetu hizi tatu zinaweka kumbukumbu zake zote kwenye Hansard. Napenda kuwashukuru kikosi cha Ulinzi cha Ofisi ya Bunge, kwa kuandamana na Kamati kwenye ziara mbalimbali kwa ajili ya kutoa ulinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wataalamu kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Msajili wa Hazina na Maafisa kutoka Shirika Hodhi linaloshughulikia Madeni na Mali (CHC), kwa ushirikiano mkubwa waliouonesha katika kuhakikisha Kamati hii inatekeleza majukumu yake vyema. Pia tunatoa shukrani za dhati kwa wataalamu wengine walioshirikiana na Kamati kwa kutoa elimu na ufafanuzi mbalimbali kila walipohitajika kufanya hivyo. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, kwa uwasilishaji wako. Kamati hii Waheshimiwa Wabunge, imewasilisha ripoti yake ndani ya Bunge kwa mara ya kwanza. Tutakubaliana kabisa kwamba, wamefanya kazi yao nzuri, ripoti yao nzuri na nishauri Kamati nyingine ni vizuri zikafanya kazi na kuandika ripoti kama ilivyoandikwa ya Kamati hii.

Nawapongeza Mheshimiwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Estherina Kilasi na Wajumbe wote wa Kamati hii ya Hesabu za Mashirika ya Umma, hongereni sana. Baada ya hapo, kama mnavyofahamu, utaratibu wetu sasa ni uchangiaji, mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, halafu naomba na Mheshimiwa Engineer Stella Manyanya ajiandae.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie fursa hii ya awali, kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya mwanzo ya kuchangia mada ya leo jioni, kuhusu Taarifa ya Hesabu ya Mashirika ya Umma. Aidha, nitumie fursa hii vile vile kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Mahesabu ya Mashirika ya Umma, pamoja na Wajumbe wake, kwa kazi nzuri waliyoifanya. Kwa kweli taarifa yao hii, imesheheni mambo mengi muhimu kiasi kwamba katika uchangiaji, mtaniwia radhi kama nitajikuta narejearejea baadhi ya yale ambayo yamekwishasemwa. Nitakuwa nafanya hivyo kwa dhamira tu ya kusisitiza kwamba, hayo ndiyo mambo muhimu ambayo yanapaswa kushughulikiwa na Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo yaliyotolewa na Mwenyekiti wa Kamati, imejitokeza wazi kabisa kwamba, tatizo la Utawala Bora kwa lugha ya kigeni *(Corporate Governance*) ni moja ya tatizo kubwa sana la Mashirika yetu na tatizo hili linajitokeza katika sura zifuatazo:-

Sura ya kwanza ni ile ya kutokutimza taratibu za Manunuzi ya Umma. Sura ya pili ni baadhi ya Mashirika yetu kutokuwa na Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani. Vile vile kutokuwa na *Audit Committees* ambazo zingesaidiwa na Mkaguzi wa Ndani, kupitia mara kwa mara, mapendekezo ya Mkaguzi wa Nje ili kufanya marekebisho kwenye mambo yenye hitilafu ambayo yamekuwa yakijitokeza katika vipindi husika. Kwa hiyo, katika haya ningependa tu nisisitize kwamba, hakuna njia ya mkato kwenye Mashirika yetu isipokuwa kuhakikisha kwamba, sheria zilizopo na kanuni zilizopo hususan kanuni hasa Sheria ya Manunuzi ya Umma, inatekelezwa kama ipasavyo. Hii ni kwa sababu eneo hili la Manunuzi ya Umma ni eneo ambalo linatumia fedha nyingi sana za Mashirika, pamoja na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limetajwa suala zima la mitaji; ni kweli kabisa Mashirika yetu mengi ya Umma ni *highly under capitalise* kwa maana mitaji yake ni midogo sana wakati majukumu yake ni makubwa sana. Katika hili ningependa nigusie miongoni mwa Mashirika ambayo hoja yake mimi ni Mkurugenzi katika Bodi ya Shirika hilo. Mimi ni Mkurugenzi katika Bodi ya Shirika la Tanzania Railways Limited. Maslahi yangu katika Shirika hilo na kama Mkurugenzi ni kupata ada ya vikao na tiketi ya kunitoa Tabora kuja Dar es Salaam kwenye vikao na kurudi. Sina maslahi mengine zaidi ya kulipwa posho ya kukaa Dar es Salaam siku mbili au tatu, baada ya kutoka kituoni kwangu Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Shirika hili ni kielelezo cha hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Zitto kwamba, Mashirika yetu hayana mitaji ya kutosha. Shirika hili lilianzishwa kwa mtaji wa shilingi bilioni 20 tu, lakini kama alivyoeleza Mheshimiwa Zitto kwamba, hili ni moja ya kielelezo cha Mashirika ambayo kabla hayajabinafsishwa,

yalikaa chini ya PSRC kwa takriban miaka 10 na yalipokuwa chini ya PSRC kulikuwa hakuna uwekezaji wowote, maana yake injini zetu za *Railway* zilikuwa hazitengenezwi tena, mabehewa yalikuwa hayanunuliwi mengine. Nisahihishe ile ya kwamba zilikuwa hazitengenezwi, tulikuwa hatununui injini nyingine ila tunatengeneza zile zilizopo, lakini ikafika mahali TRC ikawa hata fedha za kununulia vipuri haina. Kwa hiyo, wakaanza kuwa wanatoa vipuri kwenye injini moja wanatengeneza injini nyingine. Mpaka Shirika hili linabinafshwa, hali ya vitendea kazi vyake ilikuwa ni mbaya. Hali yetu ya reli hadithi yake ni hiyo hiyo; Serikali ilipoingia ubia na Kampuni ya RITES kila mmoja katika hawa wabia wawili, alitoa asilimia 49 Serikali na asilimia 51 RITES za zile bilioni 20. Mahitaji ya Kampuni hii ili iweze kufanya kazi ni zaidi ya shilingi bilioni 100, hizo fedha mpaka leo hazijapatikana.

Kulikuwa na mpango wa Serikali pamoja na mbia wake kukopa kutoka IFC kiasi cha dola milioni 44, mpaka leo zimepatikana milioni 7 tu. Kwa hiyo, si jambo la kushangaza kwamba Kampuni hii haifanyi vizuri na haitofanya vizuri kama wabia wawili hawa hawatakaa pamoja na kuhakikisha kwamba, wanaongeza mtaji kwa njia moja au nyingine kwenye Shirika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika mengine ambayo yanafuatia hapa limetajwa Shirika la Bandari. Tanzania ni nchi moja yenye bahati sana, baadhi yetu ambao tumesafiri ulimwenguni katika sehemu fulani fulani tunaweza kuwa ni mashuhuda kwa jinsi ambavyo Bandari inaweza ikawa ni mahali sawa sawa na mgodi wa dhahabu. Nchi hizi ni pamoja na Singapore, Dubai pale (UAE) na Namibia wana *port* inaitwa Windhoek, hawa wanapata mapato makubwa sana kutokana na bandari zao lakini sisi Tanzania hadithi ni tofauti sana; mpaka leo tunalumbana na TICTS.

Kamati imesema kwenye TICTS pale kuna matatizo mawili makubwa; moja ni kwamba TICTS imeongezewa mkataba; lingine ni kwamba kuna *exclusivity close* kwamba asiwepo mwendeshaji mwingine isipokuwa TICTS. Ushauri wangu kama ambavyo Kamati imesema, nasisitiza Serikali ifanye maamuzi kwa namna moja au nyingine waamue ili bandari ile ifunguliwe kwa ushindani, waje *operators* wengine washindane na huyu TICTS. Huyu TICTS tumwache kwanza, masuala yake ya mkataba hayo tutaendelea kuzungumza naye, lakini tuondoe ile *exclusivity close*, tuifungue bandari kwa watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadithi ni hiyo hiyo kwenye Kampuni ya General Tyres; hivi Tanzania sisi tuna matatizo gani? Inatia uchungu; leo hii hapa nchini magari yote yanatembea kwa matairi ya kutoka nje wakati tuna Kiwanda chetu hakifanyi kazi na ni mali ya Serikali. Asilimia 74 mali ya Serikali na 26 mtu wa nje matairi yanatoka nje, tuna tatizo gani? Si suala la soko, soko lipo, kwa nini hatutumii kiwanda chetu kikafanya kazi ni ajabu na inauma! Kwa hiyo, suala hapa ni kuwekeza General Tyres ifanye kazi, tutapata ajira na biashara ipo, tutapata kodi na uchumi wetu utaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadithi ni hiyo hiyo kwa STAMICO; STAMICO imeachiwa mpaka ikafika mahali ikawa haijiwezi, lakini inaweza kuwa ndio mkono wa Serikali katika uwekezaji migodi yote ya madini hapa nchini. Imeshauriwa kwamba,

TANESCO iongezewe mtaji ili iweze kufanya kazi yake iliyostahili na mimi naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee kwenye suala zima la manunuzi ya umma, suala ni kufuatilia utaratibu wa kisheria. Kama tunashindwa kwa sababu sheria yenyewe labda kuna maeneo hayatekelezeki, basi mapendekezo yaletwe kwenye Bunge tuibadilishe; kwa mfano, kuna manung'uniko kwamba, inachukua muda mrefu toka unapotangaza mpaka unapoweza kumpata mzabuni. Kama tatizo ni kipindi basi mapendekezo yaletwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kwamba inawezekana Sheria yetu ya Manunuzi ina matatizo, lilijitokeza kwa malumbano makubwa sana katika miezi miwili iliyopita kuhusu ununuzi wa mitambo iliyopo nchini ya umeme, suala lilikuwa mitambo ile imekwishatumika. Sasa kama wakati mwingine tunataka tununue vitu vilivyotumika, basi tuleteeni hapa Bungeni. Serikali leteni mapendekezo, lakini bila ya kuibadilisha sheria. Wale waliokuwa wanasema tusinunue vitu vilivyotumika walikuwa sahihi, lakini kuna suala la muda; mimi binafsi nakubali kwamba, unatangaza siku 45, ukishapata zile *proposal* ukae siku 30, baada ya siku 30 ukae sijui siku ngapi nyingine, inachukua muda mrefu. Uzoefu umetuonesha kwamba, labda hilo nalo ni tatizo, basi sheria hii wale wenye kuhusika na masuala ya sheria hebu waitazame tena, lakini mpaka hapo itakapobadilishwa sheria inasimama pale pale. Mashirika yetu ya Umma yaanzishe Vitengo vya Manunuzi, yaanzishe *Tender Boards* na yazisimamie.

Suala la *internal control* katika Shirika lolote unapotaka utawala bora haliepukiki. Lazima tuimarishe *internal controls* zetu, kwa kuwa na *internal audit units* zinazofanya kazi, tena kwa mawasiliano moja kwa moja na *audit committee* za Bodi. Halafu kutakuwa na *noted line* kwenda kwa mtawala wa shirika ili ajue masuala ya kiuendeshaji, huyu *internal auditor* wake anahitaji afanyiwe mambo gani ili aweze kufanya kazi zake, lakini aripoti masuala yake kwa *Internal Audit Committee* ya *Board*. *Audit Committee* ya *Board* ndiyo itakayofikisha mambo yote yanayohusiana na *findings* za *internal auditor* kwa Bodi iliyo kubwa kwa ajili ya maamuzi. Tukifanya hivi masuala haya yanayojitokeza kama matatizo katika uendeshaji wa Mashirika yetu, yanaweza kupatiwa dawa; bila ya hivyo tutaendelea kila siku kusema kwamba, kanuni za mahesabu hazifuatwi, *auditor* wa nje anatoa *observations,* anatoa *recommendations* hazitekelezwi, *business as usual,* tunaendelea hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yetu ya leo ni muhimu sana, imejenga juu ya msingi wa taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali, hapa tunaijadili kwa kifupi kama tunavyofanya lakini majadiliano haya yaendelee hata nje ya Ukumbi wa Bunge katika Mashirika mbalimbali yanayohusika na hasa Msajili wa Makampuni kule Hazina. Suala la kuiimarisha ofisi hii si la mjadala; wenzangu wa Hazina wanafahamu kwamba Ofisi hii imehemewa, inahitaji kupewa kila aina ya msaada hasa kwenye upande wa nguvu kazi na wataalamu ili waweze kutimiza wajibu wao wa kuyasimamia mashirika haya kikamilifu, kama ambavyo sheria inawataka wafanye. Wakati tunafanya hayo, vile vile tunaweza tukaangalia wenzetu wa Afrika ya Kusini wamefanyaje. Wao wana chombo kinaitwa *State Office Enterprises,* kinasimamia miradi yote ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumza. Ahsante sana.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia mada iliyoko mbele yetu. Nami vile vile nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati hii, kwa ripoti ambayo ametupa kwa sababu imegusa maeneo mbalimbali. Vile vile nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa afya ambazo ametupa na hivyo kuweza kuendelea kujadili mpaka kipindi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba, pamoja na uzuri wa taarifa hii, unanikwaza kidogo ukurasa wa tano wa kiambatanisho cha 10, aya ya tatu, ambayo imo kwenye taarifa hii na kwa kuwa imezungumzia suala la mgongano kati ya Kamati yetu ya Nishati na Madini, pamoja na hii ya Hesabu za Mashirika ya Umma. Naomba kifungu hiki kichukuliwe kwamba, kina nafasi ya kupata maoni zaidi, kwa sababu kuna baadhi ya sentensi zilizoandikwa naona kama siridhiki nazo, lakini kwa kuwa hatujapata muda wa kizi-*discuss*, sitakuwa na muda huo, lakini ichukuliwe kwamba itabidi tupate na sisi muda pia wa kuangalia zaidi. Kimsingi nataka nizungumze kwamba, suala la ustawi wa jamii zetu unatokana pia na uwajibikaji wa mihimili yote mitatu ikiwemo Bunge. Tunafanya kazi zetu kwa misingi ya sera tulizojiwekea, ambazo tunaamini ni zile ambazo zinakidhi mahitaji ya Watanzania, zinajali mahitaji ya Watanzania na ustawi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo naomba nijikite katika nishati ya umeme. Taarifa zinaonesha kwamba, mpaka sasa asilimia karibu 11 ikizidi sana 12 ya Watanzania ndio wanapata umeme. Katika asilimia hiyo, wengi wao ni waishio mijini hususan Mkoa wa Dar es Salaam katika Wilaya zake tatu, kidogo Mkoa wa Iringa na nadhani kwa sababu Grid ya Taifa inapita eneo hilo. Katika maeneo ya mikoa mingine, imekadiriwa mpaka asilimia mbili kufuatana na taarifa hizi. Unaweza ukaona ni jinsi gani ambavyo nishati hii ilivyo muhimu na ambayo haijaweza kutosheleza kuwa kama ni chachu ya maendeleo kwa ajili ya Watanzania. Hivi karibuni tulikuwa tumepitia na kujadili taarifa kuhusu mpango kabambe wa kuzalisha na kusambaza umeme Tanzania. Katika mpango huu na kwa hali ya sasa iliyopo ni dhahiri inaonesha kwamba, tuna upungufu wa umeme. Upungufu huo haumaanishi kusahau na kukiuka misingi yetu na taratibu zetu na hali ya kuwajali wananchi kama ambavyo sera zetu zinaelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ripoti hii inaonesha kwamba, TANESCO iliweza kupata unafuu wa kurekebisha ukwasi wake katika kipindi hiki na vile vile kupunguza upotevu wa umeme unaojitokeza. Ni kweli kabisa nami nawapongeza kwa juhudi walizozifanya, lakini tukienda pia katika mtazamo halisia, utakuta kwamba hayo maongezeko ya fedha zilizojitokeza yametokana hasa na kupandishwa kwa bei ya umeme. Kwa hiyo, ufanisi upo lakini ilichochangia sana ni kuongezeka kwa gharama za umeme, lakini pia TANESCO wakati tukijadili nao wamezungumza wazi kwamba, karibu asilimia 100 ya mapato yao yalikuwa yakitumika katika kulipia gharama za mitambo ile ambayo iliwekwa na wawekezaji wengine na ndio maana sasa katika hilo huwezi kujitenga ukasema kwamba, Kamati hii inahusika na hii haihusiki kwa sababu

lazima tuwe na jicho la darubini kuona ni wapi Watanzania wanashindwa kupata ustawi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania baada ya kuamua kubinafsisha Mashirika yake kama wenzangu walivyosema, Shirika la Umeme Tanzania limekuwa kwa muda mrefu halikuwekeza na sio tu katika uzalishaji hata usambazaji. Ukiangalia mipango mingine ya Wizara nyingine kama Ujenzi, ongezeko la matumizi limekuwa ni kubwa sana, lakini mipango madhubuti imekuwa ina *delay*, yaani inakuwa nyuma ya matumizi na ndiyo hiyo inapelekea kuwa na maamuzi ya haraka. Kama ilivyojitokeza mara ya mwisho, TANESCO iliomba fedha shilingi bilioni 300 kwa ajili ya kurekebisha ukwasi wake na ikapewa kwa kukopa. Mimi ninachoshauri badala ya sisi kuendelea kulumbana kwa yaliyopita, tuangalie njia ya kwenda mbele. Watanzania wameona tatizo wanaridhika na kuelewa wanajua wapi tulikosea, basi ni msingi kabisa kuiwezesha TANESCO ikope tena na iwekeze katika mitambo hiyo ili iweze kuzalisha umeme wenye bei nafuu na hivyo Watanzania wengi kuweza kufaidi matunda ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu hata hivi karibuni tulipozungumza kwamba, tuangalie uwezekano wa kupata mitambo mipya, katika mpango ule TANESCO inazungumzia kupata megawatt 100. Unakuta kwamba, inafikia karibu sawa na mahitaji; hautoshi baada ya siku mbili tutaanza kugombana tena. Hivyo hivyo tena kuna taarifa zinazoonesha katika miaka ya 35 kumekuwa na hali ya upungufu wa maji na mabadiliko ya hewa. Kwa hiyo ni kitu ambacho kipo; ni endelevu na sasa hivi tunazungumzia suala la *global warming*. Kwa hiyo, nalo ni tatizo ambalo litahusika katika nishati hii ya umeme, badala ya kusema tu kwamba macho yanaangalia hicho tu kana kwamba hakuna *alternatives* nyingine.

Sheria mpya tumetunga, wadau mbalimbali waweze kuingia kuzalisha wenyewe na wauze umeme kama ulivyo; si kuuza tu kila kitu kwa TANESCO halafu inabeba hizi *capacity charge;* kwa nini? Sisi tunasema mitambo yoyote ile hata kama iliyopo ni chakavu, ikiwa imebakia mikononi mwa yule mwenye mitambo yake, ina maana kwamba TANESCO au mlaji atakagua leo ninunue kwa nani, TANESCO wakisema wao *unit* ni shilingi 70 Stella Manyanya atasema aah mimi nauza shilingi 50; kwa hiyo, *operator* atasema anza kuleta Stella Manyanya ukimaliza atafutia TANESCO mwenye bei kubwa, ndicho tunachokihitaji katika ushindani huu. Ushindani haupo katika mambo mengine tu, hata bidhaa hii ya umeme inawezakana. Nimeshakuwa Oslo, Norway wanafanya hivyo, nimekaa pale na nimefanya kazi kwenye Shirika lile, haya mambo yapo kwa nini sisi tunajifungia; kwa nini hatutaki kuona mbali? Wataalamu wetu kwa nini basi hawajaweza kuona hayo? Naamini kuna wanaojua; kwa nini wasiwezeshwe basi tuweze kwenda mbele?

Mimi binafsi naguswa sana tunapofikia sasa kuona kwamba, labda kuna mtu anakuwa na nia fulani au maslahi fulani tukaacha suala la msingi. Tunahitaji umeme kwa Watanzania, umeme ulio safi na ulio bei nafuu; hiyo peke yake ndiyo itamwezesha Mtanzania kutoka mahali alipo na kwenda katika hatua nyingine. Tukiendelea na hali hii, tunakataa kwamba tusiingilie wakati huo huo mwingine anasema tufanye hivi; hatutafika ndugu zangu. Mimi hilo naliomba sana, TANESCO wanao uwezo pia kama

Shirika la Serikali kuwa wao kwanza kama ndio nguzo lakini wakati huo huo wazalishaji binafsi wapewe nafasi na ikiwezekana na sio ikiwezekana, nashauri kuwe na chombo maalum pembeni; sio TANESCO ndio iseme sasa mimi ndio nitaingia mkataba na fulani kwa sababu na wao wana *interest* watakuwa wanamzoea yule mwingine. Kama kutakuwa na chombo pekee hapa hapa katikati, ambacho kitakuwa kinaangalia mpango huu kamambe na wakati huo huo kuwaalika watu mbalimbali kuingia katika shughuli za uzalishaji, ina maana matatizo haya yote baada ya muda mfupi hayatakuwepo.

Hilo naomba tulizingatie na tulifanyie kazi kwa haraka, kwa sababu tumechelewa tulitegemea Mradi wa Umeme wa Gesi ambao uko pale Kinyerezi, ungeanza kufanya kazi mwaka 2009 lakini tumechelewa. Kiwira tumechelewa, ARTUMUS ana uwezo wa kuzalisha megawati 300 lakini ziko pale. Tulipokwenda Songosongo kuna wengine wameshazalisha gesi, akina Ndovu na wengine; zote hizi ni rasilimali za Watanzania, hakuna haja ya kuhamisha gesi kwenda kuuza nje wakati tungeweza kuzalisha umeme Tanzania tukatoa ajira ya kutosha na baada ya hapo tukauza umeme kama umeme. Uwezekano huo upo, kinachohitajika ni maamuzi na kama hatutaamua sasa hivi kutumia maporomoko yaliyopo; kwa mfano, *Stiglers' Gorge*, kutumia gesi zilizopo, kutumia makaa yaliyopo, ina maana sisi tumeamua utajiri wetu kuugeuza kuwa makumbusho; *do we want our resources to be museum*? Naomba sana tufanye maamuzi sasa yale yenye kuleta ustawi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya tatu. Nimpongeze Mwenyekiti kwa kuwasilisha taarifa vizuri, lakini niipongeze Kamati kwa kazi nzuri sana waliyoifanya.

Kwanza, naomba kutoa ushauri wa ujumla kwamba, Kamati hizi za *oversight* zinasaidia sana Kamati zetu za Kisekta kama taarifa hizi watazitumia kuzifanyia kazi. Kwa hiyo, ombi langu la kwanza kwa Kamati za Kisekta kwa sababu hizi ni Kamati za *Oversight*, zimeona mambo mengi, lakini ukiunganisha mambo yaliyoonekana humu na sera, itasaidia sana kusimamia sekta zetu tunazotekeleza kufanya kazi. Hili ndilo lilikuwa ombi langu la kwanza kwa Wabunge wenzangu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili naiomba Serikali inachelewa kufanya maamuzi kwa mambo makubwa. Taifa letu limeshaingia kwenye giza kwa muda mrefu sana na hakuna sababu ya kuwa kwenye giza. Bahati mbaya nchi yetu haijakuwa na orodha ya rasilimali ambazo haziwezi kuchezewachezewa na hasa katika madini, wataalamu wengine wanaita *industrial minerals*. Kwa mfano, tunao makaa ya mawe; ukiangalia kwenye Wizara sasa hivi makaa ya mawe yamegaiwa watu mbalimbali. Kwa wenzetu wengine makaa ya mawe ndiyo *industrial mineral*, haiwezi kuchezewa na mtu yeyote na inawekwa pale na kuna chombo cha kusimamia. Tunayo gesi hivyo hivyo, tunayo *uranium* hivyo hivyo inachezewachezewa, tunayo *copper* hivyo hivyo na kadhalika. Kwa hiyo, naiomba Serikali sasa ifike mahali iseme kwamba, tunahitaji kumaliza tatizo la *source of energy in this country*.

Vyanzo vya umeme vya kutosha vipo, yapo maji ya kutosha, ipo gesi ya kutosha, yapo makaa ya mawe ya kutosha, upo upepo wa kutosha, lipo jua la kutosha na kadhalika na hata *waste* za kutosha. Dar es Salaam peke yake takataka zinaweza kuzalisha umeme usiopungua *megawatt 150* takataka tu, lakini bado hatujaamua, leo tunaendelea kupambana na akina Dowans na wengine na kadhalika. Hatuna sababu, *source of energy* ingekuwa ni *solution* kwa Tanzania leo hatuzungumzi na mfano upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, NDC ina maeneo machache ya makaa ya mawe. Wamefanya utafiti wa miezi sita tu na wamegundua Ngaka peke yake kuna tani milioni 92. Wanaweza kuzalisha umeme wa *megawatt 400* kwa muda wa miaka 30. Serikali maamuzi yamekuwa *slowly.* Leo 2010/2011 tungekuwa hatuzungumzi tena suala la *source of energy* kwa TANESCO, kazi yetu ingekuwa ni *distribution* ya umeme. Naomba Serikali tuamue sasa kwamba, suala la *source of energy* Tanzania ni hadithi. Nalisema hili kwa sababu gani?

Msumbiji wana makaa ya mawe kwa mwaka watatoa tani milioni 20, miaka miwili ijayo watatoa *megawatt 600*. Taarifa ya Mwenyekiti inasema, tujitahidi TANESCO ndiyo iwe mhimili katika eneo la Maziwa Makuu. Msumbiji peke yake wakizalisha hiyo hakuna *investor* atakayekuja kuweka *600 million USD* kuzalisha *400 megawatt* Tanzania na wakati kule kuna *20 millions tans* za *coal;* anaweza kuzalisha umeme na akauza *coal* nje. Ukiacha hiyo *opportunity*, kesho kutwa itakuwa ni *white elephant* kama alivyosema Mheshimiwa Eng. Manyanya hivi sasa. Hii miradi yote ya Mchuchuma na mingine itakuwa ni hadithi. Tutakwenda kuangalia milima na kuondoka, wenzetu wanafanya hivi sasa. *We need to make a decision*. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Idara inayosimamia Mashirika yetu na ukiangalia hali ya uchumi inavyoendelea hivi sasa duniani; ni dhahiri tutafika mahali tutahitaji hiki chombo tukitaka *to bail out* tunakiambia chombo hiki simamia. Tulitegemea NDC itafanya hiyo kazi au STAMICO, lakini bahati nzuri Watanzania ni hodari sana wa kuuwa watoto wetu na kuwaelea watoto wa wengine. Tumeviua hivi vyombo. Leo ukitaka ku-*bail out* hapa lazima ukae uanze kubuni ni namna gani utaanza ku-*bail out* kampuni ya *private* ili Serikali iweze kufaidika. Vyombo vya kufanya kazi hiyo vyote umeviua. Hata *dividend* tunazozipata katika Mashirika yote hapa yaliyosemwa hazijulikani ukiacha BOT. Juzi Williamson Diamond, Willcraft ilikwenda kwenye Kamati ya Nishati wanasema wanadai milioni 57 USD. Kampuni hii toka 1994 haijawahi kulipa *dividend* hata siku moja, wala kodi katika Serikali na Serikali iliuza hisa zake asilimia 25 kwa USD 183,000 na hizi 25 zilizobaki nasikia zinataka kuuzwa sasa hivi.

Tunahitaji kuwa na vyombo vya kuweza kusimamia hii rasilimali ya Watanzania. Kama tunataka kuhakikisha ajira katika nchi inapatikana ni vyombo hivi peke yake ndivyo vinavyoweza kuweka *guarantee* ya ajira ya Tanzania na si mashirika binafsi kama wanavyodai. Huwezi kuwakagua, wanaweza wakati wowote wakafilisika wakaondoka na rasilimali. Yameshatokea, AIG ya Marekani na kadhalika. Hivi ndivyo vyombo vya kusimamia uchumi wa Taifa letu, lakini kila wakati tumekuwa tunauza rasilimali zake.

NDC wameuza rasilimali zao zote, STAMICO wameuziwa rasilimali zote halafu unawaambia ninyi endeleeni kukua; watakuaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya nasema ni mambo ya msingi, Serikali lazima ijipange kupambana na maamuzi. Mimi nasema tushindane, tuwe na vyombo vyetu vya kitaifa vya nchi lakini tuviruhusu vifanye biashara. Tuviruhusu kufanya biashara kwa maana ya kwamba, tuweke na Bodi ndogo yenye wataalamu na ujuzi, wapewe mtaji wa kutosha halafu waambiwe waingie kwenye soko bila kuingiliwa na urasimu wa maamuzi ya Serikali. Ndivyo Mashirika yote tulivyoyaua na mimi nilikuwemo. Tumeyaingilia katika maamuzi Mashirika yamekufa, hakuna sababu ya kufa. Weka mtaji wa kutosha, weka menejimenti *proper*, weka *accounting system proper* na *supervision* iwe *proper;* waambie wafanye biashara kama wanavyofanya watu wengine na mashirika yetu yatafanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna wataalamu wazuri wengi sana Tanzania. Mheshimiwa Fatma hayupo, ameniambia walipokwenda Botswana, walikwenda kwenye *Referral Hospital* na Mheshimiwa Rais wakakuta Madaktari waliopo pale ni Watanzania 30. Tuna wataalamu wa kutosha; ni namna gani tunawatunza au tunawasaidia wataalamu kufanya kazi za Kamati ndiyo Tatizo tulilonalo. *We are politicising each and everything in this country*. Kila kitu ni siasa hatufiki, tatizo tunapiga siasa kila mahali. Hatuwezi kufika mahali. Tumeshindwa Tanzania leo hata kujilisha kwa chakula chetu. Juzi Waziri alikuwa anasema, tunahitaji hekta laki nne za umwagiliaji ili tuweze kuzalisha mpunga wa kutosha. Tukipiga hesabu, kila kata kumi ni hekta mbili, tumeshindwa kufanya hivyo, ni tatizo. Kwa hiyo, tunahitaji kujipanga vizuri, tuondokane na *source of energy,* tuondokane na tatizo la chakula. Ardhi tunayo; sasa hii migogoro tunayoipata ya ardhi ni kwa sababu gani? Ni kwa sababu hatujasema katika mipango yetu kwamba, ardhi fulani inaruhusiwa mwekezaji aje awekeze.

Juzi tuliambiwa kwamba, ukienda TIC kuna *Land Bank*, nimekwenda TIC nauliza kuna *Land Bank* wanasema hakuna, *don't tell me*. Wanasema hakuna mzee labda kuna watu wamekuja hapa wanasema wanatafuta wawekezaji mkakubaliane nao. Hiyo ndiyo *Land Bank?* Kweli *investor* atakuja hapa akakae na wananchi huko, akazungumze nao kufanya *investment.* Tunajitahidi kujipanga, hebu tujipange vizuri. Mimi naomba mambo mawili; umeme na chakula.

Tatu, kama walivyosema Kamati; tuyapitie hayo mashirika ambayo yana uwezo wa kufanya vizuri, yana uwezo wa kutupa ajira, tuyaimarishe ili yawe mashirika ya kweli na yaingie katika soko la kufanya biashara. Huo ndiyo uhai wa Watanzania. Leo uhai wa Tanzania uko CRDB, NMB, ndiko kwenye matumaini yao na ndiko kwenye hisa zao. Tumeiua NBC bure; na hii tabia ya kusikiliza *donors* kila wakati hebu tuwasikilize Watanzania wenyewe wanataka nini, ndiyo wenye majibu ya matatizo yao na si wageni. Kwa hiyo, nasema hii taarifa ni muhimu na naomba ifanyiwe kazi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *area* moja naziomba Kamati zote, juzi tulimuuliza Mkurugenzi wa PPRA; je, mnafanya tathmini ya *consultancy service* zinazotolewa katika nchi? Wakasema hatujafanya. Ukichukua hiki kitabu chao hapa na ukiona hizi *billions of*

*money* zilizofanyiwa *consultancy;* vitambulisho peke yake ni 9.9 bilioni; ukiitizama *report* yenyewe thamani yake sijui kama inafika dola laki moja. Taarifa za uchunguzi zilizofanywa zipo kwenye *shelves* hazijafanyiwa kazi miaka na miaka na pesa za wananchi zimetumika. Baya zaidi ni kwamba, uchambuzi unafanywa baada ya miaka miwili, ile taarifa haifai na kazi ile inafanywa upya. Matokeo yake kazi moja ya ushauri mara tatu, nne au tano. Someni hivi vitabu vya Mkurugenzi wa PPRA; ni hatari *billions and billions of money* zipo kwenye *shelves* Watanzania wanaendelea kuwa maskini. Kwa hiyo, naomba vilevile Kamati zetu za *oversigh*t, Kamati za Kisekta na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, watazame hizi kazi zinazofanywa za ushauri. Kazi inayofanywa inatumika au inabaki kwenye *shelves* ili tufike mahali tupate *value for money* kwa kila kazi tunayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, tulikubaliana katika Bunge hili kwamba, tumefika mahali Serikali sasa katika manunuzi inunue *bulk.* Ukisoma hizi taarifa, unapata kiwewe. Naomba niseme jambo moja nililolisema la Serikali kufikiria kununua *bulk* ni njia pekee ya kupunguza gharama za matumizi tulizonazo Tanzania. Kuacha kila Idara au kila Wizara inunue vyake hata magari tunahitaji 200 hadi 300 ni hasara kwa taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii muhimu, ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Awali ya yoyote, nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati hii, kwa uwasilishaji mzuri, lakini pia niwapongeze Wajumbe wa Kamati hii, kwa umahili wao kwa kuleta hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba, mengi ambayo ningependa kuyaongea yameshaongelewa lakini nimpongeze CAG, kwa sababu ninaamini bila Ofisi yake kutayarisha mahesabu hayo, basi Kamati hii isingeweza kuleta taarifa hii. Pamoja na kumpongeza CAG, napenda niseme ripoti hii inasikitisha kwa sababu moja kubwa; kwamba, tumeona maeneo mengi katika mashirika ya umma kumekuwa na upotevu mkubwa wa fedha lakini vilevile unaona kabisa ushauri wa CAG kutokana na matatizo mbalimbali ambayo yamejitokeza katika mashirika haya, bado hayakuweza kutatuliwa. Kwa hiyo, ninaamini Serikali itazingatia mapendekezo yaliyotolewa ili waweze kurekebisha pale ambapo tunaona fedha za walipa kodi zinapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo pia limenisikitisha katika mapendekezo haya ni kwamba, Sheria inasema kwamba yale mashirika ambayo yamebinafsishwa na yana hisa pungufu ya asilimia 50, basi Kamati haina uwezo wa kuyafanyia ukaguzi. Hili ni tatizo kubwa sana; kwa mfano, tukichukulia Kiwanda cha Urafiki, hiki kina asilimia 49 za hisa za Tanzania na asilimia 51 kutoka Serikali ya China. Kama Kamati hii haitapewa uwezo wa kwenda kukagua mahesabu katika mashirika hayo na mengine mengi; mimi naamini kabisa mtu yeyote unapowekeza hata kama ni shilingi moja, bado una uwezo wa kufuatilia shilingi ile uone inakwendaje, lakini kwa Tanzania inakuwa ni

tatizo kubwa sana kuona mashirika ambayo tuna ubia na hisa pungufu ya asilimia hamsini hatuwezi kuyakagua; maana yake ni nini? Je, tunajua wafanyakazi ambao ni Watanzania katika mashirika hayo wanakuwa *treated* vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitoe mfano wa Kiwanda cha Urafiki ambacho nipo karibu nacho. Kiwanda kile kama nilivyosema, Tanzania ina hisa asilimia 49, lakini ukiangalia kwa upande wa utawala, *General Manager* pale ni Mchina; anapoondoka Kaimu General Manager ambaye ni Mtanzania hawezi kukaimu isipokuwa anakuja kukaimu Mwenyekiti wa Bodi ambaye pia ni Mchina. Mimi nadhani hii ni kinyume kabisa cha utaratibu. Vilevile ukiangalia maslahi ya wafanyakazi wa kiwanda kile, yanatia mashaka makubwa sana. Utaona kuna ubaguzi wa hali ya juu kati ya Watanzania na wenzetu kutoka China. Unaweza kukuta kazi wanazofanya zinafanana, lakini mishahara yao ina tofauti kubwa sana. Wao wanapata kati ya shilingi 80,000, lakini wenzao ambao wanafanya kazi za kufanana wanapata Dola 600. Hili ni tatizo kubwa, kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwamba, yale mashirika ambayo Serikali ina hisa chini ya asilimia 50 na hata kama ni kidogo, basi Kamati ya Bunge inayohusika ikafanye ukaguzi.

Vilevile pia kutokufanya hivyo tunakuwa na mambo mbalimbali ambayo yanaendelea ya ufujaji. Kwa mfano, nikizungumzia kiwanda hicho hicho; *spinning machine* ambayo ilinunuliwa wakati ule Tanzania ikiwa inakimiliki ni ya gharama lakini sasa hivi imeharibika na kinachoendelea ni kwamba, ile mashine sasa hivi inauzwa kama vyuma chakavu. Kwa maana hiyo, kama tungekuwa na ukaguzi wa kwetu wenyewe, sidhani kama yote haya yangetokea. Vilevile nyumba za wafanyakazi wa urafiki ambazo ziko pale pembeni, zilikuwa ni kwa ajili ya wafanyakazi, lakini sasa hivi zimeuzwa na si kwa wafanyakazi kwa watu wengine kabisa.

Kwa hiyo, ninadhani kuna haja ya Kamati husika kufanya ukaguzi ili kuona wafanyakazi wetu wanatendewa vipi kimaslahi, lakini vilevile kuangalia ni jinsi gani ya kuboresha maslahi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili limejitokeza hata katika mashamba. Tumeona ni jinsi gani katika ripoti hii, wawezekezaji wanavyoweza kuwanyanyasa Watanzania kwa sababu tu wamepewa hiyo sehemu. Kwa hiyo, ninadhani kuna haja kubwa ya kuona ni jinsi gani tunaweza, hata kama ni sheria; tuone jinsi gani tunaweza kuibadili ili wananchi wetu wawe na haki katika nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, labda niongelee suala zima la mwekezaji katika Bandari. Mwenzangu mmoja amesema, lakini labda nisisitize kwamba, Tanzania tumebahatika sana kuwa katika *geographical position* ya kuwa na bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari ni zaidi ya madini. Nchi ya Singapore ambayo zamani ilikuwa na uchumi karibu sawa na sisi, sasa hivi uchumi wake umepaa ipo katika nchi kumi tajiri duniani na hii ni kwa sababu tu ya bandari. Bandari ya Singapore wanaweza ku-*handle* makontena ya ukubwa wa mita 20, ambayo wanayaita TEU milioni 35 kwa mwaka. Tanzania tuna-*handle* makontena chini ya laki tatu kwa mwaka.

Hili ni tatizo kubwa sana, lakini naamini kama tungekuwa na udhibiti na ufanisi mzuri wa kuweza ku-*handle* hayo na hii ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya barabara ili yale makontena yanapotoka pale yaweze kusafirishwa. Vilevile nchi yetu inazungukwa na nchi ambazo zinaitwa *land locked*, ambazo hazina uhusiano wa moja kwa moja na bahari. Kwa mfano, nchi ya Zambia, Malawi, Rwanda, Burundi na nyingine. Kwa hiyo, katika *position* hiyo, Tanzania tungeweza kabisa kutumia uwepo wa nchi hizi ili kuweza kuinua uchumi wetu, lakini tunashindwa na sasa hivi nchi nyingi zinatumia Bandari ya Mombasa na hivyo fursa ya kuwa na bandari inashindikana.

Kwa hiyo, ninaomba pamoja na kwamba kuna ukiritimba wa kuwa na kampuni moja tu ya kuweza kuhudumia mkampuni, ninaomba na ninashauri kama ambavyo amependekeza, tuwe na kampuni nyingine moja au zaidi za kuweza kushindana ili tuweze ku-*handle* makontena mengi zaidi kwa wakati. Labda tutoe mfano, tutaona wazi kwamba, Wabunge wengi wamekuwa wakilalamikia Kampuni ya Bohari ya Madawa kwa sababu iko peke yake na hivyo inashindwa kufanikisha kazi za kusafirisha au kusambaza madawa. Hivyo hivyo tuangalie katika makampuni ya simu; siku za nyuma tulikuwa na kampuni moja na tuliona jinsi gani kulikuwa na ukiritimba na bei kupanda na sasa hivi tuna makampuni mengi ya simu za mkononi na hizi zimesaidia sana kuboresha au keleta ufanisi katika huduma hizo. Kwa hiyo, naamini kabisa suala la bandari kama tutakuwa na kampuni nyingine za ushindani za kuweza kuhudumia makontena yetu pale bandarini, basi uchumi wa Tanzania utapaa hatutakuwa na tatizo kubwa la kiuchumi kama tulilonalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nizungumzie suala zima la mashamba. Tunajua ni jinsi gani sasa hivi kuna mtikisiko wa uchumi wa dunia. Inasikitisha kusoma katika vyombo vya habari kwamba, kuna baadhi ya mashamba yamekaa zaidi ya miaka kumi bila kufanyiwa shughuli zozote za kilimo. Mbaya zaidi, pamoja na vitendea kazi vilivyokuwa pale kama matrekta, yote hayo yameharibikia. Mimi naamini Watanzania wakulima wanapenda sana kufanya kazi za kilimo, lakini katika mashamba hayo hasa ile la Bassotu siku za nyuma tulikuwa tunapta ngano nzuri sana kutoka pale, lakini kwa miaka kumi sasa mashamba yale yamekaa bila shughuli yoyote. *(Makofi)*

Ninaomba hata kama kuna kesi zifanywe haraka ili tuweze kuhakikisha kwamba, wakulima wanafanya kazi za uzalishaji hasa tukitambua kwamba, sasa hivi hali ya uchumi si nzuri na wataalamu wa masuala ya kiuchumi wanaelekeza kabisa kwamba, nchi za kiafrika ambazo ndizo tutakazoathirika kabisa, basi kimbilio letu ni kilimo. Kwa maana hiyo, nilikuwa nasisitiza kwa Serikali na kuiomba ihakikishe kwamba, mashamba hayo sasa hivi yanainuliwa upya ili wakulima waweze kulima. Pendekezo zuri sana limetoka kwa Kamati kwamba, majeshi yetu yapewe kazi hiyo au magereza na tumeona Makutupora jinsi gani Jeshi letu limeweza kuboresha kilimo. Kwa hiyo, ninaamini kama zoezi hilo litaendelea na Serikali ikakubaliana na mapendekezo ya Kamati kwamba, mashamba hayo sasa yaweze kuzalisha upya ili tuweze kuepukana na janga kubwa la mtikisiko wa uchumi, ambao kwa kiasi kikubwa sana utaathiri maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo nataka nizungumze ni suala zima la mashirika ya umma, ambayo ni ya kutoa huduma. Labda nizungumzie masuala ya vyuo vya elimu ya juu. Kwa mfano, *core function* unakuta ni *teaching, research and consultancy*. Mara nyingi hasa kipindi cha hivi karibuni, unakuta vyuo hivyo pia vinajihusisha na biashara kubwa kubwa. Sasa kwa mfano, *University of Dar es Salaam* tuna *Mlimani City Project*; naomba kujua hivi shirika la huduma linapokuwa shirika la kibiashara kibali huwa kinatoka wapi na je, mahesabu yanakuwaje?

Vilevile ninataka kuzungumzia suala la maamuzi. Nina mfano wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wana eneo kubwa sana la ardhi na bado halijatumika, lakini cha ajabu utakuta mabweni kwa mfano kule mabibo hosteli yalijengwa na NSSF na yako mbali sana, hivyo kusababisha gharama kubwa kwa wanafunzi kwenda na kurudi. Je, maamuzi kama haya huwa yanazingatia kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kwa kifupi niseme kwamba, naipongeza sana Kamati na ninaishauri au ninaiomba Serikali izingatie mapendekezo hayo. Vilevile maamuzi yafanywe haraka, kwa sababu yakifanywa haraka ni kwa manufaa ya taifa letu na wananchi wote wa Tanzania. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Mwenyekiti, Kanuni.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 28(5). Ninachotoka kusema hapa kutokana na maelezo uliyoyatoa kwamba, wanaopata nafasi..

**MWENYEKITI:** Soma kwanza hiyo Kanuni.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inasema hivi: "Iwapo shughuli zilizopangwa kwa siku hiyo zimemalizika kabla ya saa 1.45, Spika au Naibu Spika au Mwenyekiti ataliahirisha Bunge bila kuhoji, lakini iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kufikia muda wa kuahirisha kikao Bunge au Kamati ya Bunge Zima au Kamati ya Matumizi bado haijamaliza shughuli zake, Spika au Naibu Spika au Mwenyekiti anaweza kuongeza muda usiozidi dakika 30 bila kulihoji Bunge na Kamati ya Bunge Zima au Kamati ya Matumizi ili kukamilisha shughuli zilizobaki."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia yangu ni kama unaweza kutumia mamlaka yako ili uweze kutuongezea muda huo wa nusu saa baada ya muda kwisha, kutokana na unyeti na umuhimu wa hoja yenyewe iliyoko mbele yetu, ambayo tunatakiwa tupate muda wa kutafakari ili tuweze kuwapata wengine wawili. Kama mamlaka hayo unayo, nilikuwa nahitaji mwongozo wako kama inawezekana kwa kutumia kanuni hiyo au kanuni nyingine yoyote.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni aliyoisoma Mheshimiwa Ole-Sendeka inasema, kama zimesalia dakika kumi kabla ya kufikiwa muda huo Mwenyekiti aweza ... Kwa hiyo tuendelee tutaona tunavyokwenda.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi nataka niungane na wenzangu, kwanza kabisa, kwa dhati kuipongeza Kamati hii kwa kazi nzuri waliyoifanya na pia nimpongeze Mheshimiwa Mwenyekiti kwa jinsi alivyoiwasilisha hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze kidogo kwa kusema kwamba, mwanzo katika miaka ya 1960 na miaka ya 1970, Serikali ilipofanya maamuzi ya kuanzisha mashirika haya, ilikuwa na nia njema kabisa. Lengo hasa la kuanzishwa mashirika haya; kwanza ni kutoa ajira kwa vijana wa Kitanzania. Pili, kutoa biashara kwa nchi yetu, lakini la tatu ni kutafuta utaalamu kutoka kwa nchi ambazo tayari utaalamu ule wanao ili na sisi tuweze kuupata kupitia katika mashirika yale. Kama utakumbuka kwenye miaka 1980, namshukuru Mheshimiwa Hamad Rashid amezungumza vizuri sana; kwenye miaka ya 1980 tulipoanza kufungua milango kwa kubinafsisha baadhi ya huduma zikaanza kuchukuliwa na sekta binafsi, baadhi ya mashirika yetu yakaanza kuyumba na kuonesha udhaifu katika ushindani ndani ya soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niseme haya mashirika yapo katika hutua mbalimbali; kuna baadhi ya mashirika yanafanya vizuri hivi sasa na kuna baadhi unaweza ukayaweka katika *category* ya kati kwa kati na kuna baadhi ya mashirika hali yake si nzuri. Hata hivyo hivyo, baadhi ya maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumzia ni dhahiri kwamba, hakuna shirika hata moja lenye mamlaka ya kufanya hivyo ambavyo wanafanya hivi sasa. Limeelezewa suala zima la manunuzi; kwa mujibu wa taratibu za kiserikali, nataka niseme kwamba, shirika lolote linapasa kufuata Sheria ya Manunuzi katika manunuzi yake anayotarajia kuyafanya; vinginevyo, kwenda kinyume na Sheria ya Manunuzi na hivyo nakubaliana na Kamati kwamba Serikali iliangalie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile nataka niseme tu kwamba, Bunge lako Tukufu huwa linatoa ushauri na maoni kwa Serikali. Serikali itaangalia ushauri huo na kuona pale ambapo tunapasa kutekeleza basi tutatekeleza katika kipindi muafaka. Vilevile niseme kwamba, haya mashirika ambayo Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ameyaeleza, yako mengi na kama nilivyosema, yapo katika hatua mbalimbali. Tutayaangalia yote ili kuweza kuona ni eneo gani tunapaswa kulisaidia hilo shirika ili liweze kufanya kazi kwa mujibu wa taratibu ambazo tumejiwekea. Kamati imeeleza kwamba, kuna baadhi ya mashirika yanahitaji mitaji, lakini huwezi ukalipatia mtaji shirika hili kama hujaanza kulifanyia ukarabati. Ukilipatia mtaji kama hujalifanyia ukarabati ni dhahiri kwamba, huo mtaji unaweza ukaanguka vile vile kama tunavyoona hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutayaangalia mashirika hayo ambayo tunapaswa kuyafanyia ukarabati, kama hivi sasa tunalifanyia ukarabati Shirika la Bima la Taifa ili hatimaye liweze kufanya vizuri na liweze kushindana katika soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wengi wamezungumzia suala zima la kumbukumbu katika mashiria yetu. Nakubaliana na hoja ya Kamati na Wajumbe kwamba, kweli kuna udhaifu huo kwa baadhi ya mashirika yetu. Tutajitahidi kuona kila shirika linakuwa na kumbukumbu sahihi na kwa wakati muafaka zinapohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile limezungumziwa suala la kuwa na vitengo vya ukaguzi. Kitengo cha Ukaguzi cha Ndani, lengo lake hasa kusaidia Shirika lenyewe, lakini nashangaa kusikia kwamba, baadhi ya mashirika hayana vitengo hivyo. Tutaangalia sheria zilizoanzisha makampuni yale ili kuona vitengo hivyo vinakuwepo ili kuweza kuyasaidia makampuni yale kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati vile vile imezungumzia suala la makato ya wafanyakazi kwa ajili ya kuweka katika mashirika haya ya hifadhi ya uzeeni. Nataka niseme tu kwamba, haya makato yapo kwa mujibu wa sheria. Kama shirika linakata makato, lakini haliwasilishi katika mashirika yanayohusika, hilo ni kosa na mimi nataka nikwambie Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ripoti tutaisoma ili tuweze kuona ni mashirika gani ambayo hayatekelezi kazi hiyo au jukumu hilo ili tuweze kulifuatilia kwa karibu zaidi na yaweze kufanya kazi hiyo ambayo ipo kwa mujibu wa sheria. Haya makato yanayokatwa ni ya mfanyakazi, ambayo yanamsaidia wakati atakapokuwa mzee. Kwa hiyo, ni wajibu na ni lazima yakatwe na yapelekwe kwa mujibu wa sheria ambazo tumewekeana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumziwa ni suala la wajibu na majukumu ya mbia. Ni kweli, Serikali inapoingia katika ubia na shirika lolote au kampuni yoyote au na mtu yeyote katika kutekeleza majukumu ya shirika fulani; ni dhahiri kwamba mkataba unaonesha majukumu ya kila mbia. Tutajitahidi sana kuangalia majukumu ya Serikali katika mkataba ule na majukumu ya wadau wenzetu katika mkataba ule ili tuweze kuona mkataba unaheshimika na unafanya kazi kama tulivyokubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo lilizungumziwa ni kwamba, mashirika yetu haya kupunguza matumizi yasiyokuwa ya lazima. Nadhani kuna wakati fulani niliwahi kuzungumza na Mwenyekiti wa Kamati, nikamwambia kwamba, wenzetu wanaotutazama wanauliza kwamba, shirika lenu la Air Tanzania linaruka katika mikoa ya ndani, lakini *management* na *board members* wanaruka mpaka Europe na America. Sasa nataka nikuhakikishie kwamba, tutajaribu kuangalia yale matumizi ambayo si ya lazima katika mashirika haya ili tuweze kuzungumza na bodi za mashirika na *management* kwa ajili ya kuweza kuyapunguza matumizi ambayo si ya lazima na hatimaye fedha hizo kuweza kutumika kwa yale maeneo ambayo yatakuwa ni ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo lilizungumzwa na Wajumbe wengi pamoja na Ripoti ya Kamati; ni Serikali kuingilia utendaji wa baadhi ya mashirika. Nataka niseme kwamba, siyo nia ya Serikali kuingilia utendaji wa baadhi ya mashirika, lakini kuna baadhi ya nyakati Serikali inakuwa na wajibu wa kuingilia utendaji wa Shirika lile kabla mambo hayajaharibika. Hilo ndilo lengo la Serikali, lakini tungependa

kuona mashirika yote yanafanya kazi kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na tusingependa kuliingilia shirika lolote katika utendaji wake. Kama nilivyoeleza awali kwamba, kuna wakati kabla utendaji wa shirika haujaanza kuharibika, tunapaswa kuliangalia na kuweza kuliingilia ili lisije likaenda kombo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limezungumzwa ni suala la hisa za Serikali. Wameeleza kwamba, baadhi ya hisa hazionekani na baadhi ya hisa huuzwa pasipokuwa na *proor records* na pasipokuwa na *proper procedures*. Nataka niihakikishie Kamati na Bunge lako Tukufu kwamba, hili nalo tutaliangalia kwa undani zaidi. Hisa za Serikali ni mali za wananchi na ni lazima tuweze kujua hisa hiyo iko wapi na iko kiasi gani na kama itauzwa, basi inauzwa kwa nani na inauzwa kwa utaratibu gani. Hilo tutaliangalia ili tuweze kuwa na utaratibu mzuri ambao tumejiwekea sote katika utekezaji wa suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana wakalititilia mkazo ni kuiimarisha Ofisi ya Msajili wa Hazina. Nataka nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge na Kamati kwamba, kweli Ofisi hii inahitaji kuimarishwa. Nadhani leo asubuhi Mheshimiwa Jeremiah Sumari, alijibu swali juu ya uimarishaji wa Ofisi hii. Hivi sasa Ofisi hii ina wafanyakazi 26, lakini lengo lake ili iweze kufanya kazi kwa uhakika inahitaji wafanyakazi kama 51.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niliahidi Bunge lako Tukufu kwamba, kila muda utakapokuwa unakwenda na hali ya fedha itakapokuwa inaimarika, tutajitahidi sana kuimarisha Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kuipatia Watendaji walio bora zaidi na kuipatia vitendea kazi ili waweze kutekeleza majukumu yao kama inavyotakiwa na kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nataka niseme tu kwamba, lazima Waheshimiwa Wabunge tufike mahali sote kwa umoja wetu, Mheshimiwa Hamad Rashid amezungumzia vizuri sana kwamba tuache siasa. Si kwamba upande wa Serikali tu, nasema hata kwa upande wa Wabunge; tunapokwenda kwenye mashirika haya, tuache siasa, badala ya kuzungumza siasa, tuzungumzie uchumi sasa ili tuweze kusaidiana katika kuinua mashirika haya. Tunapokwenda kuyatembelea mashirika haya, tukianza kuzungumzia siasa tu, tutawaachia siasa kwenye mashirika badala ya kuwaachia uchumi. Mimi naomba sana sisi sote Wabunge na Serikali tuna wajibu wakati tunapokwenda katika mashirika haya, hebu tuzungumzie uchumi basi; twendeni katika lugha ya kiuchumi, twendeni katika lugha ya kuwasaidia wananchi ili mashirika haya yaweze kutusaidia katika uchumi zaidi kuliko katika siasa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu wakati wa bajeti hapa tuliizungumzia sisi Wizara ya Fedha kwamba, haya mashirika tunataka nayo yachangie katika Bajeti ya Serikali Kuu, lakini la ajabu Wabunge wengi walipinga hili. Sasa bila kuwaambia wachangie hawa, maana yake hamuwapi nafasi ya kufanya kazi, wao watakuwa wanazalisha, lakini hatimaye kwa sababu hawana *mandate* ya kuchangia kile wanachokizalisha, dio hicho hicho wataendelea kutumia watakimaliza. Sasa nasema na sisi Wabunge, tuna wajibu wa kuzungumzia uchumi ndani ya mashirika haya.

Mheshimiwa Hamad Rashid amezungmzia vizuri sana; AIG limeporomoka na mashirika mengine makubwa yameporomoka ni kwa sababu hii. Nataka niseme kwamba, bila ya haya mashirika kuweza kufanya kazi kwa ukamilifu, Serikali itakuwa inatoa fedha za kusaidia haya mashirika, lakini hatimaye kinachozalishwa hakitaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme nakubaliana na hoja za Kamati na tunaisubiri kwa hamu kubwa sana, Ripoti hii ya Kamati ili tuweze kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yoyote duniani, lazima iwe na uwezo wa kusimamia na kudhibiti kwa karibu vyanzo vyake vya mapato na matumizi yake. Fedha nyingi za Serikali zinapotelea kwenye manunuzi. Manunuzi ya mashangingi siyo matumizi mazuri ya fedha za Serikali; huku Watanzania wanakula mlo mmoja wengine wanatanua na mashangingi. Tunashukuru Waziri Mkuu amesitisha.

Benki Kuu ni vurugu tupu; kuanzia EPA, ujenzi wa majengo pacha hadi bima yake ya bilioni saba. Maana yake Serikali katika vita hii ya ufisadi bado iko mbali. Watanzania wote waungane kupiga vita ufisadi, umaskini wa kipato na njaa. Wanaotuhumiwa ama hata kuhisiwa na mafisadi watajwe hadharani.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kumpongeza Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wanzangu wote, kwa taarifa nzuri sana, ambayo imegusa maeneo yote na kwa uwazi mkubwa ilivyowasilishwa pamoja na Mwenyekiti kuisoma kwa ufasaha wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunakagua mahesabu ya mashirika mengi tumegundua kuwa, Serikali inajisahau sana kuyawezesha mashirika na kusababisha mashirika hayo kujiendesha. Ninaiomba Serikali kusahihisha udhaifu huu ili mashirika yapate nguvu ya kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niyashukuru na kuyapongeza mashirika ambayo yanatekeleza Sheria ya Manunuzi katika kununua samani na vitendea kazi mbalimbali vinavyohitajika katika mashirika yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha pale shirika linapotaka kupindisha Sheria hii ya Manunuzi kwa kutaka kununua mitambo iliyotumika. Ninaiomba Serikali isimame imara kwenye sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali inapotaka kubinafsisha shirika lolote, kama wapo Watanzania wenye uwezo wapewe kipaumbele kwani na wao wataajiri Watanzania na fedha zitabaki Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, sio lazima kubinafsisha endapo Serikali itakuwa na usimamizi mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, baada mchango huu, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Kamati kwamba, Serikali iangalie au ifanye juhudi ya kununua mitambo ya IPTL, ambayo hufanya gharaza za umeme kuwa kubwa sana kutokana na *capacity charges*. Kwa kuanzia IPTL mpaka hapo nakubaliana, yatakapokubalika wahimizwe waweze kutumia gesi ambayo tayari imeshagundulika nchini. Kwa kutumia gesi angalau bei itashuka kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la PTDC lina watafiti na tayari tumeona gesi imegundulika kupatikana hapa nchini na nina uhakika mafuta yanaweza kupatikana pia. Ningeshauri shirika hili la TPDC, lipewe bajeti ya kutosha ili liweze kujiendesha na kutimiza miradi iliyo mbele yake, ambayo itaweza kutuletea unafuu wa maisha kama kila kitu kitafanywa na Watanzania.

Mfano, wakiwezeshwa vya kutosha, wataweza kuendeleza mradi wa gesi uliogundulika Mkuranga na tunajua kabisa matumizi ya gesi ni nafuu na zaidi tutatunza mazingira yetu.

Shirika la STAMICO ni muhimu sana katika kuangalia na kutunza madini yetu; kuna kila sababu ya kuliwezesha shirika hili. Nakubaliana na Kamati shirika hili lisibinafsishwe. Kwa sasa hivi tunajua madini yalivyo na bei, ukiondoa kipindi hiki cha mtikisiko wa uchumi duniani, tumekuwa tukidanganywa sana na wawekezaji katika sekta hii. Kwa mfano, mwekezaji anachimba Tanzanite inayopatikana Tanzania tu, lakini wanabeba mchanga ambao utakuwa na madini mengine wanapeleka kwao halafu ndiyo wanatueleza walipata madini kiasi gani; huu ni udanganyifu. STAMICO wakiwezeshwa wanaweza wakafanya shughuli zote hapa nchini na Taifa likafaidika na hatimaye uchumi wetu utakua na kuweza kuendeleza mambo mengi; kwa mfano, miundombinu ya barabara na kadhalika.

Kwa kuwa TICTS imeshindwa kabisa kuboresha au kutoa huduma nzuri ya kutoa vitu bandarini na kupelekea wafanyabiashara wengi kukimbilia Mandari ya Mombasa kupitisha bidhaa zao. Hii imetufanya Tanzania kukosa mapato mengi.

Nashauri, ili kuondoa hii *monopoly* ni wakati muafaka sasa kwa sababu kuna soko huria, iruhusiwe iwe zaidi ya kampuni moja na ziwe na vifaa vya kutosha kufanyia kazi.

Mwisho kabisa, napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, pamoja Wajumbe wote wa Kamati kwa kuandaa *report* hii.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nichukuwe nafasi hii kuipongeza Kamati ya POAC, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na kuiwasilisha leo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii inashughulika zaidi na kusimamia mashirika ya umma, ambayo Serikali ina hisa kwayo. Mashirika mengi haya ya umma ni yale ambayo Serikali ina hisa kuanzia asilimia 50 na zaidi ya hapo.

Ni dhahiri kwamba, Serikali imewekeza kiasi fulani cha fedha ili ipate faida. Bahati mbaya, mashirika ya umma baadhi yao hayatengenezi faida na kuwa mzigo kwa Serikali.

Tatizo hili linatokana na ama Bodi za Mashirika hayo kuwa dhaifu kuwasimamia Watendaji au baadhi ya mashirika ya umma kuwa na uchache wa mitaji.

Ni vyema, basi chombo kinachosimamia uteuzi wa Wajumbe wa Bodi wawe makini katika utenzi huo ili kupatikane Wajumbe walio na uelewa na uwezo wa kuendesha mashirika hayo.

Aidha, Serikali nayo kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina, iimarishe mitaji ya mashirika ambayo Serikali imewekeza ili iweze kujiendesha kwa ufanisi zaidi. Moja katika mambo ambayo Kamati ya POAC imebaini na kadhalika Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni kitendo cha baadhi ya Mashirika ya Umma, kutotekeleza na kufuata Sheria ya Manunuzi.

Hali hii imetokana na sababu kwamba, baadhi ya mashirika ya umma na taasisi nyingine, hazikuwa na vitengo vya usimamizi wa manunuzi ya umma. Aidha, Kamati ilibaini kulikuwa na udhaifu mkubwa katika usimamizi wa mikataba ya manunuzi au baadhi ya vitengo vilivyomo katika mashirika ya umma vinahudumiwa na watendaji waiso na ujuzi wa kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii imesababisha Serikali au Mashirika yanayohusika, kupoteza fedha nyingi au fedha hizo kuliwa kijanja. Ni vyema basi Serikali kupitia kwa Msajili wa Hazina, kuhakikisha kwamba, mashirika yote ya umma pamoja na taasisi nyingine za umma, zinaunda vitengo vya kusimamia manunuzi ya umma. Aidha, vitengo hivyo visimamiwe na watendaji waliobobea katika fani hiyo.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, kwa taarifa nzuri na yenye kuonesha kazi kubwa inayofanyika. Katika maelezo ya taarifa, ukurasa wa nne unasema kuwa mashirika yaliyotajwa ni yale waliyoyateuwa kutona na umuhimu katika uchumi wa nchi. Je, *ATCL* hamwoni pia ni vyema Kamati ingepata uchambuzi wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutembelea mashamba yaliyobinafsishwa; je, Kamati imewahi kutembelea ranchi zilizobinafsishwa? Je, Kamati imewahi

kuitembelea Bandari ya Tanga? Ina *potential* kubwa endapo itaimarishwa; tunangoja nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wanakuja lakini hawajibiwi au wanakuwa *discouraged.* Ni vyema Kamati yako ikazingatia hilo. Napenda kuwapa hongera tena.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana na Wajumbe wa Kamati hii, kwa kazi nzuri wanayofanya. Bado ni wapya lakini kishindo na ubora wa kazi yao unaonekana na kutikisa mashirika mengi ambayo yalishajisahau na kufanya kama wanavyopenda. Pia naomba muingilie kati ili bodi zinazotolewa kwenye masharika yote ya umma, ziwe na wajumbe wenye taaluma hizo; kwa mfano *TANESCO*, *TANAPA* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mingi tumekuwa tunalalamika juu ya ujangiri Wizara ya Maliasili na mashirika yake. Baada ya kupiga kelele kwa miaka mingi, juzi Waziri mwenyewe kagundua uozo ndani ya hifadhi zetu. Uozo huo ukihusisha hata Wajumbe wa Bodi na baadhi ya Wabunge wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe na Kamati yako sasa ni jukumu lenu kuingia kwa undani zaidi. Bado kuna uozo mkubwa zaidi; kugawa umeme kwa upendeleo na bei kubwa za kuingiza umeme ndani ya nyumba zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kukupongeza wewe, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote, kwa taarifa nzuri iliyowasilishwa Bungeni.

Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

(i) Naishauri Serikali iweke kitengo maalumu cha kushughulikia hati miliki za viwanja kwa kuwa kuna urasimu katika kuzitoa na ucheleweshaji usio wa lazima.

(ii) Kwa kuwa mashirika mengi hayafuati sheria na kanuni za manunuzi; hivyo naishauri Serikali kwamba, mashirika yote yaweke kitengo cha manunuzi kama Sheria ya Manunuzi ya 2001 na kurekebishwa 2004 inavyotaka.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Ninashauri yafuatayo:-

- Wastaafu wa Mashirika ya Umma waongezewe na kulipwa kwa mkupuo;

- Kamati iishauri Serikali ili iweze kutembelea Mashirika yote yaliyobinafsishwa na viwanda ambavyo vipo nchini;

- Kukagua vyama vya Wafanyakazi sehemu ya kazi kama vipo;

- Kuangalia kima cha chini cha mishahara;

- Kuangalia kama Wafanyakazi wamewekewa akiba (PPF, NSSF) kwani makampuni makubwa ni wababaishaji;

- Kukagua vitendea kazi kwenye viwanda vya uzalishaji;

- Kamati iangalie maji yanayotiririka kwenye makazi ya watu toka viwandani;

- Kamati itembelee Shirika la IPTL iangalie huduma yake na ikiwezekana isafiri kwa njia ya reli mpaka Kigoma/Mwanza;

- Ninaomba Kamati ya Bunge itembelee Kiwanda cha Nyuzi Tabora; na

- Serikali iendelee kulipa madeni ya watumishi wa Kiwanda cha Nyuzi ambao bado wanadai haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Kamati za Bunge, zinazojishughulisha na Mahesabu ya Serikali za Mitaa, Serikali Kuu na hii ya Hesabu za Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema tukawa tunajali miradi au utekelezaji wa miradi kuliko kuangalia kwa nini pesa hazikutumika ipasavyo. Ni jambo linalokera sana, kuona hoja zinaletwa mwaka unaofuata zimejibiwa risiti zote zinapatikana, lakini ukienda *field* kukagua unakuta hazifanani na kwenye makaratasi yaliyokaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya majukumu ya Kamati hii ni kutathmini ufanisi wa mashirika ya umma na kufuatilia utekelezaji wa sera ya ubinafsishaji wa mashirika ya umma. Mambo haya ni muhimu kufanyika, kwa sababu mmiliki wa mali zote ni Serikali chini ya Msajili wa Hazina na Bunge kazi yake ni kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona mpaka leo bado kuna Mashirika ambayo hayana Kamati ama vitengo vya ukaguzi wa ndani, ingawa Kanuni ya 30 ya Sheria ya Fedha za Umma, 2001 inalitaka kuwa na Kamati ya Ukaguzi wa ndani, kwa

lengo la kuongeza nidhamu zaidi katika kusimamia fedha za umma na kuweza kugundua mapema na hivyo kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza hadi 2006/2007, bado kuna mashirika hayakidhi hiyo kanuni ya 30 ya Sheria ya Fedha, mfano bodi ya chai, Tume ya Vyuo Vikuu nchini, Shirika la Soko la Kariakoo, Bima na Chuo cha Ushirika Moshi. Haya ni madhara makubwa sana kwani kunakosekana udhibiti wa mali za umma katika shirika husika na kazi zao hazina ubora wa ukaguzi wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili lisijirudie tena. Naungana na maoni ya Kamati kwa agizo lao kwamba, mashirika haya yatimize hayo ya kisheria kupitia Kanuni ya 30 na wasipotekeleza, Kamati itumie vifungu mahususi vya Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge dhidi ya maafisa masuhuli wanaohusika na uzembe huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mwenyekiti wa Kamati, kwa kuliweka wazi suala la kukosekana mitaji ya kujiendesha. Ni jambo la kusikitisha sana; kuna mashirika kama *ATCL*, *TANESCO, NIC, TPDC*, haya ni mashirika muhimu sana yanayoendeshwa kwa kusuasua na ambayo yanatoa huduma kwa Watanzania yakiwemo hayo mengine niliyoyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashirika yametoa maombi yake kwa Serikali yapatayo bilioni 60 ila hayakupewa. Pamoja na hilo, mashirika hayo ambayo mengi yanatoa huduma ila uendeshaji wake ndiyo mbovu, watendaji hawazingatii misingi ya kazi zao; matokeo yake mashirika yanajiendesha kwa hasara ingawa huduma hazitolewi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe pesa hizo lakini iwe makini kuwawajibisha wale wanaofanya mashirika hayo yashindwe kwenda mbele. Waajiriwe watu wenye uwezo. Mfano mwingine ni *TRL*, shirika hili kabla likiitwa *TRA*, lilitoa huduma zaidi ya mara tano kwa wiki, reli ilijaa kila siku lakini cha kushangaza liliishia paya sana na matokeo yake kubinafsishwa kwa wahindi. Napendekeza Serikali ianzishe utaratibu wa kuingia mikataba na maafisa masuhuli badala ya kuteuliwa kwa mtindo uliozoeleka ili wajue wamebeba dhamana na wakiharibu wafukuzwe mara moja, isiwe kwenye mashirika tu hata katika wizara, kwani maeneo mengi kwa kuzingatia Ripoti ya *CAG* kuanzia Seriakali za Mitaa, Wizara zetu kwenye mashirika hali inafanana; sheria za fedha hazifuatwi na sheria za manunuzi pia hazifuatwi hivyo, kupelekea mapato ya nchi kupotea na ufanisi wa pesa ndogo zilizopelekwa kote huko hazioneshi tija. Tukubaliane tusigeuze nchi yetu kuwa shamba la bibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninashauri kwa wale wote ambao wamegundulika kuwa kwa namna moja au nyingine wamehujumu mali ya Watanzania, wachukuliwe hatua; isiwe waliofikishwa mahakamani wakafanywa ndiyo kielelezo kuwa wameshawawajibisha wahujumu, bado wapo wengi, hatua ziendelee kuchukuliwa ili kuleta nidhamu kwa watumishi wote bila kujali vyeo vyao au nyadhifa walizowahi kuwa nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yote yaliyotolewa na *CAG,* pamoja na yale yaliyotolewa na Kamati zote tatu yazingatiwe na Serikali ili tupate tija ya kazi zinazofanyika na pesa zinazotumika kufanya kazi hizo thamani yake ionekane, wakati mwingine Kamati hizo zisijikute zinaendelea kusisitiza mapendekezo ambayo tayari yameshatolewa, mojawapo ikiwa ni pendekezo la *PAC* la kupunguza wigo wa msamaha wa kodi kwa kuleta sheria zinazosamehe kodi; turekebishe makosa twende mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya CAG inaonesha Tanzania imepoteza shilingi bilioni 791.4; hizo ni pesa nyingi sana na nchi yetu bado haijaweza kujitegemea katika kujiendesha, hayo ni makosa lazima turekebishe pote tulipokosea. Sheria zote zinazotoa mwanya wa upotevu zirekebishwe ili tusiendelee kupoteza na wajanja wengine wasiendelee kutumia zile sheria zinazotoa mwanya wa kupoteza mapato.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niwe mmojawapo wa wachangiaji wa hoja hii ya Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma. Nichukue nafasi ya pekee, kumshukuru Mwenyekiti kwa kunigawia dakika 15 kwa sababu ameleta tofauti katika Kamati kwamba na Makamu ni Makamu anayeweza kuchangia kwa nafasi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kuchangia, kwanza kwa kupitia baadhi ya hoja ambazo wajumbe wameweza kuchangia; atawataja na baadhi ya hoja lakini kuna zile ambazo mimi mwenyewe naomba nipunguze ili kumsaidia Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza imetoka kwa Mheshimiwa Kaboyonga; amezungumzia sana mambo ya *procurement*, ndiyo maana Wajumbe wengi wamechangia haya tuliyotoa kwenye taarifa ni kama dokezo. Nafikiri hata mashirika ya umma walikuwa wamejisahau sana, kwa sababu mara nyingi wamekuwa hawapeleki hizi hesabu kwenye Kamati mahususi kama ya kwetu, wamekuwa wakipeleka kwenye Kamati za Kisekta. Kamati za Kisekta wanazungumzia zaidi sera, kwa hiyo, hesabu zimekuwa kama ni sehemu ya kupitia tu. Ukiangalia mashirika mengi, Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu hapa, *procurement* imekuwa kama kichaka fulani hivi cha kuchulia pesa za Serikali. (*Makofi*)

*Internal control* kote ni kuzuri, lakini unapokuja kwenye manunuzi, labda niungane Mheshimiwa Kaboyonga alivyosema kwamba, inawezekana Sheria hii ya Manunuzi ina matatizo. Ukiangalia kuanzia kwenye Serikali za Mitaa na Serikali Kuu, kwa sababu kote huko nimepita na sasa niko Mashirika ya Umma, imekuwa ni tatizo sugu; sasa sijui kuna matatizo gani? Mashirika yote haya makubwa ukizungumzia TANESCO, Benki Kuu na hata *NSSF*, utakuta ni tatizo kubwa sana kwenye upande wa manunuzi na ni hela nyingi sana zinatumika.

Ukienda hata kwenye Bodi ya Mikopo, mfano ulio rahisi tu, tulikutana na jambo ambalo sisi wenyewe tulishangaa; walikuwa wanafanya manunuzi kwanza kitu kingine cha kushangaza sasa *signatory* walikuwa ni *Board Members* wenyewe ndiyo wanaosaini *cheque* za matumizi, pamoja na manunuzi. Kulikuwa kuna kununua *software computer,* zilizogharimu Dola za Kimarekani kama laki moja na themanini na nne, ambayo ni

milioni 200 na zaidi. Ile kusaini mkataba 70% ya *cash* inalipwa, anapoanza kufanya kazi ile 30%; hivi unafikiri yule mtu atakuja? Mpaka tunapozungumza sasa, ule mtambo ulikuwa haujafungwa na haufanyi kazi na yule mtu sijui ameingia mitini wapi. Sasa huo ni mfano mdogo. Unashangaa hii sheria ina matatizo gani; kwa kweli inagusa kama alivyosema Mheshimiwa Hamad Rashid, Mheshimiwa Kaboyonga na wengine.

Ninafikiri ilitungwa mwaka 2001 tukiwepo hapa wengi na wengine lakini ikaonekana ina matatizo imerekebishwa 2004, sasa sijui tena kuna matatizo wanasema kuna kucheleweshwa manunuzi, nafikiri kuna vipengele fulani ambavyo vinahitaji kurekebishwa. Niseme Mheshimiwa Waziri wa Fedha, pamoja na kujibu; pesa nyingi zimepotea sana kwenye manunuzi. *(Makofi*)

Lingine ambalo Mheshimiwa Kaboyonga na Msemaji wa Kambi ya Upinzani wamelisemea ni upande wa ubinafsishaji; ubinafsishaji haukulenga yale ambayo yalikuwa yanalengwa. Nafikiri Mwenyekiti aliongea hapa kwa msisitizo, lakini ukienda kwenye sera ya ubinafsishaji haijatekelezwa kadiri Serikali ilivyokuwa imepanga kufanya.

Kwenye kile kichaka cha *specification*, una-*specify* shirika halafu watu wanachukua mali bila kuweka rekodi. Hatujui ni mali gani ambazo zimechukuliwa kienyeji na zimewekwa wapi. Mtu anauza shirika hajali nyaraka za Serikali zimeachwa ndani ya mashirika na sehemu nyingine tumekuta nyaraka za Serikali ambazo Shirika limeuzwa, zinatumika kukusanyia mapato ya shirika hilo ambalo wamenunua. Sasa maana yake walipouza hawakujali kuondoka na vitabu, wala hawakujali kuangalia ni kitu gani wamekikabidhi. Kwa hiyo, hilo tumeliona kama Kamati, ninafikiri ni sehemu muhimu sana. Sisi kama Kamati tumependekeza kitu kimoja; tumesema SHC ipite iangalie mashirika yote yaliyobinafsishwa; shirika moja baada ya lingine kufanya uchunguzi wakishirikiana na CAG, kuona ni mahali gani ambapo utaratibu haukufanywa, tuletewe taarifa Kamati tuipitie tuweze kuwasilisha mbele yenu muone ni hali halisi kiasi gani ambayo imefanyika. Kwa hiyo, tunafikiri hilo kwa yale mashirika ambayo yamebaki kama kuna mahali tuliteleza tutarekebisha na tutakwenda vizuri.

Naibu Waziri wa Fedha umesema hapa kwamba, tukienda huko tuache siasa, mengine tulikuwa tunayasikia uchumi ni siasi na siasa ni uchumi. Tunakokwenda hatufanyi mchezo tunafanya kazi na hamuwezi kuamini Waheshimiwa Wabunge, Kamati yetu kupitia mashirika yote 78, tumekuwa muda mwingine tukikaa mpaka saa mbili za usiku bila kwenda kupumzika hata mchana, siku nzima mashirika manne au matatu. Kwa kufanya hivyo, tungeweza kufanya shirika moja moja, nafikiri mngeona madudu mengi zaidi na tumeweza kupitia yale ambayo CAG ameyaainisha. Kwa hiyo, tuko *serious* na nafikiri hesabu za 2008 mtaona mabadiliko makubwa sana.

Kingine niseme kwamba, kitengo cha msajili kimetuangusha kwa muda mrefu, nafikiri kuna makosa pale yalikuwepo. Ukisoma idadi ya watu 26 si hoja, lakini watu walioko ndani ya kile kitengo nafikiri ndiyo tatizo. Inasikitisha mnapokaa kuhoji shirika mnaanza kutazamana, yule unayemtegemea mwenye mali akupe jibu hajui; unamuuliza kuna tatizo gani hafahamu! Sasa sisi Wabunge tunabaki kumtegemea *Chief Executive*

atupe historia na kama kuna makosa yamefanyika huwezi kupata majibu sahihi. *Board Member* huwezi kukaa zaidi ya vipindi vitatu, sita, nane, wewe uko kwenye shirika moja tu; baadaye unazoena na menejimenti na hata uwoga haupo. Nafikiri tungepitia mashirika mengine, wakae *term* mbili za miaka mitatu, mitatu, ije Bodi nyingine ili kuleta changamoto mpya.

Tumezigundua Bodi nyingine zimekuwa *part and parcel* ya *managementi* ya shirika au taasisi. Kwa hiyo, usimamizi unakuwa haupo. Tukafiri hili na sisi kama Kamati tupendekeze kwamba, hapa kunahitaji kuangaliwa kwa undani zaidi.

*Internal Control,* Kitengo cha Ukaguzi na jana nimesikia kwenye zile Kamati mbili watu wamechangia hapa kuna tatizo. Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kinatakiwa kiwe chini ya nani; kiripoti kwa nani; na je, ni *part and parcel* ya menejimenti ya shirika? Ninafahamu kwamba, Bodi zote zina Kamati ya Bodi ya Ukurugenzi na ninavyoamini *Chief Internal Auditor* anatoa taarifa kwa Bodi ya Ukaguzi na anakuwa kama mshauri; lakini kama atakuwa anaripoti kwa Mkurugenzi, tayari pale hakuna *internal control* yoyote inayokuwepo.

Kwa hiyo, usimamizi wa mashirika haya haupo. Mashirika yote tuliyopitia mfano wa Shirika la NDC, *of course,* kuna *internal auditor* na kila kitu; utashangaa upande wa umiliki wa mali wanahati miliki za nyumba nyingi na hati miliki za viwanja lakini viwanja vile vimeshamilikiwa na vimeshabadilishwa na watu wengine na havipo. *(Makofi)*

Mkaguzi alishaangalia hicho kitu, lakini tunasema *internal auditor* kazi yako ni kupitia hii mali yote iliyoko hapa, unakagua nini na inakuwaje ukabidhi yale maifaili ya hati lakini kumbe *asset* yenyewe inayowakilisha ile hati huna, maana yake nini? Kwa hiyo, tumeona upungufu mwingi sana. Mashirika haya ya pensheni alichosema Mwenyekiti kwamba, Serikali isiingilie utendaji wa mashirika ya umma au taasisi za serikali; ameongea tu kistaarabu kwa maana ya kuandika si kwa maana ya usimamizi; *instruction* za matumizi zinatoka zaidi Wizarani kwenda kwenye mashirika; wale watu wanashindwa kujitegemea ndiyo maana yake. Nafikiri tunapitisha bajeti kwa ajili ya Serikali Kuu kwa maana ya Wizara, lakini wanapokuwa wamekwama wanaangalia sasa tuombe NSSF wakopesheni hapa, kopesheni PPF hapa na nini, kwa hiyo, wanashindwa kujiendesha. TICRA mnaelea kidogo, pelekeni hela za kutengeneza Barabara ya Msata, pelekeni hela za kutengeneza Kiwanja cha Ndege Mwanza, lakini tulishawapitishia bajeti hapa na Serikali Kuu na hela zenu mnazo mnaendeaje kuchukua zile kienyeji; *how do you account that money*? Kwa hiyo, tumeona huo upungufu. *(Makofi)*

Tunafikiri hii mifuko hii isiwe ndiyo mahali pa kukimbilia, kwa sababu unapozungumzia NSSF sasa ina bilioni 117 zimewekezwa kwenye vitu ambavyo ni vya kudumu; fikiria leo kwa hali halisi iliyopo wanaotaka kuchukua mafao yao wakatokea na hela nyingi tumewekeza mahali ambako *cash* haiwezi kurudi baada ya mwezi mmoja, maana yake wale wanaostahili kupata mafao yao hawatapa kwa wakati unaofaa. Kwa kufanya hivyo, kwa kuwekeza kwenye majengo tujifunze, bima tumewekeza kwenye majengo lakini baadaye sasa bima imekufa inahitaji pesa za kujiendesha za kila siku.

Huwezi ukauza nyumba leo au ukakodisha nyumba leo, maana yake na PPF, *NSSF* zitakuja kufa baadaye. Nilikuwa nafikiri Serikali iache kudhamini madeni kwa kutegemea mifuko hii ya pensheni. *(Makofi)*

Limezungumzwa sana suala la Bodi ya Mikopo, ambayo inaunganisha na Waheshimiwa Wajumbe ambao wamechangia hapa hali halisi kwa maana ya *internal control;* kikubwa tulichokiona kwenye Bodi hii ni kwamba, wana-*lack internal control*, kunahitaji kufanya *restructuring* kule kwa sababu jinsi kilivyoanzishwa chombo chenyewe na watu walioko na madeni yaliyolimbikizwa, sasa hivi wanataka kudai madeni kwa kutumia wakala. Sasa ukiangalia ile *procurement* yao ya kupata wakala, utashangaa kidogo wanaposema kutathmini na ku-*identify* nani anadaiwa watamlipa 4% ya deni ya orodha ya watu wanaodaiwa. Akishapata orodha anze kudai 3.5%, ambao sisi Kamati tulisitisha tukasema huo utaratibu haufai waangalie njia nyingine ya kupata hayo madeni. Kwa kuwa Serikali iko hapa, tunafikiri kwamba wawasaidie Bodi ya Mikopo, pesa nyingi *billions* ziko kule.

Tunajua wafanyakazi waliomaliza chuo wengi wako TAMISEMI; wanaweza wakaongea na Katibu Mkuu wa TAMISEMI akaainisha ni wanafunzi wangapi ambao wanafanya kazi huko. Vilevile tukasema awasiliane na Makatibu Wakuu, kwa sababu wako Mawizarani huko wanafanya kazi na kwenye Mashirika ya Umma; wawarahisishie hawa Bodi ya Mikopo kukusanya mikopo na baadaye iwe kama *revolving fund* ya kusaidia kukopesha wanafunzi wengine. Kwa sasa hivi pesa hazikusanyiki ziko huko nje.

Hoja nyingine ambayo imechangiwa na Mheshimiwa Stella Manyanya, ambayo Mwenyekiti ataisisitiza zaidi lakini nilikuwa naomba niliweke vizuri tu kwamba, kilichopo kwenye kiambatanisho kile ilikuwa ni kuwekana sawa kwamba, tulishaelewana Kamati hizi mbili tunafanya kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zilizobaki atakamilisha Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 69(1); Mbunge anayependa mjadala unaoendelea juu ya hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadaye, anaweza kutoa hoja kwamba, mjadala sasa uahirishwe na atataja mjadala huo uhairishwe hadi wakati gani na pia atalazimika kutoa sababu kwa nini anataka mjadala uahirishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni hiyo, nimelazimika kusimama kuomba mjadala huu uahirishwe na usihitimishwe kutokana na sababu zifuatazo: Kwa bahati mbaya sana tangu tumeanza kikao hiki, muda umekuwa adimu katika kujadili masuala mazito ambayo ni matakwa ya Katiba, Bunge letu kupokea taarifa hizi za Kamati na kuzitendea haki. Leo tumepokea Taarifa ya Kamati ya Mashirika ya Umma na kwa bahati mbaya sana, kutokana na ufinyu wa muda, Wabunge wachache sana nadhani kama sijakosea ni watano wamepata fursa ya kuijadili hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili zito linahitaji kupata muda wa kufafanuliwa vizuri na Wabunge wapate nafasi ya kueleza na kutafakari na kutoa mwelekeo juu ya hatua madhubuti zinazopaswa kuchukuliwa, kutokana na ufisadi mkubwa uliojidhihirisha kwenye mashirika haya umma. Iwapo Bunge hili litahitimisha hoja hii ambayo imeonesha ubadhirifu mkubwa katika mashirika ya umma, kwa mapendekezo machache yaliyoko, mimi naomba kutoa hoja kwamba, hoja hii iahirishwe kwa sababu nakusudia na mimi kuleta mapendekezo ya maazimio iwapo Wabunge wenzangu wataniunga mkono na kwamba napendekeza ijadiliwe kwenye kikao kijacho cha Bunge na kama haitawezekana kwenye kikao kitakachofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja na naomba wenzangu waniunge mkono.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Mheshimiwa Ole-Sendeka leo ananipa mitihani, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Sendeka mimi ndiye niliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati iliyotengeneza kanuni hizi kwa kiwango kikubwa sana; kwa hiyo nazifahamu vizuri.

Nianze na hoja yake ya mwanzo ili nitoe maelezo kidogo; mwanzoni alikuja na Kanuni ya 28(5) ambayo inasema; iwapo shughuli zilizopangwa kwa siku hiyo zimemalizika kabla ya saa 1.45, Spika ataliahirisha Bunge bila kuhoji, lakini iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kufikia muda wa kuahirisha Kikao cha Bunge au Kamati ya Bunge Zima au Kamati ya Matumizi bado haijamaliza muda wake, Spika anaweza kuongeza muda.

Kifungu hiki kinanipa mimi nafasi ya kufanya maamuzi haya bila kuambiwa na mimi vilevile nimewekewa masharti kwamba, zikibaki dakika kumi na kumi hizo hazijafika; kwa hiyo ndiyo maana ile ya kwanza ilikuwa ngumu. Ambacho angekifanya Mheshimiwa Sendeka au Mbunge mwingine yeyote wakati ule ni kutumia Kanuni ya 150. Sasa hapa nakufundisha; Kanuni ya 150 kwamba; kwa idhini ya Spika, kanuni yoyote inaweza kutenguliwa kwa madhumuni mahususi baada ya Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Mbunge yeyote kutoa hoja kwa ajili hiyo. Hoja ya kutengua Kanuni za Bunge haitahitaji kutolewa taarifa.

Sasa ni hoja gani ambayo ungeiomba wakati ule itenguliwe, hoja hiyo ni fungu la 28(4) kwamba, Bunge litaendelea kukaa hadi saa 1.45 usiku, wakati ambapo Spika atasitisha shughuli na kuliahirisha hadi kesho yake au siku nyingine atakayoitaja; hii ndiyo ungeomba itenguliwe, wakati ule sasa ukaja na *style* ambayo ni tofauti kidogo.

Umekuja na Kanuni ya 69(1), umeisoma na mimi nairudia ili twende pamoja; Mbunge anayependa mjadala juu ya hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadaye, anaweza kutoa hoja kwamba, mjadala sasa uahirishwe na atataja mjadala huo uahirishwe hadi wakati gani na pia atalazimika kutoa sababu kwa nini anataka mjadala uahirishwe.

Mheshimiwa Sendeka amefuata masharti ya kifungu hiki, lakini ambacho hakufanya ni kuendelea 69(2) inasema; kama Spika atakuwa na maoni kwamba kuahirishwa kwa hoja hiyo ni kinyume cha uendeshaji bora wa shughuli za Bunge, atakataa kutoa hoja hiyo ili iamuliwe na kwa jinsi hiyo, nakataa kutoa hoja ili iamuliwe. Namwomba Mheshimiwa Zitto aje hapa amalizie hoja yake.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mweyekiti, nakushukuru sana, siyo kwa maamuzi yako lakini kwa sababu inawezekana kabisa labda ni kutokana na unyeti wa suala hili, Wabunge walikuwa wanataka wajadili sana, lakini pia kutokana na ufanisi wa uendeshaji wa shughuli na kwa kuwa bado *CAG* ndiyo kwanza ametoa taarifa mpya ya mashirika ya umma; mambo haya yataendelea kujadiliwa kwa sababu tutatengeneza ripoti nyingine tena kutokana na taarifa ya sasa ya *CAG*. Kwa hiyo, bado Waheshimiwa Wabunge wana nafasi tu ya kuweza kujadili. Nakushukuru kwa uamuzi ambao umeweza kutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata wachangiaji kumi na nne waliochangia kwa kuzungumza humu Bungeni; nao ni Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Kiongozi wa Kamabi ya Upinzani Bungeni; nakushukuru sana kwa kunilea katika Shughuli za Bunge, Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, kaka yangu na Naibu Waziri ambaye ametoa ufafanuzi wa hoja za Kiserikali na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Estherina kilasi; nakushukuru sana kwa kujibu hoja, maana yake wenzetu waliopita Mwenyekiti alikuwa anajibu kila kitu, tunasahau kwamba Kamati zina Makamu ambao wanafanya kazi kwa kiasi kikubwa sana na pia kwa uongozi wako, maana yake ni zaidi ya kuwa Makamu ni kama mama na umekuwa ukitoa *guidance* mbalimbali katika shughuli zetu za Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Mgana Msindai, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya LAAC, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajibu tu kwa ujumla kwa sababu michango mingi ni ya kuboresha na nimtoe tu wasiwasi Mheshimiwa Stella Manyanya, kama alivyosema Makamu Mwenyekiti kwamba; ni kweli ulitokea mgongano na katika jamii migongano ni vitu vya kawaida na inaboresha majadiliano. Ninaamini kabisa kwamba, kila Kamati ilikuwa ina maslahi ya Taifa na tulikaa katika Kamati ya Uongozi na kulitatua suala hilo na kukumbushana tu majukumu mbalimbali ya Kamati za Bunge, kwa sababu yameainishwa katika Kanuni za Bunge ili tuweze kufanya kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu imekuwa ikifanya kazi kwa pamoja na Kamati nyingine mbalimbali. Itakumbukwa kwamba, tulipoamua kufanya ziara ya kwenda kukagua Mradi wa Kagera Sugar, kwa sababu mashirika mbalimbali ya Hifadhi ya Jamii yalikikopesha kiwanda kile, tuliwaomba Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya

Jamii twende nao na Waheshimiwa Wabunge wa Kamati hiyo tulikuwa nao kwa sababu wao wanahusika na NSSF tungekwenda peke yetu wangekosa *input* ile.

Tulimwomba Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi tupate Wajumbe wa Fedha na Uchumi wanaohusika na TIB, wanaohusika na PPF na tulifanya ziara kwenda nchini Afrika Kusini na Kenya. Makamu Mwenyekiti aliungana na Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili, kwa sababu tulikuwa tunaangalia ni jinsi gani ambavyo nchi nyingine zinashughulikia Hesabu za Hifadhi za Taifa, lakini tukaona kwamba sisi kama Kamati, tutaangalia mahesabu lakini ni vizuri kuwahusisha wenzetu wa Kamati za Kisekta ili nao watakaporudi kwenye Kamati zile waweze kushughulika na masuala hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwamba, Kamati yako ilitoa ushirikiano, kwa hiyo, tumekuwa tukifanya kazi kwa pamoja na ni lazima Kamati za Bunge ziweze kushirikiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kimoja ambacho nilikuwa napenda niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, kama Taifa lazima kuwe na vitu ambavyo Mtanzania atasimama na kijivunia. Ukienda Kenya leo, Wakenya wanajivunia sana Kenya yao; kwa mfano, kwa sababu ni *National Carrier* yao ambayo inaenda kila mahali Afrika. Leo tukisema tuulizane hapa Tanzania ni nini ambacho tunasimama tunajivunia nacho, ukienda Afrika Kusini kampuni ya umeme ya AFCOM, sisi tunachokisema ni kwamba ni lazima kama nchi tutengeneze *National Champions*, tutengeneze nchi ambayo tutasimama na kujivunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya shirika ambalo Kamati imeona kwamba, tukilifanyia kazi vizuri tutajivunia nalo ni Shirika la Umeme (TANESCO). Tukilifanyia kazi vizuri, tukapunguza matatizo ambayo yapo ambayo juhudi zimeanza kufanywa za kuyapunguza nimewaeleza.

Nimeona katika kile kiambatanisho namba kumi, Mkaguzi Mkuu alifanya ukaguzi maalumu wa ubinafsishaji wa TANESCO wakati tumekodisha kwa *NetGroup Solutions* na akapima mafanikio ambayo yalifanyika wakati shirika lile linaongozwa na wale watu ambao tuliwakodishia kutoka Afrika Kusini na mwaka mmoja wa shirika kuongozwa na Watanzania Wazalendo wakakuta mabadiliko makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa *NetGroup Solution*, TANESCO ilipata hasara ya bilioni 162, mwaka mmoja wa utendaji wa uzalendo TANESCO imepunguza ile hasara kutoka bilioni 162 mpaka bilioni 67 ndani ya mwaka mmoja wa utendaji wa wazalendo na tumewaambia TANESCO wajitahidi tunataka mwakani tutakapokutana nao wawe wame-*break even*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu lengo letu siyo tu kuiona TANESCO inawekeza Tanzania tu, tunataka iwekeze Rwanda, iwekeze Burundi, iwekeze Kenya, iwekeze nchi nyingine za hapa na ndiyo tuitumie kama silaha yetu ya siasa za Maziwa

Makuu. Kwa hiyo, unapowaona Watanzania wenzako mmewapa majukumu, wanajitahidi kuyatekeleza yale majukumu; jambo la kwanza na la muhimu kabisa kufanya ni kuwapa moyo na ndicho tulichokifanya sisi Kamati ni kuwapa moyo ili waongeze juhudi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia kumi na mbili tu ya nyumba za Tanzania zina umeme na kama alivyosema Mheshimiwa Stella Manyanya kwamba, kwa mfano, Dar es Salaam nusu ya nyumba zake hazina umeme na ndiyo Makao Makuu ya Nchi kwa maana ya mji wa kibiashara. Tunafahamu kwamba, Makao Makuu ni Mji wa Dodoma kwa mujibu wa sheria na Wilaya zinazoongoza kwa upatikanaji mkubwa wa umeme.

Kwa mfano, wilaya tatu ni Wilaya ya Ilala asilimia 46, Kinondoni asilimia 45 na Iringa Mjini asilimia 45; hizo ndiyo za juu kabisa chini ya asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ambazo hazina kuliko zote katika Tanzania ni Mtwara asilimia 0.1 ya nyumba ndiyo zina umeme, Sumbawanga asilimia 0.1, Biharamulo asilimia 0.2; hali hii ni lazima tuirekebishe na kama Taifa ni lazima tuamue kwamba, sasa tumeamua kwenda namna hii na lazima tukumbuke *we have a country to govern.* Tunaweza tukazungumza sana, tunaweza kupiga kelele sana, *at the end of the day we have the country to run, and we have to run it*.

Mheshimiwa Mwenyekiti na sisi kama Wabunge, ambao tumepewa mamlaka ya kufanya kazi hii, ni lazima tu-*provide leadership*. Kwa hiyo, hicho ni kitu cha msingi sana kuweza kuzingatia na ndicho kinachotuongoza sisi tunaposhughulikia mashirika. Kwenye mapendekezo yetu hapa, tumeainisha matatizo na tumependekeza ni hatua gani za kuchukua kuweza kuyamaliza hayo matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kaboyonga, amezungumzia kuhusu mtaji TRL; ni suala la msingi sana kulizingatia. Malalamiko ya mlundikano wa mizigo bandarini, hata tufanye miujiza gani, kama hatutaiimarisha reli, kama hatutaimarisha barabara, mizigo itaendelea kurundikana tu pale, kuna mambo mengi sana ya kuweza kuzingatia na ushauri wake wote kuhusiana na masuala ya *TICTS* na *exclusivity* tumeuchukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kulizungumza kwa sababu pia kengele imelia ni suala la Bodi; hili tunalielekeza kwa Serikali kwa sababu Mawaziri ndiyo wana majukumu ya kuteua Wajumbe wa Bodi.

Tunaomba Mawaziri wanapoteua Wajumbe wa Bodi kwenye mashirika, wazingatie uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakutana na watu wa ajabu sana kwenye Bodi za Wakurugenzi za Mashirika; Waziri anaamka asubuhi anatangaza Wajumbe wa Bodi na

*Treasury Registrar* ambaye ndiye mwenye mali hajui! Unawauliza Wajumbe wa Bodi wanakwenda kwenye vikao vya bodi wanarudi hamumtaarifu *TR* mwenye mali; kitu gani ambacho kimetokea? Hili napenda nilisisitize kwa sababu baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe wa Bodi kwenye mashirika haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuelezane ukweli, maana wajibu wako ni kwenda kulinda mali ya nchi kule. Tunafahamu kuna watu ambao tunawafahamu ni Wajumbe wa Bodi na wanafanya kazi yao vizuri na wanakuwa ni *agents* wa hayo mashirika katika mahusiano na Serikali *which is very good*, lakini ni lazima suala la uteuzi wa Wajumbe wa Bodi liangaliwe kwa kina sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed amezungumzia kuhusu rasilimali kwa utajiri tulionao na hata Mheshimiwa Manyanya amezungumzia; ni kweli na Wajumbe wa Kamati wanasema kwamba, nchi hii ni tajiri, mashirika ya umma ndani ya mwaka mmoja, mwaka jana tumezungumzia *investment* ilikuwa ni trilioni 4.1, hesabu ya sasa mashirika ya umma *investment* yake ni trilioni 5.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, robo ya *GDP* ya nchi iko kwenye mashirika ya umma. Kwa hiyo, tukifanya kazi vizuri na haya mashirika tutaweza kuikomboa sana nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, kwa suala la utekelezaji wa maoni ambayo tumeyatoa.

Mheshimiwa Beatrice Shellukindo katika mchango wa maandishi amesema suala la *ATCL* hatukulishughulikia; mtakumbuka kwamba, *ATCL* ilitengenezwa upya kwa hiyo haikuwa na hesabu ambazo zilikuwa zinaangukia mwaka ambao tuliushughulikia, lakini katika hesabu za sasa hivi tutaweza kulishughulikia.

Makamu Mwenyekiti amezungumzia suala la mifuko ya hifadhi ya jamii. mifuko hii imefanya kazi sana; Chuo Kikuu cha Dodoma mmeona kimekuwa kama uyoga ni kazi ya mifuko ya hifadhi za jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifuko hii imefanya *investment* kubwa sana, kwa hiyo ni lazima ushauri ambao Mheshimiwa Estherina Kilasi ameutoa tuangalie aina ya *Investment* ambazo wanafanya, maelekezo ambayo Serikali inayatoa kwenye mifuko hii, tuweze kuona ni jinsi gani ambavyo tutahakikisha kwamba fedha zinapotakiwa zinapatikana hasa wakati ambapo wastaafu watakapokuwa wanahitaji kulipwa fedha zao. Suala ni lazima liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza tena suala la *TANAPA*, hali ya sekta ya utalii ni mbaya sana; tunaiomba Serikali izingatie suala zima la kuhakikisha kwamba, *TANAPA* hawaingii kwenye matatizo kwa kutekeleza ile sheria ya kuchukua pesa; na iangalie hasa ni jinsi gani ambavyo tunaweza kushughulikia kwa sababu kuna tatizo

kubwa sana *TANAPA.* Tatizo zaidi ni Arusha, kwa sababu sekta zake zote ambazo ilikuwa inazitegemea, zimeporomoka kutokana na mtikisiko wa kiuchumi.

*TANZANITE* imeshuka bei by 80 *percent*, maua watu wameshaanza kufanya *retrenchment,* utalii ambao ulikuwa unawalipa vijana wengi sana pale Arusha ndiyo umeingia kwenye matatizo makubwa; lazima tuangalie haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bodi za mazao Waziri wa Kilimo aangalie ni kwa namna gani tunaweza tuka-*rescue* baadhi ya mazao, kwa sababu zao kama mkonge limekufa kabisa. Mkonge wetu ulikuwa unanunuliwa na mashirika mawili tu ambayo yanahusika na utengenezaji wa magari, makampuni ya magari yamekufa na hamna bei kabisa ya mkonge. Lazima tuangalie ni kwa jinsi gani tutakavyoweza kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu yote; tutaifanyia kazi katika shughuli za Kamati zijazo ambazo tutazianza rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma ilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, niwakumbushe kwamba, kila Mbunge anapoingia hapa Bungeni asubuhi pale mlangoni anapewa karatasi ya *Order Paper*; karatasi hii kama mnavyofahamu, ndiyo inayoorodhesha shughuli za siku kwa ujumla na kwa kawaida inaanza na hati za kuwasilisha mezani, ambazo mara nyingi ni za Serikali au Kamati mbalimbali, baadaye ina maswali na kurasa za mwisho huonesha shughuli zinazofuata hasa ule ukurasa wa mwisho kabisa.

Niwaombe Waheshimiwa Wabunge, mnapoingia hapa kama maswali yako si ya mwanzo, uanze kuusoma ukurasa wa mwisho kwa sababu unaonesha baada ya maswali ni shughuli gani zitakazofuata.

Waheshimiwa Wabunge, waombaji wa kuchangia hoja hii tuliyoiamua hivi sasa walikuwa 12, hata kama tungeongeza nusu saa, bado wale wanane waliokosa nafasi nisingewatendea haki, sana sana tungeongeza wawili tu.

Kwa hiyo, kwa ufanisi wa shughuli za hapa bado isingekuwa sawa sawa. Wapo waombaji wengi ambao wamekosa nafasi, nilikuwa pia na maombi ya Naibu Waziri wa Nishati na Madini, alitaka na yeye azungumze kidogo kuhusu muono wa Serikali kuhusiana na *TANESCO, TPDC, STAMICO* na kadhalika, lakini kwa sababu ya muda hakuweza kupata nafasi.

Mheshimiwa Ole-Sendeka ni mmoja wa watu waliokosa nafasi, lakini ameniletea maombi yake hapa saa kumi na moja na robo kuelekea na nusu jioni hii; kwa hiyo ukisoma pale asubuhi *Order Paper* utapeleka maombi yako na utakuwa katika nafasi nzuri ya kuchangia mwanzoni.

Waheshimiwa Wabunge, ushauri wangu ni kwamba, ukishaona jambo limepangwa katika shughuli za siku hiyo katika ukurasa wa mwisho, basi unaomba saa ile ile asubuhi ili uwe miongoni mwa wale waliowahi kabisa, lakini tukija hapa jioni inakuwa tabu kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo nizungumzie matangazo mawili madogo; moja nawatangazia Wenyeviti na Makamu Wenyeviti kuwa, wote mnaalikwa kwenye chakula cha jioni kilichoandaliwa na Mheshimiwa Spika katika Hoteli ya St. Gaspar, mara baada ya kuahirishwa kwa shughuli za Bunge. Lipo basi ambalo litawachukua hadi St. Gaspar.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la pili na la mwisho, linahusiana na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira; mnaombwa keshokutwa saa nne kamili asubuhi muwe katika Uwanja wa Ndege wa Dodoma kwa ajili ya safari ambayo tayari mna taarifa nayo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa shughuli zilizopangwa katika *Order Paper* ya siku ya leo na muda wa shughuli zetu umekwisha, naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,*
*Tarehe 30 Aprili, 2009 Saa Tatu Asubuhi*